الخوارج

بين الحقائق والأساطير

الْجُزْءُ الأَوَّلُ

KHAWARIJ

BAINA YA UKWELI NA VISA VYA KUTUNGA

JUZUU YA KWANZA

Juma Muhammad Al-Mazrui

ISTIQAAMA

Kimetayarishwa na:
Said Al Oufy, Doha-Qatar For
Istiqaama Islamic Recordings
istiqaama@hotmail.com
www.istiqaama.com
Chapa ya Kwanza: 2010

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO

UTANGULIZI 8

UANDISHI WA HISTORIA 14

UCHAMBUZI WA HISTORIA 16

VITABU NILIVYOVIPITIA 22

KITABU TAARIKH AL-RUSUL WA AL-MULUUK CHA AL-IMAMU AL-TABARI 24

KITABU AL-FUTUH CHA IBN A'ATHAM 26

SURA YA KWANZA 32

MAANA YA AL-KHAWARIJ KILUGHA (LITERALLY) NA KITAALAMU (TECHNICALLY) 32

MGAWANYIKO YA NENO KHAWARIJ KATIKA ELIMU YA SARFU YA KIARABU 33

CHIMBUKO LA NENO "KHAWARIJ" KILUGHA 33

NINI MAANA YA KHAWARIJ KITAALAMU 34

MAANA YA KHAWARIJ KATIKA MTAZAMO WA SHEIKH MUHAMMAD ABDUH 46

NENO KHAWARIJ KATIKA MATUMIZI YAKE YA KIHISTORIA 50

TUKIREJEA KATIKA TAARIFU YA AL-SHAHRASTANI 52

JINA KHAWARIJ LIMETOKA WAPI? 54

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU 58

SURA YA PILI 60

WALIOITWA KHAWARIJ 60

KUNDI LA KWANZA: AL-MUHAKKIMA (AHLU NAHRAWAAN): CHIMBUKO LA IBADHI 60

VITA VYA SIFFIN 62

SABABU NA MATOKEO 62

LENGO LA MU'AWIYA 67

KUANZA KWA VITA VYA SIFFIN 71

KUULIWA KWA SAHABA AMMAR BIN YASIR (R.A.) 73

KUNYANYULIWA KWA MISAHAFU NA KUGAWANYIKA KWA JESHI LA ALI 75

JE NI NANI KATIKA JESHI LA ALI ALIYETAKA VITA VISITISHWE NA PAFANYIKE SULHU? 79

HOJA SABA ZA WAZI 79

HOJA NA. 1: KUGONGANA KWA RIWAYA MBILI NA PIA KUGONGANA KWA RIWAYA NA MSIMAMO WA WATETEZI WA ALI 80

HOJA NA. 2: RIWAYA YA AL-BALADHIRI NAMSIMAMO WA WATAFITI WA SASA 84

HOJA NA. 3: KUZIOANISHA RIWAYA MBILI ZENYE KUGONGANA 86

HOJA NA. 4: MGONGANO MWENGINE WA RIWAYA 88

HOJA NA. 5: WALIOTAKA SULHU NI WALIOKUWA WENGI 91

HOJA NA. 6: MANENO YA ALI MWENYEWE 94

HOJA NA. 7: MSIMAMO WA AL-AHNAF BIN QAIS NA KUZOZANA KWA JESHI LA ALI 96

NATIJA 97

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU 97

NINI KILIENDELEA HUKO SIFFIN BAADA YA HAPO 101

UANDISHI WA MKATABA NA KUFUTWA KWA JINA LA UAMIRI 102

KURUDI KWA ALI AL-KUFA, KUJITENGA KWA AL-QURRAA NA MJADALA WAO NA IBN ABBAAS 107

HOJA ZA IBN ABI AL-HADID 111

SURA YA TATU **120**

HOJA ZA WATETEZI WA ALI NA JAWABU ZA WATU WA NAHRAWAAN 120

JAWABU YA WATU WA NAHRAWAAN 121

MSIMAMO WA IBN ABBAAS BAADA YA KUPATA HOJA ZA WATU WA NAHRAWAAN 125

IBN ABBAAS AJITENGA NA ALI 127

MJADALA WA ALI NA WATU WA NAHRAWAAN *128*

MAELEZO YA AL-MUBARRAD *133*

MAELEZO YA AL-SHAHRASTANI *136*

NATIJA NA MUKHTASARI WA SEHEMU HII *137*

SURA YA NNE **139**

KUFUTWA JINA LA UKHALIFA: JAMBO LA PILI LILILOWAPELEKEA WATU WA NAHRAWAAN KUJITENGA NA ALI NA KUCHAGUA IMAMU WAO *139*

MUKHTASAR NA NUKTA MUHIMU *145*

SURA YA TANO **147**

SULHU YA "DUMAT AL-JANDAL" NA NATIJA YAKE *147*

ALI AKUSANYA JESHI UPYA ILI KUMPIGA MU'AWIYA; NA WATU WA NAHRAWAAN WAKATAA KUJIUNGA NA ALI *150*

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU *151*

SURA YA SITA **154**

KUULIWA KWA ABDULLAHI BIN KHABBAB NA KUANZA KWA VITA VYA NAHRAWAAN *154*

RIWAYA YA KUULIWA KWA SAHABA ABDU-LLAHI BIN KHABBAAB *154*

UCHAMBUZI WA MATN YA RIWAYA HIO *155*

MAELEZO ZAIDI KUHUSU MATN YA RIWAYA HII *159*

RIWAYA YA PILI *163*

MATN YA RIWAYA HII *164*

RIWAYA YA TATU *164*

MATN YA RIWAYA *165*

TAKHRIJ NA UCHAMBUZI WA SANAD ZA RIWAYA HIZO *168*

UCHAMBUZI WA UJUMLA WA SANAD YA RIWAYA HII *173*

UCHAMBUZI WA SHEIKH NASSIR AL-SABI'I WA RIWAYA YA KUULIWA KWA ABDILLAHI BIN KHABBAB *174*

TANBIHI *179*

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU *182*

SURA YA SABA **184**

ITIKADI WALIZOHUSISHWA NAZOWALIOITWA KHAWARIJ *184*

MJADALA WA RAI HIZI *184*

KUUA BILA YA HAKI *185*

WALIOKUJA BAADAE: HARAKATI ZA SHEIKH MUHAMMAD ABDIL-WAHHAB NA WAFUASI WAKE *194*

KUWAITA WAISLAMU MAKAFIRI *198*

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU *210*

SURA YA NANE **213**

KUULIWA KWA AL-IMAMU ALI *213*

MATN YA RIWAYA *216*

SANAD YA RIWAYA *218*

USHAHIDI WA WANAOSEMA KUWA ALI KAULIWA KWA NJAMA ZA MU'AWIYA *218*

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU *226*

SURA YA TISA **229**

MASAHABA WA NAHRAWAAN *229*

MAJINA YA MASAHABA WA NAHRAWAAN *236*

MUKHTASARI WA JUMLA NA NUKTA MUHIMU *244*

HATIMA **250**

بسم الله الرحمن الرحيم

الْحَمْدُ لِلهِ رَبِّ الْعَالَمِيْنَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِيْنَ وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَ عَلَى الظَّالِمِيْنَ, وَأَشْهَدُ أَنْ لا إلـه إلا الله وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَـهُ ولـي المتقين، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُوْلُهُ وَصَفِيُّهُ مِنْ خَلْقِهِ وَخَلِيْلُهُ بَلَّغَ الرِّسَالَةَ وَأَدَّى الأَمَانَةَ وَنَصَحَ الأُمَّةَ وَكَشَفَ اللهُ بِهِ الغُمَّةَ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَسَلَّمَ

UTANGULIZI

Historia ya binaadamu ni historia ya kupanda na kuporomoka kwa maadili. Na hii inatokana na ukweli kwamba akili ya binaadamu haina uwezo wa kujiongoza katika kila kitu, ongeza na ukweli kwamba matamanio ya nafsi na maslahi ya kibinafsi ni matatizo sugu katika historia nzima ya binaadamu. Na kwa hivyo, jamii tafauti zimekuwa mara kwa mara zikisibiwa na maradhi ya kuwepo kwa tabaka za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa kuzingatia ukweli huu, basi imekuwa ni Sunna ya Mwenyezi Mungu katika ardhi kutuma Mitume (A.S.) ili kutoa mafunzo sahihi yenye kuhakikisha usawa na uadilifu baina ya wanaadamu wote. Pia ili wawafunze watu namna ya kujenga uhusiano wao na Muumba wao.

Halkadhalika kabla ya kuja Mtume (s.a.w.), ulimwengu ulikuwa umesibiwa na kila aina ya maradhi – ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, n.k .

Kwa hivyo, Allah (S.W.) akamtuma Mtume (s.a.w.) ili kuja kuuokoa ulimwengu kutokana na aina zote za upotovu. Mtume (s.a.w.) akaongoza kwa muda wa miaka ishirini na tatu (23), baina ya kipindi cha Utume wake alipokuwa Makka na alipokuwa Madina. Akatoa mafunzo – katika kipindi hicho – kutoka kwa Mola wake, na akaweza kuibadilisha jamii, kisiasa na kiuchumi – jambo ambalo linaeleza ukweli kwamba Uislamu unatoa *itikadi* kamili ya kisiasa (political ideology), tafauti na Wamagharibi wanavyotaka kuupotosha ukweli huu na kuzifanya harakati za Waislamu ziishie katika kurukuu na kusujudu tu, ili wapate kuwatawala kwa dhulma!

> Baada ya jihadi na juhudi; na kutoa mafunzo makubwa yasio na kifani, Mtume (s.a.w.) akafariki duni mwaka wa 11 H., akiwa na umri wa miaka 63 na siku nne. Akaondoka duniani hali ya kuwa karidhiwa na Allah (s.w), Malaika na Waumini bali na kila mkweli: hakuna aliyemchukia isipokuwa watu wa aina mbili: Kafiri mwenye hasad katika moyo wake na mnafiki aliyekosa mas-lahi yake ya kibinafsi. Basi rehema na amani ziwe juu yake milele na milele na laana na ghadhabu za Allah ziwe juu ya wote wanaomchukia na kumtusi. **'Hakika ya wale wenye kumuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Allah amewalani duniani na akhera na amewaandalia adhabu yenye kudhalilisha.**[1] ……**Hakika wale wenye kumuudhi Mtume watapata adhabu iumizayo.'**[2]
>
> Mtume (s.a.w.) akaondoka duniani, naye ametuachia vitu viwili ili tujiongoze kwavyo: Qur-ani na Sunna zake..[3]

Baada ya Mtume (s.a.w.) kuondoka duniani, Waislamu wakakubaliana kumchagua Abu Bakr Al-Siddiq (r.a.) kuwa Khalifa wao, naye akawaongoza kwa uadilifu wa hali ya juu hadi akaondoka duniani hali ya kuwa Masahaba wote wamemridhia. Na baada ya kuondoka duniani Waislamu wakamchagua Umar Al-Faruq (r.a.), naye akaongoza kwa uadilifu sawa na Abu Bakr. Baada ya kufa Umar, Waislamu wakamchagua Uthman bin Affan. Uthman aliongoza kwa uadilifu katika miaka sita ya mwanzo, na miaka sita ya pili utawala wake ukawa ni wenye mzozo mkubwa baina yake na Masahaba wenzake. Masahaba waliutia kasoro sana utawala wake na hatimae hilo lilipelekea Uthman kupoteza maisha yake.[4] Na hapo ikawa ndio chanzo cha fitna baina ya Waislamu: fitna ambayo iliendelea moja kwa moja hadi kufikia kugawanyika kwa watu na kuwa makundi matatu makubwa na hatimae

---

[1] - Sura ya 33 Aya ya 57.

[2] - Sura ya 9 Aya ya 61.

[3] - Maneno haya nimeyanukuu kutoka katika utangulizi wa kitabu *Historia Ya Kiibadhi* cha ndugu yetu Sh. Hafidh Al-Sawaafi. Kitabu hiki bado hakijachapishwa, sijui labda mwenyewe baadae anaweza kubadilisha au kuondoa kabisa yaliomo katika utangulizi huu.

[4] - Waliomuua Uthman ni Masahaba na Wafuasi wao, kama utavyoona humu ushahidi juu ya hilo. Lakini kwa hali yoyote ile hali inajionesha kwamba Uthman hakuwa mtu mbaya lakini alikuwa na udhaifu katika uongozi kwa sababu ya uzee. Na kheri alizozifanya ni nyingi sana.

kugawanyika tena na kuwa madhehebu tafauti. Na baada ya Uthman kuondoka duniani, watu walikubaliana kumchagua Ali bin Abi Talib (k.w.). Naye aliongoza kwa uadilifu sawa na waliomtangulia. Lakini utawala wake alipata mitihani mingi kuliko waliomtangulia. Kwanza baada ya kuuliwa Uthman, baadhi ya Masahaba, ambao *walimbaii* (waliahidiana naye kumtii) wakawa dhidi yake wakidai kutaka kisasi cha Uthman. Hawa ni Talha, Zubair na waliokuwa pamoja nao. Na kwa hivyo, vikaanza vita vijulikanavyo katika historia kuwa ni vita vya *Jamal*, ambavyo vilipiganwa baina ya Ali na wafuasi wake kwa upande mmoja na Talha na Zubair na wafuasi wao kwa upande wa pili. Vita hivi viligharimu roho nyingi za Waislamu na viliishia kwa kufuzu Ali na kuuliwa kwa Talha[5] na Zubair.[6] Baadae Mu'awiya bin Abi Sufyaan – ambaye alikuwa Liwali (Gavana) wa Uthman huko Sham – akakataa pia kuutambua Ukhalifa wa Ali kwa madai ya kutaka watolewe waliomuua Uthman kwanza. Baada ya vuta-nikuvute na kufeli kwa njia zote za kidiplomasia – kama tutakavyoona huko mbele – Ali na waliokuwa pamoja naye miongoni mwa Masahaba na wafuasi wao wakaamua kumpiga vita Mu'awiya. Hapo vikaanza vita vijulikanavyo katika historia ya Kiislamu kuwa ni vita vya ***Siffin***. Baada ya vita hivyo kudumu kwa siku nyingi, ikawa ushindi unamuelekea Ali. Mu'awiya alipoona kwamba anakaribia kushindwa akatafuta mbinu ya kusimamisha vita na kulifarikisha jeshi la Ali. Amru bin Al-'Aas akamshauri kunyanyua Misahafu ikiwa ni kama ishara ya kutaka sulhu na hapo jeshi la Ali likagawika baina ya wenye kukubali ombi hilo na wenye kukataa. Ali alikuwa ni katika wenye kukataa lakini baada ya kuwa walio wengi katika jeshi lake walikuwa wanasisitiza sulhu, Ali akakubaliana nao. *Al-Qurraa*

---

5 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 30,44.

6 - Lakini Zubair yeye hakufa vitani, bali Ali – kwa mujibu wa riwaya zinavyonena - alimkumbusha maneno ya Mtume (s.a.w.) kwamba Zubair atampiga Ali kwa dhulma. Hapo Zubair akaondoka kuelekea Madina na njiani akauliwa na mtu aitwaye 'Amru bin Jurmuz. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 50. Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 3, uk. 274-275, *tarjama* na. 592. (Katika *Siyaru Al-A'alam* j.3, uk. 40-41, jina la aliyemuua Zubair ni 'Umair bin Jurmuz). Lakini riwaya isemayo kwamba Ali alimkumbusha Zubair kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo: "Itakuaje wewe (Zubair) utapompiga (Ali) kwa dhulma" ni riwaya ambayo wajuzi wameidhoofisha kama ilivyo katika maelezo ya chini yaliotiwa na Muhammad Buyumi na wenzake katika kitabu *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya* cha Ibn Kathir, j. 7, uk. 239, kwa sababu katika *sanad* yake kuna Abu Jar-wi naye hajulikani, na pia kuna Abdul-Malik bin Muslim, anasema Al-Bukhari "Hadithi zake hazikusihi" na pia kuna Abdullah bin Muhammad naye ni dhaifu.

(Wasomi) waliokuwemo katika jeshi la Ali – nao ni Masahaba wanavyuoni wafikao elfu nne – wakalipinga jambo hilo, na wakamshikilia sana Ali kuwa asikubali sulhu, na kwamba ama Mu'awiya akubali kuingia katika utawala wa Ali au apigwe vita hadi kuuliwa na kumalizwa jeshi lake lote.[7] Baada ya kuonekana kwamba Ali kashikilia msimamo wake; na mkataba wa kusimamisha vita ukawa umeshaandikwa na kuonekana kwamba kilichomo katika mkataba huo ni kinyume na Qur-ani, Masahaba hao *(Al-Qurraa au Wasomi)* walijimegua na kujitenga kutoka katika utawala wa Ali na kwenda katika sehemu iitwayo Al-Harauraa,[8] na kwa sababu hio ndio watu hao huitwa kuwa ni *Al-Harauriyya* au *Al-Haruriyya* au *Ahlu Al-Harauraa* yaani watu wa Harauraa. Na hapo wakajichagulia Imamu wao mpya[9] kwa njia ya Shura kwa lengo la kuamrisha mema na kukataza mabaya,[10] kwani

---

7 - Yaani likikataa kutubia.

8 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12. Vitabu vyengine vimeiita sehemu hio kuwa ni "Al-Haruraa" kama ilivyo katika *Al-Taarikh* cha Al-Tabari na *Sharhu Al-Nayl* cha Al-Shaukani na *Sharhu Nahji Al-Balagha* cha Ibn Abi Al-Hadid na vyenginevyo; na vitabu vyengine vimeiita sehemu hio kuwa ni "Al-Harauraa" kama Ibn Sa'ad katika *Al-Tabaqat* lakini niliporejea *Mu'ujamu Al-Buldan* cha Yaqut Al-Rumi j. 3, uk. 138, nimeona kuwa yeye kaandika "Al-Harauraa" na si "Al-Haruraa", kwa hivyo nimetegemea zaidi nakala yake kwani yeye ndiye anayetegemewa sana katika maarifa ya miji. Hata hivyo, watu wengi wanatumia neno "Al-Haruraa".

9 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 135.

10 - Anasimulia Al-Baladhiri kwamba: "Baada ya watu wa Nahrawaan kukusanyika kwa Abdillahi bin Wahb Al-Rasibi (r.a.), akawahutubia na akawalingania kuamrisha mema na kukataza maovu na kusema haki hata ikiwa chungu na ikadhuru…(Akasema): 'Tokeni enyi ndugu zetu mwende sehemu za Al-Sawaad na majabalini muzikatae bidaa hizi zenye kukirihi…..kisha wote wakasema wakiidharau dunia na kulingania kuwa watu waikatae na kufanya juhudi katika kutafuta haki na kupinga bidaa na dhulma". Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 137. Hili ndilo lilowafanya watu wa Nahrawaan kujitenga – kukimbia na dini yao kutokana na fitna na bidaa, si kufanya ufisadi katika ardhi, tafauti na watu wanavyowapakazia. Halkadhalika walipotaka kuchagua Imamu wao: kila mmoja aliukataa uimamu na hatimae Al-Imamu Abdullah bin Wahb Al-Rasibi (r.a.) akaukubali akisema: "*Wallahi* siuchukui kwa kupenda dunia wala siukatai kwa kuogopa mauti". Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 134. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18. Na mfano wake kimaana ni katika Al-Darjini *Al-Tabaqat* j. 2, uk 202. Yote haya yanathibitisha kwamba watu hawa hawakumuacha Ali kwa kutaka dunia, bali kwa kuona kwamba sulhu alioifanya ni kinyume na Qur-ani. Ndio maana ikawa wanamrejea sana Ali ili waanze vita upya. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 133,135.

waliona kwamba kwa kukubali sulhu,[11] Ali amekwenda kinyume na Qur-ani na hakukubali kusikiliza nasaha zao na wao ndio wanavyuoni, kwa hivyo waliona Ali hawezi tena kuwa Khalifa kwani wao walimbaii kwa masharti ya kufuata Kitabu cha Allah na Sunna ya Mtume (s.a.w.), akienda kinyume na kimoja katika hivyo basi hawana haki ya kumtii kama Mtume (s.a.w.) alivyobainisha kwamba: **"Hakuna kumtii kiumbe ukamuasi Muumba".**[12]

Kisha baada ya hapo, Masahaba hao na wafuasi wao wakaenda katika sehemu inayoitwa Al-Nahrawaan,[13] na kwa sababu hio watu hawa pia huitwa *Al-Nahrawaaniyyun* au *Ahlu Al-Nahrawaan* yaani watu wa Nahrawaan. Baadae wakaungwa mkono na idadi nyengine ya Waislamu wanaofikia elfu nane.[14] Kwa hivyo, hawa ndio watu ambao waandishi wa historia na makala[15] wanawaita kuwa ni Khawarij[16] wakimaanisha kuwa wametoka katika dini. Kitabu hiki kinatafiti suala hilo na kubainisha ukweli ni upi na hoja sahihi ziko wapi. Lakini wakati umo katika kuutafuta ukweli, basi elewa kwamba ukweli ni kitu chenye thamani kubwa ambacho hakuna anayeweza kukifikia ila:

1) Anayekusudia kutafuta haki.
2) Anayejua kwamba kipimo ni Qur-ani na Sunna ya Mtume (s.a.w.): si fulani na fulani.
3) Aliyetayari kujifungua pingu za kufuata kama bendera.
4) Anayejifungua pingu za *urithi kutoka kwa wazee* na kukusudia kufuata haki popote itakapombainikia. Na si kila tulilolirithi ni sahihi wala si kila tulilolirithi ni kosa, kuna yaliokuwa sahihi na yasiyokuwa sahihi
5) Anayejua kwamba majina mazuri kama: *Ahlu Sunna Wal-Jamaa'a* **(**kama wanavyojiita madhehebu za Kisuni) *Ahlu Al-Haqqi Wal-*

---

11 - Na kwa sababu nyengine tutazozibainisha humu *Inshaa Allah.*

12 - Ahmad *Al-Musnad* j. 1, uk. 366, Hadithi na. 1065, uk. 372-373, Hadithi na. 1095. Na mfano wake ni katika Al-Nasai *Al-Kubra* j. 8, uk. 71, Hadithi na. 8667-8668.

13 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 135. Wengine huitamka "Nihrawaan" kama alivyotaja Yaqut Al-Rumi katika *Mu'ujamu Al-Buldaan* j. 8, uk. 818.

14 - Kama tutavyoeleza na kutoa marejeo baadae.

15 - Si makala kwa maana ya *Article,* bali ni makala kwa maana ya zile imani na itikadi zilizomo katika vikundi tafauti, yaani kauli zao ambazo wanahusika nazo wao tu.

16 - Kwa hivyo, popote katika kitabu hiki utapoona nimetumia neno "Watu wa Nahrawaan" au "Watu wa Harauraa" au "Al-Muhakkima" basi makusudio ni watu hao walioitwa kuwa ni Khawarij.

Istiqama, (kama wanavyojiita Ibadhi) *Madrasatu Ahli Al-Bait (*kama wanavyojiita Shia), ni majina ya madai tu, hayathibitishi haki wala ukweli, kwani ni majina ambayo watu wenyewe walijichagulia, wala haikuja Aya kutoka mbinguni au Hadithi ya Mtume (s.a.w.) ikasema kuwa madhehebu fulani ndio madhehebu ya haki au ya Sunna na madhehebu fulani ni madhehebu batili au ya bidaa. Halkadhalika majina mabaya kama: *Al-Rawafidh* (kama wanavyoitwa Shia) au *Al-Nawasib* (kama Shia wanavyowaita Sunni) au *Al-Khawarij* (kama walivyoitwa makundi tafauti likiwemo kundi la Ibadhi), haya ni majina mabaya ambayo hayathibitishi kuwa aliyeitwa hivyo yuko katika batili, bali ni majina tu – kama ulivyo utani wa kisiasa – kila kundi lilikuwa likiwaita wafuasi wa kundi jengine ili kuwafanya watu waliepuke kundi hilo na walipige vita, ni sawa sawa na leo Waislamu *Mujahidina* kuitwa magaidi. Kwa hivyo, ni lazima – kwa anayetafuta ukweli – kipimo chake kiwe ni Qur-ani na Sunna, si majina mazuri na mabaya,[17] na huu ndio wito wa Sheikh Al-'Allama Ali Yahya Ma'amar kama alivyobainisha katika kitabu chake *Al-Ibadhiyya Baina Al-Firaqi Al-Islamiyya* chini ya kichwa cha habari kisemacho: *"Mafuhumu ambayo ni wajibu kutoweka".*[18]

6) Na la muhimu kuliko yote ni kujua hoja za kila kundi badala ya kuwa siku zote watu wanafanya kazi ya kusoma hoja za upande mmoja tu.[19] Na pia kujua kwamba wingi na uchache si kipimo sahihi

---

17 - Kwa mfano leo Mawahabi wanajiita "Ansaru Sunna" (Wenye kuzinusuru Sunna za Mtume s.a.w.) au "Al-Salafiyya" (Wafuasi wa waliotangulia yaani Masahaba na wafuasi wao) na wanasema kuwa wao ndio "Ahlu Sunna wal Jamaa". Wakati wafuasi wa madhehebu nyengine za Kisuni hawakubaliani na "Mawahabi" au "Ansaru Al-sunna" au "Al-Salafiyya" au "Ahlu Sunna wal Jamaa" katika mambo mengi ya itikadi na matendo. Bali Waislamu wengi duniani hawakubaliani na kikundi hicho. Sasa ikiwa tutachukua jina kuwa ndio kipimo, basi Wahabi atakuwa ndiye aliye sahihi kwa jinsi alivyobeba majina mengi mazuri yenye kupendeza. Basi kwanini tusimfuate naye ana majina hayo mazuri?! Kwa hivyo, ni wazi kwamba chenye kuzingatiwa ni ile itikadi yenyewe na matendo yenyewe kwa kuyarejesha katika ushahidi wa Qur-ani na Sunna na kuyatazama kwa misingi sahihi ya elimu, na hapo tutaweza kujua nani Ansaru Sunna, Al-Salafiyya au Ahlu Sunna; na nani kaenda kinyume na sunna.

18 - Ali Yahya Ma'amar *Al-Ibadhiyya Baina Al-Firaq* j. 2, uk. 127-134.

19 - Na hili limewapelekea watu wengi kuwa na fikra finyu na wakati mwengine kuwasema watu wa madhehebu nyengine kwa kitu ambacho hakipo kwao kwamwe, kama Ibn Hazm alivyosema – akinukuu maneno ya kusikia – kwamba Ibadhi hawali

katika dini,[20] kwani wingi umekuwa na sababu zake na uchache umekuwa na sababu zake ambazo si sababu za kutafuta haki au kuepuka batili.

Ni matarajio yangu kwamba kitabu hiki kimetoa maelezo ya wazi juu ya suala hili. Kitabu hiki ni juzuu ya kwanza na kitafuatiwa na juzuu nyengine, *Inshaa Allah.*[21]

UANDISHI WA HISTORIA

Jambo moja muhimu katika usomaji wa historia ni kujua tatizo la njia iliyotumika kuandikwa historia yenyewe. Tatizo la uandishi wa historia hasa hasa ya migawanyiko (nitafupisha sana ili kukuleta katika nukta (point) tu ili kuhifadhi wakati) ni kuwa haikuandikwa kwa ajili ya kuudhihirisha ukweli na kuibainisha haki, bali iliandikwa kutokana na matashi au matamanio binafsi ili kuupamba na kuupa nguvu msimamo fulani wa kisiasa au kumpamba fulani kisiasa na kuupaka matope msimamo pinzani. Lakini ili jambo hili liweze kufaulu, ililazimika historia iundiwe riwaya kadhaa wa kadhaa za uwongo. Huhitaji kuwa mwanachuoni *Mujtahid* ili uweze kuugundua ukweli huu, bali ni kiasi cha kufunua kitabu kimoja tu, basi utaona riwaya inaposimuliwa, jinsi gani mwanzo wa riwaya hio unavyogongana na mwisho wake. Chukua mfano mmoja wa riwaya inayosimulia matukio ya Nahrawaan inayosema kwamba Ali alipokwenda huko ili kuwataka watu hao wa Nahrawaan wawatoe waliomuua Abdullah bin Khabbaab vyenginevyo atapigana nao vita, Ali aliwambia wafuasi wake kwamba musianze

---

samaki mpaka wamchinje na wanasali sala ya fardhi rakaa mbili tu: moja asubuhi na moja jioni! Tutaoa maelezo na marejeo baadae.

[20] - Tazama Al-Sawaafi *Historia Ya Kiibadhi* katika hatima ya kitabu chake ana maelezo marefu kidogo na mazuri juu ya maudhui hii.

[21] - Juzuu hii ni kuhusu historia ya watu wa Nahrawaan tu. Juzuu nyengine zitahusu vikundi vyengine vilivyoitwa kuwa ni Khawarij; nyengine ni utafiti wa Hadithi tu zenye kuhusu suala hili na nyengine ni mkusanyiko wa mijadala yote tulioifanya na watu tafauti juu ya suala hili. Yote hayo yatatimia kwa matakwa ya Allah.

kuwapiga mpaka wao wakuanzeni![22] Sasa ikiwa utatumia mantiki sahihi hapa basi utaona kwamba hapa kuna mgongano. Na hii ni kwamba ikiwa Ali kaenda huko ili kutaka watolewe waliomuua Ibn Khabbaab au vinginevyo kuwapiga vita watu hao wa Nahrawaan ikiwa watakataa kuwatoa wauaji, basi maneno "Musiwapige hadi wakuanzeni" – nao kwa mujibu wa riwaya hio walikataa kuwatoa waliomuua Ibn Khabbaab – basi yatakuwa hayana maafikiano na dai kwamba Ali kaenda huko ili kudai waliomuua Ibn Khabbaab au vinginevyo kuwapiga vita watu hao wa Nahrawaan. Changanya hili na maneno ya Ali katika riwaya nyengine – baada ya Watu wa Nahrawaan kujitenga naye – kwamba aliwaambia wafuasi wake "Musiwapige mpaka wazue jambo",[23] sasa jambo – kwa mujibu wa riwaya hio – tayari wameshalizua na wameshaua naye Ali kaenda huko kwa sababu hio ya kuzua kwao jambo la kuua mtu bila ya haki, sasa vipi tena Ali aseme: "Musiwapige hadi wakuanzeni…..…musiwapige mpaka wazue jambo?" Utaona hapa kuna mgongano wa wazi katika *mutun* (*text*s au maneno) ya riwaya hizi.

Jambo hili la kuwepo kwa mgongano mkubwa katika riwaya tafauti zinazohusu historia, lilitarajiwa litowe changamoto katika kuisoma upya historia kwa kuyachambua maelezo yake na kuzitazama vyema *sanad* zake. Na kwa bahati mbaya sana asilimia tisiini au zaidi ya maelezo ya matokeo yaliyomo katika vitabu vya historia yamesimuliwa na wasimulizi waongo, dhaifu sana au wasiojulikana kabisa.[24] Changanya na

---

22 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 146.

23 - Ibn Abi Shaiba *Al-Musannaf* j. 8, uk. 732, Hadithi na. 13.

24 - Aghlabu ya matukio ya kihistoria ya Kiislamu yamesimuliwa na: Mosi: Abu Mikhnaf, naye ni Shia dhaifu sana. Anasema Al-Dhahabi katika *Al-Mizan* na Ibn Hajar katika *Lisanu Al-Mizan* kuhusu Abu Mikhnaf huyu: "Ni mtoaji habari mbovu, haaminiki, kaachwa na Abu Hatim na wenzake." Na akasema Al-Daraqutni: "Dhaifu." Na akasema Yahya bin Ma'in: "Si muaminifu." Na akamtaja Al-'Uqaili katika wapokezi dhaifu. 24 Na akaongeza Al-Dhahabi kutoka kwa Ibn Adey akisema kwamba ni "Shia wa kuungua (Shia mkereketwa) msimulizi wa habari zao." Tazama *Lisanu Al-Mizan* j. 4, uk. 55-56, *tarjama* ya 1368. Pili: Saif bin Umar Al-Tamimi, naye ni mwongo mkubwa, mtunzi wa Hadithi. Anasema Ibn Ma'in, Al-Daraqutni na Al-Nasai: "Hadithi zake ni dhaifu". Anasema Abu Hatim ni "Mwenye kuachwa". Anasema Ibn Adey: "Hadithi zake zote ni munkar". Anasema Ibn Hibbaan: "Anasimulia Hadithi za kutunga kutoka kwa watu waaminifu..na wamesema kwamba alikuwa akitunga Hadithi". Na akasema Ibn Hibbaan na Al-Daraqutni: "Alituhumiwa kwa uzandiki (unafiki, yaani katuhumiwa kuwa akijifanya Muislamu naye si Muislamu)". Tazama Ibn

ukweli kwamba asilimia kubwa ya waandishi wa historia waliishi katika zama za Banii Umayya na walikuwa ni wafuasi wa dola hio, na wengine waliishi katika zama za dola ya Abbasiyya nao pia walikuwa ni wafuasi wa dola hio, na wengine walikuwa ni wafuasi wa watawala waliokuwa wakimili katika mrengu wa Ali au wao wenyewe walikuwa ni Mashia, na wote hawa ni wapinzani wa Watu wa Nahrawaan, na juu ya yote hayo, ni kuwa waandishi hao hawakuwa na uadilifu kama maadishi yao wenyewe yanavyoonesha.[25] Halkadhalika riwaya za historia zinazoonyesha kuwa Watu wa Nahrawaan ni wabaya – hata zile zilizomo katika *Sahihu Al-Bukhari* na *Sahihu Muslim* – ni riwaya za wasimulizi wa Kishia wa Al-Kufa, nao ni maarufu kwa uzushi wa Hadithi kama tulivyobainisha katika makala na vitabu vyetu tafauti.[26] Kwa hivyo, historia inataka uchambuzi maalumu uliojengeka katika uadilifu na upekuzi wa kina wa riwaya.

UCHAMBUZI WA HISTORIA

Ama kuhusu uchambuzi wa maandishi ya Kihistoria utaona kuwa umeathirika sana kwa sababu ya upendeleo uliotokana na kurithi fikra na maoni ya wachambuzi ambao wameathirika na matamanio ya nafsi. Wakati mwengine mpekuzi hufikia *natija ya makosa* kwa sababu ya

---

Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 4, uk. 259-260, *tarjama* na. 517. Tatu: Al-Waqidi, naye ni Muhammad bin Umar, alikuwa mwongo akitunga Hadithi. Anasema Al-Imamu Ahmad bin Hanbal: "Al-Waqidi ni mwongo mkubwa anazigeuza Hadithi". Anasema Al-Nasai: "Katika madhaifu waongo waliomaarufu kwa uwongo ni wane: (mmoja wao ni) Al-Waqidi". Na wakasema: Abu Hatim, Al-Nasai na Is-haq bin Rahawaih: "Alikuwa akitunga Hadithi". Na maelezo yake ni marefu. Tazama Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 323-326, *tarjama* na. 606. Nne: Muhammad bin Qudama Al-Ansari naye ni dhaifu. Tazama Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 363-364, *tarjama* na. 668. Tano: Ibn Is-haq, naye hali yake haijambo ukilinganisha na wengine lakini ni dhaifu na anaghushi. Maelezo yake ni marefu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 34-40, *tarjama* na. 50. Sita: Muhammad bin Saib *Al-Kalbi* naye ni mwongo alikuwa akisimulia Hadithi za kutunga. Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 157, *tarjama* na. 268. Na wako wengi wengineo wasiokuwa hawa.

[25] - Tafauti na walioitwa Khawarij ambao wanavyuoni na watafiti wamethibitisha kwamba hakuna watu wakweli kama wao. Tumelibainisha hili katika vitabu na makala tafauti. Tazama kitabu chetu *Mezani Ya Haki* uk. 19-21.

[26] - Tazama utangulizi wa kitabu chetu tulichokiita *Ukhalifa* j. 1.

udhaifu wake wa kutafiti au kwa kufanya haraka. Labda kwa leo – baada ya kuanzishwa katika sehemu nyingi za dunia vyuo vyenye *manhaj* yaani vyenye njia ya uchambuzi wa kichuo (Academic Methodology) – basi utaona kwa kiasi fulani kumepatikana maendeleo ya uchambuzi wa historia. Hili linadhihiri katika utafiti (research) mwingi unaofanywa katika vyuo vikuu tafauti katika ulimwengu wa Kiislamu ambapo watafiti hao huibuka na natija tafauti baina yao na pia huibuka na natija zilizo tafauti na zile za wanavyuoni wa zamani.

Lakini labda tutoe baadhi ya mifano michache ya uchambuzi uliojengeka katika matamanio ya nafsi na upendeleo. Mfano mmoja wa namna gani watu wanachambua mambo kwa matamanio na upendeleo na si kwa uadilifu na utafiti wa kielimu, unadhihiri katika tukio la vita vya Jamal. Katika vita hivi Sahaba aitwaye Talha bin Ubaidillah aliuliwa na mtu aitwaye Mar-waan bin Al-Hakam.[27] Sasa utaona watu wanamlaumu Mar-waan kwa sababu ya kumuua Talha,[28] lakini uadilifu unatutaka tujiulize kwanini watu hao hawamlaumu Ali ambaye alipigana na Talha kwa lengo hilo hilo: ili amuue Talha; au Talha arudi katika utawala wa Ali? Sasa jiulize wewe jambo hili limekuwa baya kwa sababu limefanywa na Mar-waan, au limekuwa baya kwa sababu Mar-waan kamuua Talha naye hastahiki kuuliwa? Kama kamuua naye hastahiki kuuliwa, basi uchambuzi sahihi unatupa natija kwamba na Ali ni mbaya kwa kupigana na Talha na Zubair[29] ambao hawastahiki kuuliwa, kwani alipopigana nao lengo lake ni kuwa ama warudi katika utawala wake au

---

27 - Mar-waan bin Al-Hakam ni jamaa wa Uthman bin Affaan. Naye alimuua Talha kwa sababu ni mmoja wa waliohimiza kumuua Uthman kisha akadai kisasi. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 28. Bali Mar-waan kadai kwamba Talha ni katika waliomuua. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 43. Bali inasemekana kwamba Talha ndiye aliyemnyima Uthamn maji ya kunywa. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 6, uk. 211.

28 - Tazama maneno ya Al-Ismaili katika "*Tahdhibu Al-Tahdhib"* j. 10, uk. 83, ambapo anamlaumu Al-Bukhari kwa sababu ya kusimulia riwaya kutoka kwa Mar-waan huyu, ilhali kafanya dhambi kuu kwa kumpiga Talha. **Ninasema:** Mar-waan bin Al-Hakam kweli ni muovu sana lakini uchambuzi huu si uchambuzi wa uadilifu.

29 - Sisemi kuwa Talha na Zubair ndio waliokuwa katika haki na kwamba Ali ni mkosa; *Laa:* sisemi hivyo, bali ninasema kuwa Ali ndiye aliyekuwa katika haki, lakini napinga hii njia ya uchambuzi wa upendeleo; kama Talha anastahiki kuuliwa basi hatazamwi nani kamuua, na kama hastahiki basi Ali ni mkosa kwa kupigana naye, huu ndio uchambuzi sahihi.

awaue.[30] Utaona hapa kwamba watu – katika uchambuzi wao – wanatazama fulani ni nani: si fulani katenda au kanena nini. Tazama mantiki (logic) hii:

1) Mar-waan kampiga Talha = Mar-waan ni muovu.
2) Ali kawaua waliokuwa pamoja na Talha ili amuue Talha = Ali ni mtu mwema *mujtahid!*

Mfano mwengine utaupata utapomuuliza mwanachuoni, je kumpiga vita Khalifa wa Waislamu bila ya kuwepo sababu ya Kisharia inafaa? Atakujibu: "Haifai na ni uasi". Muulize: "Ali alikuwa Khalifa wa haki wa Waislamu?" Atakujibu "Ndiyo". Muulize: "Je alifanya kosa la kuwa apigwe vita?" Atakujibu: "*Laa:* hakufanya". Mwambie: "Kama hakufanya, je aliyempiga vita ni dhalimu?" Kwa msingi wake alioutanguliza, bila shaka atakwambia: "Ndiyo: aliyempiga vita ni dhalimu". Mwambie: "Basi Talha, Zubair na Mu'awiya ni madhalimu". Atakwambia "Aa wao si madhalimu, bali walijitahidi na wana fungu lao la ijtihadi!" Mwambiye: "Basi Ali ni dhalimu kwa kuwapiga wao." Atakwambia: "Aa naye si dhalimu". Mwambie: "Basi Watu wa Nahrawaan ni madhalimu". Atakwambia: "Ndiyo". Ukimuuliza: "Vipi wamekuwa hawa madhalimu wale wasiwe madhalimu na wote wamepigana vita na Ali baada ya *kubaiiwa*".[31] Labda atakujibu: kwamba "Wale ni Masahaba *mujtahidun".* Akikujibu hivyo muulize: "Kwani Usahaba unaifanya dhambi iwe thawabu na kosa liwe sahihi?" Hapa sijui atakujibu nini! Halafu muulize tena: "Kwani Watu wa Nahrawaan si Masahaba?"[32] Akikwambia "Si Masahaba". Muulize: "Wangekuwa Masahaba nao wamefanya kosa hilo hilo, je kosa lao hilo lisingelikuwa kosa?" Akikwambia: "Ndiyo" basi hapa kitakubainikia kile nilichokueleza cha watu kushindwa kuwa waadilifu katika kutoa hukumu na kushindwa kufanya uchambuzi sahihi.

---

[30] -Kwa hali yoyote ile kumpiga mtu asiye na kosa haijuzu Kisharia.

[31] - Kubaiiwa kwa kiongozi maana yake ni kuchaguliwa au kuekeana naye ahadi ya kumtii na kuwa chini ya uwongozi wake baada ya kuwa ameshachaguliwa. Lihifadhi neno hili kwani limetumika sana humu ili usije ukajiuliza na kutokufahamu.

[32] - Tazama sura ya mwisho ya kitabu hiki uone maelezo juu ya Masahaba wa Nahrawaan.

Mfano mwengine utaupata katika maneno ya watu kwamba, fulani na fulani ni wabaya kwa sababu wamejitenga na Abu Musa Al-Ash'ari. Atayekwambia hivyo, nawe muulize: "Ubaya wa fulani na fulani kwa kujitenga kwao na Abu Musa ni kwa sababu yeye ni Abu Musa au kwa sababu Abu Musa hana kosa la Kisharia la kuwa watu wajitenge naye, na kwa hivyo lingepatikana kosa, fulani na fulani wasingelikuwa wabaya?" Nadhani jawabu yake itakuwa: "Ni kwa sababu yeye hana kosa la Kisharia la kuwa watu wajitenge naye". Akikwambia hivyo, mwambiye: "Kwa hivyo, madamu yeye hana kosa la Kisharia la kuwa watu wajitenge naye, kwa maana hio waliojitenga naye wametenda dhambi kubwa na ni madhalimu, kwani kujitenga na Muislamu pasina kutenda kosa kubwa ni dhambi kubwa?" Atakwambia: "Ndiyo". Mwambiye: "Kwa hivyo, Al-Imamu Ali bin Abi Talib kafanya dhambi kubwa na kwa hivyo ni dhalimu kwa kujitenga naye".[33] Atakwambia: "Aa yeye hakufanya kosa na wala si dhalimu!" Sasa vipi fulani na fulani wamekuwa wabaya kwa kosa la kuiba lakini mwengine asiwe mbaya kwa kosa hilo hilo la kuiba au katika Uislamu kuna hukumu tafauti: hizi za wanyonge na walalahoi na zile za wakuu na waheshimiwa? Basi hivi ndivyo zilivyo akili za watu wengi na ndio njia ya uchambuzi inayofuatwa na watu wengi: kitu kile kile akikifanya mtu wanayempinga ni kosa na ni haramu; na akikifanya mtu wanayemkubali si kosa na ni halali – uadilifu katika uchambuzi ni ugonjwa na tatizo sugu kwa wasomi wa Umma huu, na kwa hivyo siku zote watu wanafikia natija zisizo sahihi.

Mfano mwengine utaupata katika msimamo wa wafuasi wa Banii Umayya waliokuwa Al-Andalus (Spain). Wao walikuwa hawaukubali

---

33 - Anasimulia Al-Baladhiri kwa *sanad* dhaifu kwamba Ali alisema baada hukumu iliofanywa na Abu Musa na Amru bin Al-'Aas: "Basi Allah kajitenga nao (kawachukia) na Mtume wake na Waislamu wema (pia wamejitenga nao)". Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 140. Kwa hali yoyote ile hali inaonesha kwamba baada ya tokeo hilo uhusiano wa Ali na Abu Musa ulizidi kuharibika, nao tangu mwanzo walikuwa na uhusiano dhaifu. Pia ni kuwa vitabu vyote vya historia vinakubaliana kwamba Ali – baada ya hukumu hio – aliwaambia Watu wa Nahrawaan (r.a.) kwamba: "Waamuzi wawili wamekwenda kinyume na hukumu ya Qur-ani" na kwa hivyo hakuna cha ajabu kuwa Ali aseme: "Basi Allah kajitenga nao (kawachukia) na Mtume wake na Waislamu wema", kwani mwenye kwenda kinyume na Qur-ani "Allah, Mtume wake na Waislamu wema wanajitenga naye (wanamchukia)".

Ukhalifa wa Ali bin Abi Talib, na walikuwa wakisema kwamba Ali hakuwa Khalifa kwani hawakukubaliana watu wote juu ya Ukhalifa wake. Na kwa hivyo, katika hutuba za Ijumaa walikuwa wakiwaombea dua Abu Bakr, Umar, Uthman na Mu'awiya. Walikuwa wakisema kwamba Mu'awiya ndiye Khalifa wa nne kwani watu walimkubali baada ya kufanyika kwa sulhu baina yake na Al-Hasan bin Ali! Sasa jiulize wewe kwani Al-Hasan bin Ali ndio Umma mzima! Je Al-Hasan mwenyewe baada ya kufanya hivyo si ndiye ambaye watu walimchukia na kumtukana[34] na kujitenga naye na wakimwita "Ewe mwenye kuwadhalilisha Waislamu"[35] na wengine – alipokwenda Madina yeye na ndugu yake, Al-Husain – wakamwambia: "Ewe mwenye kuwadhalilisha Waarabu"?[36] Sasa cha ajabu – ninachotaka kukieleza hapa – si hicho; cha ajabu ni kuwa baada ya wafuasi wa Banii Umayya waliokuwa Al-Andalus (Spain) kuwa na msimamo huo, Al-Imamu Ahmad bin Hanbal alisema: "Aliyekuwa hakumfanya Ali kuwa ni mtu wa nne (katika dua ya Ijumaa) basi ni mpotovu kuliko punda wa wenyewe".[37] Na akafuatiwa na Ibn Taymiyya kwamba: "Atakayeuponda Ukhalifa wa mmoja katika (Makhalifa) hawa (wanne), basi ni mpotovu kuliko punda wa wenyewe".[38] Sasa kama ni hivyo, suali ni kuwa Al-Imamu Ahmad na Sheikh Al-Islam, Ibn Taymiyya munasemaje kuhusu Talha, Zubair na Mu'awiya ni wapotovu kuliko punda na hasa hasa Mu'awiya ambaye yeye alikuwa akimlaani Ali? Al-Imamu Ahmad haoni kwamba hawa ni wapotovu kuliko punda nao hawakumkubali Ali, lakini anawaona wafuasi wao waliokuwa Spain kuwa ni wapotofu kuliko punda ilhali wafuasi hao wamewafuata viongozi hawa! Halkadhalika Ibn Taymiyya: naye haoni kwamba hawa ni wapotofu kuliko punda, bali anatutajia Talha na Zubair kuwa ni miongoni mwa waliobashiriwa Pepo![39] Tazama uchambuzi huo! Wale hawamuombei dua Ali ni wapotofu; hawa

---

34 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 293.

35 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 166. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 289.

36 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 75.

37 - Ibn Taymiyya, *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 208. Yaani punda wa kufuga. Kasema hivyo, kwa sababu – katika nchi za Kiarabu hasa – kuna punda wengi huwa hawana mwenyewe wanazunguka zunguka tu katika miji na majangwa.

38 - Ibn Taymiyya, *Al-Aqidatu Al-Wasatiyya* uk. 26.

39 - Ibn Taymiyya, *Al-Aqidatu Al-Wasatiyya* uk. 2. Hakuwataja kwa majina lakini kashuhudia kwa ujumla kwamba G. 10, waliobashiriwa Pepo ni ukweli uliothibiti.

hawamuombei dua Ali na wengine wanamlani, lakini wao ni watu wema mujtahidun na wamebashiriwa Pepo – kosa moja malipo tafauti! [40]

Na kosa jengine ambalo watu wengi huwa wanalifanya ni kuchanganya kwao baina ya hukumu za ghaibu za Mwenyezi Mungu na hukumu za dhahir za kibinaadamu. Na hili ni jambo moja muhimu kulifahamu kiundani kwa mchambuzi wa mambo kama haya. Kwa mfano utakuta Hadithi inamnukuu Mtume (s.a.w.) akisema: "Fulani ni mtu wa Peponi". Basi itakapotokea kwamba fulani huyo aliyebashiriwa Pepo katafautiana na mwengine ambaye hakubashiriwa Pepo, basi wasiojua kuyaweka mambo mwahala mwake watakwambia: "Aaa lakini fulani kabashiriwa Pepo, au ndio mjuzi zaidi" au mfano wa maneno hayo. Sasa cha kufahamu ni kuwa tunaposema kuwa katika kesi fulani mkosa ni

[40] - Na kosa hili linaendelea hadi leo hii: Shafi akichukua mtasbihi au akisoma maulidi basi kaleta bidaa katika dini; Ibn Taymiyya akisema kwamba Aina ya ulimwengu haina mwanzo au 'Arshi ndio ya mwanzo kuumbwa yeye kajitahidi na kukosea: wengine hawajitahidi na kukosea bali ni watu wa bidaa tu! Anasema Al-Albani kuhusu madai ya Ibn Taymiyya aliposema kwamba Arshi ndio ya mwanzo kuumbwa:

وفيه رد على من يقول بأن العرش هو أول مخلوق، ولا نص في ذلك عن رسول الله صلى الله عليه وسلم ، وإنما يقول به من قاله كابن تيمية وغيره – استنباطا واجتهادا فالأخذ بهذا الحديث - وفي معناه أحاديث أخرى - أولى لأنه نص في المسألة، ولا اجتهاد في مورد النص كما هو معلوم.

Na ndani yake (hadithi hii) kuna kuwarudi wale wenye kusema kwamba 'Arshi ndio kiumbe cha mwanzo, ilhali hakuna andiko lolote juu ya hayo kutoka kwa Mtume (s.a.w.). Bali wamesema hivyo baadhi ya watu kama Ibn Taymiyya na wengine kwa uchambuzi tu na kujitahidi. Basi kushikana na Hadithi hii, na kuna Hadithi nyengine zenye maana kama ya Hadithi hii, ni bora kwani ni andiko la wazi juu ya mas-ala haya; kwani kama inavyojulikana kwamba hakuna kufanya ijtihad pale penye andiko. Tazama Al-Abani, *Al-Sahiha* j. 1, uk. 258, Hadithi na. 133. Sasa maneno hayo hayo alioyasema Ibn Taymiyya lau aliyasema mtu wa madhehebu mengine, basi kiama kingelimsimamia, na angelikuwa mtu wa bidaa. Tazama pia katika kitabu hicho hicho ukurasa huo huo, utaona Al-Albani anamrudi Ibn Taymiyya kuhusu suala la kutangulia kwa Aina ya ulimwengu, lakini hakumkafirisha wala hakumtolea maneno makali, wakati kitu kama hicho lau walikisema wengine wangelikuwa makafiri waliotoka katika Umma, kama vile wenye kusema kuwa Allah hauonekani au Qur-ani ni kiumbe wanavyoitwa makafiri! Bali wengine waliosema kuwa Allah kaiumba Nafsi yake kutoka katika jasho la farasi, na waliosema kuwa Allah kaonekana juu ya mti ana vazi la sufu na viatu si watu wa bidaa bali ni *Ahlu Sunna:* anayechukua mtasbihi ndiye mtu wa bidaa. Akili gani hii!

fulani, haina maana kuwa mkosa atakwenda motoni wala mkosewa atakwenda Peponi: haya ni mambo mawili tafauti. Kesi inawezekana ikawa baina ya Muislamu mcha Mungu na Yahudi, lakini katika kesi hio Yahudi akawa ndiye mwenye haki na kosa likawa ni la Muislamu. Kwa hivyo, katika Uislamu huwa hatumtupii kosa hilo Myahudi kwa sababu ya itikadi yake, na kuwa yeye ni mtu wa motoni, bali sisi tuna hukumu zetu za kidunia mbali, na akhera Allah ana hukumu zake mbali, yaani sisi hukumu zetu za hapa duniani ni hukumu za dhahiri tu: si za ghaib. Kwa mfano, sisi tunapomuona mtu mlevi, mwizi, anadhulumu mali na roho za watu, basi tunatakiwa tujitenge naye, yaani tusimpende mapenzi ya Kiislamu; na tunapomuona mtu ana juhudi katika uchaji basi ni wajibu wetu wa Kisharia kumpenda, na hizi ni hukumu za dhahir za kidunia. Ama akhera Allah anahukumu kwa elimu yake ya ghaib, kwani huenda ikawa yule tuliyemuona kuwa ni mchaji akawa ndiye mtu wa motoni – Allah atulinde na moto – kwa sababu ama katika hatima yake aliharibu au kwa sababu hakuwa na ikhlas; na – kinyume chake – yule tuliyemuona kuwa ni dhalimu hatima yake huenda akatubia japo kuwa saa moja tu kabla ya kufa na Allah akaipokea toba yake na yote hayo sisi hatuyajui. Kwa hivyo, wanaoona kuwa Ali (k.w.) kakosea katika suala kadhaa, si kwamba wao wanasema kuwa yeye atakwenda motoni, au yeye si mjuzi, lakini wanasema kwamba kesi hio hukumu yake imetajwa katika Qur-ani na kwa hivyo kilichowajibu kwetu ni kuihukumu kesi kwa mujibu wa Qur-ani na kila mwenye haki kumpa haki yake; na hukumu za akhera anazijua Muumba (S.W.).

Hii ni mifano miwili mitatu inayoweza kukupa picha ya namna gani watu wenye ubinafsi wasivyoweza kufanya uchambuzi sahihi uliojengeka katika misingi ya uadilifu. Mifano iko mingi na katika kazi hii utaweza kujionea udhaifu mwingi katika uchambuzi unaofanywa na watu wengi wakiwemo wanavyuoni wakubwa. Na kwa hivyo ndio maana ninasema kwamba mtazamo mpya unahitajika katika usomaji na uchambuzi wa historia.

VITABU NILIVYOVIPITIA

Marejeo muhimu ya historia nilioyachungulia kabla ya kuandika kitabu hiki ni:1) Al-Tabari, *Taarikhu Al-Rusuli Wa Al-Muluk*. 2) Al-Baladhiri,

Ansabu Al-Ashraf. 3) Ibn A'atham, *Al-Futuh*. 4) Al-Mas'udi, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf*. 5) Al-Mas'udi, *Muruju Al-Dhahab*. 6) Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid*. 7) Ibn Sa'ad, *Al-Tabaqat*. 8) Al-Ya'aqubi *Taarikh Al-Ya'aqubi*. 9) Al-Shahrastani *Al-Milal*. 10) Ibn Hazm, *Al-Fasl*.[41] 11) Ibn Abi Al-Hadid, *Sharhu Nahji Al-Balagha*. 12) Ibn Kathir, *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya*. 13) Ibn Al-Athir, *Al-Kamil*. 14) Al-Mubarrad, *Al-Kamil*. Kitabu, *Al-Siyar* cha Al-Allama Al-Darjini. Kitabu *Al-Siyar* kilichokusanya sira na risala za wanavyuoni wa Oman wa awali (r.a.).[42] Ama vitabu vya wachambuzi – japo kuwa hapo zamani nilikuwa nikijisomea wakati mwengine maandishi ya huyu na yule lakini – kwa siku za karibu sikubahatika kujisomea isipokuwa kitabu *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* cha Sheikh Nassir Al-Sabi'i, nacho asili yake ni utafiti wa kujipatia Shahada ya Pili (Master Degree).[43] Pia nimekipitia kitabu *Al-Ibadhiyya Fii Mawkibi Al-Taarikh* na kitabu *Al-Ibadhiyya Baina Al-Firaqi Al-Islamiyya* vya Sheikh Ali Yahya Ma'amar. Ama kitabu *Al-Jawahir* cha Al-Baradi na kitabu *Al-Kashf* cha Al-Qalhati na kitabu *Al-Siyar* cha Al-Imamu Badru-ddin Al-Shammakhi, utaona kwamba vitabu hivyo nimevinukuu humu, lakini ukweli ni kuwa vitabu hivyo sikuvipata nikavisoma bali nimevinukuu kupitia kwa mtu mwengine. Kwa hivyo, popote utapoona nakala za vitabu hivyo, basi elewa kwamba ninavinukuu kupitia kwa mtu mwengine naye ni Sheikh Nassir Al-Sabi'i.

---

41 - Lakini Ibn Hazm yeye kakihusisha kitabu chake hicho na mambo ya itikadi ambazo tutazielezea kwa urefu katika juzuu nyengine za kitabu hiki *Inshaa Allah,* naye Ibn Hazm kataja mambo ya uwongo katika kitabu hicho ambayo hata watu wa barazani hawaukubali kama tutavyoona katika juzuu zijazo *Inshaa Allah*.

42 - Hivyo ni vitabu vya historia na makala. Ama vitabu vya Hadithi nimechungulia vitabu tafauti lakini maelezo juu ya vitabu vya Hadithi yatakuja *Inshaa Allaah* katika juzuu ambayo itakuwa ni mahususi kwa utafiti wa riwaya zilizopokewa kuhusu Khawarij.

43 - Sheikh Nassir Al-Sabi'i ni kijana mnyenyekevu sana hodari wa kufanya research (utafiti), hodari wa elimu ya Hadithi, hodari wa kujadiliana. Katika mtandao wa Oman wa Intaneti ambao tulikuwa tukijadiliana na Wasaudia, alikuwa akiona mtu mwenye elimu basi hutwambia akina sisi kaeni upande huyu ni mzito kidogo. Miongoni mwa hao alikuwa ni Dr. Sa'ad Ali-Humaid ambaye alikuja kwa mafamba makubwa lakini hatimae alikunja virago vyake na kumkimbia baada ya mjadala uliochukua masiku. Kitabu cha Sh. Nassir, ni research ambayo – kwa vijana wote wa Oman waliofanya research zao katika vyuo vikuu – hakuna hadi sasa aliyetoa research bora kama hio. *Allah* amzidishie nuru na ampe khatima njema *Aamin*.

Nia yangu ilikuwa ni kukielezea kila kitabu kimoja ili tuweze kujua uzuri na ubaya wa kila kitabu, lakini hatimae nikaona kuwa hilo litachukua kurasa nyingi za kitabu hiki. Na kwa hivyo, nimeona nielezee vitabu viwili tu vya historia, navyo ni: kitabu *Taarikhu Al-Rusuli Wa Al-Muluk* cha Al-Tabari, na kitabu *Al-Futuh* cha Ibn A'atham. Uamuzi wangu wa kuvihusisha vitabu hivi pasina vyengine, umetokana na ukweli kwamba *Taarikhu Al-Rusuli Wa Al-Muluk* cha Al-Tabari, ndio marejeo makuu ya waandishi wote *taqriban* wa zamani na wa sasa wa kila madhehebu. Ama kitabu *Al-Futuh* cha Ibn A'atham, nimekihusisha kwa sababu mbili. Moja: ni kuwa ni kitabu pekee katika vitabu vyote nilivyovipitia ambacho nimeona kwamba kinatoa maelezo kwa ufafanuzi mkubwa sana; na hio ni sifa njema. Ama pili: ni kustaajabishwa kwangu na Ibn A'atham jinsi anavyojiandikia mambo yasio na ukweli hata chembe! Jambo hili pia lilinipelekea kutaka kukielezea kitabu hicho japo kidogo.

KITABU *TAARIKH AL-RUSUL WA AL-MULUUK* CHA AL-IMAMU AL-TABARI

Kitabu ***Taarikhu Al-Rusuli Wa Al-Muluuk*** cha Al-Imamu Muhammad bin Jarir Al-Tabari,[44] ndio tegemeo kubwa la Wanahistoria wengi wa zamani na wa sasa. Kitabu hiki kimeelezea maudhui ya walioitwa Khawarij – kama kilivyoelezea maudhui nyengine – kwa *sanad,* ambapo mtunzi wa kitabu analielezea kila tukio moja kwa kusema nani aliyemsimulia naye kasimuliwa na nani hadi kufikia mtu wa mwisho, nao ndio uzuri wa kitabu hiki. Lakini tatizo lake ni kuwa katika maudhui hii ya walioitwa Khawarij, kuanzia vita vya Siffin, Ibn Jarir anategemea

[44] - Ibn Jarir ni mwanachuoni mkubwa sana, bingwa wa kila fani ya elimu, Imamu wa Wafasirina, imamu wa lugha, bingwa wa riwaya na mengineo, Mcha Mungu sana. Anasema Al-Dhahabi: "Alizaliwa mwaka 224 A.H. na alikuwa ni mtu adimu katika dahari kwa elimu na akili kali na kutunga vitabu vingi, macho mara chache sana yalidiriki kuona mtu mfano wake…..alikufa mwaka 310, A.H". Al-Dhahabi, *Al-Siyar* j. 11, uk. 291-301, *tarjama* na. 2696.

karibu 100% riwaya za Abu Mikhnaf(Lut bin Yahya), naye ni Shia ambaye ni dhaifu sana katika Hadithi kama wanavyuoni wa Hadithi walivyomuelezea.[45] Na kwa hivyo, mimi nimeigawa historia iliyosimuliwa na Ibn Jarir Al-Tabari katika sehemu nne: moja: ni kitu ambacho watu wote wamekubaliana kwamba kweli hivi ndivyo ilivyokuwa, kama vile tukio la kunyanyuliwa Misahafu huko Siffin au tukio la Ibn Muljam kamuua Ali. Kitu kama hiki au vitu kama hivi huwa sitazami tena aliyevisimulia kwani makubaliano ya wote peke yake yanatosha kuwa ni hoja. Pili: ni kitu ambacho wote wamekubaliana kuwa hakina ukweli. Hiki huwa hakina haja ya kukisimulia. Tatu: ni kitu ambacho wametafautiana: hawa wanadai hivi na wale wanakanusha. Kitu kama hiki huwa sitegemei tena riwaya za Abu Mikhnaf au msimulizi yeyote yule dhaifu, bali namwambia yule aliyekisema: "Lete riwaya sahihi". Nne: iwe kitu kakisema mtu mwenye kufuata kundi fulani au madhehebu fulani na kiko dhidi yake au hakiungi mkono itikadi yake au hakiwapondi makundi mengine, kitu kama hiki nakikubali kwani msimulizi huwa hana tuhuma hapa.

Lakini cha kufahamu ni kuwa Ibn Jarir – kama kawaida yake – hakusimulia kila riwaya iliyomo katika kitabu chake kwa maana kwamba

[45] - Sasa ikiwa wasimulizi wa historia katika vitabu vyote *taqriban* ni Mashia na watu wa Banii Umayya na wote hawakuwa waadilifu, je unadhani watasema haki kuhusu wapinzani wao, na hawa wote ni maadui wa hao walioitwa kuwa ni Khawarij? Na kwa sababu ya kukosekena ukweli, basi utaona kwamba maneno ya msimulizi mmoja yanagongana kama utavyoona humu. Chukua – kwa mfano – suala la kukubali sulhu.Kuna riwaya kwamba walioitwa Khawarij ndio waliokubali sulhu na kwamba Ali alikuwa hataki hilo. Maneno haya yamesemwa kwa sababu watu hao walijitenga na Ali kwa sababu alikubali kufanya sulhu, kwa hivyo riwaya inasema kwamba waliomlazimisha Ali kukubali sulhu ni wao kisha wakajitenga naye kwa sababu hio kisha wakakihisabu kitendo cha kukubali sulhu kuwa ni kosa. Riwaya nyengine inatwambia kwamba Ibn Abbaas alipokwenda kujadiliana na watu hao aliwabainishia kwamba Ali kwa kukubali sulhu hakukosea kwani "Sulhu ni kheri" kama Aya inavyosema. Sasa tazama mgongano huo! Utakaji wa sulhu unapohusishwa na hao walioitwa kuwa ni Khawarij, hufanywa hilo kuwa ni kosa nao hulaumiwa kwalo bali hata Ali mwenyewe kwa mujibu wa riwaya hizo kawalaumu kwa kosa hilo; inapokuja kuzungumziwa kwamba Ali kakubali sulhu, kitendo hicho huhalalishwa kwa Aya za Qur-ani – kesi moja; hukumu tafauti! Sasa nani aliyetaka sulhu na je sulhu ni bora au si bora? Ni wazi kwamba watu walikuwa wakijitungia maneno tu ili kutaka kumtia fulani katika kosa na kumtoa fulani katika kosa na walikuwa wakitazama – na hadi leo wanatazama – nani kasema badala ya kutazama nini kimesemwa!

hio ni riwaya sahihi, bali yeye kawatwika majukumu ya riwaya hizo wale waliomsimulia. Anasema:

> Chochote kilichomo katika kitabu chetu hiki kuhusu habari tulizozitaja za baadhi ya watu waliopita ambazo msomaji anaziona kuwa ni habari *munkar* au msikilizaji anaona kuwa ni (habari) mbaya kwa ajili ya kuwa hakuona kuwa zina muelekeo wa usahihi wala hazina ukweli, basi na-ajue kwamba (habari) hizo hazitoki kwetu, bali zimetokana na baadhi ya waliotunukulia na hakika ya sisi tumezifikisha tu kwa namna tulivyoletewa.[46]

Kwa maana hii, Ibn Jarir kajitoa katika jukumu la usahihi wa baadhi ya riwaya zilizomo katika kitabu chake, na kwa hivyo**,** hakuna maana ya watu kutegemea kila kilichomo katika kitabu cha Ibn Jarir bali inavyotakiwa ni kuwa wazichunge riwaya hizo kwa chungio la *minhaj (methodology)* inayokubalika kielimu.

KITABU *AL-FUTUH* CHA IBN A'ATHAM

Kitabu ***Al-Futuh*** cha Ibn A'atham Al-Kufi, ndio kitabu pekee – katika vitabu nilivyovipitia – ambacho nimeona kuwa kinaeleza kila kitu kwa ufafanuzi, ambapo muandishi wa kitabu hicho ameelezea kila tukio moja kwa kunukuu maneno waliyokuwa wakijibizana na barua walizokuwa wakipelekeana na mashairi waliyokuwa wakiyatoa na kila kitu kwa ufafanuzi. Lakini – yeye tafauti na Ibn Jarir – hakutoa *sanad* yoyote.[47] Na kwa hivyo, Sheikh Al-Sabi'i anasema kwamba kitabu cha Ibn A'atham "Ni (kitabu cha) historia kilichokaa kama (kitabu cha) visa

---

46 - Ibn Jarir Al-Tabari, *Taarikh Al-Rusul Wa Al-Muluuk* j. 1, uk. 24, katika*Khutbatu Al-Kitab.*

47 - Isipokuwa katika j. 4, uk. 36-37, kataja *sanad* kisha akaeleza matokeo mengi. Dhahir ni kuwa matokeo yote hayo yanategemea *sanad* hio. Nayo ni *sanad* ya Abu Mikhnaf, Lut bin Yahya Al-Azdi, naye ni dhaifu sana. Na katika j. 2, uk. 147-149, kakusanya idadi ya *sanad* sita kwa pamoja na ya saba akaitaja bila ya ufafanuzi akisema kwa ujumla tu kwamba "Na wengine wasiokuwa hawa". Kisha akaeleza matokeo mengi, dhahir – kama tulivyosema kabla – ni kuwa matokeo yote yaliofuata baada ya hapo yanategemea *sanad* hio. Jambo hili linatufanya tusijue *sanad* gani iliotumika katika masimulizi ya kila tokeo moja. Na juu ya yote hayo, *sanad* zote hizo alizozitegemea ni zenye mushkila mkubwa.

(hekaya au paukwa pakawa)".[48] Na kilicho wazi kabisa katika historia yake, ni kwamba Ibn A'atham hakuwa mwenye kujichaguliwa riwaya sahihi katika utunzi wa kitabu chake. Na kwa sababu yeye ni mtu wa Al-Kufa na aliishi miaka mingi baada ya matukio ya vita vya Siffin na Nahrawaan ni wazi kwamba kiasi fulani alitegemea masimulizi ya riwaya za watu wa Al-Kufa, na watu wa Al-Kufa ni Mashia nao hawakuwa wenye uaminifu katika riwaya kama ilivyowazi katika vitabu vyao.[49] Na kwa sababu hii, watu wamemuona Ibn A'atham kuwa ni Sunni mwenye kumili katika Ushia kama Sheikh Al-Sabi'i alivyomnukuu Shakir Mustafaa akisema hivyo katika kitabu chake *Al-Taarikh Wa Al-Muarrikhun*[50] na Faruq Umar katika kitabu chake *Tabi'atu Al-Da'awa Al-'Abbaasiyya.*[51] Na hili la Ibn A'atham kumili katika Ushia liko wazi

---

48 - Al-Sabi'i, *Al-Khawarij Wal-Haqiqtu Al-Ghaiba* uk. 47-48. Kwa hakika kitabu cha Ibn A'atham ni paukwa pakawa. Ukichanganya kwamba mambo mengi anayaeleza tafauti na wanahistoria wengine na anazidisha mambo mengi ya ajabu. Kama mjadala wa Abdullahi bin Wahb Al-Rasibi (r.a.) na Abdillahi bin Abi 'Aqb, ambao ni upuuzi mtupu: eti Abdullahi bin Wahb kamuuliza Abdillahi bin Abi 'Aqb masuala ya sala na zaka kisha akaanza kumuuliza ule upuuzi tunaosimuliana barazani: "Niambie mmoja asiyekuwa na wapili; wawili wasiokuwa na watatu; watutu wasiokuwa na wanne". Hivi kweli mwanafunzi wa leo anaweza kupoteza wakati wake kujadili upuuzi huu, basi vipi itakuwa Abdullah bin Wahb aliyesifika kwa elimu na ucha Mungu katika zama za Masahaba. Tazama Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 108-119. Lakini dhahir ni kuwa uwongo huu umetungwa huko Al-Kufa ili kuonesha kwamba watu hawa walikuwa vichwa vitupu: si watu wa elimu, ndio maana baada ya Abdillahi bin Wahb kuuliza hivyo – kwa mujibu wa riwaya hio ya kutunga – muulizwaji alisema: "Subhana Allah! Aliyekusanya mkusanyiko huu na akatoka dhidi ya mtu kama Ali bin Abi Talib naye anajua kuwa ndiye kadhi kuliko wote na mjuzi wao wa halali na haramu anamuuliza mjumbe wake masuala kama haya!" Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 116. Halafu katika uk. 117 akasema kumwambia Hurqus bin Zuhair: "Na mimi nakuuliza masuali yangu ambayo (kwetu) huulizana watoto wetu", akauliza masuala yake lakini Hurqus na wenzake wote wakashindwa kuyajibu! Yote haya ni uwongo wa kutaka kuonesha kwamba watu wa Nahrawaan (r.a) hawakuwa na elimu. Bali katika riwaya hii kuna mambo ambayo hayakubaliki hata kwa Shia na Sunni.

49 - Vitabu vya riwaya vya Shia – kama alivyosema Dr. Musa Al-Musawi – ni masikitiko makubwa. Mimi binafsi nilikuwa na hamu kubwa ya kutaka kujua riwaya zilizomo ndani ya vitabu vyao ili nijipatie faida, lakini hatimae nilichoshwa na kukata tamaa kwa jinsi riwaya za kutunga zilivyokithiri, na nikaona ni kupoteza wakati kwa kitu kisichonipatia faida katika dini yangu!

50 - Shakir Mustafaa, *Al-Taarikh Wa Al-Muarrikhun* j. 2, uk. 43.

51 - Faruq Umar ,*Tabi'atu Al-Da'awa Al-'Abbaasiyya* uk. 33.

katika kitabu chake ambapo utaona – kwa mfano – ananukuu maneno ya Ali akisema:

> …Na munawaacha Watu wa Mtume wenu (Ahlu Al-Bait) ambao haikupini nyinyi nafasi ya kuvutana nao wala kufarikiana nao wala kwenda kinyume nao na wala musiwalinganishe na yeyote katika Maimamu.[52]

Na anasimulia maneno ya Al-Husain bin Ali aliyomjibu Ubaidi-Lahi bin Umar bin Al-Khattab baada ya Ubaidi-Lahi bin Umar kumtaka Al-Husain amuuzulu baba yake ili wamtawalishe yeye, akasema Al-Husain: "…Mimi sitomkufuru Allah na Mtume wake na Wasii[53] wake".[54] Na pia ananukuu mashairi ya Qais bin Sa'ad bin Ubada akitoa hoja ya Uimamu wa Ali kwamba umetajwa katika Qur-ani, kisha akatoa hoja kwa Hadithi[55] isemayo: "Yule ambaye mimi ni Maula wake, basi na Ali ni Maula wake."[56] Na akanukuu mashairi ya Hujr bin Adeiy na mtu wa kabila la Yashkur wakisema kwamba Ali ni wasii wa Mtume (s.a.w.).[57] Na akanukuu maneno ya Ibn Abbaas akisema kuhusu Ali: "Naye ni binaami yake Mtume (s.a.w.) na wasii wake na waziri wake".[58]

---

52 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 29. Bila shaka hii ni riwaya ya kuundwa huko Al-Kufa.

53 - Wasii – katika itikadi ya Kishia – ni Ali, kisha wanafuata Mawasii wengine kumi na moja baada yake. Na hii ni kuwa wao wanasema kwamba Mtume (s.a.w.) kausia kuwa Ali ndio awe Khalifa baada yake. Nalo si suala lenye ukweli. Tumelizungumzia suala hilo kwa urefu katika kitabu chetu "*Ukhalifa"* na tukalizungumzia kiasi fulani katika kitabu "*Mezani Ya Haki"*. Rejea huko utazame.

54 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 57.

55 - Tazama dai lake hapa: Ali katajwa katika Qur-ani, lakini anatoa ushahidi kwa Hadithi!

56 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 61.

57 - Ibn A'atham, *Al-Futuh"* j. 4, uk. 18, na j. 3, uk. 246. Huenda ikawa sehemu inayotaja uwasii wa Ali, katika j. 3, uk. 246, ni ziada ilioundwa huko Al-Kufa kwani katika kopi nilionayo sehemu hio imetiwa katika breketi na ukiitazama ladha yake ya kilugha inatafautiana na beti zilizotangulia.

58 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 256-57. Lakini maneno haya ya Ibn Abbaas yanathibitisha kile tulichokibainisha katika kitabu chetu *Ukhalifa* kwamba uwasii wa Ali – ikiwa ni sahihi – basi haukuwa wasia wa Ukhalifa, bali ni wasia wa usimamizi wa familia yake kama riwaya nyengine zinavyosema. Tazama ukweli kwamba riwaya hii ya Ibn Abbaas inasema: "Naye ni Binaami yake Mtume (s.a.w.) na wasii wake na waziri wake" lakini inamalizikia kwa kusema: "..Na hakika ya ukhalifa ni wa yule ambaye

Na picha ya wazi ya utunzi wa Shia na fikra ya Kishia iko katika riwaya yenye maneno ya mmoja wa wafuasi wa Ali aliposema kumwambia Abdillahi bin Wahb Al-Rasibi (r.a.) wakati wa mjadala wake na Ali:

> Ewe adui wa Mungu!...Hujui kwamba wewe unazungumza na Amiri-L-Mu-uminin na Wasii wake na mteule wake na mume wa mwanawe na baba wa wajukuu wake.[59]

Ibn A'atham anasimulia pia kutoka kwa Mu'awiya akisimulia kutoka kwa Mtume (s.a.w.) kwamba kasema kumwambia Ali: "Mimi na wewe tunatokana na udongo mmoja".[60] Na akanukuu maneno ya Al-Ash'ath bin Qais akisema kwamba: "Pamoja nasi kuna Masahaba wa Mtume (s.a.w.)…na binaami yake na mrithi wa elimu yake".[61] Na akanukuu maneno ya Ibn Umar (r.a.) akimwambia Al-Husain bin Ali: "Wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwa amjaaliye mjukuu wa Mtume wake kuwa awe katika makosa".[62] Cha ajabu kuliko yote yaliyotajwa na Ibn A'atham ni kisa cha mwanamke aitwaye Sauda bint Ammara Al-Hamdhaniyya na Mu'awiya bin Abi Sufyaan, ambapo bibi huyo anasema kwamba alikwenda kwa Ali akamkuta anasali alipomuona basi Ali aliikata sala akaja kumuuliza haja yake![63] Jamani huyu Ali alikuwa hajui kusali? Baada ya haya utaona kwa uwazi kwamba Ibn A'atham katika uandishi wake alijiokotea riwaya kadha wa kadha zilizokuwa zimezagaa katika uwanja wa mji wake wa Al-Kufa – mji wa Mashia

---

kafanyiwa shura". Kwa hivyo, tukisema kwamba wasia huu ni wasia wa ukhalifa basi riwaya hii itakuwa inajigonga yenyewe kwa yenyewe ambapo mwanzo wake inathibitisha wasia na mwisho wake inathibitisha shura nayo ni mambo mawili tafauti.

[59] - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 126. Maneno haya "…Na wasii wake na mteule wake na mume wa mwanawe na baba wa wajukuu wake" yanatokana na utunzi wa Shia wa Al-Kufa. Maneno *Wasii* na *mteule* ni uwongo: haikuthibiti kwa riwaya yoyote sahihi kuwa Ali ni *Wasii* au ni *mteule*. Maneno "..Na mume wa mwanawe na baba wa wajukuu wake" hayana faida yoyote katika dini kwani mazingatio si kuwa mtu kaoa mtoto wa Mtume au ni jamaa ya Mtume, bali mazingatio ni kauli ya haki inayoafikiana na Qur-ani na Sunna.

[60] - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 71.

[61] - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 74. Hakuna yeyote katika mgongo wa ardhi tangu mwanzo wa dunia hadi mwisho wake mwenye elimu au atayekuwa na elimu ya Mtume (s.a.w.), huu ni uzushi wa watu wa Al-Kufa huko Iraki.

[62] - Ibn A'atham, *Al-Futuh"*j. 5, uk. 41-42.

[63] - Ibn A'atham, *Al-Futuh"*j. 3, uk. 92.

uliokuwa maarufu kwa utunzi wa Hadithi. Na juu ya yote hayo, hakuna hata riwaya moja anayotupa *sanad* yake tukajua alipoitoa![64] Na kwa hivyo, kama tulivyosema kwamba wako wanaomuona Ibn A'atham kuwa ni mwenye kumili katika Ushia,[65] na wengine wanamuona kuwa anakusudia kuandika makosa, kama alivyosema aliyetia maelezo kitabu chake. Mfano wa haya ni pale alipotaja tukio la uandishi wa mkataba baina ya Ali na Mu'awiya ambapo muandishi wa Ali katika mkataba huo aliandika kuwa Ali ni "Kiongozi wa Waislamu", basi Mu'awiya akawa hayakukubalika kwake maneno yasemayo kuwa "Ali ni kiongozi wa Waislamu". Basi Ali akatoa mfano wa Sulhu ya Hudaibiyah iliyofanyika baina ya Mtume (s.a.w.) na makafiri wa Makka ambapo mmoja wa makafiri wa Makka aitwaye Suhail bin Amri alikataa kuandikwa "Muhammad, Mjumbe wa Allah" na akataka liandikwe jina la "Muhammad bin Abdillah" tu. Basi Ibn A'atham kakipotoa kisa hiki na akasema kwamba aliyetaka jina hilo lifutwe ni Abu Sufyaan, baba yake Mu'awiya, na akasema kuwa Mtume (s.a.w.) kasema kumwambia Ali: "Wewe una siku kama yangu; mimi naandika kwa baba (zao) nawe utaandika kwa watoto (wao)". Na huu – dhahir – ni upotoshaji wa kusudi wa historia.[66] Jambo jengine ni kuwa *taqriban* historia nzima ya Ibn A'atham inazungumzia kuwa Ali na jeshi lake ndio waliokuwa wakiua na kushinda kila siku katika vita vya Siffin. Na hii ni tafauti na wasimulizi wengine ambao wamekuwa wakieleza kuwa mara akishinda huyu; mara akishinda yule na mara nyengine wakitoka sare, ingawa wote wanaonesha kuwa mara nyingi zaidi ushindi ulikuwa ukenda kwa Ali. Kwa hivyo, minhaji yangu katika kuisoma na kuinukuu historia ya Ibn

64 - Isipokuwa kwa namna ile tulioielezea kabla ya kuzikusanya *sanad* kisha akatoa maelezo marefu.

65 - Kama tulivyonukuu maneno ya Shakir Mustafaa na Faruq Umar kupitia kwa Sheikh Al-Sabi'i.

66 - Na mfano wa hili ni kama tukio la Ubaidillahi bin Ziyaad aliposimama akasema: "Nitamtia mkononi asiyekuwa na hatia yoyote kwa (maslahi au kwa kumlinda na kumtetea) mwenye hatia". Hapa alisimama Abu Bilal Mirdas (r.a.), miongoni mwa waliobaki katika Watu wa Nahrawaan (r.a.), akamwamba: "Allah anasema: '(Nafsi) haibebi mzigo wa (nafsi) nyengine". Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 5, uk. 189. Al-Darjini. *Al-Tabaqat* j. 2, uk. 215. Al-Mubarrad. *Al-Kamil* j. 2, uk. 607. Basi Ibn A'atham kalibadilisha jina la aliyesema hivyo, na badala yake akasema kuwa aliyeyasema hayo ni: "Mtu aitwaye Asad bin Abdillah Al-Muri. Tazama Ibn A'atham. *Al-Futuh* j. 5, uk. 67. Dhahir ni kuwa kafanya upotoshaji huo kwa sababu hii ni sifa njema anaona tabu kumpa sifa hio mtu katika watu wa Nahrawaan, kwa hivyo kaona bora abadilishe jina!

A’atham, ni kutegemea kile alichokubaliana na wengine japo kimaana; hata kama ni katika riwaya moja; au kuinukuu riwaya na kuitolea muelekeo wake na maana yake pindipo tukijaalia tu kuwa hio ni riwaya sahihi.

Ahsante
Ndugu yenu
Juma Muhammad Rashid Al-Mazrui

SURA YA KWANZA

MAANA YA *AL-KHAWARIJ* KILUGHA (LITERALLY) NA KITAALAMU (TECHNICALLY)

Maudhui ya *Khawarij* – kama munavyojua – ni ngoma ambayo mshindo wake umeenea katika ndimi za wanavyuoni na watu wa kawaida. Lakini usistaajabu kuona kwamba hata msomi akashindwa kukupa ufafanuzi wa neno *Khawarij* licha ya kuweza kukupa ufafanuzi uliojengeka juu ya riwaya sahihi. Kwa leo watu wanapolitamka neno hili, aghlabu hukusudiwa wafuasi wa madhehebu ya Kiibadhi. Ukimuuuliza mtu: "Kwanini Ibadhi ni Khawarij?" Atakwambia wametoka katika kumtii Sayyidna Ali! Ukimwambia kwamba basi kwa mantiki hii Talha na Zubair na Mu'awiya ni *Khawarij,* anashindwa kukupa jibu sahihi!

Sasa kwa ufupi ni kuwa mas-ala ya Khawarij yanahitaji utafiti wa kielimu: haitoshi mtu kusema tu kuwa fulani kanena; fulani katongoa. Kwa hivyo – ili kufikia uhakika wa maudhui hii – tunahitaji kujua:

1) Nini maana ya neno *Khawarij* kilugha.[67]
2) Nini maana ya neno *Khawarij* kitaalamu.
3) Chimbuko la hao walioitwa Khawarij, na je nini hoja zao katika misingi yao waliyoshikana nayo na nini hoja za wapinzani wao.
4) Kuzitafiti Hadithi zote juu ya maudhui hii.

[67] - Hili halina umuhimu sana katika maudhui yenyewe, bali umuhimu wake ni katika kujipatia maarifa tu.

MGAWANYIKO YA NENO KHAWARIJ KATIKA ELIMU YA SARFU YA KIARABU

Kilugha neno *Khawarij* ni wingi wa neno *Kharijah*. Hiki ndio kipimo chake cha kilugha kwa mujibu wa elimu ya *Sarfu* ya Kiarabu. Lakini pamoja na yote hayo, imekuwa ni kawaida iliyozoeleka kwa wataalamu na watu wa kawaida kumwita mmoja kuwa ni *Kharijiy* na wengi kuwa ni *Khawarij,* nayo ni kinyume na kipimo cha asili cha *Sarfu* ya Kiarabu. Ilivyo ni hivi:

Mmoja	Wawili	Wengi.
Kharijiy	*Kharijiyyaani*	*Kharijiyuun.*
Kharijatun	*Kharijataani*	*Khawarij.*[68]

Kwa hivyo neno *Khawarij* ni wingi wa neno *Kharijah*[69] nalo – kilugha – linamaanisha kikundi kilichotoka, sawa ikiwa kutoka huko ni kwa haki au ni kwa batili.[70]

CHIMBUKO LA NENO *"KHAWARIJ"* KILUGHA

Ama tukija katika chimbuko la neno *Khawarij* kilugha, ni kama inavyobainishwa katika kitabu *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* cha Sheikh Nasir Al-Sabi'i, Anasema:

> (Neno) *Al-Khawarij* limechukuliwa kutokana na (neno) *Al-Khuruj* (ambalo ni) chimbuko la neno *kharaja.* Na asili hii ina migawanyiko

---

68 - Lakini tunaposema *Kharijatun* basi maana ni kikundi kimoja cha *Khawarij* na tunaposema *Kharijataani* basi maana ni vikundi viwili. Na tukisema Kharijiy ni mtu mmoja na Kharijiyyani ni Makhawarij wawili. Lakini katika kitabu hiki nitalitumia neno "Khawarij" kama ni neno la Kiswahili, na kwa hivyo inawezekana mwahala mwengine nikalitumia kumaanisha mmoja na mwahala mwengine nikalitumia kumaanisha wengi, na inawezekana sehemu nyengine wengi nikawaita "Makhawarij".

69 - Yaani ukisimama utaitamka *Kharijah* na ukiendelea utaitamka *Kharijatun* kama ilivyo katika jadueli.

70 - Ama kukihusisha kikundi cha fulani kuwa ndio khawarij, kufanya hivyo kumetokana na itikadi za waandishi wa historia na makala. Rejea Ali Yahya Ma'amar, *Al-Ibadhiyya Baina Al-Firaq* j. 2, uk. 209-213.

> mingi, Ibn Al-Faris kairejesha katika maana mbili: kukivuka kitu *(au kutoka au kupenya kutoka katika kitu),* na ya pili ni kutafautiana rangi mbili.[71]

Lakini bila ya kumbabaisha msomaji wa Kiswahili, ni kuwa maelezo hayo tuliyoyanukuu kutoka kwa Sheikh Al-Sabi'i, yanatupa chimbuko tu la kilugha la neno *Khawarij,* lakini najua kwamba msomaji wa kawaida anahitaji kuelewa kwa ufupi tu nini maana ya *Khawarij.* Kwa ufupi ni kuwa kilugha, neno *Khawarij* ukilifasiri kwa Kiswahili basi maana yake ni *"Watokaji* au *Waliotoka."* Lakini je kutoka huko ni vipi? Hapa ndipo inapotulazimu kutafuta maana ya kitaalamu ya neno hilo.

NINI MAANA YA *KHAWARIJ* KITAALAMU

Anasema Al-Shahrastani:

> Kila aliyetoka[72] dhidi ya kiongozi wa haki ambaye *Jamaa* (Walio wengi) wameafikiana juu yake basi anaitwa *Khawarij,* sawa ikiwa kutoka huko ni katika zama za Masahaba (ikawa kutoka huko ni) dhidi ya Makhalifa waongofu au ikiwa ni baada yao (ikawa kutoka huko ni) dhidi ya *Tabiina* (Wafuasi wa Masahaba) na viongozi katika kila zama.[73]

Taarifu (definition) hii ya Sheikh Al-Shahrastani – kwa kuanzia – ina vipengele viwili vya kutazamwa vinavyotokana na maneno: "Kiongozi wa haki":

Mosi: ni kuwa ima Sheikh Al-Shahrastani iwe anakusudia kwa maneno hayo: "Kiongozi wa haki," kiongozi aliyechaguliwa kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna naye anaongoza kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna na wala hajenda kinyume na chochote katika hayo wala hakujiuzulu au kuuzuliwa na *Ahlu Al-halli wa Al-'aqdi* (Wanavyuoni ambao wanastahiki kuchagua kiongozi).

---

71 - Sheikh Nasir Al-Sabi'i, *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. 151.

72 - Yaani kutoka kwa maana ya kufanya mapinduzi au jaribio la kufanya mapinduzi.

73 - Al-Shahrastani, *Al-Milalu Wa Al-Nihal* j. 1, uk. 129.

Pili: iwe makusudio ya "Kiongozi wa haki," ni kiongozi Muislamu aliyechaguliwa na Waislamu, bila kuzingatia njia aliyochaguliwa au uhalali wa kuwepo kwake kisiasa kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu.

Ikiwa makusudio yake ni ya kwanza, basi bila shaka *taarifu* yake itakuwa ni sahihi, lakini bado kuna mambo mengine ya kutazamwa:

Moja: ni kwamba ufafanuzi huo wa neno *Khawarij* unawafanya Masahaba kadhaa wa kadhaa ambao kwa mtazamo wa Waislamu walio wengi si *Khawarij*, kuwa nao ni katika *Khawarij*. Mifano miwili mashuhuri, ni tukio la vita vya *Jamal* na vita vya *Siffin***.** Vita vya *Jamal* ni vita vilivyopiganwa baina ya Sayyidna Ali (k.w.) na wafuasi wake kwa upande mmoja (baada ya kuwa *ameshabaiiwa* kuwa Khalifa wa Waislamu) na Masahaba wawili: Talha na Zubair na wafuasi wao wakiungwa mkono na Sayyidat Aisha (r.a.)[74] kwa upande wa pili. Vita hivi vilitokea mwezi wa mfunguo nane[75] mwaka wa 36 A.H. katika mji wa Al-Khuraiba huko Basra (Iraki).[76] Ama vita vya *Siffin*, ni vita vilivyopiganwa mwaka wa 37 A.H.[77] baina ya Sayyidna Ali (k.w.) na jeshi lake kwa upande mmoja na Sahaba Mu'awiya bin Abi Sufyaan na jeshi lake kwa upande wa pili. Pia katika vita hivi, Mu'awiya na jeshi lake walimpiga vita Al-Imamu Ali (k.w.) baada ya kuwa ameshachaguliwa kuwa Khalifa wa Waislamu kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna.

Kwa hivyo, utaona kwamba kwa mujibu wa *Taarifu* (Definition) au ufafanuzi huo uliotolewa na Sheikh Al-Shahrastani, Waislamu wengi waliopo leo duniani ni *Khawarij:* Sunni – kwa mujibu wa *Taarifu* hio – watakuwa ni *Khawarij* kwani wao – katika migawanyiko hio ya awali –

---

74 - Usije ukaniuliza: "Mbona Aisha yeye unamuombea radhi za Allah ilhali naye kaingia katika kupigana na Imamu wa haki na wewe umesema kuwa tuwe waadilifu?" Basi elewa kwamba kumuombea dua Al-Sayyidat Aisha si kwa sababu yeye ni Aisha au kwa sababu yeye ni mke wa Mtume (s.a.w.), bali ni kwa sababu riwaya zinaeleza kwamba yeye alijuta na kutubia kuungana na Talha na Zubair. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kumpenda na kumuombea dua.

75 - Na kauli nyengine ni kuwa vita hivyo vilipiganwa mfunguo tisa. Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 35.

76 - Al-Ya'aqubi, *Taarikh Al-Ya'aqubi"*j. 2, uk. 182.

77 - Al-Bukhari, "*Al-Taarikh Al-Awsat"* j. 1, uk. 175, *tarjama* na. 263.

walikuwa ni wafuasi wa Mu'awiya bin Abi Sufyaan,[78] naye kamuasi kiongozi wa Waislamu;[79] na Ibadhi nao watakuwa ni *Khawarij* kwani wao – katika migawanyiko hio ya awali – ni wafuasi wa *Ahlu Al-Nahrawaan*

[78] - Watawala wa Banii Umayya walikuwa wakijiita "Ahlu Sunna Wal Jama'a". Tazama barua ya Ubaidillahi bin Ziyad, katika *Al-Futuh* j. 5, uk. 108. Kisha wafuasi wao wakalirithi jina hilo, nalo ni jina zuri na ndani yake kuna watu wazuri, wakweli na wacha Mungu, lakini waasisi wa jina hilo hawakuwa watu wema wala hawakulianzisha jina hilo kwa wema bali ni katika jumla ya propaganda zao za kisiasa kwa kujiita wao majina mazuri na kuwaita wapinzani wao "Khawarij" wakati uhakika ni kuwa wao ndio waliokuwa Khawarij na aghlabu ya walioitwa Khawarij uhakika wao ndio "Ahlu Sunna". Anasema Sh. Ali Yahya Ma'amar akimnukuu Al-Shammakhi: "Hakika jina "Ahlu Sunna wal Jama'a" lilikuwa likitumiwa na Mu'awiya bin Abi Sufyaan na wafuasi wake, kwa sababu waliukanusha uimamu wa Ali bin Abi Talib na wakafanya (kule) kumtukana na kumlaani katika membari kuwa ni sunna yenye kufuatwa, basi wakawaita wale walioafikiana nao kuwa ni "Ahlu Sunna Wal Jama'a". Tazama kitabu cha Ali Yahya, *Al-Ibadhiyya Fii Mawkib Al-Taarikh* uk. 135. Na Al-Salimi, *Sharhu Jami'i Al-Sahih* j. 1, uk. 59. Kisha Sh. Ali akanukuu maneno ya wanavyuoni wa Kisuni kama inavyofuata: "Anasema Al-Mas'udi: 'Hakika ya wafuasi wa Mu'awiya kumtii yeye kuliwafikisha daraja ya kufanya kumlani Ali (bin Abi Talib) kuwa ni sunna; mdogo hukuwa juu ya (sunna) hio na mkubwa anakufa juu ya (sunna) hio, (akawa Mu'awiya) anamlani (Ali) katika membari". Tazama Ali Yahya,*Al-Ibadhiyya Fii Mawkib Al-Taarik"h* uk. 136. Anasema Al-Hakim: "Na kwa hakika jina la usuni lilipata nguvu kwao, kwa sababu Mu'awiya alipoamrisha kumlani Ali bin Abi Talib, alidai kuwa hio ni sunna, basi kila aliyekuwa akiona kuwa uimamu wa Mu'awiya (ni haki) akastahiki jina hilo mpaka (Ali) akauliwa na jambo (la ukhalifa) likatulia kwa Mu'awiya na watu wote wakamfuata yeye, basi wakazidisha jina "Jama'a' juu ya (neno) "Suuna" (ikawa Al-sunna wa Al-jama'a) wakajiita hivyo (Ahlu Sunna Wal Jama'a)". Tazama Ali Yahya, *Al-Ibadhiyya Fii Mawkib Al-Taarikh* uk. 136. Na kwa hivyo, Sheikh Ali Yahya anaishia kwa kutwambia: "Na kutokana na haya, inatubainikia kwamba neno "Ahlu Sunna Wal Jama'a" halikutumika kwa madhehebu ya kidini, bali limetumika katika madhehebu ya kisiasa ambayo yakilinganiwa na Banii Umayya" ili kuhodhi utawala kutoka kwa Banii Hashim. Na madhehebu hii (ya kisiasa ya Mu'awiya) iliojiita jina lenye kupendeza kwa Waislamu, basi (imekuwa ndio) imepindukia mpaka ambao hakuufika yeyote kwa kadiri ninavyojua katika matokeo ya historia nilioyaona..". Tazama Ali Yahya, *Al-Ibadhiyya Fii Mawkib Al-Taarikh"*uk. 136. Tukirudi katika maneno kwamba "Na kutokana na haya, inatubainikia kwamba neno "Ahlu Sunna Wal Jama'a" halikutumika kwa madhehebu ya kidini, bali limetumika katika madhehebu ya kisiasa", **Ninasema:** ukweli ni kuwa majina yote makuu ya kimadhehebu – Ahlu Sunna, Shia, Ibadhi au Khawarij – yote haya – waliojipa na waliopewa – ni majina yaliotokana na harakati za kisiasa japo kuwa nyengine zilikuwa ni siasa za kidunia tu na nyengine ni siasa za kidini.

[79] - Hili halina khilafu.

(Watu wa Nahrawaan (r.a.)) ambao walijitenga na Sayyidna Ali (k.w.) na wafuasi wake.

Pili: ni kuwa Watu wa Nahrawaan – na kwa hivyo Ibadhi – wao kinachowaombea – katika kuingia katika *taarifu* hio – ni ukweli kwamba wao walipojitenga na Ali, Ali hakuwa tena Khalifa wa Waislamu kwa mujibu wa Sharia, kama tutakavyoeleza hoja zao baadae juu ya suala hilo *in shaa Allah*. Na kwa hivyo, katika *taarifu* hio wanaingia Talha, Zubair, Mu'awiya na wafuasi wao. Lakini suali ni kuwa je kweli hivyo ndivyo alivyokusudia Al-Shahrastani kwa *taarifu* yake hio? Ikiwa hakukusudia hivyo, basi elewa kwamba taarifu yake bado ni kitu cha kufikiriwa upya.

Ama maana ya pili inayopatikana kutoka katika *taarifu* ya Sheikh Al-Shahrastani, ni – kama tulivyosema – kuwa iwe makusudio ya "Kiongozi wa Haki," ni kiongozi Muislamu aliyechaguliwa na Waislamu, bila kuzingatia njia aliyochaguliwa au uhalali wa kuwepo kwake kisiasa kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu. Lakini *taarifu* hii – kama unavyoona – haimtoi Muislamu yeyote duniani kutoka katika ukhawarij. Ama Sunni na Ibadhi, ni kama ulivyoona kwamba watangulizi wao walitoka katika kumtii Ali bin Abi Talib; ama Shia wao nao watakuwa ni *Khawarij* kwani Imamu wao Sayyidna Al-Hasan alitoka dhidi ya Mu'awiya bin Abi Sufyaan.[80] Na Sayyidna Al-Husain bin Ali alitoka dhidi ya watawala wa Banii Umayya, na akamtuma Muslim bin 'Aqil kwenda Iraki ili kuwataka watu wambaii yeye Al-Husain kuwa ndiye Khalifa.[81]

Kwa hivyo, utaona kwamba wanavyuoni wengine wameona kwamba watoe sababu tu ya kwanini *Khawarij* wameitwa *Khawarij*. Anasema Al-

[80] - Ibn A'atham, *Al-Futu j.* 4, uk. 153-157. Lakini Al-Hasan katika jaribio hili alighairi njiani na Mashia wake wakakasirika wakamchania nguo zake na kumnyanganya aliokuwa nayo, na wakatawanyika wakamuacha peke yake akarudi na njiani akapigwa akaumizwa katika paja lake! Ibn A'atham, *Al-Futuh j.* 4, uk. 155. Al-Ya'aqubi,*Taarikh Al-Ya'aqubi"* j. 2, uk. 215. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 73.

[81] - Tazama Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 5, uk. 26-222.

Imamu Al-Hafidh Ibn Hajar katika *Al-Fat-hu*[82] na akafuatwa na Al-Imamu Al-Shaukani katika *Sharhu Al-Nayl*:[83]

> Al-Khawarij ni wingi wa (neno) Kharija yaani ni kikundi; wameitwa hivyo kwa sababu ya kutoka kwao katika dini,[84] (na) kuleta kwao bidaa.[85]

Lakini na *Taarifu* (Definition) hii pia – kama unavyoona, chambilecho watu wa elimu ya misingi ya Falsafa *"It is not a normative definition,"* yaani si taarifu pambanuzi au si yenye kujenga misingi; kwani inamfanya kila aliyetoka katika dini ya Kiislamu – akiwa Yahudi, Kiristo, Pagani, Komredi n.k. – kuwa ni *Khawarij,* na bila shaka hili si lengo la yeyote yule anayelitamka au kuliandika neno *Khawarij*. Kwa hivyo, utaona bado tuna tatizo la kuweza kutoa *Taarifu* (Definition) pambanuzi inayotoa vigezo na kanuni zitakazomuwezesha kila mtu kujua sifa za *Khawarij* ambazo kwazo tutaweza kumjua *Khawarij* ni nani. Sababu ya kutokuwepo huko kwa *Taarifu* (Definition) pambanuzi, kunarejea katika ukweli kwamba sifa zote au nyingi ya sifa zilizotajwa kuwa ni sifa za *Khawarij* wamesifika nazo pia Waislamu wa madhehebu nyengine zote. Na kwa hivyo, baada ya kujitupa huku na kule na kuzamia katika bahari ya elimu yenye kina kirefu, Sheikh Nassir Al-Sabi'i ana hiki cha kutwambia:

---

82 - Ibn Hajar *Al-Fat-h"u* j. 14, uk. 8524, katika sherehe ya Hadithi na. 6930-6931-6932.

83 - Al-Shaukani, *Sharhu Al-Nayl* j. 7, uk. 164, katika sherehe ya Hadithi na. 3186-3187. Lakini Al-Shaukani baadae akanukuu maneno ya wanavyuoni tafauti yenye kuonesha kwamba si *Khawarij* wote wametoka katika haki bali wengine ni watu wa haki. Na huu ni mgongano baina ya *Taarifu (definition)* yake na maelezo hayo aliyoyanukuu kutoka kwa wanavyuoni wengine.

84 - Yaani kutoka katika dini ya Kiislamu.

85 - *Khawarij* ni kweli wametoka katika dini, lakini *Taarifu* hii inawaingiza waliokuwemo na wasiokuwemo. Pia ni kuwa baadhi ya hao wanoaitwa *Khawarij* – nao ni Ibadhi – utashindwa kuwaingiza, kwani kwa itikadi yako wao ni *Khawarij,* lakini suali ni vipi Ibadhi wametoka katika dini? Mbona munakula wavichinjavyo na munaowana nao na munasali nao na munawaachia kuingia Makka kwa Ibada za Hija, kama wametoka katika dini? Isipokuwa Abdalah Muhsin wa Tanzania na Maimamu wake wa Kiwahabi hawatopata tabu kujibu baadhi ya Masuali haya, kwani Abdallah Muhsin yeye katoa fat-wa ya kutojuzu kwa mwanamme wa Kiibadhi kumuoa mwanamke wa Kisunni! Je huu wa Abdallah Muhsin si ukhawarij? Vipi unawahukumu Waislamu kwa hukumu za washirikina?

> Ni mara chache sana hupatikana aliyeweka Taarifu ya neno Khawarij, (Taarifu) ambayo inawezekana kupitia katika (Taarifu) hio kuiainisha fikra maalamu kuwa ndio fikra ya Khawarij. Na sababu ya tatizo lililopo katika jambo hili, ni mfungamano uliopo baina ya Khawarij – kwa kuwazingatia kuwa ni kikundi (maalumu) – na baina ya Hadithi walizohusishwa nazo, kwa sababu sifa na vihusisho ambavyo vinahisabiwa kuwa kama ni vipambanuzi vya Khawarij…..haviishii kwao tu (Khawarij), bali tunakuta wasiokuwa wao pia wako wanaosifika navyo au na baadhi yake. [86]

Kwa sababu ya kutokuwepo *Taarifu* moja yenye kuonesha sifa halisi ya *Khawarij*, wengi wa waliozungumzia suala hili huwa moja kwa moja wanakurupuka na kufikia katika maamuzi – ama kwa haki au kwa batili – kwamba watu fulani ndio *Khawarij,* na wao ndio waliokusudiwa katika Hadithi kadhaa za Mtume (s.a.w.). Cha kusikitisha – kama tulivyoashiria kabla – ni kuwa sababu zile zile ambazo zinatarajiwa kuwa ndio kigezo cha kuwazingatia watu fulani kuwa ni *Khawarij* na kupelekea Hadithi kadha hio – kwa mfano – kuhusishwa na watu hao, utaona kwamba sababu hizo hizo na ziada ziko kwa wale wenye kuwaita wenzao *Khawarij!* Lakini hawa ni *Khawarij* wale si *Khawarij!*

Miongoni mwa waliokurupuka wakaacha kutoa *Taarifu* (Definition) ya *Khawarij,* na badala yake wakatoa hukumu tu ya moja kwa moja juu ya nani ni *Khawarij,* ni Sheikh Al-Islam Ibn Taymiyyah Al-Harraani aliposema: "Al-Khawarij: (ni) walinganiaji wa mwanzo wa mtafaruku katika Uislamu". Alianza kwa anuani hio, kisha Sheikh Al-Islam akatoa maelezo haya:

> Mtafaruku wa mwanzo katika Uislamu baada ya kuuliwa Uthman na kufarikiana Waislamu, Ali na Mu'awiya walipokubaliana kufanya sulhu, *Makhawarij* wakapinga na wakasema: 'Hakuna hukumu isipokuwa ya Allah' na wakafarikiana na kundi la Waislamu…[87]

Utaona kwamba maneno haya ya Al-Imamu Ibn Taymiyya, yanatoa hukumu ya moja kwa moja juu ya nani ni *Khawarij*, nao – kwa mujibu wa maneno haya – ni wale waliojitenga na Ali baada ya kukubali kwake

[86] - Sh. Nassir Al-Sabi'i ,*Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. 152.
[87] - Al-Imamu Ibn Taymiyya, *Al-Tafsiru Al-Kabir* j. 2, uk. 8.

kufanya sulhu na Mu'awiya katika vita vya *Siffin*. Lakini – kama unavyoona – maelezo haya yanamfanya Ibn Abbaas naye kuwa ni katika *Al-Khawarij* kwani naye ni miongoni mwa waliojitenga na Ali baada ya vita hivyo.[88] Lakni Dr. Ahmad Subhi anaona kwamba:

> Kujimegua tu kutoka katika utawala wa Ali siko kunakotoa ufafanuzi wa *Khawarij*, bali (kunakotoa ufafanuzi wa Khawarij) ni kujimegua (kutoka katika utawala wa Ali) pamoja na yaliyofuata baada ya hapo ya kupigana vita na Ali.[89]

Lakini Sheikh Ali Yahya Ma'amar (r.a.) akamjibu kwa kile tulichokinena na kukikariri mara nyingi kwamba: "Talha na Zubair wamejimegua kutoka kwa Ali na wakampiga vita, je jina *Khawarij* linawafaa?"[90]

Ama dai la Al-Imamu Ibn Taymiyya kwamba: "Al-Khawarij: (ni) walinganiaji wa mwanzo wa mtafaruku katika Uislamu" ubatili wake uko wazi: hauhitaji maelezo. Waislamu wote wanajua kwamba watu wa mwanzo kuleta mtafaruku katika Uislamu ni Talha na Zubair ambao walimuasi Al-Imamu Ali na wakapigana naye vita na damu ikamwagika. Kisha akaasi Mu'awiya na sahibu yake Amru bin Al-'Aas na kundi lao la watu wa Sham dhidi ya Al-Imamu Ali, nao pia wakapigana naye vita ambavyo vilipoteza roho za maelfu ya Waislamu, Masahaba na wafuasi wao. Kwa hivyo, dai hilo la Sheikh Al-Islam, Ibn Taymiyya, ni dai ambalo halina msingi. Lakini – pamoja na kumuheshimu Ibn Taymiyya – tatizo la Ibn Taymiyya linajulikana kwamba amekuwa akimili upande wa Mu'awiya kwa kumtetea na kuwapinga wote walio dhidi yake akiwemo Ali mwenyewe, hata akawa Ibn Taymiyya – katika jawabu yake anayomjibu mwanachuni wa Kishia alioiita *Minhaju Al-Sunna* – anatafuta njia ya kuwafanya watu wawe na shaka juu ya usahihi wa Hadithi ambayo Umma umekubaliana juu ya usahihi wake, bali wanavyuoni wenye kutegemewa katika elimu ya Hadithi wamesema

---

88 - Japo yeye hakuwa pamoja na hao waliojitenga na Ali huko Harauraa, lakini alithibitisha kwamba wao ndio waliokuwa katika haki kama tutakavyonukuu riwaya yake baadae *Inshaa Allah*.

89 - Dr. Ahmad Subhi: nakala kutoka katika kitabu, *Al-Ibadhiyya Baina Al-Firaq*cha Ali Yahya Ma'amar, j. 2, uk. 213.

90 - Ali Yahya Ma'amar, *Al-Ibadhiyya Baina Al-Firaq* j. 2, uk. 214.

kuwa Hadithi hio ni Mutawatir.[91] Hadithi yenyewe ni Hadithi inayomnukuu Mtume (s.a.w.) akisema kumwambia Ammar bin Yaasir kwamba: "Ammar atauliwa na kikundi cha waasi".[92] Naye akauliwa na jeshi la Mu'awiya. Hadithi hii hata Mu'awiya mwenyewe kaikubali kuwa ni sahihi, lakini Mu'awiya akasema kwamba yeye siye aliyemuua bali waliomleta vitani ndio waliomuua! Basi utastaajabu kwamba Ibn Taymiyya alikuwa akitafuta njia ya kuidhoofisha Hadithi hii kwa sababu inamgonga Mu'awiya, lakini ikawa njia zote zimefungika na kwa hivyo akawa anajigongagonga tu na kuwatupia mizigo watu wengine wasiojulikana kwa kusema: "…Wengine[93] wameidhoofisha na wengine

---

91 - Tazama Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7, uk. 357-358, *tarjama* na. 665. Al-Qannubi *Al-Tufan* j. 3, sehemu ya pili uk. 628, na akanukuu maneno ya Ibn Al-Wazir kutoka katika kitabu *Al-'Awasim Wa Al-Qawasim* j. 2, uk. 170-171, na Al-Dhahabi, *Al-Siyar* j. 1, uk. 421.

92 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 119. Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 317-418. Ibn Al-Athir. *Al-Kamil* j. 2, uk. 663-677. Ibn Abi Shaiba *Al-Musannaf* j. 8, uk. 723, riwaya na. 15, uk. 728, riwaya na. 39-40. Al-Ya'aqubi *Taarikh Al-Ya'aqubi* j. 2, uk. 188. Muslim, *Sahihu Muslim* j. 9 katika *Sharhu Al-Nawawiy"*uk. 172-173, Hadithi na. 70_2915, na 72_2916 na 73_2916. Al-Bukhari *Sahihu Al-Bukhari* Hadithi na. 447. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 93. Tumetaja wengine walioipokea riwaya hii katika sehemu nyengine.

93 - Anasema Al-Imamu Al-Qannubi: "Hatujui nani anaowakusudia Ibn Taymiyya kwa (kusema kwake): 'Wengine'. Na yatakuja (maelezo) karibu *Inshaa Allah* kwamba zaidi ya mmoja katika wanavyuoni wameihukumu Hadithi hii kuwa ni mutawatir kutoka kwa Mtume (s.a.w.). Na anayekitafakari (kitabu cha Ibn Taymiyya) kiitwacho *Minhaju Al-Sunna* nacho kwa hakika ni *Minhaju Al-Bid'a* inambainikia kwa uwazi kwamba Ibn Taymiyya anaghushi na kufanya utatanishi (kwa kukusudia) kama kawaida yake ili amtafutiye udhuru Mu'awiya hata ukiwa ni dhaifu kama nyumba ya buibui….bali sisi hatuna uwezo wa kuthibitisha kuwepo kwa khilafu juu ya usahihi wake (kwa kutegemea maneno ya Ibn Taymiyya) kwani tumemjaribu Ibn Taymiyya tukamkuta hana ukweli katika mambo mengi aliyoyanasibisha kwa wanavyuoni na tumetaja mfano wa hayo katika mwisho wa (kitabu chetu) *Al-Saifu Al-Had* anayependa na-arejee huko". Tazama Al-Qannubi *Al-Tufan Al-Jarif* j. 3, sehemu ya pili uk. 625 katika maelezo ya chini. **Ninasema:** bali aliyemtaja Ibn Taymiyya kuwa kaikanusha Hadithi hio ni Al-Imamu Ahmad bin Hanbal lakini Ibn Taymiyya huyo huyo kasema kuwa hatimae Al-Imamu Ahmad kaikubali Hadithi hio, na yeye mwenyewe Ibn Taymiyya baada ya kutapatapa huku na kule hatimae akakubali kuwa hio ni Hadithi sahihi. Tazama Ibn Taymiyya, *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 211. Kwa hivyo, hakuna aliyeidhoofisha Hadithi hio, na ikiwa yuko basi tunamtaka atupe ushahidi wa kielimu juu ya udhaifu wake, na *Haihata Haihata* kuleta ushahidi huo: hatoweza kuleta ushahidi huo hata ngamia akipenya kwenye tundu ya sindano! Anasema Ibn Al-Wazir

wameiletea tafsiri".[94] Na akasema: "Watu wana kauli tafauti katika Hadithi ya Ammar, miongoni mwao wako walioiponda".[95] Na akasema: "Bali watu wenye elimu ya Hadithi hii wana kauli tatu. Kundi moja limeidhoofisha kwa sababu ya kupokewa kwake kwa *sanad* ambazo hazikusihi kwao!"[96] Lakini mara Ibn Taymiyya akakubali kuwa hii ni Hadithi sahihi akasema: "Na Hadithi hio ni yenye kuthibiti na ni sahihi kutoka kwa Mtume (s.a.w.)",[97] lakini akadai Ibn Taymiyya kwamba "Waliomuua ni wale walioshika silaha wakamuua":[98] si Mu'awiya! Na akasema: "Na (neno) muuaji linapotumika bila ya kufungamanishwa na kitu, basi (linamaanisha) yule aliyeua si yule aliyemuamrisha (muuaji

---

katika "*Al-'Awasim Wa Al-Qawasim"* j. 3, uk. 145 – kama alivyonukuliwa na Al-Qannubi – katika *Al-Tufan* j. 3, sehemu ya pili, uk. 628: "Hakika yake ni Hadithi iliyoafikiwa juu ya usahihi wake na umashuhuri wake katika zama hizo, na kwa hakika hakuna yeyote katika (wanavyuoni) waliotangulia aliyeiponda (Hadithi hio)".

94 - Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 208. Maneno ya Ibn Taymiyya kwamba: "Na wengine wameiletea tafsiri", tafsiri yenyewe alioitaja katika kitabu chake ni tafsiri ya Mu'awiya kwamba waliomuua Ammar ni wale waliomleta vitani! Tazama kitabu hicho uk. 208-209. Nayo ni tafsiri ambayo hata Ibn Taymiyya mwenyewe kaipinga. Tazama Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 210-211.

95 - Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna"*j. 2, uk. 204.

96 - Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 212. Ewe Sheikh wa Uislamu! Mbona hututajii majina ya hao walioidhoofisha Hadithi hio pamoja na vitabu vyao. Sisi tunahofia isiwe maneno yako haya ni kama pale ulipodai kwamba wanavyuoni wengi wa Hadithi wanasema kwamba aina ya ulimwengu ina sifa ya kutangulia! Unasema:

"وأما أكثر أهل الحديث ومن وافقهم فإنهم لا يجعلون النوع حادثا بل قديما ويفرقون بين حدوث النوع وحدوث الفرد من أفراده"

"Ama waliowengi katika watu wa Hadithi na walioafikiana nao hawaifanyi AINA kuwa ni kitu kilichozuka bali ni kitu kilichotangulia, na wanatafautisha baina ya kuzuka kwa *Aina* na kuzuka kwa sehemu za *Aina*." Tazama Ibn Taymiyya *Bayanu Muwafaqati Sarihi Al-Ma'aqul Lisahihi Al-Manquul* kilichochapishwa pembeni mwa kitabu *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk.75. Lakini Al-Qannubi katika *Al-Saif Al-Had* chapa 3, uk. 200, katoa chalenj watajwe hao wanavyuoni wa Hadithi waliosema hivyo. Na tangu chalenj hio hadi sasa imepita si chini ya miaka kumi bila ya kuona jawabu ya wafuasi wa Ibn Taymiyya juu ya maudhui hii. Kwa hivyo, sisi nakala za Sheikh wa Uislamu Ibn Taymiyya tunaziogopa mpaka tuzithibitishe. Kwa hali yoyote ile Hadithi hio ya kuuliwa kwa Ammar hata wakikusanyika binaadamu wote na majini wote basi hawana njia ya kuonesha udhaifu wake, bali ni Hadithi mutawatir. Na imepokewa na wapokezi wengi mno akiwemo Al-Bukhari na Muslim kwa *sanad* sahihi kabisa, kama tutavyoitolea marejeo baadae *Inshaa Allah.*

97 - Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 211.

98 - Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 211.

huyo kuua)".[99] Ninasema: na hii ni ajabu kubwa sana, inaonesha kwamba lau Ibn Taymiyya alikuwepo leo angelisema kwamba wanaoua watu huko Iraki si wale Maraisi na viongozi wa nchi za Magharibi pamoja na wakuu wao wa kijeshi, bali ni wale askari wanaokwenda vitani! Halkadhalika huko Palestina, wauwaji si serikali ya Israili bali ni lile jeshi linalochukua bunduki! Lakini Hadithi yeyenyewe ukiitazama utaona kwamba inamrudi Ibn Taymiyya: Hadithi inasema: **تقتله الفئة الباغية** (Atauliwa na kikundi cha waasi) na katika riwaya nyengine **تقتلك الفئة الباغية** (Utauliwa na kikundi cha waasi). Ni wazi kwamba hakusudiwi mtu mmoja au wawili bali kundi lote lile ni kundi la wenye kuasi na kwa hivyo, limeshiriki katika kumuua.

Pili: Ni kuwa wakati Sheikh Al-Islam, Ibn Taymiyya anamtetea Mu'awiya kwa nguvu zake zote kwamba siye aliyemuua Ammar, tunamkuta Mu'awiya mwenyewe anajisifu kwa hilo. Anasema : "Ali alikuwa na mikono miwili ya kuume (Wasaidizi wawili wa nguvu); mmoja nimeukata siku ya (vita vya) *Siffin*, Yaani Ammar bin Yasir, na mmoja nimeukata leo, yaani Al-Ashtar".[100] Utaona kwamba mteteaji na mtetewa wenyewe kwa wenyewe hawajakubaliana! Halkadhalika Masahaba wengi waliokuwa katika vita vya *Siffin,* ukisoma historia, utaona kuwa kosa la kuuliwa kwa Ammar ndilo lililowabainishia zaidi kujua kundi la haki na la batili. Na kwa hivyo, Sahaba Khuzaima bin Thabit[101] hakujiunga na Ali wala Mu'awiya mpaka alipouliwa Ammar akajiunga na Ali akisema: "Sasa upotovu umemfikia"[102] na katika riwaya nyengine Khuzaima bin Thabit alisema: "Sasa upotovu

---

99 - Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 212. Ningelikuwa na maelezo marefu sana kuhusu maneno haya lakini nahisi tutatoka nje ya maudhui. Lakini kwa ufupi ni kuwa je Hadithi isemayo: "Atayesaidia kwa nusu ya neno tu katika kuuliwa Muislamu basi atakuja siku ya kiama kaandikwa baina ya macho yake mawili: 'Ni mwenye kukata tamaa kutokana na rehema ya Allah". Tazama Al-Rabi'u bin Habib *Al-Jami'u Al-Sahih* uk. 368, Hadithi na. 960. Ibn Majah *Al-Sunan* uk. 444, Hadithi na. 2620. Sasa vipi Ibn Taymiyya anadai kwamba aliyeamrisha hayumo?

100 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, 133. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 705.

101 - Kuna khilafu juu ya Khuzaima bin Thabit huyu, wengine wanasema si yule "Dhu Shahadatain" na kwamba huyu kafa wakati wa Uthman. Tazama Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 582. Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 279-280, *tarjama* na. 2254.

102 - Al-Hakim *Al-Mustadrak* j. 3, uk. 435, Hadithi na. 5657.

umenibainikia",[103] na hapo Khuzaima akajiunga na Ali akapigana mpaka akauliwa.

Kwa hivyo, Sheikh Al-Islamu alikuwa anatafuta njia za kuwafanya watu wawe na shaka juu ya usahihi wa Hadithi hio iliyothibiti bila khilafu ili kumtoa Mu'awiya katika lawama. Utakapoelewa hilo, basi hutoona ajabu kwamba awachupe Talha, Zubair na Mu'awiya walioasi na kutangaza vita dhidi ya Ali, na badala yake awataje Watu wa Nahrawaan (r.a.) kuwa ndio "Walinganiaji wa mwanzo wa mtafaruku katika Uislamu!" – uadilifu katika kutoa hukumu bado ni tatizo sugu kwa Waislamu wengi!

Ama kauli ya Al-Imamu Ibn Taymiyya kwamba: "Makhawarij wakapinga na wakasema: 'Hakuna hukumu isipokuwa ya Allah' na wakafarikiana na kundi la Waislamu…", ninasema: kwani kauli hio: "Hakuna hukumu isipokuwa ya Allah" ina dhambi gani ?! Hivi katika Uislamu kuna hukumu nyengine zaidi ya Allah?[104] Hapa pia kuna riwaya kwamba Al-Imamu Ali aliposikia kauli hio ya Watu wa Nahrawaan kwamba: "Hakuna hukumu isipokuwa ya Allah" alisema (Al-Imamu Ali): "(Hilo ni) Neno la haki (lakini) limekusudiwa (kufanyiwa) batili".[105] Al-Imamu Abu Ubaida, Muslim bin Abi Karima (r.a.), Imamu wa pili wa Kiibadhi, aliposikia kauli hio ya Ali, alijibu kwamba: "Watu hao wamelinena hilo kwa ndimi zao, nini kilimjuilisha Ali kilichomo katika mioyo yao". Anachokisema Abu Ubaida ni kuwa Uislamu – katika hukumu zake za kidunia – huwa haumuhukumu mtu kwa yaliyo moyoni mwake, bali unamuhukumu kwa kauli yake au kitendo chake; sasa ikiwa watu hao wamesema kwamba "Hakuna hukumu ila ya Allah" kwa ndimi zao, kipi kimemfanya Ali awahukumu kwa yaliyo moyoni mwao? Ninasema: hata Mtume (s.a.w.) alikuwa anahukumu kwa mujibu wa maneno na matendo tu. Na kwa hivyo, Mtume (s.a.w.) alimkaripia sana Sahaba aliyemuua mtu baada ya mtu

103 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 278-279, *tarjama* na. 2253.

104 - Tutaizungumzia nukta hii mahala pake *Inshaa Allah.*

105 - Al-Ya'aqubi, *Al-Taarikh* j. 2, uk. 191. Al-Shahrastani, *Al-Milalu Wa Al-Nihal* j. 1, uk. 133. Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 17. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 685. Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, 603. Al-Baladhiri,*Al-Ansab* j. 3, uk. 126,129,135. Abdul-Razzaaq, *Al-Musannaf* j. 9, uk. 448, riwaya na. 18926. Ibn Abi Shaibah, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 741, riwaya na. 50. Al-Bayhaqi:, *Al-Kubra* j. 12, uk. 325, riwaya 17168.

huyo kutamka Shahada (Lailaha Illa Allah; Muhammadan Rasulu Allah). Alipomuuliza kwanini kamuua baada ya kuwa ameshatamka Shahada, alijibu: "Hakuitamka ila kwa ajili ya kuogopa upanga". Mtume (s.a.w.), akamjibu: "Je uliupasua moyo wake ukayajua yaliyomo ndani yake". Kwa hivyo, hivi ndivyo ambavyo Mtume (s.a.w.) alikuwa akihukumu: alikuwa akihukumu kwa mujibu wa dhahiri tu: ama ya moyoni alikuwa hahukumu ila apate Wahyi. Sasa sijui na Ali naye alikuwa akipata Wahyi! Na turudi katika maelezo ya Al-Imamu Ibn Taymiyya. *Tunasema:* Ama dai la Ibn Taymiyya kwamba "Ali na Mu'awiya walipokubaliana kufanya sulhu….", ni maneno yenye upendeleo wa wazi. Cha kujiuliza ni kuwa je Mu'awiya alifanya sulhu kwa kuwa kweli anataka sulhu au alifanya hivyo kwa ajili ya kulifarikisha jeshi la Ali na kupata nguvu yeye? Moja ya nakala za Al-Tabari inamnukuu Amru bin Al-'Aas, mshauri mkuu wa Mu'awiya, akimshauru Mu'awiya katika vita vya *Siffin* kwa kusema:

> Je nikuoneshe jambo ambalo halitotuzidishia sisi ila umoja na halitowazidishia wao ila mfarakano? Akasema (Mu'awiya): 'Ndio". Akasema (Amru bin Al-'Aas): 'Tunyanyue Misahafu kisha tuseme: 'Kilichomo humu ndio hukumu baina yetu na nyinyi'. Ikiwa kuna baadhi yao watakataa basi utawapata wengine watasema: 'Ndiyo inatupasa tukubali', na hapo patatokea mfarakano baina yao. Na wakisema (wote): 'Ndiyo' tutajiondoshea vita hivi mpaka baada ya muda.[106]

Na riwaya ya Ibn A'atham, inamnukuu Amru bin Al-'Aas akisema: "'Tunyanyue Misahafu"[107] katika vichwa vya mikuki ikiwa kama ni alama ya kutaka sulhu "Ili kulizuia jeshi la Ali na kulivunja nguvu zake".[108] Na katika riwaya ya Al-Baladhiri, Amru bin Al-'Aas anasema kumwambia Mu'awiya:

> Je utanikubalia ushauri nitakaokupa? Muamrishe mtu afunue Msahafu kisha aseme: 'Enyi watu wa Iraki baina yetu sisi na nyinyi kuna Kitabu cha Allah, tunakulinganieni katika hicho kuanzia

106 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 329-330. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 667.

107 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 305-306. Al-Ya'aqubi, *Taarikh Al-Ya'aqubi* j. 2, uk. 188.

108 - Al-Ya'aqubi ,*Taarikh Al-Ya'aqubi* j. 2, uk. 188.

> mwanzo wake hadi mwisho wake, hakika yako (Ewe Mu'awiya) ukifanya hivyo (basi wao) watakhitalifiana.[109]

Haya! Ni sulhu gani alioitaka Sheikh Mu'awiya ewe Sheikh Al-Islam! Baada ya haya utaona kuwa maelezo ya Sheikh Al-Islam, Ibn Taymiyya, kwamba Mu'awiya alikuwa akitaka sulhu bado ni maelezo yenye mushkila mkubwa.

MAANA YA *KHAWARIJ* KATIKA MTAZAMO WA SHEIKH MUHAMMAD ABDUH

Mwanachuoni mwengine aliyetupa *Taarifu* ya Khawarij ni Sheikh Muhammad Abduh. Yeye – katika maelezo yake aliyoyatia katika kitabu *Nahju Al-Balagha* – ametoa maelezo yenye kutupa faida mbili: moja ni kutujuilisha nini maana ya *Khawarij* ingawa yeye katumia neno jengine, nalo ni *"Al-Mariqun"*. Pili ni kutujuilisha hao Khawarij ni nani. Anasema:

> Na *Al-Mariqun (yaani Al-Khawarij)* ni wenye kutoka katika dini: wenye shaka ambao hawana yakini, naye Ali(k.w.) aliwagonga kwa hoja za wazi akawashinda![110]

Lakini *Taarifu (Definition)* hii ya Sheikh Muhammad Abduh – pamoja na kuwa alikuwa na tabia ya kukataa kusalim amri kwa fikra za wanavyuoni wengine – haikutokana na kawaida yake ya kuzitafakari vyema fikra za wanavyuoni wengine na kuzipima kisha kuzikubali au kuzikataa kwa mujibu wa misingi sahihi ya elimu. Bali Sheikh hapa alikuwa akifuata na kukariri maneno aliyoyarithi kutoka kwa waliomtangulia bila kuyapekuwa na kuyaweka katika mezani sahihi. *Taarifu (Definition)* hii – kama unavyoona – ina tupa nukta mbili muhimu:

1) *Khawarij* wametoka katika dini kwa kuwa na shaka na kutokuwa na yakini katika dini!

---

[109] - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 103.

[110] - Sheikh Muhammad Abduh, *Shar-Hu Nahji Al-Balagha* uk. 78, maelezo ya hutuba na. 81.

2) Watu wenyewe waliokuwa na sifa hizo ni wale waliopingana na Ali!

Na hayo – bila shaka – ni maneno ya ajabu sana! Ama tukija katika maneno ya kwanza, tunakuta kwamba ni maneno ambayo hayaelezeki kabisa, na sidhani kwamba hata Sheikh Muhammad Abduh mwenyewe – kama aliulizwa – angeweza kuyatolea maelezo sahihi. Suali ambalo tunajiuliza hapa ni lile lile tulilojiuliza kabla nalo ni kuwa watu hao vipi na ni kwa sababu gani wametoka katika dini, lakini Talha, Zubair na Mu'awiya wasitoke? Tukichukulia kuwa sababu ilikuwa ni kumpinga Ali, basi – bila ya kutafuta nani alikuwa katika haki na nani alikuwa katika batili – tunakuta kwamba Talha, Zubair, Mu'awiya na wafuasi wao walimpiga vita Ali pia. Tukichukua kuwa sababu ilikuwa ni kitendo chao cha kumuua Abdillah bin Khabbab – nayo si riwaya sahihi na inahitaji maelezo marefu kama tutavyobainisha baadae *Inshaa Allah* – basi tunakuta kwamba Mu'awiya kaua maelfu kwa maelfu ya Waislamu bila ya haki. Sasa vipi hawa wamekuwa Waislamu wema, wale wakawa ni wenye kutoka katika dini? Hii ndio mezani ambayo hata wanavyuoni wakubwa wa Umma huu – kama hawa – wanaitumia katika kupima matokeo haya ya Kihistoria – tukio moja linapimwa kwa mezani mbili tafauti: Makame na Pandu wamefanya kosa moja, lakini Makame ana hukumu yake mbali na Pandu ana hukumu yake mbali! Bali tunasema kwamba hakuna kamwe kitu ambacho Kisharia kinahalalisha kuwatoa watu hao wa Nahrawaan katika Uislamu hata wangelikuwa watu hao ndio waliokosea, sana sana tungesema kuwa ni "Waislamu walioasi". Na kwa hivyo, Ali mwenyewe alipinga kuitwa watu hao kuwa ni wanafiki au makafiri na akasema: "Kutoka katika ukafiri wameshakimbia (si makafiri); na mnafiki hamtaji Mwenyezi Mungu ila kidogo…."[111] Alipoulizwa ni nani basi? Akajibu: "Ni watu wametuasi tukapewa ushindi juu yao".[112] Bali Ali mwenyewe alikuwa akiwaona watu hao wa Nahrawaan kuwa ni bora zaidi kuliko Mu'awiya na kundi

111 - Ali alikuwa akiwaona watu hao kuwa wameasi; nao walikuwa wakimuona kuwa kenda kinyume na Qur-ani. Na wote walikuwa wakionana kuwa ni watu wema lakini kila mmoja alikuwa akiona kuwa mwenzake kakosea.

112 - Ibn A'atham katika, *Al-Futuh* j. 4, uk. 128, kaipotoa riwaya hii kama kawaida yake. Yeye kaiandika hivi: "Kutoka katika ukafiri wamekimbia nao humo wametumbukia….wao ni watu ambao wametoka katika dini ya Kiislamu kama mshale unavyotoka katika kiwindwa".

lake.[113] Basi vipi sisi leo tunamtetea Mu'awiya ambaye ni asi kwa ushahidi wa Hadithi sahihi ya Mtume (s.a.w.) na kwa ushuhuda wa Ali mwenyewe; na – badala yake – kuwatoa katika dini watu waliokuwa na sifa za ucha Mungu na elimu kubwa, bila kuchunguza vyema na kuyapima mambo kwa mezani ya Qur-ani kisha ndio tukatoa uamuzi adili?

Ama maelezo ya Sheikh Muhammad Abduh kwamba watu hao walikuwa na shaka: hawakuwa na yakini! Sijui maelezo hayo kayotoa wapi![114] Vitabu vyote vya historia vinakubaliana kwamba watu hao walikuwa ni wenye kuabudu sana na walikuwa wachaji sana,[115] bali vitabu vinaeleza kwamba wao ndio Masahaba wanavyuoni, na riwaya ya Ibn Abbaas – kama tutavyoona baadae – inaeleza kwamba wao ndio Masahaba wa awali. Na kwa hivyo, Ibn Abdi-Rabbih anasema: "Wala hakuna katika vikundi vyote na watu wote wa bidaa,[116] watu wenye uoni

---

113 - Halkadhalika Al-Hasan bin Ali alikuwa akiona kuwa wale waliokuwa wakiitwa Khawarij waliokuja baada ya Watu wa Nahrawaan ni bora zaidi kuliko Mu'awiya, na alikuwa Al-Hasan akiwaita watu hao kuwa ni Waislamu. Alipotakiwa na Mu'awiya kuwa awapige watu hao, alisema: "Mimi nimejizuia na wewe ili kuizuia damu za Waislamu, na sifikirii kwamba hilo (la kuwapiga vita wao) linanipa nafasi (katika dini yangu). Basi vipi niwapige watu ambao wewe unastahiki zaidi kupigwa vita kuliko wao?" Ibn Abdi-Rabbih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 1, uk. 177, *Babu min akhbari al-Azariqa.* Ni wazi kwamba kwa mtazamo wa Al-Imamu Al-Hasan bin Ali, Hadithi "Wanatoka katika dini kama mshare unavyotoka katika kiwindwa" haiwahusu watu hao, vyenginevyo asingeliwaona kuwa ni Waislamu.

114 - Labda kayafahamu hayo katika Hadithi isemayo: "Watatokea watu miongoni mwenu munadharau sala zenu mbele ya sala zao; funga zenu mbele ya funga zao; matendo yenu (yote mema) mbele ya matendo yao (lakini) *wanatoka katika dini* kama mshare *unavyotoka* katika kiwindwa". Lakini je Hadithi hii inamuhusu nani? Maelezo kwa ufupi juu ya Hadithi hii yatakuja katika sehemu ijayo, na kwa urefu na ufafanuzi yatakuja katika juzuu maalumu ya kitabu hiki juu ya utafiti wa Hadithi za Khawarij.

115 - Vitabu vinaandika kwamba Abu Bilal alimpitia Bedui ambaye alikuwa akimpaka ngamia wake lami. Abu Bilal akaanguka akazimia, Bedui akadhania kwamba labda kaangushwa (na jini); akamsomea kwenye masikio. Alipozinduka akamwambia: "Mimi sina hayo unayoyahofia wewe, lakini nimemuona ngamia wako kachanganyika lami nikakumbuka lami ya (moto wa) Jahannam". Tazama Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 627, Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 5, uk. 190, na katika riwaya hii ya Al-Baladhiri, Abu Bilal alipozinduka alisoma Aya ya Qur-ani isemayo: **سَرَابِيلُهُمْ مِنْ قَطِرَانٍ (Nguo zao (watu wa motoni) zinatokana na lami".** Sura 14, Aya 50.

116 - Hivi ndio vichekesho vya wanavyuoni! Ukisoma vitabu utastaajabu na unaweza kucheka mpaka ukaanguka. Utaona mtu anakutajia kuwa fulani aliua bila ya haki

mkali kuliko Al-Khawarij, wala wenye jitihadi kubwa na wenye kujidhatiti katika mauti kuliko wao".[117] Halkadhalika Al-Baladhiri, kawasifu watu hao kuwa ni: "Wale waliokuwa na busara na wenye kuabudu (sana)".[118] Kwa hivyo, utakapojua ukweli huu na kujua ukweli kwamba itikadi ya baadhi ya Waislamu ni kutokumjeruhi (kutokumtia ila) Sahaba yeyote awaye, basi utajua kwamba tatizo moja sugu kwa watu wengi – hata wanavyuoni wakubwa – ni kufuata fikra – hasa za kisiasa na kiitikadi – za waliowatangulia na kuzifanya fikra hizo kuwa ni kanuni ambazo si halali hata kuzijadili! Maelelezo hayo ya Sheikh Muhammad Abduh yanatokana na fikra za aina hii za kufuata kitu bila kukipima!

Ama tukija katika maneno ya Sheikh Muhammad Abduh aliposema: "Naye Ali (k.w.) aliwagonga kwa hoja za wazi akawashinda", yanaonesha – maneno haya – kuwa Imamu wetu huyu alipoisoma maudhui hii, aliisoma haraka haraka: hoja za Watu wa Nahrawaan zilimfanya hata Ibn Abbaas (r.a.) asalim amri, nawe ndugu msomaji utajionea mwenyewe huko mbele hoja za Ali (k.w.) na hoja za Watu wa Nahrawaan (r.a.) halafu – ikiwa unatafuta ukweli: na si kasumba za kimadhehebu – basi utajua ukweli uko wapi.[119]

---

mamia au maelfu ya watu, halafu anamwita *Ahlu Sunna*! Halafu atakutajia mwengine akupe sifa zake nzuri ambazo ni nadra hata kwa Masahaba, na kwamba alikuwa mchaji sana mwenye khofu kubwa ya Allah, hakubali kuua mtu bila ya kosa, halafu atamwita Khawarij au mtu wa bidaa! Ni kama yale tulioyanukuu katika *Mezani Ya Haki* kutoka kwa Abu Daud na Ibn Taymiyya na wengine. Wanasema: "Hakuna katika watu wenye kufuata matamanio yao watu ambao Hadithi zao ni sahihi kuliko *Khawarij!*" Tazama *Minzanu Al-I'itidal* cha Al-Dhahabi j. 4 uk. wa 156 katika *tarjama* ya Imran bin Hittan. Anasema Ibn Taymiyya: "Hakuna katika watu wanaofuata *matamanio yao* watu wakweli na waadilifu kuliko *Khawarij*.…wao si katika wanaokusudia kuzua uwongo bali wao ni maarufu kwa ukweli mpaka inasemwa kwamba Hadithi zao ndio Hadithi sahihi kuliko zote." Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 3, uk. 3. Dr. Al-Sibai *Al-Sunna Wa Makanatuha Fii Al-Tashrii Al-Islami* uk. 99- 101.

117 - Ibn Abdi-Rabbih *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 1, uk. 179.

118 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 112.

119 - Bali hata leo hii Sheikh Nassir Al-Sabi'i kaandika utafiti wake juu ya suala hili na hakuna yeyote aliyeweza kunyanyua kichwa chake akakijibu pamoja na kuwa tabia yao ni kujibu hoja za haki kwa hoja dhaifu kama nyumba ya buibui! Na kabla ya kitabu hicho kila siku ilikuwa zogo "Khawarij weee Khawarij". Ni wazi kwamba watu hawa hawasomi isipokuwa kile kile walichokirithi kutoka kwa baba na babu!

Hizo ndizo *Taarifu (Definitions)* walizozitoa wanavyuoni tafauti[120] kuhusu maana ya neno Khawarij, nazo – kama unavyoona – si *Taarifu* pambanuzi zenye kuweza kujenga tafauti itakayoweza kutujuilisha nani Khawarij na nani si Khawarij

NENO *KHAWARIJ* KATIKA MATUMIZI YAKE YA KIHISTORIA

Tukirudi katika historia na kutazama matumizi ya awali kabisa kabla ya miaka ya sitini (60's) A.H. ya neno *Khawarij*, tunakuta kwamba watu walikuwa wakilitumia jina *Khawarij* kwa maana nzuri tu: wakikusudia *Al-Kharijun Fii Sabili-Llahi* (Wenye kutoka katika njia ya Mwenyezi Mungu). Anasema Al-Imamu Nuru Al-Din Al-Salimi (r.a.):

> Na jua kwamba jina *Khawarij* lilikuwa katika zama za mwanzo ni sifa nzuri kwani ni wingi wa neno *Kharija* nacho ni kikundi kilichotoka kwa ajili ya kupigana katika njia ya Allah. Anasema Allah Mtukufu: **'ولوأرادوا الخروج لأعدوا له عدة' (Na lau walikusudia *Kutoka* basi wangeuandalia (utokaji huo) maandalizi (ya kivita).**[121] Kisha likawa na sifa mbaya kwa sababu ya tafsiri nyingi za wapinzani za Hadithi zenye sifa mbaya (wakazinasibisha na wale) waliosifika na sifa hio (ya kutoka jihadi katika njia ya Allah).[122]

Na kwa hivyo, Sheikh Ali Yahya Ma'amar (r.a.), ametoa matumizi matatu ya neno "Khawarij":

Moja: ni maana inayotumiwa na waandishi wa historia, nayo ni maana wanayowakusudia kwayo: "Wale waliojitenga na Amiri-l-Mu-uminin Ali bin Abi Talib alipokubali sulhu, kwani – kwa mtazamo wa

- Wanavyuoni wengine wote *taarifu* zao ni hizo hizo.[120]

[121] - Sura 9, Aya 46. Tumesema kwamba neno *khawaarij* maana yake ni waliotoka. Sheikh Al-Salimi hapa anakupa Aya inayoonesha kwamba awali neno hilo lilikuwa likitumika kumaanisha wale waliotoka kwenda Jihadi.

[122] - Hili ndilo nililolieleza hapo nyuma kidogo kuhusu *Mujahidina* wa leo kuitwa *Khawarij* au kuitwa magaidi. Siasa ndio ambayo maisha yote inawadanganya watu na kuwapoteza. Tazama nakala hio ya Al-Imamu Al-Salimi katika *Sharhu Jami'i Al-Sahih* j. 1, uk. 59.

(wanahistoria) hawa, (watu hao) wamevunja ahadi yao ya utiifu iliokuwa shingoni mwao na wakatoka katika Uimamu (uongozi) wa Kisharia".[123]

Pili: ni maana "Inayotumiwa na watu wenye kuzungumzia mambo ya Tawhidi na itikadi katika dini, nao hukusudia (kwa neno *Khawarij*), kutoka katika dini, wakitegemea Hadithi ya Mtume (s.a.w.) isemayo: "Hakika watu katika Umma wangu watatoka katika dini kama mshare *unavyotoka* katika kiwindwa".[124]

Tatu: ni "Kundi linalolitumia neno hilo na wanakusudia kwalo (kutoka) Jihadi katika njia ya Allah".[125]

Ninasema: Lakini bila shaka kila anayesoma yaliyoandikwa vitabuni au kusikiliza yanenwayo midomoni, basi anaona kwamba watu wakizungumzia sula la Khawarij huwa wanakusudia mchanganyiko wa maana ya kwanza na ya pili kwa pamoja, na kwa hivyo wanakusudia kwa neno hilo kwamba Khawarij ni "Watu waliotoka katika utawala wa Ali na ambao – kwa sababu hio – wametoka katika dini," kama tulivyoona maelezo katika *Taarifu* tafauti tulizozinukuu. Lakini baada ya yote, utaona kwamba hayo yanawabomokea kwa matokeo ya Talha, Zubair na Mu'awiya ambayo ni sawa au mabaya zaidi ya matokeo yaliyotokea baina ya Ali na hao waliohusishwa na *Ukhawarij*. Bila kusahau kwamba katika maana ya mwanzo inayotumika kwa wanahistoria na ambayo katunukulia Sh. Ali Yahya Ma'amar kwamba Khawarij ni: "Wale waliojitenga na Amiri-l-Mu-uminin Ali bin Abi Talib alipokubali sulhu na kuiridhia, kwani – kwa mtazamo wa (wanahistoria) hawa, (watu hao) wamevunja ahadi yao ya utiifu iliyokuwa shingoni mwao na wakatoka katika Uimamu wa Kisharia", tukirudi katika maelezo haya, ni kuwa – kama Sheikh Ali Yahya mwenyewe alivyoyajibu maneno hayo kwa urefu ambayo ufupisho wake ni kuwa – suala la Uimamu kama vile ambavyo ni mzigo ulio katika shingo za raia, basi vivyo hivyo ni mzigo na jukumu lililo katika shingo ya Imamu, na kwa hivyo Imamu akifanya chenye kukhalifu Sharia, au akijiuzulu au kuuzuliwa na wanaofaa kumuuzulu

123 - Ali Yahya Muammar *Al-Ibadhiyya Fii Mawkibi Al-Taarikh* uk. 19.
124 - Marejeo k.h.j.
125 - Marejeo k.h.j.

basi Uimamu wake unabatilika na raia wanawajibika kuchagua Imamu mwengine.[126]

TUKIREJEA KATIKA TAARIFU YA AL-SHAHRASTANI

Sasa tukirudi nyuma kidogo, kuitazama *taarifu* ya Sheikh Al-Shahrastani kwamba "Kila aliyetoka dhidi ya kiongozi wa haki ambaye *Jamaa* (walio wengi) wameafikiana juu yake basi anaitwa *Khawarij*"[127] tutaona kwamba Waislamu wote tangu zamani hadi leo hii wanafanya majaribio ya mapinduzi wanapoona kwamba mfumo uliopo si mfumo adilifu au – kwa uchache – wanajitenga na mfumo huo ukiwa ni mfumo wenye sifa hio. Tumedokeza kwamba *Ahlu Al-Nahrawaan* (Watu wa Nahrawaan r.a.) ambao ndio chimbuko la fikra ya kisiasa ya Kiibadhi, wamejitenga na Sayyidna Ali (k.w.) kama walivyojitenga na Mu'awiya; Al-Imamu Al-Husain bin Ali – Imamu wa tatu wa Shia – kafanya vita dhidi ya dola ya Banii Umayya; Mu'awiya kaingia katika vita dhidi ya Sayyidna Ali na baada ya Sulhu ya Dumat Al-Jandal[128] ikawa mara kwa mara anatuma watu kuivamia miji iliyokuwa chini ya utawala wa Ali. Talha na Zubair, wamefanya jaribio la kumpindua Ali lililo mwaga damu. Kwa leo, utaona kwamba wafuasi wa Usama bin Laden wanafanya majaribio kadhaa dhidi ya watawala wa nchi za Waislamu. Su'udia na Pakistani – kwa mfano – kumefanyika majaribio kadha wa

---

126 - Na hivi ndivyo wanavyosema watu wa Nahrawaan katika kesi yao na Ali kama tutavyoona maelezo hayo baadae *Inshaa Allah*. Cha kustaajabisha ni kuwa kama watu wa Nahrawaan walivyochagua Imamu wao mpya Al-Imamu Abdullah bin Wahb Al-Rasibi (r.a.) ndivyo walivyofanya watu wa Sham wakamchagua Mu'awiya. Lakini watu wa Nahrawaan wamekuwa wabaya, Khawarij kwa hilo; watu wa Sham ni wema, *Mujtahidin*! Tazama Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 205.

127 - Lakini suali ni kuwa je hilo kundi lililomuacha Ali mkono na kuunda serikali yake lilipofanya hivyo, Ali (k.w.) alikuwa bado ni Khalifa wa Waislamu?! Na je wao walitoka dhidi yake **(خرجوا عليه)** au walitokana na yeye kwa maana kwamba walitoka katika kumtii yeye **(خرجوا من طاعته).**

128 - Wengine huutamka mji huu "Daumat na Dumat" lakini Ibn Duraid – katika wanavyuoni wa lugha – anaona kwamba kuutamka "Daumat" ni kosa na sahihi ni "Dumat". Tazama Al-Hamwi ,*Mu'ujamu Al-Buldan* j. 2, uk. 325.

kadha;[129] watu wa chama cha FIS huko Algeria wameingiana mara kwa mara na jeshi la serikali; Somalia harakati za Waislamu zapelekea kung'olewa kwa Rais aliyekuwepo;[130] Misri mara kadhaa wa kadhaa *Ikhwanu Al-muslimin* wafanya majaribio ya hapa na pale; Iran Ayatullah Khomeni ampindua Shaa; Yemen hivi karibuni harakati za Kishia zaanzisha vita dhidi ya serikali; Zanzibar, Kenya na Tanganyika mara nyingi kumekuwa na upinzani wa wazi wa Waislamu dhidi ya serikali zao. Na wote hawa wanachokitaka ima ni kuwa mifumo inayotawala ibadilishe siasa zake au kuondoa kabisa mifumo hio na kuimarisha mifumo inayokubaliana na Uislamu. Na wote hao – ukitoa upinzani wa Watu wa Nahrawaan kwa Ali – ni wafuasi wa madhehebu manne za Kisuni na madhehebu mbili za Kishia.[131] Sasa jiulize wewe nini tafauti baina ya hawa na hao walioitwa kuwa ni *Khawarij?* Je:

1) Uharamu wa kuipinga serikali ni mahususi kwa Watu wa Nahrawaan pasina wengine: wengine wana haki ya kupinga na kuunga mkono?[132]
2) Kuna sababu maalumu za Kisharia – kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna – ambazo kiongozi yeyote awaye akizifanya hupingwa hata akiwa Umar au Abu Bakr; au Sahaba ana haki maalumu ya kufanya atakavyo na Sharia haimkamati: inawakamata walalahoi tu?[133]
3) Ile Hadithi ambayo watu wamekuwa wakiitumia – hasa hasa Banii Umayya na wafuasi wao – kuonesha ubaya wa *Khawarij* inayosema kwamba tusiwapinge watawala waovu vyovyote vile iwavyo madamu hawatuzuii kusali imekwenda wapi sasa? Je huko Zanzibar, Pakistani, Kenya na kwengine ubaya wa watawala umepata kufikia hadi ya kuwazuia Waislamu wasisali? Kama haijafikia hali hio kwanini basi tuwapinge? Hapa nadharia (theory) imegongana na uhakika wa mambo (reality) au ukipenda sema imegongana na matendo (practices).

---

129 - Watu wa Al-Qaida nao pia wanaitwa *Khawarij* huko Su`udia. Kuanzia hapa utaweza kujua kwanini watu wa Nahrawaan wameitwa *Khawarij.*

130 - Baadae karejea tena kwa msaada wa Wamarekani na Waithiopia.

131 - Hili linaeleza kwamba fikra ya walioitwa *Khawarij* kuhusu siasa ya dola ndio fikra sahihi inayokubaliana na Qur-ani na Sunna na akili na kwamba fikra nyengine zote kimatendo zimefeli.

132 - Bali Watu wa Nahrawaan walipojitenga na Ali, Ali hakuwa Khalifa tena kama tutavyoona maelezo yetu baadae.

133 - Hii sio Sharia ya Allah na Mtume wake.

Sasa baada ya haya utaona kwamba watafiti na wanavyuoni bado wamekabiliwa na changamoto ya kutafuta sababu zilizowapelekea watu wa kila kundi kujitenga na mtawala; au zilizowapelekea kufanya mapinduzi au jaribio la mapinduzi. Kisha – hatua ya pili – kuzipima sababu hizo katika mezani ya Sharia: Qur-ani na Sunna (Hadithi). Kwa kufanya hivyo, tutaweza kujua ni nani *Khawarij* aliyekusudiwa katika Hadithi isemayo:

> Watatoka watu miongoni mwenu munadharau sala zenu mbele ya sala zao; funga zenu mbele ya funga zao; matendo yenu (yote mema) mbele ya matendo yao (lakini) wanatoka katika dini kama mshare unavyotoka katika kiwindwa.

Ama tukisema kuwa *Khawarij* ni fulani tu, basi lugha hii anaweza kuitumia mtu yeyote anayekupinga hata kama ushahidi unamsuta.

JINA *KHAWARIJ* LIMETOKA WAPI?

Tumeona kwamba neno *Khawarij* kilugha maana yake ni *Wenye kutoka,* kama tulivyobainisha katika maelezo ya Al-Imamu Al-Salimi kwamba asili ya neno hili hapo awali lilikuwa likitumiwa kwa maana nzuri tu, likimaanisha wenye kutoka katika njia ya Mwenyezi Mungu. Baadae watu wakalitumia kwa maana ya waliotoka dhidi ya mtawala. Na hatimae likahusishwa na makundi maalumu, hususan *Al-Muhakkimah Al-Ula (Ahlu Nahrawaan r.a.).* Katika sehemu hii, tutatazama chimbuko la jina hili limetoka wapi.[134]

Elewa ndugu msomaji – nawe umo katika kupekuwa kurasa za kitabu hiki – kwamba Hadithi za Mtume (s.a.w.) zinazotumiwa kumaanisha watakaotoka katika dini ni zile Hadithi zilizobeba ndani yake lafdhi: *"Al-Mariqun"* au *"Yamruqun"*. Lakini *Al-Mariqun* na Al-Khawarij ni maneno mawili yenye maana moja kilugha. Na kwa hivyo, Hadithi zilizotaja *Al-Mariqun* ndizo ambazo watu wamezichukua na kuwabandika nazo wale

134 - Yaani chimbuko la kimatumizi: si chimbuko la kilugha: chimbuko la kilugha la neno hilo tayari tumeshalielezea.

walioitwa "Khawarij". Hadithi mashuhuri miongoni mwa hizo, ni Hadithi inayosema:

> Watatokea watu miongoni mwenu munadharau sala zenu mbele ya sala zao; funga zenu mbele ya funga zao; matendo yenu (yote mema) mbele ya matendo yao (lakini) *wanatoka katika dini* kama mshare *unavyotoka* katika kiwindwa.[135]

Maneno ya Kiarabu yaliyotumika katika Hadithi hii kumaanisha *wanatoka katika dini* ni maneno *"Yamruqun mina Din"*. Katika Hadithi hii – kama unavyoona – kuna jambo moja la wazi na jengine la kitandawili! Jambo lililowazi ni kuwa Hadithi inatabiri kuja kwa watu watakaotoka katika dini. Hili linaeleweka katika Hadithi hii bila ya kujikalifisha, lakini bila shaka kitandawili ni kuwa je Hadithi hii inamuhusu nani au inakihusu kikundi au madhehebu gani? Watu wameichukua Hadithi hii na kuwabandika nayo Watu wa Nahrawaan, lakini tatizo – kama tulivyoeleza zaidi ya mara moja – ni kuwa kile kilichotarajiwa kuwa ni sababu ya Watu wa Nahrawaan kuhusishwa na Hadithi hii, kipo pia katika madhehebu zote. Na kwa hivyo, Al-Hakim katika *Al-Mustadrak* anasimulia riwaya kutoka kwa Abu Said Al-Khudri (r.a.) alipoulizwa kuhusu Al-Khawarij ni nani akajibu jawabu yenye kumaanisha kuwa Al-Khawarij ni Mu'awiya na wafuasi wake. Hadithi hio inasema:

> Kutoka kwa Ikrima kutoka kwa Ibn Abbaas (r.a.) kwamba alisema kumwambia yeye na mwanawe:[136] 'Nendeni kwa Abi Said (Al-Khudri) musikilize mazungumzo yake kuhusu habari za *Khawarij*. Basi wakaondoka, kutahamaki yeye (Abu Said Al-Khudri) yupo kwenye ukuta wake anatengeneza. Basi alipotuona alichukua nguo yake ya juu kisha akajifunga nayo (miguuni na kiunoni hali ya kuwa kakaa kitako), kisha akaanza kutuhadithia mpaka sauti yake ikapaa msikitini, akasema: 'Tulikuwa tunabeba tufali moja moja na Ammar (bin Yasir alikuwa) anabeba matufali mawili mawili. Basi Mtume (s.a.w.) akamuona akawa anampangusa udongo katika kichwa chake na anasema: 'Ewe Ammar! Hubebi tufali moja moja kama wanavyobeba wenzako?' Akasema: 'Mimi nataka ujira mbele ya Allah.' …Basi akawa

[135] - Tutawataja walioipokea Hadithi hii katika juzuu ya pili ambayo ni mahususi kwa utafiti wa riwaya za Khawarij *in shaa Allah*.

[136] - Yaani Ibn Abbaas aliwambia Ikrima na mwanawe.

> Mtume (s.a.w.) anapangusa (kumpangusa Ammar) na huku anasema: 'Namuhurumia Ammar! Atauliwa na kundi la waasi.[137]

Ni wazi kwamba Abu Said (r.a.) anamuona Mu'awiya na kundi lake kuwa ndio *Al-Khawarij,* kwani alipoulizwa habari za *Al-Khawarij* alijibu kwa habari za waliomuua Ammar bin Yasir nao ni Mu'awiya na kundi lake.

Na mfano wa maelezo hayo ya Sahaba Abu Said (r.a.) – katika riwaya hio iliyotangulia – ni kile kilichosimuliwa kutoka kwa Al-Sayyid Al-Husain bin Ali bin Abi Talib alipojiwa na Ubaid-Llahi bin Umar bin Al-Khattab katika vita vya *Siffin* akimtaka amuuzulu baba yake Ali bin Abi Talib ili wamchague yeye kuwa ndiye Amiri-l-Mu-uminin. Al-Husain alimjibu:

> ….Kwa hakika shetani amekupambia matendo yako maovu, akakuhadaa hata akakutoa katika dini yako kwa kuwafuata waovu na (kwa) kumnusuru (kwako) huyu *Mariq* (Khawarij au aliyetoka) katika dini .[138]

Al-Husain kwa maneno yake haya aliposema: "Kumnusuru (kwako) huyu *Mariq* (Khawarij au aliyetoka) katika dini" anamkusudia Mu'awiya kwani Ubaid-Llahi bin Umar bin Al-Khattab aliyeambiwa maneno haya alikuwa katika jeshi la Mu'awiya.

Halkadhalika, Mu'awiya bin Hudaij Al-Sukuni alipotoka – kwa amri ya Mu'awiya bin Abi Sufyaan[139] – dhidi ya Muhammad bin Abi Bakr, Liwali (Gavana) wa Ali huko Misri, Ali alimwambia Al-Ashtar: "Nilikuwa nimempa Uliwali Muhammad bin Abi Bakr, wakatoka dhidi yake hawa *Khawarij".[140]* Na waliotoka dhidi yake ni Mu'awiya na jeshi lake.

---

137 - Tazama Al-Hakim *Al-Mustadrak* j. 2, uk. 162-163. Hadithi na. 2653., mlango *Qitalu Ahli Al-Baghyi.* Ibn Abdi Rabih *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 318-319. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 663. Lakini katika riwaya ya Ibn Abdi Rabbih na Ibn Al-Athir kuna tafauti kidogo ya mfumo wa maneno.

138 - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 57.

139 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 34. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 707.

140 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 31.

Na katika vita vya Siffin, Hammam bin Al-Aghfal, mmoja wa wafuasi wa Ali, alisema: **"إذ ظفـرت كتائـب العـراق**نحن قتلنـا صـاحب المُـرّاق"** (Viliposhinda vikosi vya (kijeshi vya) Iraki, Sisi tumemuua rafiki wa wenye kutoka (katika dini yaani Khawarij).[141] Na hapo vita vilikuwa baina ya Ali na Mu'awiya.

Baada ya haya utaona kwamba Hadithi hio inayosema: "Watatokea watu miongoni mwenu munadharau sala yenu mbele ya sala zao….." ni Hadithi yenye utata mkubwa juu ya nani inayemuhusu. Maelezo yake kwa urefu yatakuja katika juzuu mahususi kwa utafiti wa Hadithi za Khawarij *Inshaa Allah.* Ama kwa hapa, kimsingi nilichokusudia kukubainishia kwa ufupi ni kuwa watu huwa wanazungumzia neno *Khawarij (Waliotoka),*[142] lakini je neno hili wamelitoa wapi? Basi elewa kwamba chimbuko la neno hilo limetolewa kutokana na Hadithi hii:

> Watatokea watu miongoni mwenu munadharau sala zenu mbele ya sala zao; funga zenu mbele ya funga zao; matendo yenu (yote mema) mbele ya matendo yao (lakini) *wanatoka katika dini* kama mshare unavyotoka katika kiwindwa.

Kilichobaki ni kujua je Hadithi hii inamuhusu nani? Hili tutalibainisha katika sehemu nyengine *Inshaa Allah.* Ama kwa sasa, kwa sababu, tumekosa *taarifu* pambanuzi ya neno *Khawarij* – jambo ambalo limewapelekea watafiti na wanavyuoni kuchupa moja kwa moja hadi kututajia fulani na fulani kuwa ndio *Khawarij* – basi hatuna budi kuainisha makundi yote ambayo waandishi wa makala, historia na wanavyuoni wa Fiq-hi wameyaita kuwa ni *Khawarij,* kisha kuzitazama sababu ambazo kwazo makundi hayo yameitwa kuwa ni Khawarij pamoja na kuzijadili hoja zao na hoja za wapinzani wao. Lakini hilo halitofanyika katika juzuu hii kwa ufafanuzi, kwani juzuu hii ni mahususi kwa kuzungumzia Watu wa Nahrawaan tu, na maelezo kwa ufafanuzi juu ya makundi mengine yatakuja *Inshaa Allah* katika juzuu nyengine za kitabu hiki. Sura inayofuata inataja makundi hayo, kisha inazungumzia kundi la mwanzo kwa kubainisha historia na kutoa hoja za hawa na jawabu za wale.

---

141 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 218.

142 - Yaani waliotoka katika dini.

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

1) Tulichokitafiti katika Sura hii ni hizi *Taarifu (Definitions)* zilizotolewa ili kubainisha maana ya neno *khaawarij*.
2) Tumeona kwamba *Taarifu* zote zilizotolewa hazikuweza kutoa maana ya wazi ya neno hilo, kwani:

a) Sifa zote ambazo wamesifika nazo au wamebandikwa nazo wale walioitwa *Khawarij*, wamesifika nazo pia – na zaidi – watu wote wa madhehebu nyengine.

b) *Taarifu* hutolewa ili kuonesha tafauti iliopo baina ya kitu chenye kutolewa *Taarifu* na vitu vyengine; wakati – kwa hapa – kila *Taarifu* moja basi ina mgongano au imeshindwa kujenga kanuni itakayomuwezesha mtu kumpambanua *Khawarij* na asiyekuwa *Khawarij;* na kwa hivyo, utakuta kwamba baadhi ya *Taarifu* hizi zimewaingiza Masahaba kama Mu'awiya, Talha, Zubair na wafuasi wao kuwa miongoni mwa *Khawarij* waliokusudiwa katika Hadithi hio ya Mtume (s.a.w.) isemayo: "Watatokea watu miongoni mwenu munadharau sala yenu mbele ya sala zao….. ", wakati baadhi ya *Taarifu* nyengine zimewaingiza hata wasiokuwa Waislamu kabisa.

3) Mgongano huu hauwezi kufasirika ila kwa namna mbili:

a) Watu wamekuwa wakifuata matamanio ya nafsi zao katika kuhukumu mambo na si kwa kutafuta haki.

b) Ubatili wa wazi ambao umekuwa ukihubiriwa dhidi ya hao walioitwa *Khawarij,* vyenginevyo haki haijigongi yenyewe kwa yenyewe wala haiwi na *Taarifu* isiyopambanua uhakika wake.

4) Ni kuwa, wakati watu wanawaita Watu wa Nahrawaan kuwa ndio *Khawarij,* basi Sahaba Abu Said Al-Khudri anamuona Mu'awiya kuwa ndio *Khawar*ij. Halkadhalika Al-Imamu Ali, Al-Imamu Al-Husain na wafuasi wao walikuwa wakimuona Mu'awiya na wafuasi wake kuwa ndio *Khawarij* kama tulivyobainisha kwa uwazi.

5) Kwa hivyo, tunachoweza kukisema hadi hapa ni kuwa hakuna *Taarifu* sahihi na ya wazi juu ya *Khawarij* ni nani hata kama watu wametaka kulichukua jina hilo na kuwabandika nalo Waislamu waliokuwa wakipigania haki. Kilichobaki ni kuyatazama matokeo ya kihistoria na kuyapima katika mezani ya Qur-ani na Sunna, na

kutazama riwaya zilizosimulia juu ya suala hili ili kufikia uhakika wa jambo hili. Na hapo itajulikana haki na batili ni ipi.

SURA YA PILI

WALIOITWA *KHAWARIJ*

Makundi ambayo yameitwa kuwa ni *Khawarij* ni:

-Al-Muhakkimah Al-Ula (Ahlu Nahrawaan(r.a.).
-Ibadhi(Ahlu Al-Haqqi Wa Al-Istiqama; Baqiyyatu Al-Salafi Al-Salih).
-Al-Azaariqa.
-Al-Najadat.
-Al-Bayhasiyyah.
-Al-Tha'alibah.
-Al-Sufriyyah.[143]

KUNDI LA KWANZA: *AL-MUHAKKIMA (AHLU NAHRAWAAN)*: CHIMBUKO LA IBADHI

Kundi hili ndilo hasa ambalo watu huliita kuwa ni *Khawarij,*[144] na hilo ni jina walilopewa na maadui zao kama alivyosema Dr. 'Awadh Khalifa wa

143 - Ama Al-Mubarrad yeye kataja makundi mane ukitoa *Al-Muhakkimah:* hakulitaja kundi la *Al-Tha'alibah*. Rejea Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 2, uk. 643. Ama Ibn Hazm yeye kataja makundi mengi lakini dhahir ni kuwa makundi hayo yote ni matawi yenye kurejea katika asili hizi hizi. Kwa mfano kasema: "Na wakasema Maimuniyya nao ni kikundi cha Al-'Ajaarida na Al-'Ajarida ni kikundi cha Al-Sufriyya….". Ibn Hazm, *Al-Fasl* j. 5, uk. 53. Lakini kitabu hiki cha Ibn Hazm kina kasoro kubwa ya kunakili mambo mengi yasio na ukweli! Tutayaeleza na kuyabainisha hayo katika juzuu nyengine za kitabu hiki *Inshaa Allah.* Ama Al-Shahrastani yeye kataja makundi manane; saba ni hayo yaliotangulia na la nane ni Al-'Ajarida. Kisha kila kundi *taqriban* akaligawa makundi mengine madogo mdogo ikawa jumla ya vikundi alivyovitaja havipungui thalathini. Naye – sawa na Ibn Hazm – hakusema ukweli, bali kawatungia Ibadhi vikundi na Maimamu ambao hawajulikani katika ulimwengu wa Kiibadhi wa kale wala wa sasa, kama tutavyoona katika juzuu zitazofuata za kitabu hiki *Inshaa Allah.* Tazama Al-Shahrastani, *Al-Milal* j. 1, uk. 131-154.

144 - Al-Mas'udi, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 272. Al-Mas'udi ,*Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 534. Al-Shahrastani, *Al-Milalu Wa Al-Nihal* j. 1, uk. 131.

Chuo Kikuu cha Jodan.[145] Na kama utavyoona – ndugu Muislamu – kwamba kundi hili ni kundi la Masahaba watukufu ambao ndio warithi sahihi wa mwenendo wa bwana Mtume (s.a.w.). Lakini kundi hili limeitwa hivyo na wanasiasa wa Banii Umayya na wapambe wa Ali, kwa sababu ya msimamo wao thabiti wa kushikamana na Qur-ani na Sunna. Na utakapojua sira yao na kulinganisha na sira ya hao Banii Umayya na wengine, basi utaweza kujua nani dhalimu na nani madhlumu. Kundi hili ndilo chimbuko la fikra ya kisiasa ya madhehebu ya Kiibadhi. Ninatumia maneno ***fikra ya kisiasa*** kwa sababu, katika migawanyiko hio ya awali hakukuwa na tafauti za kifiq-hi na kiitikadi ambazo zilipelekea kuwepo kwa Madhehebu tafauti za Kifiq-hi na kiitikadi: watu wote wakati huo walikuwa wakisali namna moja na walikuwa na itikadi moja: tafauti zilizopelekea kuwepo kwa makundi tafauti tangu zama za Masahaba ni tafauti za kisiasa tu – nani awe Khalifa nani asiwe. Ama Madhehebu za kifiq-hi na kiitikadi zilianza baada ya kuenea kwa uwongo mwingi na uzushi wa Hadithi uliojitokeza katika zama za Matabiina na Masahaba wa mwisho mwisho, na kupamba moto zaidi katika zama za *Tabii Al-tabiina* (wafuasi wa wafuasi wa Masahaba). Pakajitokeza tafauti hizo kwa sababu ya kuwa hawa wana riwaya hizi na wale wana riwaya hizi; hawa hawazikubali riwaya hizi na wale hawazikubali riwaya zile.

Sasa kwa ufupi, ni kuwa ili ujue watu hao wa Nahrawaan *(Ahlu Nahrawaan)* au *Al-Muhakkima* ni watu gani na kwanini wameitwa *Khawarij* na ili uweze kuihukumu kesi kwa haki na uadilifu, basi unahitaji kwanza na kabla ya yote kujua historia ya vita vya *Siffin* kwani hiki ndio chanzo hasa na ndio msingi uliopelekea wao – kwa dhulma – kubandikwa jina hilo, na hatimae kuwaacha watu kwenye kiza kwa kuwachanganyia haki na batili na ukweli na uwongo. Maudhui yetu katika sura hii ni vita vya *Siffin* – sababu zake na matokeo yake.

[145] - Dr. Awadh Khalifa, *Al-Usulu Al-Taarikhiyya Lil-Firqat Al-Ibadhiyya* uk. 5.

VITA VYA SIFFIN

SABABU NA MATOKEO

Mara nyingi – kama si mara zote – tukio la vita huwa lina sababu zake ambazo zimepelekea kuweko kwa vita hivyo. Tukirudi kutazama sababu za vita hivyo vya *Siffin,*[146] tunakuta sababu yake inarejea katika kitendo cha Sayyidna Ali – baada ya kuchaguliwa kwake kuwa Khalifa wa Waislamu – kumtaka Mu'awiya autambue Ukhalifa wake; na kitendo cha Mu'awiya cha kukataa matakwa hayo na – badala yake – kumtaka Al-Imamu Ali awatoe watu waliomuua Uthman bin Affaan kwanza kisha baada ya hapo ndio atautambua Ukhalifa wake. Hio ni kwa mujibu wa riwaya moja; na kwa mujibu wa riwaya ya pili ni kuwa Mu'awiya alidai kwamba baada ya Ali kuwatoa waliomuua Uthman, basi hatua itakayofuata ni kuwa pafanywe shura na uchaguzi mwengine ufanywe na watu wamchague Khalifa wamtakaye, Ali au Mu'awiya.[147] Na akawa Mu'awiya – baada ya kulinganiwa sana na Ali – anasema: "Je tuiwachie damu ya Uthman bure bure? *Wallahi* sitofanya hivyo milele",[148] na akasema:

> Hakika ya Sahibu yenu (Ali) kamuua Khalifa wetu (Uthman)..naye anadai kwamba hakumuua. Je munaonaje waliomuua Sahibu yetu (Uthman): je si wafuasi wa Sahibu yenu (Ali)? Basi na-atupe tuwaue kisha tutawakubalia kuingia katika utiifu (wake Ali) na kuwa pamoja na jamaa.[149]

Na akasema Mu'awiya – kwa ulimi wa mjumbe wake, Habib bin Maslamah –: "Tupe waliomuua (Uthman)..tuwaue kisha jiuzulu tuliwache jambo hili kwa watu kuwa ni Shura wamtawalishe jambo lao

---

146 - Vita hivyo vimeitwa hivyo kwa sababu ya kupiganwa katika sehemu iitwayo Siffin.

147 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 27. Na sijui kwanini Mu'awiya akagombania Ukhalifa kama kweli yeye ni mtu mwenye ucha Mungu moyoni mwake ilhali anajua kwamba kuna mamia ya Masahaba – ukimtoa Ali (k.w.) – kama vile Ibn Abbaas (r.a.) na Ibn Umar na wengine ambao ni bora zaidi kuliko yeye. Kwanini asiseme: "Baada ya hapo watu wachague Khalifa wamtakae ikiwa ni Ali au Ibn Abbaas au Ibn Umar" na badala yake ajiweke yeye mbele?

148 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 302. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 636.

149 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 5, uk. 304. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 26-27. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 642.

yule watayeafikiana",[150] na wakasema wajumbe wake wengine waliokwenda kwa Ali: "Tunashuhudia kwamba Uthman kauliwa hali ya kuwa ni mwenye kudhulumiwa". Ali akajibu: 'Sisemi kuwa kauliwa hali ya kuwa ni mwenye kudhulumiwa wala kauliwa hali ya kuwa ni dhalimu".[151] Na riwaya ya Ibn A'atham imemnukuu Ali akisema kuwajibu waliomwambia maneno hayo: "Haachi Uthman ima kuwa dhalimu au kuwa ni mwenye kudhulumiwa".[152] Na akasema Al-Walid bin 'Uqba – ambaye alikuwa katika jeshi la Mu'awiya – siku ya vita vya *Siffin* kumwambia Ibn Abbaas: "Mumeukata (uhusiano na) jamaa zenu na mukamuua Imamu wenu (Uthman)".[153] Na kijana mmoja – katika wafuasi wa Mu'awiya – akasema siku ya *Siffin:*

إني أتاني خبر فأشجانأن عليا قتل ابن عفان**

Hakika mimi imenifikia habari ikanitia huzuni,
Kwamba Ali kamuua (Uthman) Ibn Affani.[154]

Na akasema Mu'awiya:

> Kama wewe ni mkweli tuletee waliomuua Uthman tuwaue kisha sisi tutakuwa ndio wepesi wao kuja kwako, vyenginevyo hakuna baina yetu na wewe wala wafuasi wako isipokuwa upanga.[155]

Baada ya dai hilo la Mu'awiya, Al-Imamu Ali naye akamwambia Mu'awiya kwamba ingia katika kunitii kwanza halafu wewe kama unawajua hao waliomuua Uthman basi niletee tuwahukumu kwa mujibu

---

150 - Al-Tabar, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 305. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 642.

151 - Tazama Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 305. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 643. Na hii ni ajabu! Kwani mwenye kuuliwa kwa kukusudiwa hakuna chengine katikati: ama atakuwa kauliwa kwa udhalimu wake au waliomuua wamemdhulumu.

152 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 29.

153 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 308.

154 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* uk. 326. Ama Ibn Al-Athir katika *Al-Kamil* j. 2, uk. 665, yeye kayasimulia mashairi hayo hivi:

نبأنا قراوٗنا بما كانأن عليا قتل ابن عفان**

Wasomi wetu wametupa habari ilivyokuwa
Kwamba Ali kamuua (Uthaman) Ibn Affan.

155 - Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 310.

wa Sharia.[156] Mu'awiya akakataa na kudai kuwa Ali alikuwa anawajua waliomuua Uthman na kwa hivyo awatoe wahukumiwe kwanza halafu na yeye ndio atamtambua Ali.[157]

Basi ikawa kuna *murasalati* (mawasiliano) kwa njia za barua na pia kwa kutumiana wajumbe waliokuwa wakifikisha *risala* za mdomo baina ya Ali na Mu'awiya; *murasalati* ambao wakati mwengine ulikuwa ndani yake una maneno makali na wakati mwengine ulikuwa na maneno laini na ya nasaha. Miongoni mwa barua za Ali kwa Mu'awiya ni barua isemayo:

> *Bismi Allahi Al-Rahmani Al-Rahim.* Kutoka kwa mja wa Mwenyezi Mungu Ali, Kiongozi wa Waumini, kwenda kwa Mu'awiya bin Sakhr.[158] Baada ya hayo! (Jua kwamba) Hakika kuchaguliwa[159] kwangu kumekulazimu (wewe) na mimi niko Madina nawe uko Sham (Syria). Na hio ni kwa kuwa wamenichaguwa watu (wale wale) ambao walimchagua Abu Bakr, Umar na Uthman, aliyekuwepo hakuwa na haki ya hiari; na aliyekuwa hayupo hakuwa na haki ya kukataa. Ama Uthman yeye jambo lake liliwatatiza watu: mwenye kutoa habari ni kama kipofu na msikilizaji ni kama kiziwi. Na watu walimtia aibu (Uthman) naye hakuwakubalia; na wengine wakampenda nao hawakumnusuru na wakamkadhibisha aliyekuwepo na kumtuhumu asiyekuwepo. Na kwa hakika watu wamenichagua uchaguzi wa Umma (wote kwa pamoja), atakaeuchukia (uchaguzi huo) basi katoka (katika haki) na atakaebakia nyuma basi kaangamia, basi ukubali uzima[160] na utekeleze yale niliokuandikia. *Wa-ssalam!*[161]

Na barua nyengine ya Ali kwa Mu'awiya inasema:

---

156 - Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 310.

157 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 374-375-280.

158 - Mu'awiya bin Sakhr ndiye Mu'awiya bin Abi Sufyaan.

159 - Tazama Ali hakusema hakika wasia wangu umekulazimu baada ya kuwa Mtume (s.a.w.) amenitangaza na kuusia kuwa niwe Khalifa, bali kasema: "Hakika kuchaguliwa kwangu (na Masahaba) kumekulazimu (wewe) na mimi niko Madina nawe uko Sham (Syria)".

160 - Yaani (likubali jambo litakalokupa salama mbele ya viumbe wenzako duniani na mbele ya Allah huko akhera).

161 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 352-353. Pia barua hii kaiashiria Al-Tabari katika *Al-Taarikh* j. 6, uk. 293-294.

> *Bismi Allahi Al-rrahmani Al-rrahim*. Kutoka kwa mja wa Mwenyezi Mungu Ali, Kiongozi wa Waumini, kwenda kwa Mu'awiya bin Sakhr. Baada ya hayo! Ewe Mu'awiya! Unajua vyema kwamba *Shura*[162] ni ya Muhajirina na Ansaar pasina wengine. Wakikubaliana juu ya mtu wakamchagua kuwa ni Imamu basi hilo limekuwa ni lenye kumridhisha Allah. Akitoka katika jambo lao mwenye kutoka kwa kuponda au kwa bidaa basi wanamrejesha katika kile alichotoka kutoka katika kitu hicho. Na akikataa basi wamuue kwa sababu ya kufuata kwake njia isio ya Waumini.[163]

Na katika vitabu vya Kishia barua hio imekuja kwa lafdhi hii:

> Hakika *wamenibaii*[164] watu ambao wamewabaii Abu Bakr na Umar na Uthman kwa masharti yale yale *waliyowabaia* wao. Aliyekuwepo hakuwa na haki ya hiari na aliyekuwa hayupo hakuwa na haki ya kukataa. Hakika Shura ni ya Muhajirina na Ansar. Wakikubaliana juu ya mtu watakaemtaja kuwa ni Imamu, basi Mwenyezi Mungu analiridhia hilo. Akitoka katika jambo lao mwenye kutoka kwa kuponda au kwa bidaa basi wanamrejesha katika kile alichotoka kutoka katika hicho. Na akikataa basi wamuue kwa sababu ya kufuata njia isio ya Waumini.[165]

Barua ya mwanzo ilipomfika Mu'awiya, akamwambia yule mjumbe wa Ali: "Rudi kwa rafiki yako bila ya jawabu kwani mjumbe wangu yuko nyuma yako *Inshaa Allah"*.[166]

Na vitabu vyengine vinataja kwamba Mu'awiya baada ya kupata barua hizo alijibu:

> Naapa lau walikuchagua hao uliowataja nawe uko mbali na damu ya Uthman basi ungelikuwa kama Abu Bakr na Umar na Uthman; lakini wewe umewachochea Muhajirina (kumwaga) damu ya Uthman na ukawafanya Ansar wamuache mkono, basi mjinga akakutii na dhaifu

---

162 - Kushauriana juu ya nani awe Khalifa.

163 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 374. Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 309.

164 - Wameekeana ahadi na mimi ya kunitii kama ni khalifa wao.

165 - Nimeinukuu riwaya hii kutoka kwa Al-Musawi, *Al-Ttas-Hihu* uk. 20, naye kainukuu kutoka katika *Nahju Al-Balagha* j. 3, uk. 7.

166 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 353.

> akapata nguvu kwa sababu yako. Na watu wa Sham hawataki ila kukupiga vita wewe mpaka uwape waliomuua Uthman, ukifanya hivyo basi patafanyika shura (mashauriano) baina ya Waislamu…(wachague Khalifa upya).[167]

Ali naye akamjibu Mu'awiya:

> ……Ama kauli yako (uliposema): 'Nipe waliomuua Uthman, wewe hayo yamekuhusu nini? Na hapa wapo watoto wa Uthman nao ndio wenye kustahiki zaidi kwa hayo (ya kudai kisasi) kuliko wewe? Ukiwa unadai kwamba wewe una nguvu zaidi za kudai damu ya Uthman kuliko wao, basi rejea katika *kunibaii* (kuingia katika Ukhalifa wangu) ambao umekulazimu kisha niletee hao watu (waliomuua Uthaman).[168]

Hizo ni baadhi ya barua walizokuwa wakipelekeana viongozi wawili hao – Ali na Mu'awiya. Ama miongoni mwa ujumbe wa mdomo alioutuma Ali kwa Mu'awiya, ni ule ujumbe uliofikishwa na Bashir bin 'Amri bin Mihsan Al-Ansari, Said bin Qais Al-Hamdani na Shabath bin Rib'iy Al-Tamimi.[169] Watu watatu hao walitumwa na Ali kwenda kwa Mu'awiya, akawambia: "Muendeeni mtu huyu mumlinganie katika kumtii Allah na kuwatii Jamaa".[170] Mu'awiya akawambia: "Na mimi namlingania rafiki yenu (Ali) anipe waliomuua Uthman niwaue, kisha ajiuzulu ili pafanywe shura (upya)".[171] Cha muhimu, katika ujumbe huu, pia ikawa jawabu ya Mu'awiya si yenye kufurahisha; bali hakufahamiana kamwe na wajumbe hao na badala yake walirushiana maneno na Mu'awiya; na Mu'awiya

---

167 - Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 310.

168 - Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 310.

169 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* uk. j. 6, 301. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 636. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 23, lakini katika riwaya ya Ibn A'atham waliotumwa kwenda kwa Mu'awiya ni wawili tu: Bashir bin 'Amri bin Mihsan Al-Ansari na Said bin Qais Al-Hamdani. Pia Ali alimtuma Jarir bin Abdillahi Al-Bajali. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 65,72. Na alimtuma Dhumra bin Yazid na Amru bin Zaraara. Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 78, 84.

170 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 301. Al-Baladhiri katika *Al-Ansab* j. 3, uk. 84.

171 - Al-Baladhiri katika *Al-Ansab* j. 3, uk. 84. Kwa kweli maneno haya aliyokuwa akiyasema Mu'awiya yanatosha kuonesha kuwa Ukhalifa unathibiti kwa Shura na kwamba hakukuwa na andiko la Qur-ani wala Hadithi ya Mtume (s.a.w.) kwamba ukhalifa baada ya Mtume (s.a.w.) ni wa Ali au wa mwengine, vyenginevyo Ali mwenyewe na wafuasi wake wangeweza kumjibu Mu'awiya kwamba Khalifa hachaguliwi kwa Shura bali Allah na Mtume wake wameshamchagua.

akawafukuza na kuwambia: "Niondokeeni! Hakuna baina yangu na nyinyi isipokuwa upanga".[172]

LENGO LA MU'AWIYA

Kwa kweli – kama maandiko tafauti yanavyoonesha[173] – Mu'awiya alikuwa kaazimia kujitenga na kuunda Dola yake Sham (Syria), na kwa hivyo akakataa kuutii Ukhalifa wa Ali baada ya kuwa Waislamu – Masahaba Muhajirina na Ansari – wameshamchagua awe Khalifa wao. Lakini kilichowazi ni kuwa Mu'awiya alitumia tukio la kuuliwa kwa Uthman kama kisingizio[174] tu cha kutaka kujimegua kutoka katika Ukhalifa wa Ali.[175] Na kwa kweli Mu'awiya hakuwa na nia ya kutaka kuwaua waliomuua Uthman, hayo yanathibitishwa na alilolisema Ibn Taymiyya katika kitabu chake *Minhaju Al-Sunna*:

> Mu'awiya watu walikubaliana juu yake baada ya kufa Ali na akawa ni kiongozi wa Waislamu wote, na pamoja na haya hakuwaua waliomuua Uthman ambao waliasi. Na imesimuliwa kwamba alipopita Madina

172 - Al-Tabar, *Al-Taarikh* uk. 302. Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 23. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 637.

173 - Kama tutavyonukuu humu.

174 - Tunaita kisingizio kwani Mu'awiya mwanzo hakuwa na fikra hio kamwe, bali alipotakiwa kuingia katika Ukhalifa wa Ali, alimshauru mjanja wa Warabu, Amru bin Al-'Aas, naye akamshauru hivyo. Tazama Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 629. Al-Baladhir, *Al-Ansab* j. 3, uk. 73-74. Na kauli nyengine ni kuwa aliyetoa ushauri huo ni Shurahbil bin Al-Simt. Tazama Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 630. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 65. Na kwa hivyo, Shabath bin Rib-'i alimwambia Mu'awiya: "Hakika yako hukupata kitu cha kuwapotoshea watu na kuyavutia matamanio ya nafsi kwacho..ila kauli yako kwamba Imamu wenu (Uthman) kauliwa kwa dhulma na sisi tunadai damu yake. Basi wakakutii wajinga madhaifu. Na tumejua kwamba wewe hukumnusuru bali ulipenda auliwe kwa ajili (upate) hiki cheo unachokigombania**".** Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 636.

175 - Kwani Uthman alizingirwa huko Madina zaidi ya mwezi mmoja na akatuma ujumbe huko Sham kwa Mu'awiya ili aje amsaidie lakini si Mu'awiya wala si Amru bin Al-Aasi alikwenda kumnusuru Uthman!. Je huyu ndiye mtetezi wa Uthman? Bali Amru bin Al-'Aas kasemwa kuwa miongoni mwa waliohimiza kuuliwa kwa Uthman. Na hili haliko mbali kwa mtu kama Amru bin Al-'Aas hasa hasa ukizingatia ukweli kwamba tangu mwanzo Amru bin Al-'Aas alikuwa akimchukia Uthman kwa sababu alimuuzulu katika Uliwali (Ugavana). Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 6, uk. 162.

> kwenda Hija alisikia sauti katika nyumba ya Uthman (inaita): 'Ewe Amiri-L-Mu-uminin! Akasema (Mu'awiya): 'Nini hio?' Wakasema: 'Sauti ya binti wa Uthman anamlilia Uthman…akamuendea akamwambia: 'Watu wameshakubali kututii bila ya kupenda basi na sisi tumewafanyia upole juu ya chuki (zetu tulizonazo)…basi baada ya leo nisikusikie ukimtaja Uthman.[176]

Haya! Mbona Mu'awiya sasa hawahukumu hao waliomuua Uthman naye anao uwezo kamili kwani hatamu za dola ziko mikononi mwake? Hapa ukiyatazama maneno ya Sheikh Mu'awiya, utayakuta yanatoa tangazo la wazi kwamba yeye alikuwa akipigania Ufalme tu, na kwa hivyo madamu sasa kashaupata anamwambia binti ya Uthman: "Nyamaza wewe mtoto; usije ukaharibu mambo: ukaja kumuamsha aliyelala; sisi tunachokitaka tumeshakipata; wacha kumtaja Uthman huyo!"[177]

Na kwa hivyo vitabu vya historia vimeandika kwamba Mu'awiya alikuwa akidai kwamba yeye ndiye anayestahiki Ukhalifa. Anasema Ibn A'atham:

> Kisha Mu'awiya akawaelekea wafuasi wake akasema: 'Enyi watu! Hebu niambieni ni kwa jambo gani Ali bin Abi Talib kawa bora zaidi kwa jambo hili (la Ukhalifa) kuliko mimi? *Wallahi* mimi ni muandishi wa Mtume (s.a.w.), na dada yangu alikuwa chini ya Mtume (s.a.w.) na mimi ni *Liwali* (Gavana) wa Umar bin Al-Khattab na Uthman bin Affan….Na ikiwa yeye (Ali) kachaguliwa na watu wa Iraki[178] basi mimi nimechaguliwa na watu wa Sham, na hawa wote katika jambo (hili) ni sawa,[179] na anayeshinda kitu, basi huwa ni chake.[180]

---

176 - Ibn Taymiyya, *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 209.

177 - Halkadhalika kuna wakati Ali na Mu'awiya walifanya sulhu ya muda, Mu'awiya akasema kumwambia Ali: "Ukipenda yako iwe Iraki na yangu iwe Sham, na upanga uzuilike katika Umma huu wala tusimwage damu za Waislamu". Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 60. Je huyu ndio kweli anadai damu ya Uthman, au anadai kiti tu?!

178 - Sivyo hivyo Ewe Mu'awiya! Ali hakuchaguliwa na watu wa Iraki, bali kachaguliwa kwa makubaliano ya Masahaba watukufu, Muhajirina na Ansar huko Madina.

179 - *(Kalla thumma kalla Yaa Mu'awiya)* Hapana: si hivyo ewe Mu'awiya! Wachaguzi walikuwa ni Masahaba Muhajirina na Ansar na hawa wote *taqriban* walikuwa Madina na wote walimchagua Ali. Tena hata kama watu wa Sham wamekuchagua, basi walikuchagua baada ya kuwa Ali ameshachaguliwa kwa hivyo uchaguzi wao ni batili. Bali wengine wanasema kwamba watu wa Sham hawakukuchagua wewe kuwa Khalifa ila baada ya kumalizika vita vya Siffin na kudhoofika kwa utawala wa Ali baada ya

Wakati katika kikao hiki Mu'awiya anawashawishi watu namna hii, utaona kwamba katika vikao vyengine alivyokutana na watu wa upande wa Ali – au barua zake kwa Ali mwenyewe[181] – alikuwa akijifanya kwamba yeye hana anachokitaka isipokuwa watolewe waliomuua Uthman na baada ya hapo ataingia katika kumtii Ali. Inasema riwaya ya Ibn A'atham ikimnukuu Mu'awiya:

> ..Lakini mimi napigana hadi anipe waliomuua Uthman, akifanya hivyo basi mimi nitakuwa ni mmoja wa Waislamu (wa kawaida tu) nitaingia katika ule (utiifu) walioingia watu (wengine) katika huo.[182]

Hapa utaona kwamba kuna ujanja wa wazi: kule Mu'awiya anawalingania watu kuwa wamfanye yeye kuwa ndiye Khalifa na kwamba yeye na Ali ni sawa sawa; huku hataki jengine ila kutolewa kwa waliomuua Uthman! Lakini mshauri mkuu wa Mu'awiya, anaweka wazi lengo lao kwa kumwambia Ammar bin Yasir huko *Siffin:* "..Na murejee mulikotoka na mutuachie yale yaliyo mikononi mwetu"[183] yaliyo mikononi mwao ni utawala wa Sham, na kwa hivyo: "Mutuachie utawala wetu wa Sham". Na mfano wa maneno hayo ya Amru bin Al-'Aas, ni maneno ya Utba bin Abi Sufyaan, ndugu yake Mu'awiya bin Abi Sufyaan, aliyomwambia Ja'ada bin Hubaira, mfuasi wa Ali:

> Sisi *Wallahi* hatudai kwamba Mu'awiya ni mwenye kustahiki zaidi Ukhalifa kuliko Ali lau si habari yake katika (damu ya) Uthman; lakini Mu'awiya ni mwenye kustahiki zaidi (Ukhalifa wa) Sham kwa kuridhika (naye) watu wake (watu wa Sham), mwambie mjomba wako atuachie sie hio (Sham).[184]

---

kurudi kwake katika vita vya Nahrawaan na kufanyiwa khiyana na jeshi lake la Al-Kufa. Ama kabla ya hapo watu wa Sham walikuchagua kufa na kupona ili uwe kiongozi wao katika vita dhidi ya Ali tu: si uwe Khalifa. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 82,103.

180 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 428.

181 - Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 67.

182 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 94. Na mfano wake ni riwaya ya Al-Baladhiri katika *Al-Ansab* j. 3, uk. 66. Na mara nyengine akiongeza sharti kuwa aachwe kwenye Uliwali wake wa Sham. Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 78.

183 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 126.

184 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 177.

Hatimae tunamuona Mu'awiya mwenyewe anathibitisha hilo katika barua yake aliyompelekea Ali akisema:

> Na nilikuwa nimekuomba (unipe) Sham kwa sharti kwamba usinilazimishe kukutii (wewe) wala (usinilazimishe) jukumu lolote, (lakini) ukanikatalia.[185]

Na akasema Shurahbil, mjumbe wa Mu'awiya, kumwambia Ali:

> ..Na tumeona ewe Aba Al-Hasan (Al-Imamu Ali) kwamba uondoke (hapa vitani *Siffin)* wewe na walio pamoja nawe, tukuachie Iraki yako na Hijaz yako na utuachie Sham yetu... [186]

Baada ya jawabu za namna hii za Mu'awiya na wakuu wa serikali yake, na kufeli kwa majaribio yote ya Ali ya kujaribu kulitatua tatizo hilo kwa njia za kidiplomasia, ikawa imemthibitikia Al-Imamu Ali kwamba sasa kweli kuna sehemu ya Waislamu imeasi. Kama kuna sehemu ya Waislamu imeasi, je ufumbuzi ni nini? Ikawa hakuna ufumbuzi isipokuwa ule ule uliotangazwa na Qur-ani kwamba:

وَإِنْ طَائِفَتَانِ مِنْ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا فَإِنْ بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَى فَقَاتِلُوا الَّتِي تَبْغِي حَتَّى تَفِيءَ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ

> **Na ikiwa makundi mawili ya Waislamu yatapigana, basi fanyeni sulhu baina yao, ikiwa moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah.**[187]

Hatua za mwanzo za sulhu – kama ulivyoona – zikawa zimeshindikana, ikawa hakuna kilichobaki ila kuingia katika hatua ya pili, nayo ni: **"Ikiwa kundi moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah."**

---

185 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 259.
186 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 286.
187 - Sura ya 49, Aya 9.

KUANZA KWA VITA VYA SIFFIN

Hapo – baada ya vitangulizi hivyo – basi – katika siku ya Jumatano[188] ya Mfunguo tano mwaka 37 A.H.,[189] – vikaanza vita hivyo vya *Siffin* vilivyopiganwa baina ya Al-Imamu Ali na wafuasi wake wa Iraki wakiwemo Masahaba Muhajirina na Ansar kwa upande mmoja; na Mu'awiya bin Abi Sufyaan na wafuasi wake wa Sham (Syria) kwa upande wa pili. Vita hivyo, vilitanguliwa na vita vya hapa na pale vilivyoanza – kwa mara ya kwanza – baina ya kikosi cha utangulizi cha Ali kilichokuwa chini ya uongozi wa Malik bin Al-Harith Al-Ashtar na kikosi cha Mu'awiya kilichokuwa chini ya uongozi wa Abu Al-A'awar Al-Sulami.[190] Katika vita hivi vya kwanza, jeshi la Mu'awiya lilikimbia usiku; na jeshi la Ali lilipopambazukiwa na asubuhi hawakukuta mtu: jeshi lote la Mu'awiya likawa limeshakimbia.[191] Kabla ya hapo Ali – pamoja na sehemu nyengine ya jeshi lake – alikuwa bado hajafika katika eneo hilo la vita. Asubuhi ndio Ali akafika na akamuamuru amiri jeshi wake, Malik bin Al-Harith Al-Ashtar, aondoke na kikosi chake cha utangulizi kuelekea *Siffin* alikokuwa Mu'awiya.[192]

Wakaondoka kama Ali alivyowaamuru na walipofika Siffin, wakamkuta Mu'awiya tayari ameshafika hapo na ameshaitwaa sehemu muhimu iliyokuwa na maji ya kunywa[193] na akakataa Mu'awiya kuliruhusu jeshi la Ali kuchota maji. Washauri wa Mu'awiya walimwambia kwamba tusiwaruhusu wafuasi wa Ali kunywa maji:

---

188 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 307. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 516.

189 - Al-Ya'aqubi, *Taarikh Al-Ya'aqubi* j. 2, uk. 188. Al-Mas'udi, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 272. Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 85.

190 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 297-298. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 634. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 81.

191 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 298. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 634.

192 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 298.

193 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 514. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 81. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 299.

> Wanyime maji kama walivyomnyima Uthman! Walimzingira kwa muda wa siku arubaini bila ya (kumpa) ubaridi[194] wa maji wala chakula kizuri. Waue kwa kiu; Allah awajaalie wafe kwa kiu.[195]

Na mwengine akasema: "Allah awanyime maji siku ya kiama".[196] Mu'awiya – baada ya kusomewa mashairi – akaikubali rai hii na akasema:

> *Wallahi* rai ni hii unayosema wewe….Allah amjaaliye Mu'awiya na baba yake wasinywe (maji) katika Hodhi la Muhammad (siku ya kiama) ikiwa Ali au wafusi wake watakunywa maji ya (mto) Furat milele labda washinde (vita).[197]

Hapa vilianza vita vya pili[198] vinavyojulikana katika historia kuwa ni *Al-Qitalu 'Alaa Al-Maai* (Vita vya Maji),[199] na baada ya kupiganwa vita hivyo kwa muda wa masaa tu, jeshi la Ali likashinda na likaweza kuyaweka maji mikononi mwake, na Ali – tafauti na Mu'awiya – aliwaruhusu watu wa Mu'awiya kunywa maji katika sehemu hio.[200]

Kisha – katika mwezi mzima wa mfunguo tatu wa mwaka huo wa 37 A.H. – ikawa kuna vita vya kila siku lakini si vile vita vya kuingiana kwa pamoja, bali ilikuwa ni vita vya kikundi kimoja kutoka upande wa Ali na chengine kutoka upande wa Mu'awiya; na wakati mwengine hupigana kwa ule mtindo wao wauitao *Al-Mubaraza* nao ni mtu mmoja kutoka upande huu na mwengine kutoka upande wa pili kisha wakapigana. Ilipoingia mfunguo nne, vita vilisimamishwa. Riwaya ya Ibn A'atham

---

194 - Hii ni ibara ya Kiarabu na maana ni "Walikataa kumpa maji". Wametumia neno "ubaridi" kwa sababu kawaida ya maji ya kunywa hayawi maji ya moto, bali ni maji baridi.

195 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 301. Na mfano wake ni katika Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 2, na Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 635. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 81.

196 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 2. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 635.

197 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 2.

198 - Navyo ndio vya kwanza kupiganwa katika eneo la Siffin.

199 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 299. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 2. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 514-515. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 635.

200 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 301. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 15, na j. 3, uk. 23. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 635. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 82.

inaonesha kwamba wakati Ali alizuia mashambulizi yake katika mwezi wa mfunguo nne ili kuheshimu utukufu wa mwezi huo, Mu'awiya hakufanya hivyo.[201] Lakini kwa mujibu wa riwaya ya Al-Tabari,[202] Ibn Al-Athir[203], Al-Mas'udi[204] na Al-Baladhiri,[205] ilipoingia mfunguo nne walikubaliana – watu wa pande mbili – kusimamisha vita; na mara tu baada ya kuingia mfunguo tano Ali akamtaka tena Mu'awiya na kundi lake kuwa warejee katika haki, lakini ikawa hakuna jawabu kutoka kwa Mu'awiya isipokuwa kuanza kupanga jeshi lake na kusema: "Baina yetu na nyinyi ni upanga tu au aliye dhaifu baina yetu aangamie";[206] na ilipofika siku ya Jumatano ya Mfunguo tano mwaka 37 A.H., ndio vikaanza vita vikuu vya *Siffin*, ambapo Ali alisema siku moja kabla, yaani siku ya Jumanne: "Hadi lini tutakuwa hatusimami nao watu hawa kwa pamoja?".[207] Hapo Ali akaanza kuandaa jeshi lake kwa ajili ya vita vya pamoja[208] na siku ya pili yake (Jumatano) vikaanza vita hivyo vikali vya *Siffin.*[209]

KUULIWA KWA SAHABA AMMAR BIN YASIR (R.A.)

Katika vita hivi, Sahaba Ammar bin Yaasir (r.a.) – ambaye alikuwa katika jeshi la Ali – aliuliwa.[210] Hapo watu wakapaza sauti wakisema: "Sahaba wa Mtume (s.a.w.) kauliwa na Mtume (s.a.w.) kasema: 'Ammar atauliwa na kundi la waasi".[211] Ninasema: hili alilolisema Mtume (s.a.w.)

---

201 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 31.
202 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 5, uk. 303.
203 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 637.
204 - Al-Mas'ud,i *Al-Muruj* j. 2, uk. 516.
205 - Al-Baladhir,i *Al-Ansab* j. 3, uk. 84.
206 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 516.
207 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 308 Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4,uk. 647.
208 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 308. Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 647.

209 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 5, uk. 309. Ibn Abdi Rabih *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 647-648.
210 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 5, uk 325.
211 - Al-Ya'aqubi, *Taarikh Al-Ya'aqubi* j. 2, uk. 188. Riwaya hii inatoa ushahidi tosha kwamba Mu'awiya na kundi lake walikuwa *Bughat* (Waasi). Cha kustaajabisha ni kuwa hadi leo hii watu wakimtaja Mu'awiya husema "*Radhiya Allahu 'Anhu*"! (Allah amuwiye radhi)! Sasa Allah amridhie nini: amridhie huo uasi wake aliousema Mtume (s.a.w.)

pekee, lilitosha kutoa jawabu ya kuwa nani aliyekuwa katika haki baina ya Ali na Mu'awiya. Bali Hadithi hii inayosema: "Ammar atauliwa na kundi la waasi" au "Kundi la madhalimu" ilikuwa ni mashuhuri kiasi cha kwamba hata Mu'awiya mwenyewe alipokumbushwa kwayo na sahibu yake Amru bin Al-'Aas,[212] basi hakuweza kuipinga lakini aliipotoa maana ya Hadith hio na kusema: "Waliomuua ni wale waliomleta vitani".[213] Lakini Ali akamjibu[214] kwamba basi: "Na Mtume (s.a.w.) kamuua Hamza kwani yeye ndiye aliyempeleka vitani".[215] Na lafdhi nyengine ya riwaya hii inamnukuu Ali akisema: "Na sisi tumemuua Hamza kwani ndio tuliomtoa (kwenda vitani)". [216]

Baada ya kuuliwa Ammar, wakaja watu wawili wanazozana kila mmoja anadai kuwa yeye ndiye aliyemuua.[217] Amru bin Al-'Aas akasema: "Wanagombana kwenye moto".[218] Mu'awiya akamwambia: "Unawaambia haya watu waliozitolea nafsi zao kwa ajili yetu".[219] Amru akamjibu: "Wallahi ndio hivyo hivyo nawe unajua!".[220]

---

katika Hadithi *mutawatir!* Hebu tujifungue pingu za umadhehebu na tufate ushahidi wa Qur-ani na Hadithi. Mtume (s.a.w.) anamwita mtu ni muasi; wewe unasema ni mtu mwema! Riwaya hio ya uasi wa Mu'awiya imepokewa na wapokezi wengi kama vile *Sahihu Muslim* j. 9 katika *Sharhu Al-Nawawiy* uk. 172-173, Hadithi na.70_2915, na 72_2916 na 73_2916. Na Al-Bukhari *Sahihu Al-Bukhari* Hadithi na. 447. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 93.

212 - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 268.

213 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk 326. Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 268. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 663. Ibn Kathir, *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya* j. 7, uk. 265,266,267. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 7, uk. 95. Al-Hakim katika *Al-Mustadrak* j. 3, uk. 436, Hadithi na. 5659-5660.

214 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 268. Ibn Taymiyya, *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk.208. Riwaya zinakhitalifiana juu ya nani katoa jawabu hii. Katika riwaya nyengine kama riwaya ya Ibn A'atham katika *Al-Futuh* j. 3, uk. 268, tunapata kwamba aliyesema maneno hayo ni Abdullahi bin Amri bin Al-'Aas; wakati riwaya nyengine kama riwaya ya Ibn Abdi Rabih katika *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 319, msemaji wa maneno hayo ni Ali. Nadhani (sina hakika) niliwahi kuona katika baadhi ya vitabu kwamba maneno hayo yakinasibishwa na Ibn Abbaas. *Wa Allahu A'alam.*

215 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 268.

216 - Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 319.

217 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 92.

218 - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 92.

219 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 92.

220 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 92.

KUNYANYULIWA KWA MISAHAFU NA KUGAWANYIKA KWA JESHI LA ALI

Baada ya vita hivyo kudumu kwa siku nyingi, na *taqriban* kila siku ushindi ukawa unakwenda kwa Ali na jeshi lake la Iraki, Mu'awiya na Amru bin Al-'Aas wakaona sasa wanaelekea kushindwa moja kwa moja, na kwa hivyo, iliwabidi watafute mbinu ya kulibomoa jeshi la Ali. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kutaka kumuhadaa Ibn Abbaas ili amshawishi Ali asitishe vita, lakini Amru bin Al-'Aas akamwambia Mu'awiya kwamba njama hii haiwezi kufaulu kwani Ibn Abbaas si mtu wa kuhadaiwa. Hata hivyo, Amru bin Al-'Aas alifanya jaribio la kumpelekea Ibn Abbaas barua, lakini jawabu aliyoipata ilimkatisha tamaa.[221]

Vita vikawa vinaendelea na baada ya masiku ikawa sasa hakika Al-Imamu Ali na jeshi lake wanashinda vita hivyo, hasa hasa katika vita vinavyoitwa katika historia kuwa ni *Al-Waqia Al-Khamisiyya*[222] yaani "*Tukio la Alkhamisi*", pamoja na tukio la usiku wake – yaani usiku wa kuamkia Ijumaa – linaloitwa kuwa ni *Lailatu Al-Harir* yaani "*Usiku wa Vishindo"*,[223] ambao inasemakana kwamba walikufa watu wengi kupita kiasi ambapo Ali pekee – inasemekana – aliua watu mia tano na ishirini na tatu[224] na jumla ya waliokufa katika usiku huo mmoja ilifikia watu

221 - Tazama maelezo haya na barua hio na majibu yake katika Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 249-252.

222 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 293.

223 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 326-329. Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 322. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 666. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 303. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 7, uk. 95. *Al-Harir* – kwa mujibu wa kamusi la Kiarabu – ni sauti ya mvumo wa upinde pia ni sauti ya mbwa anapotoa sauti bila kubweka, hivyo ndivyo ilivyoelezwa katika kamusi, lakini kwa Kiswahili inaelekea zaidi kuuita usiku huo kuwa ni usiku wa vishindo kuliko kuuita usiku wa sauti.

224 - Tazama Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 305. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 524. Usahihi wa idadi hii ni jambo la kufikiriwa. Na vita vyote vya Siffin inasemekana viliondoa roho za watu elfu sabiini. Tazama Al-Mas'udi ,*Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 498. Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 319.

thalathini na sita elfu.[225] Mu'awiya ikabidi atake ushauri kutoka kwa mshauri wake mkuu, Amru bin Al-'Aas, akasema Mu'awiya:

> Ewe Aba Abdillahi! Ziko wapi hila zako nilizokuwa nikizijua! Amru (bin Al-'Aas) akasema: 'Unataka nini?' (Mu'awiya) akasema: 'Ninataka uvisimamishe vita hivi kwani watu wa Sham wameteketea sana, kwani mimi nina hakika kwamba vita hivi vikidumu leo, basi hatobaki mtu yeyote mwenye kubeba silaha katika ardhi ya Sham.[226]

Na akasema Mu'awiya kumwambia Amru bin Al-Aas: "Iko wapi hakiba yako uliyoilimbika ewe Ibn Al-'Aas: tumeangamia na ikumbuke Misri".[227] Amru bin Al-'Aas, sahibu wa Mu'awiya, akasema kumwambia Mu'awiya kile tulichokinukuu kabla:

> Je nikuoneshe jambo ambalo halitotuzidishia sisi ila umoja na halitowazidishia wao ila mfarakano? Akasema (Mu'awiya): 'Ndiyo". Akasema (Amru bin Al-'Aas): Tunyanyue Misahafu kisha tuseme: 'Kilichomo humu ndio hukumu baina yetu na nyinyi'. Ikiwa kuna baadhi yao watakataa basi utawapata wengine watasema: 'Ndiyo inatupasa tukubali', na hapo patatokea mfarakano baina yao. Na wakisema (wote): 'Ndiyo' tutajiondoshea vita hivi mpaka baada ya muda.[228]

Na katika riwaya nyengine, Amru bin Al-'Aas anasema: "Tunyanyue Misahafu katika vichwa vya mikuki"[229] ikiwa kama ni ishara ya kutaka sulhu "Hakika yako ukifanya hivyo hakuna atayempiga mwenzake"[230] na akasema Amru: "Haikubakia ila hila moja tu: unyanyue Misahafu ili

---

225 - Idadi hii sidhani kama ina ukweli. Tazama Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 305.

226 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 305.

227 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 524. Maneno "Na ikumbuke Misri" maana yake ni kuwa Mu'awiya alitaka msaada wa Amru bin Al-'Aas katika vita hivi. Amru akamwambia Mu'awiya kwamba mimi natoa dini yangu kwa dunia: je utanipa nini? Akamwambia Misri itakuwa ***kula*** yako, yaani nitakufanya kuwa Liwali wa kudumu wa Misr! Tazama Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 499,532. Tazama pia Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 319. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 707. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 71,74.

228 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 5, uk. 329-330. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 667. Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 103.

229 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 305. Al-Ya'aqubi, *Taarikh Al-Ya'aqubi* j. 2, uk. 188.

230 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 306.

kulizuia jeshi la Ali na kulivunja nguvu zake"[231] Hapo amri ya kunyanyua Misahafu ikatolewa, na mmoja wa wafuasi wa Mu'awiya akakaa baina ya majeshi mawili, kisha akafungua Msahafu na kusoma Aya hizi:[232]

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيباً مِنْ الْكِتَابِ يُدْعَوْنَ إِلَى كِتَابِ اللَّهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ يَتَوَلَّى فَرِيقٌ مِنْهُمْ وَهُمْ مُعْرِضُونَ (آل عمران 23)

> **Huwaoni wale waliopewa (kufahamu) sehemu ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu. Mayahudi na Manasara) wanaitwa kukiendea Kitabu cha Mwenyezi Mungu ili kiwahukumu (haki) baina yao; kisha taifa moja miongoni mwao hukengeuka[233].**

وَإِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ مُعْرِضُونَ (48) وَإِن يَكُنْ لَّهُمُ الْحَقّ يَأْتُوا إِلَيْهِ مُذْعِنِينَ (49) أَفِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ أَمِ ارْتَابُوا أَمْ يَخَافُونَ أَن يَحِيفَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَرَسُولُهُ بَلْ أُوْلَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ (50) إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَنْ يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأُوْلَئِكَ هُمْ الْمُفْلِحُونَ (النور48-51)

> **Na wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili awahukumu baina yao; baadhi yao wanayakataa hayo (wanapohisi kuwa wao ni madhalimu, hawatapata kitu).**Na kama ikiwa haki ni yao, wanamjia (upesi Mtume) kwa kutii.**Je, wana maradhi katika nyoyo zao, au wanaona shaka, au wanaogopa ya kuwa atawadhulumu Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Bali hao ndio madhalimu.**Haiwi kauli ya Waislamu wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila kusema: 'Tunasikia na tunakubali," na hao ndio watakaofuzu.**[234]

Hizo ndizo Aya alizozisoma mfuasi huyo wa Mu'awiya kuonesha kwamba madamu Mu'awiya sasa anataka sulhu basi ni wajibu wa Waislamu waukubali wito wake. Lakini – kama unavyoona – Aya hizi hazileti maana ya kuhalalisha usimamishaji wa vita dhidi ya *Bughat* (waasi au rebels), kwani Aya zinahimiza kuwa watu wafuate Kitabu cha Allah

---

231 - Al-Ya'aqubi, *Taarikh Al-Ya'aqubi* j. 2, uk. 188.

232 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 308. Na mfano wake ni katika Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 736, riwaya na. 34, lakini yeye Aya za pili hakuzitaja.

233 - Sura 3, Aya 23. *Tarjama* ya: Sheikh Abdullahi Salih Al-Farisi.

234 - Sura 24 Aya 48-51. *Tarjama* ya Sheikh Abdullahi Salih Al-Farisi.

tu; na wala hazitoi ufafanuzi wenye kutoa ufumbuzi juu ya khilafu hizo zilizotokea. Kwa hivyo, Aya zinahimiza tufuate Kitabu cha Allah. Na tukirudi katika Kitabu cha Allah tunakutana na Aya isemayo:

> **Na ikiwa makundi mawili ya Waislamu yatapigana, basi fanyeni sulhu baina yao, ikiwa moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah.**[235]

Kundi la Mu'awiya limeasi – baada ya kufeli njia zote za sulhu – na kwa hivyo, kwa mujibu wa Kitabu cha Allah kimeamrisha kulipiga vita kundi hilo mpaka likubali kurudi katika haki au liuliwe.[236]
Kwa ufupi ni kuwa, kufuatia amri ya Mu'awiya, Misahafu ikanyanyuliwa, na – kama alivyotarajia Amru bin Al-'Aas iwe, ikawa – jeshi la Ali likatafautiana baina ya waliotaka kusimamishwa vita na waliotaka vita viendelee.

Al-Imamu Ali bin Abi Talib – kwa upande wake – akawa ameshajua kwamba hilo la kunyanyuliwa Misahafu halikuwa na ukweli wowote ndani yake, bali ilikuwa ni mbinu tu,[237] na kwa hivyo akasema kuliambia jeshi lake:

> Endeleeni katika (kuipigania) haki yenu na (endeleeni na) ukweli wa kumpiga adui yenu, hakika Mu'awiya na Amru bin Al-'Aas na Ibn Mu'ait na Habib bin Maslama na Ibn Abi Sarh na Al-Dhahhak bin Qais si watu wa dini wala wa Qur-ani; mimi nawajua zaidi kuliko nyinyi: nimefuatana nao tangu tuko watoto; na nyinyi mumefuatana nao baada ya kuwa ni watu wazima, basi walikua ni watoto washari walioje na (walipokua watu wazima wamekua) ni watu wazima washari walioje! E nakuhurumieni! Hakika yao hawakuinyanyua (hio

---

235 - Sura ya 49, Aya 9.

236 - Na hivi ndivyo walivyoifahamu Masahaba Aya hii, kwamba ndio yenye kutoa amri ya kuwapiga waasi. Na kwa hivyo, Ibn Umar (r.a.) baada ya kujuta kwanini hakushiriki katika vita vya Ali dhidi ya Mu'awiya, na akaja mtu kumuuliza kuhusu Aya hio, Ibn Umar alisema: "Sijapata kuumia katika nafsi yangu kutokana na jambo la Umma huu kama nilivyoumia kwa sababu sikupigana na kikundi hiki cha waasi kama Allah alivyoniamrisha". Al-Bayhaqi,: *Al-Kubra* j. 12, uk. 328-329, riwaya 17173.

236 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 307. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 516

237 - Ibn A'atham, katika *Al-Futuh* j. 3, uk. 319.

Misahafu) wala hawainyanyui wala hawakitendei kazi kilichomo ndani yake, na wala hawakuinyanyua ila ni hadaa na ujanja na mbinu tu.[238]

Na hapa ndoto za Amru bin Al-'Aas zikawa sasa zimethibiti katika ulimwengu wa hakika: jeshi la Ali likafarikiana baina ya waliokubali pendekezo hilo na waliolipinga.

إلى أن علت فوق الرماح مصاحفونادوا إلى حكم الكتاب نصيـــــــرُ**
مكيدة عمرو حـــيث رثت حبالهاوكادت بحور القاسطين تغـــــورُ**
أبا حسن ذرها حكومة فاسقجراحات بدر في حشاه تفـــــــــورُ**
أبا حســـــن أقدم فأنت على الهـــدىوأنت بغايات الغوي بصيرُ**
أبا حســـن لا تعطين دنـــــيةوأنت بسلطان القدير قديـــــرُ**
أبا حســـــــن لا تنس أحدا وخندقاوما جر عير قبله ونفيـــرُ**
أبا حســـــــن أين السوابــق غودرتوأنت أخوه والغدير غديرُ**
أبا حســـــــن إن تعطها اليوم لم تزليحل عراها فاجــر ومبيرُ**
أبا حســـــن طلقتها لطليقهاوأنت بقيد الأشعري أسيـــــرُ**[239]

JE NI NANI KATIKA JESHI LA ALI ALIYETAKA VITA VISITISHWE NA PAFANYIKE SULHU?

HOJA SABA ZA WAZI

238 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 330. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 667. Ibn Abi Al-Hadid, *Sharhu Nahji Al-Balagha* j. 2, uk. 408. Na mfano wake – pamoja na kuwepo tafauti ndogo katika baadhi ya sehemu – ni riwaya ya Ibn A'atham katika *Al-Futuh* j. 3, uk. 319, na Al-Mas'udi katika, *Al-Muruj* j. 2, uk. 525.

239 - Mashairi ya Al-Imamu Al-Rabbaani, Sha'iru Al-'Arab Sheikh Abu Muslim Al-Bahlani Al-Rawahi (r.a.), mwanachuoni wa Zanzibar. Alizaliwa Oman na kuja Zanzibar akiwa na umri kati ya miaka 18-20. Alikuwa ni bingwa wa Fiq-hi, mashairi na fani nyengine na alikuwa mcha Mungu sana na mwenye karama za kupigiwa mfano. Allah amueke katika Firdaws ya juu. *Amin!*

HOJA NA. 1: KUGONGANA KWA RIWAYA MBILI NA PIA KUGONGANA KWA RIWAYA NA MSIMAMO WA WATETEZI WA ALI

Baada ya hayo ni vyema tujue ni nani hasa katika jeshi la Ali aliyetaka vita visitishwe na pafanyike sulhu. Watu wengi huwa wanadai kwamba *Khawarij* ndio waliotaka pafanyike sulhu kisha wakageuka na kumlaumu Ali kwa jambo hilo na kujitenga naye. Watu hawa ni wale ambao wana tabia ya kutokuchunguza vyema yale wanayoambiwa na kwa hivyo hulipokea kila wanalolisikia au kulisoma. Sasa kwa ufupi ni kuwa hapa riwaya zinagongana kuhusu nani katika jeshi la Ali alikubali kusimamishwa kwa vita na kusisitiza kuwepo kwa sulhu; wakati kuna riwaya ya Al-Tabari inayosema:

> Akasema Mis'ar bin Fadaki Al-Tamimi na Zaid bin Husain Al-Tai pamoja na kikundi pamoja nao wakiwemo *Al-Qurraa* (Wasomi) ambao baadae walikuwa *Khawarij* (kumwambia Ali)*:* 'Ewe Ali itika (wito wa) Kitabu cha Allah Mtukufu ulipoitwa katika hicho, vyenginevyo tutakutupilia mbali kwa hao jamaa (Mu'awiya na jeshi lake) au tutakufanya kama tulivyomfanya (Uthman) bin Affan.[240]

Wakati Al-Tabari anasimulia riwaya hio, basi Al-Imamu Ahmad bin Hanbal, Ibn Abi Shaiba, Al-Minqari na Abu Ya'ala wanasimulia riwaya nyengine iliotafauti na hio. Riwaya ya Ahmad na wenzake inasema:

> ….Wakaja *Al-Khawarij* na sisi wakati huo tulikuwa tukiwaita *Al-Qurraau* (Wasomi),[241] na panga zao ziko mabegani mwao, wakasema: 'Ewe Amiri Al-Mu-uminin (Kiongozi wa Waislamu) tunawasubiria

[240] - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 330, na j. 6, uk. 3. Ibn Abi Al-Hadid, *Sharhu Nahji Al-Balagha* j. 2, uk. 408. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 312. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 525.

[241] - Na hii ni tafauti na jeshi la Mu'awiya ambalo halikuwa na wanavyuoni. Anasema Ali (k.w.): "Piganeni na wenye makosa, wapotovu, waovu ambao si wasomi wa Qur-ani wala si wanavyuoni wa Fiq-hi wala si maulamaa wa *Ta-wili* (tafsiri ya ndani)". Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 330, na j. 6, uk. 21. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 689.

> nini hawa watu walio mlimani: hatuwaendei na panga zetu mpaka Mwenyezi Mungu akahukumu baina yetu na baina yao.[242]

Jambo hili la kuwepo kwa riwaya mbili hizi zenye kugongana, limewapelekea watu kuwa na maamuzi tafauti na kufikia natija (conclusion) na misimamo tafauti. Lakini – kama Allah alivyoamuru kwamba – "***Akikujieni fasiki na habari basi ihakikisheni".***[243] Wajibu wa Muislamu anapopewa habari yoyote ile iwayo: ikiwa ni ya kidini au ya kidunia, basi kwanza ni kutaka kuihakikisha ukweli wake. Riwaya mbili hizi – baada ya kuzichunguza *matn* na *sanad* zake – basi utastaajabu wewe kwanini watu wasikubaliane kuiwacha riwaya ya kwanza ya Al-Tabari na kushikamana na riwaya ya pili ya Ahmad na wenzake. Riwaya ya kwanza ya Al-Tabari – mbali na udhaifu wa *sanad* yake, basi – kwa mujibu wa *matn* yake ilitakiwa isikubaliwe na Sunni wala Shia, kwani kama unavyoona kwamba riwaya hio inasema kwamba *Al-Khawarij* walimwambia Ali akubali sulhu "…au tutakufanya kama tulivyomfanya (Uthman) bin Affan", na riwaya ya Ibn A'atham inasema: "Ewe Ali wewe unajua kwamba sisi hakika tulimuua Uthman alipotushinda na kutukatalia kukifuata kilichomo katika Kitabu cha Allah"[244], na hii ina maana kwamba Ali alikuwa kweli ni katika waliomuua Uthman au kwa uchache basi alikuwa anawajua waliomuua Uthman: kwa hali zote mbili madamu watu hawa wameyasema haya kumwambia Ali naye hakuchukua hatua yoyote, ina maana kuwa naye yumo katika waliomuua au aliridhia kuuliwa kwake, na yote haya Kisuni na Kishia hayakubaliki.[245] Kwa hivyo, riwaya hio ilitakiwa isipate nafasi kabisa katika ulimwengu wa Kiislamu. Lakini kwa bahati mbaya, kwa vile watu wengi huwa hawazitafakari vyema habari zilizomo katika vitabu, basi wanapoona riwaya inayokubaliana na itikadi yao huikimbilia haraka haraka hata kama udhaifu wake uko wazi kiasi gani. Na hii si tabia ya

---

242 - Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 736, riwaya na. 34. Ahmad, *Al-Musnad* j. 5, uk. 484, Hadithi na. 16071. Na akainukuu Al-Sabi'i kutoka kwa Al-Minqari *Siffin* uk. 497 na Abu Ya'ala, *Al-Musnad* j. uk. 365.

243 - Sura 49, Aya 6.

244 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 312.

245 - Uchambuzi huu hapa unamfaa Suni na Shia tu: si Ibadhi; ama Ibadhi wao wanaamini kuwa Ali alikuwa akiwajua waliomuua Uthman naye aliridhika na tukio hilo. Na humu katika kitabu hiki utapata ushahidi wa kutosha juu ya kauli hii.

mtu anayetafuta ukweli: mtu anayetafuta ukweli huutafuta hata ukiwa ukweli huo ni dhidi yake au dhidi ya kipenzi chake.

Jambo jengine la kutazamwa hapa ni kuwa wakati Al-Tabari – kwa njia ya Abu Mikhnaf – anasimulia riwaya hio ya kuwa watu wa Al-Nahrawaan ndio waliomtaka Ali asimamishe vita na akubali sulhu; tunakuta kwamba Al-Tabari huyo huyo anasimulia riwaya nyengine – kwa njia hio hio ya Abu Mikhnaf – baada ya Ali kuwakumbusha wale walioitwa *Khawarij* kwamba wao ndio waliomtaka asimamishe vita na kufanya sulhu na kwamba yeye alikuwa halitaki jambo hilo, walimjibu sawa: "Lakini hio ilikuwa ni kufuru kutoka kwetu, basi sisi tumetubia kwa Allah Mtukufu, nawe tubia ili tukubaii (tukuchague tena kuwa Khalifa wetu)".[246] Na katika riwaya ya Al-Mubarrad, tunapata kwamba wao baada ya kuambiwa hivyo na Ali, walimjibu:

> Umewafanya (watu) wahukumu katika dini ya Allah kwa sababu ya rai yetu? Basi sisi tunakiri kwamba tumekufuru na sisi tunatubia, basi kiri kama tulivyokiri sisi na utubie (kama tulivyotubia sisi) tuondoke pamoja nawe kwenda Sham (kupigana na Mu'awiya).[247]

Na katika riwaya ya Al-Baladhiri watu hao wa Nahrawaan walimwambia Ali:

> Hakika umesema uliyoyasema, na kwa hakika yule ambaye alimili katika sulhu miongoni mwetu ametubia na kuwafanyia usawa wao kwa kuitupilia mbali na kusimamisha vita, basi ukitubu (sisi tuko pamoja nawe) vyenginevyo tunajitenga nawe.[248]

Kwa hivyo, ikiwa tutatolea hoja riwaya hizi za Al-Tabari alizozisimulia kutoka kwa Abu Mikhnaf kutoka kwa Abdul-Rahman bin Jundub Al-

---

246 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13, na uk. 25. Hata Ali mwenyewe kwa mujibu wa riwaya hizi kakiri kwamba kukubali sulhu ni kufuru kama tutavyozinukuu riwaya hizo baadae chini ya kichwa kisemacho**: *KUWAITA WAISLAMU MAKAFIRI***. Kwa mantiki hii, watu wa Nahrawaan walipotubia – kama riwaya inavyonena – na kumtaka naye atubie ili wambaii tena, ulikuwa ni msimamo uliotokana na mtazamo sahihi wa Kiislamu. Hio ni kwa kujaalia kuwa riwaya hizo za Al-Tabari ni riwaya sahihi.

247 - Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 588.

248 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 123.

Azdi,[249] basi tunakuta kwamba hata ikiwa kweli walioitwa *Khawarij* ndio waliomtaka Ali asimamishe vita basi – kwa mujibu wa riwaya hizo – wao walikiri kuwa walikosea kwa kufanya hivyo na kwamba wametubia kwa Allah. Na hili – la kukiri kosa na kutubia – ni miongoni mwa sifa za watu wacha Mungu. Kwa hivyo, bado hakuna katika riwaya hizi kitu kitachoweza kuwatia kasoro watu hao, au kumtoa Ali katika kosa kwa kuendelea kwake kukubali kufanya sulhu – kwani wale wamekubali kosa na kutubia; yeye kaendelea na kosa bila kutubia.

Kisha elewa kwamba yote hayo ni pale ambapo tutaijaalia riwaya hio ya Al-Tabari kuwa ni riwaya sahihi; vyenginevyo riwaya hio:

1) Ina mgongano katika *matn (text)* yake.
2) In udhaifu katika *sanad* yake kama tutavyobainisha.
3) Iko kinyume na isemavyo riwaya sahihi iliosimuliwa na Al-Imamu Ahmad na wengine isemayo:

> ….Wakaja *Al-Khawarij* na sisi wakati huo tulikuwa tukiwaita *Al-Qurraau* (Wasomi),[250] na panga zao ziko mabegani mwao, wakasema: 'Ewe Amiri Al-Mu-uminin (Kiongozi wa Waislamu) tunawasubiria nini hawa watu walio mlimani: hatuwaendei na panga zetu mpaka Mwenyezi Mungu akahukumu baina yetu na baina yao.[251]

[249] - Lakini Al-Baladhiri kaisimulia riwaya hii kwa *sanad* mbili, moja ni ya Abu Mikhnaf na ya pili ni ya 'Awana. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 121. Na A'wana ni mkweli kama alivyoelezwa katika *Siyaru Al-A'alam*cha Al-Dhahabi j. 7, uk. 153-154, *tarjama* na. 1079. Isipokuwa tatizo ni kuwa riwaya zote mbili njia yake ni ya Al-Kalbi naye ni mwongo mtunzi wa Hadithi. Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 157, *tarjama* na. 268.

[250] - Na hii ni tafauti na jeshi la Mu'awiya ambalo halikuwa na wanavyuoni. Anasema Ali (k.w.): "Piganeni na wenye makosa, wapotovu, waovu ambao si wasomi wa Qur-ani wala si wanavyuoni wa fiq-hi wala si maulamaa wa *Ta-wili* (tafsiri ya ndani)". Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 5, uk. 330, na j. 6, uk. 21. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 689.

[251] - Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 736, riwaya na. 34. Ahmad, *Al-Musnad* j. 5, uk. 484, Hadithi na. 16071. Na akainukuu Al-Sabi'i kutoka kwa Al-Minqari *Siffin* uk. 497 na Abu Ya'ala, *Al-Musnad* j. uk. 365.

HOJA NA. 2: RIWAYA YA AL-BALADHIRI NAMSIMAMO WA WATAFITI WA SASA

Lakini Al-Baladhiri, yeye anasimulia riwaya yenye kuonesha ukweli kwamba walioitwa *Khawarij* siyo waliotaka vita visitishwe na kufanyika sulhu. Anasema:

> Walipokusanyika Ali na Mu'awiya ili wachague mahakimu wawili, watu wakatafautiana na Ali; wakawa wengi wao na asilimia kubwa yao ni wenye kukubali kufanyika sulhu na kuiridhia; na kikawa kikundi miongoni mwao – nao ni kiasi cha watu elfu nne miongoni mwa wale waliokuwa na busara na wenye kuabudu miongoni mwao – kikapinga sulhu.....(basi) kile kikundi chenye kupinga (sulhu) kikamjia Ali kikasema: 'Rudi vitani, basi wakafarikiana naye na wengine kabla ya kuandikwa (mkataba wa) hukumu wakaondoka kwenda Al-Kufa, na wengine wakakaa naye; pamoja na kupinga kwao sulhu; wakawa wanampinga huku wanasema: 'Labda atatubia na kurejea.[252]

Ni wazi kwa mujibu wa riwaya hii kwamba waliotaka sulhu si Watu wa Nahrawaan au hao walioitwa kuwa ni *Khawarij*. Na hii ndio natija[253] sahihi waliyoifikia watafiti wengi wa sasa. Anasema Dr. Hisham Ju'ait – kama alivyonukuliwa na Sheikh Nasir Al-Sabi'i – kwamba:

> ..Haiwezekani kuikubali riwaya isemayo kwamba Al-Qurraa, ambao ni mbegu za madhehebu ya kikhawarij,[254] ndio waliomlazimisha Ali

---

[252] - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 112.

- Natija maana yake ni matokeo (results au conclusion).[253]

[254] - Tazama mtafiti huyu jinsi alivyoshindwa kujifungua pingu zake kikamilifu: kafikia kuona ukweli kwa kiasi fulani, lakini kashindwa kujua kwamba watu wa Nahrawaan ni Masahaba wakubwa wa Mtume (s.a.w.), na kwa hivyo katumia lugha isiyopendeza dhidi yao akasema: "Al-Qurraa, ambao ni mbegu za madhehebu za Kikhawarij". Wakati katika itikadi yake – ikiwa yeye ni Sunni kama yanavyoonesha maneno yake – haifai kumsema Sahaba kwa ubaya.

kukubali kusimamisha vita, na hii ndio natija iliofikiwa na watafiti wengi.[255]

Na hili linathibitishwa na Dr. Isma'il..aliposema:

> Na natija tunayoitoa mwishoni ni kuwa Al-Qurraa ambao baadae walikuwa ndio *Khawarij* walikuwa mbali na jukumu la kutaka sulhu kutokana na msimamo (wao) wa kisiasa na kidini wakati mmoja...[256]

Anasema Al-Sabi'i akimnukuu Ma'aruf Ahmad:

> …….Kama vile ambavyo Ahmad bin Sulaiman Ma'aruf kakujenga kukanusha kwake kwamba (Watu wa Nahrawaan) walitoa panga zao mbele ya Al-Imamu Ali na kumlazimisha kusimamisha vita na kukubali msingi wa kuwafanya watu wapitishe hukumu na kumlazimisha (Ali amfanye) Abu Musa (kuwa ndiye hakimu wa upande wa Ali), (Ma'aruf Ahmad kakujenga kukanusha kwake madai hayo juu ya msingi kwamba, wao Al-Qurraa wakati huo) walikuwa bado hawajajenga nguvu za pamoja zenye rai moja.[257]

---

255 - Al-Nu'aimi, *Dhuhuru Al-Khawarij* Majalla Al-Majm'a Al-'Ilmi Al-'Iraqi, j. 15, uk. 10-30. Ismai'il, *Qadhayaa Fii Al-Taarikh Al-Islamiy* uk. 53-62. Ju'ait *Al-Fitna* uk. 207. Ma'aruf, Ahmad:, *Qiraadtu Jadida Fii Mawaqifi Al-Khawarij* uk. 39. Al-Hallabi,: *Ilqau Al-Dhaw-I 'Alaa Al-Dawri Al-Maz'uum Lil-Quraa* Majallat Kulliyat Al-Adaab, "Wa Al-'Ulumi Al-Insaniyya", j. 4, uk. 13-34. *Hii ni Nakala kutoka kitabu "Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba " cha Sh. Al-Sabi'i , uk. 107.*

256 - Isma'il, *Qadhayaa Fii Al-Taarikh* uk. 61.

257 - Ma'aruf, Ahmad: *Qiraadtu Jadida Fii Mawaqifi Al-Khawarij* uk. 37. *Mwisho wa kunukuu kutoka kitabu Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba " cha Sh. Al-Sabi'i 107-108.* Lakini mimi – kwa upande wangu – naona uchambuzi huu alioutoa Sheikh Ma'aruf Ahmad si uchambuzi bara bara pamoja na kuwa natija ni sahihi.

HOJA NA. 3: KUZIOANISHA RIWAYA MBILI ZENYE KUGONGANA

Tukirudi katika riwaya mbili zenye mgongano: riwaya ya Al-Tabari isemayo kwamba Watu wa Nahrawaan ndio waliomtaka Ali asimamishe vita na riwaya ya Ahmad na wenzake isemayo kwamba wao ndio waliomsisitiza Ali aendelee na vita – *tukijaalia kuwa zote hizi ni riwaya sahihi* – basi tunasema kwamba tafsiri nyengine[258] ambayo inawezekana zikapewa riwaya mbili hizo ni kuwa wao Watu wa Nahrawaan waliposisitiza kuwa vita visimamishwe – baada ya Mu'awiya kunyanyua Misahafu – ni kuwa walitaka kujua nini Mu'awiya anataka: labda alikuwa amekiri kosa na kutubia na kurudi kwa Allah. Hii ndio tafsiri inayowezekana kupewa riwaya kwamba Watu wa Nahrawaan ndio waliomtaka Ali asimamishe vita. Na baada ya kujua kwamba Mu'awiya alikuwa si mkweli ndio ikawa wanasisitiza kuendelea na vita. Hii ndio tafsiri inayowezekana kupewa riwaya kwamba Watu wa Nahrawaan ndio waliomtaka Ali aendelee na vita.[259] Tafsiri hii imekuwa ni tafsiri ya lazima kwani riwaya zote – kwa maana ya riwaya zote – zinakubaliana kwamba *Al-Muhakkima* yaani "Watu wa Nahrawaan" au hao walioitwa kuwa ni *Khawarij* walianza upinzani wao wa wazi mara tu baada ya Al-Ash'ath bin Qais kuwasomea yale yaliyokuwemo katika mkataba ulioandikwa hapo, kwani hapo wao walijua Mu'awiya anataka nini na kwamba anachokitaka ni kinyume na Qur-ani. Hii ni kusema kuwa kabla ya hapo hawakujua hasa nini anachokitaka Mu'awiya kwa kitendo chake cha kunyanyua Misahafu na madai yake ya kutaka watu warejee katika Qur-ani: je ni kurejea katika haki iliyoelezwa na Aya isemayo: **"…Lipigeni lile (kundi) lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah,"**[260] au vipi. Na kwa hivyo, utaona kwamba Ibn A'atham anasimulia kwamba wakati wa mvutano huo wa kusimamisha vita ambapo kila mmoja katika jeshi la Ali alikuwa akitoa rai yake, alisimama

---

258 - Nimesema **Tafsiri nyengine,** kwa sababu tafsiri ya kwanza ni kuwa wao – kwa mujibu wa riwaya hizi – walitubia na wakamtaka Ali atubie.

259 - Na – kama unavyojua ewe ndugu msomaji – kwamba riwaya zenye kugongana hujumuishwa na kupewa tafsiri ya pamoja au kila moja huwekwa mahala pake ili kuondoa mgongano. Na – bila shaka – hakuna njia ya kuondoa mgongano hapa ila kuziletea riwaya hizo tafsiri mbili hizo au moja kati ya mbili hizo.

260 - Sura ya 49, Aya 9.

Rifa'a bin Shaddaad Al-Bajali akasema kwamba watu hawa tuliwaita mwanzo kuja katika Kitabu cha Allah wakakataa, lakini na tuwasikilize ikiwa watasema kitu chenye kukubaliana na Qur-ani[261] basi tutawakubalia vyenginevyo panga hizi zipo shingoni mwetu.[262] Kwa hivyo, *Al-Qurraa* au *Al-Muhakkima* waliona kuwa kilichomo katika mkataba huo ni kinyume na Aya ndio maana wakatangaza upinzani wao hapo hapo wakisema: **"Hakuna hukumu isipokuwa ya Allah".** Hii ndio tafsiri sahihi tukijaalia kuwa kweli wao ndio waliotaka vita visitishwe.

Na kwa tafsiri hii ya pili (inayopatikana kwa kuzijumuisha riwaya hizo mbili tafauti) itakuwa makusudio ya Watu wa Nahrawaan waliposema: "Lakini hio ilikuwa ni kufuru kutoka kwetu, basi sisi tumetubia kwa Allah Mtukufu..", itakuwa maana yake ni kosa la kutokumsikiliza Ali alipowaambia kuwa wasisimamishe vita: wala si kwamba walifanya kosa la kukubali sulhu, kwani kukubali sulhu riwaya zote zinaonesha (bali zinanena) kuwa wao hilo hawakulikubali na hilo ndilo lililojenga tafauti kubwa baina yao na Ali. Na hili linamaanishwa na riwaya nyengine dhaifu vile vile tutayoijadili hapo chini – *Inshaa Allah* – ambayo ndani yake kuna kifungu cha maneno kinachomnukuu Ali akisema: "Nilikutakeni juu ya hayo (ya kutokusimamisha vita) mukaniasi".[263] Ni wazi – kwa mujibu wa riwaya hizi dhaifu – kwamba Watu wa Nahrawaan:

1) Walitaka vita visimamishwe ili kujua Mu'awiya anataka nini.
2) Ali hakutaka hilo.
3) Si kwamba watu hao walitaka sulhu na Mu'awiya, bali labda Mu'awiya alikuwa katubia na kurudi katika Ukhalifa wa haki wa Ali.

---

261 - Kitu chenye kukubaliana na Qur-ani kwa hapa ni kimoja tu, nacho ni kuingia katika kumtii Khalifa aliyechaguliwa na Masahaba Muhajirina na Ansar au upanga. Hiki ndicho chenye kukubaliana na Qur-ani.

262 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 310-311. Yaani panga hizi zipo tutaendelea na kupigana nao mpaka Allah alete ushindi au tumalizike sote.

263 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18, na uk. 25. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 96.

4) Walipoona kwamba Mu'awiya hataki haki na kwamba kilichokuwemo katika mkataba ni kinyume na Qur-ani, wakataka vita viendelee.
5) Wao baadae walitubia (tukijaalia kuwa hizo ni riwaya sahihi) na kumtaka Ali naye atubie na waendelee na vita pamoja naye dhidi ya Mu'awiya.[264] Na toba yao si kwa sababu walikubali sulhu au walitaka sulhu, bali ni kwa kusitisha vita ili kumsikiliza Mu'awiya anataka nini, jambo ambalo Ali mwanzo hakulitaka.

Tumesema na tunakariri kwamba riwaya hizi zote ni dhaifu sana hazifai kuwa ni hoja dhidi ya fulani wala kuwa ni hoja za kumuunga mkono fulani, lakini nimeziletea muelekeo huu na ule kwa maana kwamba tukijaalia tu kuwa ni riwaya sahihi basi ilitakiwa tafsiri lazima ziwe ni hizo au moja ya hizo kwani ni riwaya ambazo dhahiri yake zinagongana na kwa hivyo ni lazima ziowanishwe na kuletewa tafsiri ya pamoja itayozitoa katika mgongano kama inavyotutaka elimu ya Hadithi na *Usuli-L-fiq-hi.*

HOJA NA. 4: MGONGANO MWENGINE WA RIWAYA

Tukirudi tena katika suala letu la kuwa Watu wa Nahrawaan – ambao ndio walioitwa *Khawarij* – ndio waliomtaka Ali akubali kusimamisha vita,

[264] - *Al-hasil* – chambilecho Warabu – ni kuwa watu wa Nahrawaan – kwa mujibu wa riwaya hizo – walitaka vita visitishwe ili kujua nini Mu'awiya anataka: je kakubali kurudi katika haki au vipi? Walipoona kuwa hataki kurejea wakataka vita viendelee na hapa ndio zikapaa sauti zisemazo: "***Hakuna hukumu isipokuwa ya Allah***" nayo ni kumpiga aliyeasi mpaka arejee katika haki au auliwe kama Qur-ani ilivyosema.

tunakuta hapa kuna riwaya nyengine yenye kuhusiana na maudhui hio. Riwaya hio inasema kwamba Zur'a bin Al-Burj na Hurqus bin Zuhair Al-Sa'adi waliingia kwa Ali wakamwambia: **"Hakuna hukumu ila ya Allah",**[265] Ali naye akawambia **"Hakuna hukumu ila ya Allah".**[266] Hurqus akamwambia Ali atubie kutokana na kosa lake la kukubali sulhu na Mu'awiya ili warejee tena vitani dhidi ya Mu'awiya. Ali akawambia**:** "Nilikutakeni juu ya hayo (ya kutokusimamisha vita) mukaniasi".[267] Na Ali alipoambiwa kuwa "Hio ilikuwa ni dhambi ambayo unatakiwa utubie kutokana na hio",[268] alisema: "Hio si dhambi".[269]

Sasa tazama vizuri – ewe mwenye kutumia neema yako ya akili – jinsi riwaya hii inavyojigonga yenyewe kwa yenyewe, jambo ambalo linathibitisha kwamba riwaya hizi za Abu Mikhnaf za kutaka kuonesha kuwa Watu wa Nahrawaan ndio waliomtaka Ali asimamishe vita na kukubali sulhu, ni riwaya za kutungwa bila ya wasi wasi wowote. Riwaya hii inamnukuu Ali akisema: "Nilikutakeni juu ya hayo (ya kutokusimamisha vita) mukaniasi" yaani kwa msimamo wenu wa kusisitiza hilo. Hii ina maana kwamba kusimamisha vita ni kinyume na Qur-ani na Sunna.[270] Hapo watu hao wakamjibu Ali kwamba: "Hio ilikuwa ni dhambi ambayo unatakiwa utubie kutokana na hio" na Ali akajibu kwamba "Hio si dhambi". Kwa hivyo, tunapata – kwa mjumuiko wa riwaya zote hizi – kwamba:

1) Ali kwanza alikataa kusimamisha vita, na baadae akakubali. Na kwa hivyo Ali alipokubali ni sawa sawa na kusema kuwa kakubali kwenda kinyume na Qur-ani na Sunna, vyenginevyo hakuna sababu ya kukataa mwanzo.

---

265 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 17. Ibn Al-Athi,r *Al-Kamil* j. 2, uk. 684-685.

266 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 17. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 684-685.

267 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 685.

268 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 685. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 129.

269 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 685.

270 - Kama Ali mwenyewe alivyosema katika riwaya nyengine kwamba: "...Sikuona isipokuwa (kupigana) vita (na Mu'awiya) au (vyenginevyo) nikikufuru kile alichokiteremsha Allah". Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 265. Na akasema: "….Lakini sikuona isipokuwa (ama) vita au nikikufuru kile alichokuja nacho Muhammad (s.a.w).".[270] Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 265. Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 287.

2) Kule kukubali kwake ndiko ambako Watu wa Nahrawaan wamekuita kuwa ni dhambi.
3) Yeye akajibu kuwa "Hio si dhambi". Sasa:
    a) Kama "Hio si dhambi" kwanini mwanzo akakataa kusimamisha vita na hio si dhambi?
    b) Je dhambi ilikuwa wakati gani: alipokataa kusimamisha vita au alipokubali?
    c) Kwanini akawalaumu Watu wa Nahrawaan kwamba wao ndio waliokosea kwa kutaka kwao[271] vita visimamishwe wakati hio si dhambi – anawalaumu kwa kitu ambacho si dhambi!
    d) Miongoni mwa hoja za wapambe wa Ali ambazo wamezitumia kuonesha kwamba kwa kukubali sulhu Ali hakukosea – kama tutavyoona baadae – ni Aya isemayo: **"Na Sulhu ni kheri".**[272] Sasa kama sulhu ni kheri kwanini tena Ali – kwa mujibu wa riwaya hizi mgongano – alikataa mwanzo kufanya sulhu na baadae baada ya mambo kwenda kombo (au chambilecho Wazungu *to backfire)* akawatupia kosa hilo Watu wa Nahrawaan kwamba wao ndio waliotaka sulhu na akawalaumu kwa hilo; anawalaumu nini na **"Sulhu ni kheri"?** Je anawalaumu kwa kutaka kwao kheri?

Namna hii ndivyo riwaya hizi za kupakasa (ambazo zimesukwa ili kuwatia aibu Masahaba wacha Mungu wa Nahrawaan) zinavyogongana zenyewe kwa zenyewe: E jamani nyii: walimwengu wenzangu! *Aina Al-'Uqulu Al-Wa'iyah* **(أين العقول الواعية)** ziko wapi akili zenye kufahamu?

Jambo jengine linalohusu *matn* ya riwaya hio – kama tulivyosema katika *Mezani Ya Haki* – ni kuwa vipi Ali akiwa kama Imamu wa Waislamu alikubali kuacha Aya ya Allah na kusikiliza maneno ya watu? Kama ni hivyo mkosa ni nani – Ali au waliomtaka asimamishe vita? Uamuzi wa mwisho ulikuwa ni wa nani? Na kwa hivyo jukumu ni la nani? Na

271 - Hapa najadili riwaya tu, vyenginevyo hakuna ushahidi sahihi kwamba Watu wa Nahrawaan ndio waliotaka kusimamishwa vita, bali ushahidi sahihi ni kinyume na hivyo.
272 - Sura 4 Aya 128.

wakulaumiwa ni nani? Kwa kweli riwaya hio haifai kabisa kwani inamfanya Ali kuwa kiongozi dhaifu!

HOJA NA. 5: WALIOTAKA SULHU NI WALIOKUWA WENGI

Ukiniambia "Aaa Al-Imamu Ali aliona jeshi lake linafarakana ndio maana akakubali kusimamisha vita na kukubali kufanya sulhu!" Nitakujibu: "Je kwa kukubali kusimamisha vita na kukubali sulhu, jeshi halikufarakana?" Ukiniambia "Aaa waliokubali sulhu walikuwa ni wengi zaidi kwa hivyo hakuweza kuwapinga!" Ukiniambia hivyo, nami nitakwambia: "Kweli waliotaka sulhu walikuwa ni wengi kwa mujibu wa hali yenyewe inavyojionesha kwani kama walikuwa wachache ndio waliotaka sulhu, basi Ali asingeliwasikiliza kwani yeye pia hakuwa akiiwafiki sulhu lakini kwa kuwa walioitaka walikuwa ni wengi basi hakuwa na hila tena, na hili linathibitishwa pia na riwaya ya Al-Mas'udi aliposema: "Wengi wa watu wa Iraki walipoona hivyo (walipoona Misahafu imenyanyuliwa), walisema tukiitike Kitabu cha Allah".[273] Na baada ya Mu'awiya kutaka sulhu, Al-Mas'udi – katika riwaya yake nyengine – anasema: "Waliowengi zaidi katika watu wakasema: 'Tumeridhia, tumekubali, tumesikia na tumetii".[274] Na tumenukuu – kabla kidogo – maneno ya Al-Baladhiri akisema:

> …Wakawa wengi wao ni wenye kukubali kufanyika sulhu na kuiridhia; na kikawa kikundi miongoni mwao – nao ni kiasi cha watu elfu nne miongoni mwa wale waliokuwa na busara na wenye kuabudu miongoni mwao – kikapinga sulhu….[275]

Riwaya hii inaendelea kwa kusema:

> Kile kikundi chenye kupinga kikamjia Ali wakasema: 'Rudi vitani – na Ali alikuwa anapenda hivyo – basi wale walioridhia sulhu wakasema: '*Wallahi* watu hawa (Mu'awiya na wenzake) hawakutulingania isipokuwa katika haki na insafu na uadilifu. Na alikuwa Al-Ash'ath bin

273 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 524.
274 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 525.
275 - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 112.

> Qais na watu wa Al-Yaman ndio wapinzani wakubwa wa wale wanaotaka vita (viendelee). Basi Ali akasema kuwaambia wale waliotaka vita (viendelee): 'Enyi watu! Mumeona wenzenu walivyokupingeni nanyi ni kidogo muliomo ndani ya wengi….[276]

Na akasema Al-Baladhiri: "Wengi katika wafuasi wa Ali wakamili katika kile walicholinganiwa na wakaharamisha kupigana".[277] Ninasema: Sasa kama ni hivyo, basi elewa kwamba hili linathibitisha yale niliyokwambia kwamba waliotaka pasimamishwe vita na pafanyike sulhu hawakuwa hao *Al-Qurraa* (Wasomi) ambao baadae waliitwa kuwa ni *Khawarij* kwani wao hawakuwa wengi ukilinganisha na hao wengine waliobaki chini ya uongozi wa Ali.[278] Kwa hivyo, ni wazi kwamba *Al-Qurraa* (Wasomi) ambao baadae waliitwa kuwa ni *Khawarij* sio waliosisitiza kusimamishwa vita tafauti na riwaya ya Al-Tabari inavyosema.[279] Bali wao – kama ilivyo riwaya ya Ahmad na wenzake – ndio waliosema: "Tunawasubiria nini hawa watu waliomlimani: hatuwaendei na panga zetu mpaka Mwenyezi Mungu akahukumu baina yetu na baina yao". Na hii ndio riwaya yenye *sanad* sahihi.[280] Na kwa hivyo, utaona kwamba hata maneno ya Ali

---

276 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 112.

277 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 99.

278 - Al-Qurraa walikuwa ni kama elfu nne tu, na baada ya watu wengine – ambao pia waliipinga sulhu – kujiunga nao wakawa ni idadi ya watu elfu kumi na mbili, wakati jeshi zima la Ali lilikuwa na watu si chini ya elfu tisiini. Tazama Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 314. Lakini usije ukadhani kwamba haki inapimwa kwa wingi na uchache, bali haki inapimwa kwa ushahidi sahihi wa Kisharia.

279 - Katika *sanad* ya riwaya ya Al-Tabari kuna Abu Mikhnaf, Lut bin Yahya. Anasema Al-Dhahabi katika *Al-Mizan* na Ibn Hajar katika *Lisanu Al-Mizan* kuhusu Abu Mikhnaf huyu: "Ni mtoaji habari mbovu, haaminiki, kaachwa na Abu Hatim na wenzake." Na akasema Al-Daraqutni: "Dhaifu." Na akasema Yahya bin Ma'in: "Si muaminifu." Na akamtaja Al-'Uqaili katika wapokezi dhaifu. 279 Na akaongeza Al-Dhahabi kutoka kwa Ibn Adey akisema kwamba ni "Shia wa kuungua (Shia mkereketwa) msimulizi wa habari zao." Tazama *Lisanu Al-Mizan* j. 4, uk. 55-56, *tarjama* ya 1368. Pia yumo katika *sanad* hio Abdul-Rahman bin Jundub Al-Azdi, naye hajulikani ni nani. Tazama *Lisanu Al-Mizan* j. 4, uk. 408, *tarjama*. 1610.

280 - Tumetaja walioipokea riwaya hii katika maelezo nambari 273. Ama *sanad* ya riwaya hii ni: "Katuhadithia Ya'alaa bin Ubaid kutoka kwa Abdul-Aziz bin Siyaah kutoka kwa Habib bin Abi Thabit kasema: "Nilimjia Abu Wail, nikamuliza….Kasema (Abu Wail)….*Kisha inafuata riwaya*. Ya'alaa bin Ubaid – mpokezi wa kwanza – ni mwenye kuaminika bila khilafu. Anasema Al-Imamu Ahmad: "Hadithi zake ni sahihi, na ni mtu mwema katika nafsi yake". Anasema Ibn Ma'in: "Ni mwenye kuaminika". Anasema Abu Hatim: "Ni mkweli". Tazama Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 11, uk.

mwenyewe – baada ya natija ya sulhu – yanaashiria kwamba waliotaka sulhu ni wale waliobaki pamoja naye baada ya kujitenga kwa *Al-Qurraa* (Wasomi).

353-354, *tarjama* na. 680. Na kwa ufupi ni kuwa hakuna aliyemponda mpokezi huyu isipokuwa Ibn Ma'in kasema kwamba riwaya zake alizozipokea kutoka kwa Sufyaan tu ndio zenye udhaifu. Riwaya hii hakuipokea kutoka kwa Sufyaan, bali kaipokea kutoka kwa Abdul-Aziz bin Siyaah – mpokezi wa pili – naye ni katika vigogo wa Kishia, na kasifiwa na hakuna aliyemtia ila. Wanasema Ibn Ma'in na Abu Daud: "Ni mwenye kuaminika". Anasema Abu Hatim: "Ni mkweli". Tazama Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 6, uk. 304, *tarjama* na. 657. **Tanbihi:** Mimi sitolei hoja kwa wapokezi Mashia ila wakitimiza masharti matatu nilioyaeleza katika kitabu *Ukhalifa:* moja ya hayo ni kuwa mpokezi huyo awe hana dosari na anachokisimulia hakiungi mkono itikadi ambayo ni ya Kishia tu au hakiungi mkono msimamo wa Kishia kwani hapa huwa hatuhumiwi, bali huwa kakiri. Riwaya hii haiungi mkono msimamo wa Kishia na mpokezi huyu ni Shia lakini hakutiwa dosari. Na sababu yangu hasa kwa kuzikanusha riwaya zao si kwa sababu wao ni Shia, lakini sababu ni kuwa baada ya kuzifuatilia riwaya za hao wasimulizi wa Kishia walioitwa kuwa ni sahihi, nimeona riwaya zao ni *Taammatun Kubra (Janga kuu)*: ni utunzi uliowazi, *Wallahu Al-musta'aan.* Habib bin Abi Thabit – mpokezi wa tatu – ni mwenye kuaminika lakini anaghushi. Na kwa ufupi Habib huyu hakuna kasoro aliyotiwa ila ghushi, lakini ghushi – kama tulivyoeleza katika kitabu chetu *Ushahidi Uliowekwa Wazi* na *Ukhalifa* na makala na vitabu vyengine tafauti – kwamba kanuni ni kuwa mwenye kughushi akiwa ni imara katika Hadithi, basi Hadithi yake inakuwa dhaifu ikiwa Hadithi hio ni *mu'an'an* (مُعَنْعَنٌ) au ikiwa Hadithi hio ni "مُؤَنَّنٌ *Muannan."* Pia zinaingia hapa namna zote za masimulizi atazozitumia msimulizi huyo mwenye kughushi, ikiwa namna hizo hazimaanishi kuwa yeye kaisikia Hadithi hio moja kwa moja kutoka kwa msimulizi aliye kabla yake. Hapa – katika masimulizi haya – Habib bin Abi Thabit kaisikia riwaya hii kutoka kwa Sheikh wake, na kwa hivyo riwaya yake hapa inakubalika. Anasema Al-'Ijli kuhusu Habib bin Abi Thabit kwamba ni: "Mfuasi wa Masahaba mwenye kuaminika". Wanasema Al-Nasai na Ibn Ma'in: "Ni mwenye kuaminika". Tazama Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 2, uk. 156, *tarjama* na. 323. Lakini kuna njia mbili za Hadithi za Habibi bin Abi Thabit huyu ambazo zimesemwa kuwa hazikuthibiti: 1) Hadithi zake kutoka kwa Ataa bin Yasaar, 2) Hadithi zake kutoka kwa 'Asim bin Dhumra kama ilivyo katika marejeo hayo tulioyataja hapa na pia kama ilivyoelezwa katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 5, uk. 40-41, *tarjama* na. 77. Na Sheikh wa Habib bin Abi Thabit katika riwaya hio ni Abu Wail – mpokezi wa nne na wa mwisho na ambaye ndiye anayesimulia tukio hilo – naye ni Shaqiq bin Salama Al-As'adi, naye ni mwenye kuaminika, imara. Anasema Ibn Ma'in: "Ni mwenye kuaminika, hauliziwi (juu ya usahihi wake mtu aliye) mfano wake". Anasema Wakii: "Alikuwa ni mwenye kuaminika". Anasema Ibn Sa'ad: "Alikuwa ni mwenye kuaminika, ana Hadithi nyingi". Anasema Ibn Abdil-Barr: "Wamekubaliana (Wanavyuoni wa wapokezi wa Hadithi) kwamba ni mwenye kuaminika". Tazama Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 4, uk. 317-318, *tarjama* na. 619.

HOJA NA. 6: MANENO YA ALI MWENYEWE

Anasema Al-Mas'udi:

> Ilipomfikia Ali (habari) ya yaliyokuwa baina ya Abu Musa na Amru (bin Al-'Aas), alisema: 'Mimi nilikuwa nimekutangulieni kuhusu sulhu hii na nikakukatazeni nayo, (nanyi) mukakataa na kuniasi. Sasa je munaonaje hatima ya jambo lenu muliponikatalia. *Wallahi* mimi namjua aliyekupelekeeni nyinyi mukanipinga na kuacha amri yangu, na lau nilitaka kumtia mkononi ningefanya, lakini Allah yuko nyuma yake"[281] Anasema Al-Mas'udi: "Anamkusudia kwa (maneno yake) hayo Al-Ash'ath bin Qais.[282]

Sasa Ali aliposema maneno haya, walikuwa *Al-Qurraa* (Watu wa Nahrawaan) au walioitwa kuwa ni *Khawarij* hawapo tena mbele yake: wameshajitenga naye na kwenda Harauraa na baadae Nahrawaan. Sasa kama ni hivyo, ni nani ambao Ali alikuwa akiwaambia: "Mimi nilikuwa nimekutangulieni kuhusu sulhu hii na nikakukatazeni nayo mukakataa na kuniasi….?" Ni wazi kwamba Ali kawapachika mzigo huo wa kosa la kukubali sulhu wale waliobaki pamoja naye kwani wao ndio wahubiriwa hapa, nao ndio waliokuwa wengi akiwemo – pamoja nao – Al-Ash'ath bin Qais; ama *Al-Qurraa* (Watu wa Nahrawaan), watu wamewachomeka ili kutaka kuufunika ukweli, lakini chambilecho maneno ya kwetu: "*Nkuteka maji pakachani!"*

Na labda maelezo yaliyo wazi zaidi yanapatikana katika khutuba ya Ali aliyowahutubia watu wa Al-Kufa baada ya kujitenga kwa watu wa Nahrawaan. Anasimulia Al-Tabari kwamba:

> Walipotoka Al-Khawarij…(Ali) alisimama Al-Kufa akawahutubia (watu wa Al-Kufa) akisema:..'Hakika ya maasi yanarithisha huzuni na yanafuatiwa na majuto, na nilikuwa nimekuamrisheni amri yangu kuhusu watu wawili hawa (Abu Musa na Amru bin Al-'Aas) na katika sulhu hii na nikakupeni rai yangu…lakini mukakataa (yote) isipokuwa kile mulichokitaka nyinyi.[283]

---

281 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 532.
282 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 532.
283 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 20. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 688.

Riwaya hii iko wazi kwamba Ali anaowaambia hapa ni wafuasi wake waliokuwa Al-Kufa baada ya kuwa walioitwa *Khawarij* wameshatokana naye, na kwa hivyo, utaona kuwa riwaya hii inasema kwa uwazi kwamba: "Walipotoka *Al-Khawarij*…(Ali) alisimama Al-Kufa..", na inaendelea kwa kusema:

> Kisha (Ali baada ya hapo) akateremka (katika membari) akawaandikia (barua) *Al-Khawarij* waliokuwa Nahrawaan (akiwambia): 'Hakika watu wawili hawa (Abu Musa na Amru bin Al-'Aas) ambao tumewaridhia[284] wawe mahakimu wamekwenda kinyume na hukumu ya Qur-ani na wamefuata matamanio ya nafsi zao…basi ikikufikeni barua yangu hii, njooni, hakika sisi tunamuendea adui yetu (Mu'awiya) na ni adui yenu na sisi sasa tuko katika jambo letu la mwanzo tulilokuwa tukilifuata (kwa pamoja).[285]

Kwa hivyo, yote haya yanathibitisha kwamba Watu wa Nahrawaan au walioitwa *Khawarij* siyo waliotaka sulhu, na hiki – bila shaka – ndicho kinachoeleza kwanini watu hao walikuwa wakimuendea Al-Imamu Ali kila mara ili waanze vita upya, wakati – kinyume chake – waliokuwa pamoja na Ali walimfanyia khiyana baada ya kumalizika vita vya Nahrawaan: wakakataa kwenda kupigana na Mu'awiya.[286]

---

[284] - Zingatia maneno ya Ali kwa nini alisema: "Hakika watu wawili hawa ambao tumewaridhia" na asiseme: "Ambao mumewaridhia". Kama ilikuwa watu wa Nahrawaan ndio wahusika basi angewatupia lawama wao na kusema: "Ambao mumewaridhia".

[285] - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 20. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 688.

[286] - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 153-154. Ali aliwalingania watu wa Al-Kufa – leo wanaojiita Shia wake – mpaka akawaapiza hawakumtii kwenda kupigana na Mu'awiya! Tazama Al-Baladhiri, ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 156. Na sina shaka kwamba lau leo Ali angefufuka pamoja na Hasan na Husain basi Wairaki – wakiwemo hao wajiitao Shia basi – wangelikuwa wa mwanzo kumpinga na pengine kumuua! Mitihani yote na misukosuko ya Uislamu basi imeletwa na Wairaki na Washam! Anasema Ibn Abbaas kumhadharisha Al-Husain bin Ali: "Nasikia unataka kwenda Iraki, nao ni watu wa khiyana; wanakwita kwenye vita, basi usifanye haraka". Tazama Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 3, uk. 40. Na kweli alipofika Al-Kufa watu ambao walimwita ndio waliomfanyia khiyana!!!! Pia walimfanyia khiyana kubwa Muslim bin Aqil bin Abi Talib, mjumbe wa Al-Husain bin Ali, wakamuacha vitani pekeyake wakachawanyika, na hatimae akauliwa na Ubaidillahi bin Ziyaad. Tazama Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 5, uk. 56-103.

HOJA NA. 7: MSIMAMO WA AL-AHNAF BIN QAIS NA KUZOZANA KWA JESHI LA ALI

Jambo jengine lenye kuonesha ukweli kwamba *Al-Qurrau* siyo waliotaka sulhu ni kuwa wakati watu wanazozana kusimamisha vita, Al-Ahnaf bin Qais (mmoja wa *Qurraa* waliojitenga na Ali) alikuwa akimuendea Ali na kumrejea mara kwa mara asikubali jambo hilo, akapinga sulhu na akapinga kufanywa Abu Musa kuwa ndiye muwakilishi wa Ali katika sulhu hio.[287]

Jambo jengine lenye kuonesha ukweli kwamba *Al-Qurrau* sio waliotaka sulhu ni kuwa wakati Ali alipokuwa akirudi Al-Kufa pamoja na jeshi lake kutoka *Siffin* baada ya kusimamishwa kwa vita, katika jeshi la Ali kulikuwa na mfarakano mkubwa na kutupiana maneno makali na kupigana mijeledi: ikawa *Al-Qurraa* wanawaambia wale waliotaka sulhu: "Enyi maadui wa Mwenyezi Mungu, nyinyi mumepaka mafuta kwa nyuma ya chupa[288] katika jambo la Mwenyezi Mungu".[289] Na katika riwaya ya pili:

> Mumepaka mafuta kwa nyuma ya chupa katika jambo la Mwenyezi Mungu na mumewafanya (watu) wahukumu katika (jambo alilokwisha kulihukumu katika) Kitabu chake, na mukafarikiana na jamaa.[290]

Na wale waliokubali sulhu wakawa wanasema: "Nyinyi mumefarikiana na Imamu wetu na kuusambaratisha mkusanyiko wetu".[291] Baada ya maelezo yote haya, utaona wazi kwamba waliotaka sulhu ni wale waliokuwa chini ya uongozi wa Ali: si wale walioitwa kuwa ni *Khawarij*.[292]

---

287 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 671.
288 - Mumefanya khiyana.
289 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 673.
290 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 114.
291 - Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 673.
292 - Nimeirefusha sehemu hii kidogo kwa kuitolea ushahidi wa kutosha kwani imekuwa ni ngoma ya watu kusema: "*Khawarij* walitaka sulhu kisha wakajitenga na Ali kwa sababu hio" wakitegemea riwaya ya kutunga ya Al-Tabari iliosimuliwa na Abu Mikhnaf.

NATIJA

Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo, inatubainikia kwa uwazi kabisa kwamba riwaya sahihi kuhusu msimamo wa wale walioitwa *Khawarij* ilikuwa ni kuendelea na vita hadi Mu'awiya akubali kuingia katika utawala wa Kiislamu (wa Ali) au kuuliwa Mu'awiya na jeshi lake lote, kama riwaya sahihi ya Ahmad na wenzake inavyonena. Na jambo hili – kama tutavyoona – ndio moja ya tafauti zao kubwa baina yao na Ali ambazo zilipelekea kwa watu hao kujimegua na kuchagua Imamu wao mpya. Nao ndio msimamo unaoafikiana na Aya isemayo: **"….Ikiwa (kundi) moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah."**[293] Sasa walioitwa *Khawarij* wamekuwa na Aya hii kuthibitisha msimamo wao, suali ni kuwa je wasioitwa *Khawarij* wana ushahidi gani wa kukubali kusimamisha vita. Na kama hawa wana ushahidi wa Aya na wale hawana je anayestahiki zaidi kuitwa *Khawari* au aliyetoka katika dini ni yupi: mwenye ushahidi wa Aya au asiyekuwa na ushahidi kabisa?[294] Ndio maana ninahimiza kwamba ukitaka kujua ukweli wa maudhui hii, kwanza majina mazuri na mabaya yaweke mbali usome maudhui kwa kutazama ushahidi.

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

1) Maudhui yetu katika sehemu hii ni kuhusu suala la nani alitaka vita vya *Siffin* visimamishwe na sulhu ifanyike.
2) Wapinzani wa Watu wa Nahrawaan, wakiitegemea riwaya iliyosimuliwa na Al-Tabari, wanadai kwamba *Al-Khawarij* ndio

293 - Sura ya 49, Aya 9. Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 122, ili uone kwamba waliopinga sulhu walipinga kwa mujibu wa Aya hii.

294 - Bali walikuwa na shubuhati tu kama utakavyoona wakati wa kuzijadili hoja za Ibn Abbaas na Ali.

waliotaka pafanyike sulhu kisha wakageuka na kumlaumu 'Ali juu ya hilo na baadae wakajitenga naye.

3) Tumetoa hoja saba[295] kuonesha ubatili wa madai hayo.
4) Mukhtasari wa hoja hizo ni kama inavyofuata:

a) Riwaya ya Al-Tabari ambayo wanaitegemea katika madai yao hayo, ni riwaya dhaifu. Msimulizi wa riwaya hio ni Abu Mikhnaf (Lut bin Yahya), naye ni dhaifu kama tulivyobainisha. Pia katika *sanad* ya riwaya hio kuna Abdul-Rahman bin Jundub naye hajulikani. Isitoshe riwaya hio dhaifu imegongana na riwaya sahihi ya Ahmad na wengine. Pia tumebainisha kuwepo kwa mgongano baina ya riwaya hio na itikadi ya Kisuni na Kishia kwa upande mmoja; na kugongana kwake na kile kilichomo katika riwaya hio – yaani riwaya inajigonga. Riwaya hio inaonesha kuwa 'Ali ama kweli alishiriki katika kumuua 'Uthman – kama alivyodai Mu'awiya – au hakushiriki lakini aliridhia, kwani – kwa mujibu wa riwaya hio – waliomuua walikiri mbele yake naye hakuchukua hatua yoyote. Na yote haya – ya kushiriki katika mauaji au kuyaridhia mauaji hayo – kwa Sunni na Shia hayakubaliki. Kwa hivyo, ilitakiwa na riwaya hio wasiikubali.

b) Katika hoja na. 2, tumeonesha kwamba riwaya ya Al-Baladhiri inasema kwa uwazi kwamba waliotaka vita visitishwe na sulhu ifanyike ni wale waliobakia chini ya uongozi wa Ali na kwamba waliojitenga naye, ambao ndio walioitwa *Khawarij*, walikataa kusitishwa kwa vita na kufanyika kwa sulhu. Halkadhalika tumeonesha katika sehemu hii kwamba wako miongoni mwa wapekuzi wa kisasa walioipinga fikra hio ya kuwa walioitwa *Khawarij* ndio waliotaka pafanyike sulhu.

c) Katika hoja na. 3, tumeonesha *minhaj (methodology)* sahihi ya kuzioanisha riwaya mbili hizo – riwaya kwamba walioitwa *Khawarij* ndio waliotaka vita visitishwe na sulhu ifanyike; na riwaya kwamba wao ndio waliotaka vita viendelee – tukijaalia kuwa riwaya hizo zote ni sahihi. Tumesema kwamba riwaya inayosema kuwa walioitwa *Khawarij* ndio waliotaka vita visitishwe na sulhu ifanyike ni lazima ifasiriwe kwamba wao walitaka vita visitishwe ili kujua Mu'awiya anataka nini.

[295] - Katika kitabu hiki kwa lugha ya Kiingereza, tumezigawa hoja hizi sehemu nane, lakini madhumuni ni yale yale.

Tumelazimika kuifasiri riwaya hio hivyo, kwani riwaya ya pili inasema kwamba wao ndio waliotaka vita viendelee. Ama riwaya ya pili isemayo kwamba wao ndio waliotaka vita viendelee, ni lazima ifasiriwe kwamba wao walitaka hivyo baada ya kuona kwamba matakwa ya Mu'awiya ni kinyume na Qur-ani. Kwa kutoa tafsiri hizi, tutakuwa tumezitendea kazi riwaya zote mbili na mgongano utakuwa haupo. Vyenginevyo itatubidi tuchukue riwaya yenye *sanad* sahihi na kuiwacha riwaya yenye *sanad* dhaifu. Na riwaya yenye *sanad* sahihi ni ile isemayo kwamba walioitwa kuwa ni *Khawarij* ndio waliotaka vita viendelee.

d) Katika hoja na. 4, tumeonesha mgangao mwengine uliopo katika riwaya tafauti zenye kuhusiana na maudhui hii. Ufupisho wake ni kuwa Watu wa Nahrawaan walikizingatia kitendo cha 'Ali cha kusimamisha vita kuwa ni dhambi. Yeye akajibu: "Hio si dhambi". Wakati katika riwaya nyengine tunapata kwamba 'Ali aliwalaumu watu hao kwamba wao ndio waliofanya kosa kwa kutaka vita visitishwe. Sasa jiulize wewe je anawalaumu kwa kitu ambacho si dhambi? Pia tunaambiwa katika baadhi ya riwaya kwamba walioitwa *Khawarij* ndio waliotaka vita visitishwe, nao walikosea kwa kufanya hivyo. Halafu riwaya nyengine zinamtetea Ali kwa Aya za Qur-ani kwamba hakufanya kosa kwa kukubali kufanya sulhu na Mu'awiya kwani Aya inasema **"Na sulhu ni kheri".** Kwa hivyo, natija ya haya ni kuwa **"Sulhu ni kheri kwa Ali"** na **"Sulhu ni shari kwa walioitwa *Khawarij*"!**

e) Katika hoja na. 5, tumeonesha kwamba waliotaka sulhu ni wale waliokuwa wengi; wakati watu wa Nahrawaan walikuwa wachache ukiwalinganisha na wale waliobaki chini ya uongozi wa 'Ali. Inasema riwaya ya Al-Baladhiri:

> …..Wakawa wengi wao na asilimia kubwa yao ni wenye kukubali kufanyika sulhu na kuiridhia; na kikawa kikundi miongoni mwao – nao ni kiasi cha watu elfu nne miongoni mwa wale waliokuwa na busara na wenye kuabudu miongoni mwao – kikapinga sulhu.....(basi) kile kikundi chenye kupinga (sulhu) kikamjia Ali kikasema: 'Rudi vitani, basi wakafarikiana naye na wengine kabla ya kuandikwa (mkataba wa) hukumu wakaondoka kwenda Al-Kufa…..

f) Katika hoja na. 6, tumeonesha kwamba Ali mwenyewe alipofika Al-Kufa aliwalaumu wale waliobakia chini ya uongozi wake kwa kitendo chao cha kukubali kusimamisha vita na kukubali kufanya sulhu na Mu'awiya. Na akamlaumu Al-Ash'ath bin Qays Al-Kindi. Yote haya yalifanyika baada ya kuwa walioitwa *Khawarij* tayari wameshajitenga na Ali: hawapo tena Al-Kufa. Na kwa hivyo, ndio maana Ali, baada ya kutoa khutuba ya kuwalaumu wale waliobakia chini ya uongozi wake, akawaandikia barua watu wa Nahrawan kuwataka warejee kwake ili warudi tena vitani dhidi ya Mu'awiya. Kwa hivyo, waliosisitiza sulhu ni Al-Ash'ath bin Qays na kundi lililobakia chini ya uongozi wa Ali ambao baadae pia walimfanyia khiyana huko Al-Kufa.

g) Katika hoja na. 7, tumeonesha kwamba Al-Ahnaf bin Qays alikuwa miongoni mwa waliopinga sulhu. Al-Ahnaf huyu alikuwa mtu wa karibu sana na 'Ali, baadae akajitenga naye na kujiunga na watu wa Nahrawaan. Ni wazi kwamba lau msimamo wake ulikuwa tafauti na watu wa Nahrawaan, basi asingelijiunga nao. Pia tumeonesha kwamba kulitokea mzozo mkubwa katika jeshi la 'Ali wakati walipokuwa wakirudi Al-Kufa. Walioitwa *Khawarij* wakawa wanawaambia wale waliobaki chini ya uongozi wa 'Ali:

> ..Mumepaka mafuta kwa nyuma ya chupa katika jambo la Mwenyezi Mungu na mumewafanya (watu) wahukumu katika (jambo alilokwisha kulihukumu katika) Kitabu chake, na mukafarikiana na jamaa.

Na wale waliokuwa chini ya uongozi wa Ali wakawa wanasema: "Nyinyi mumefarikiana na Imamu wetu na kuusambaratisha mkusanyiko wetu". Ni wazi kwamba waliotaka sulhu ni wafuasi wa Ali wakiongozwa na Al-Ash'ath bin Qays, jasusi wa Mu'awiya katika jeshi la 'Ali.

Sasa baada ya kuzitazama riwaya hizo kuhusu nani alitaka vita visimamishwe huko *Siffin* baada ya Mu'awiya na jeshi lake kunyanyua Misahafu, naturudi tena kutazama nini kiliendelea baada ya hapo.

NINI KILIENDELEA HUKO *SIFFIN* BAADA YA HAPO

Baada ya Ali kuona jeshi lake limegawika baina ya wenye kuunga mkono kuwepo kwa sulhu na wenye kupinga, akaona akubaliane na wale waliounga mkono na kwa hivyo, baada ya Al-Ash'ath bin Qais Al-Kindi – ambaye alikuwa miongoni mwa walioshikilia sana kuwa pafanyike sulhu[296] – kutaka aende kwa Mu'awiya kumsikiliza ana sababu gani ya kunyanyua Misahafu katika vichwa vya mikuki,[297] Ali akamruhusu kwenda.[298] Al-Ash'ath akaenda kumuuliza Mu'awiya, naye akajibu:

> Ili sisi na nyinyi turejee katika kile Allah alichokiamrisha katika Kitabu chake: toeni mtu munayemridhia miongoni mwenu; na sisi tutoe mtu miongoni mwetu, kisha tuwatake wakifuate kile kilichomo ndani ya Kitabu cha Allah: wasikivuuke, kisha tufuate kile walichoafikiana juu ya hicho.[299]

Hio ndio jawabu ya Mu'awiya bin Abi Sufayaan kwa mjumbe wa Ali bin Abi Talib.

Al-Ash'ath bin Qais Al-Kindi akarejea kwa Al-Imamu Ali na jawabu hio, na baada ya mjadala baina ya Ali na jeshi lake, Ali na jeshi lake wakamchagua Abu Musa Al-Ash'ari kuwa ndiye muwakilishi wao katika

---

296 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 524.

297 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 4. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 525. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 669.

298 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 308. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 524.

299 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 4. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 525. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 325. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 669. Na mfano wake ni maneno ya Abu Al-A'awar Al-Salami kama ilivyo katika *Al-Futuh* j. 3, uk. 320, cha Ibn A'atham,. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 99,103.

mazungumzo hayo ya sulhu baina ya pande mbili.[300] Ama kwa upande wa Sham, muwakilishi wao alikuwa ni Amru bin Al-'Aas .[301]

UANDISHI WA MKATABA NA KUFUTWA KWA JINA LA UAMIRI

Kisha baada ya hapo, ukaandikwa mkataba wa sulhu,[302] katika siku ya Jumatano ya tarehe kumi na tatu Mfunguo tano mwaka wa thalathini na saba.[303] Mkataba huu haukuwa ndio sulhu yenyewe lakini ulikuwa ni mkataba ulitoa makubaliano na masharti ya kufanyika sulhu katika wakati ujao. Mambo mawili katika uandishi wa mkataba huu yalileta upinzani baina ya *Al-Qurraa* (Wasomi)[304] kwa upande mmoja; na wafuasi wa Mu'awiya wakishirikiana na Al-Ash'ath bin Qais, ambaye alikuwa ni katika wafuasi wa Ali, kwa upande wa pili. Moja ya mambo mawili hayo ni kuwa wafuasi wa Ali (k.w.) waliandika – katika mkataba huo – maneno haya: "Hivi ndivyo walivyohukumiana Ali, Amiri L-Mu-uminina (Kiongozi wa Waislamu), na Mu`awiya".[305] Maneno yanayomtaja Ali kuwa ni: "Amiri L-Mu-uminina (Kiongozi wa Waislamu)" katika mkataba huu yakawa hayakubalika kwa upande wa Mu'awiya, na akasema: "Ikiwa wewe ni Amiri-L-Mu-uminina basi mimi ninapigania nini na wewe?"[306] Amru bin Al-'Aas naye akasema: "Andika jina lake na la baba yake; yeye ni Amiri wenu ama sisi si Amiri wetu".[307] Na hapa mmoja wa *Al-Qurraa* (Wasomi), naye ni Al-Ahnaf bin Qais[308]

300 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 4-5. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 103.
301 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 4. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 103.
302 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 5-6. Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 4, uk. 8.
303 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 7.
304 - Ambao ndio baadae walioitwa kuwa ni *Khawarij.*
305 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 5. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 670.
306 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 8.
307 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 5. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 670.
308 - Al-Ahnaf bin Qais alikuwa katika Watu wa Nahrawaan, lakini Al-Baladhiri kamtaja kuwa ni miongoni mwa waliorejea katika utawala wa Ali baada ya kujadiliana nao. Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 113. Lakini suala hili la kwamba kuna waliorejea katika utawala wa Ali linahitaji maelezo, hasa hasa ukizingatia kwamba Al-Baladhiri kamtaja Abu Bilal Mirdas (r.a.) kuwa ni miongoni mwa waliorejea. Na jambo hili la kuwa wako Watu wa Nahrawaan waliorejea katika upande wa Ali tuliwahi

akapinga vikali kufutwa kwa jina hilo la Uamiri katika mkataba huo, na akasema: "Usilifute jina la Uamiri wa Waislamu, hakika mimi nahofia kwamba ukilifuta halitorudi kwako milele; usilifute hata kama watu watauana (usikubali kulifuta)".[309] Al-Ash'ath bin Qais akasema: "Lifute hili jina",[310] na Ali naye akaunga mkono kufutwa kwa jina hilo akisema: "Allahu Akbar! Sunna kwa Sunna; mfano kwa mfano!"[311] Kisha Al-Imamu Ali akatoa mfano wa Sulhu ya Mtume (s.a.w.) na makafiri wa Makka mwaka wa Hudaibiyah ambapo makafiri hao walimzuia Mtume (s.a.w.) na Masahaba wake wasifanye ibada ya 'Umra; pakatokea mzozo ulioishia kufanyika kwa sulhu baina ya Mtume (s.a.w.) na waliopamoja naye miongoni mwa Waislamu kwa upande mmoja; na makafiri hao wa Makka kwa upande wa pili. Katika sulhu hio, mkataba uliandikwa na Ali, ndiye aliyekuwa muandishi, akaandika – katika mkataba huo – kipengele: "Muhammad, Mjumbe wa Allah". Makafiri wakakataa kuandikwa Mtume (s.a.w.) hivyo na wakasema: "Lau tunajua kuwa wewe ni Mtume wa Allah tusingelikupinga; andika jina lake na jina la baba yake". Mtume (s.a.w.) akakifuta katika mkataba huo kipengele "Muhammad Mjumbe wa Allah" kwa mkono wake[312] na akamuamuru Ali aandike: "Muhammad bin Abdil-Lahi". Ali akafanya hivyo. Kisha Mtume (s.a.w.) akasema: "Jina langu na la baba yangu haliondoshi Unabii wangu". Kwa hivyo, Ali naye akafananisha tukio hili la mzozo wake na Mu'awiya na tukio hilo la sulhu ya Hudaibiyah.[313] Lakini Al-Ahnaf bin Qais akamwambia Al-Imamu Ali:

> Wewe na Mtume (s.a.w.) wapi na wapi! *Wallahi* sisi tulipokubaii wewe[314] hatukukupendelea na hakika ya sisi lau tulimjua yeyote miongoni mwa watu anastahiki zaidi kwa jambo hili la (Ukhalifa) kuliko wewe basi tungelimbaii kisha tukapigana na wewe. Na mimi naapa kwa (jina la) Allah kwamba ikiwa utalifuta jina hili ambalo

---

kulijadili katika ukumbi wa Zanzinet: Majadiliano hayo nimeyakusanya na ndio yatayounda juzuu ya mwisho ya kitabu hiki *Inshaa Allah,* kwa hivyo, suala hilo la waliorejea litakuja katika juzuu hio.

309 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 5.

310 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 5. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 670.

311 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 670. Al-Tabari, ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 5.

312 - Baada ya kuoneshwa sehemu lilipo jina lake kwani yeye hakuwa mwenye kusoma.

313 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 5. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 670-671.

314 - Tulipokuchagua na kuwekeana nawe ahadi ya kukutii.

umeahidina na (Waislamu) juu yake na ukapigana nao (Mu'awiya na wafuasi wake kwalo),basi(jina hilo) halitorudi kwako milele.[315]

Na akamwambia tena: "Hakika yenu nyinyi hamuna (haki au sifa) za Mtume (s.a.w.)".[316] La muhimu ni kuwa Ali ndiye aliyekuwa na uamuzi wa mwisho na kwa hivyo, jina hilo – kufuatia amri yake – likafutwa katika mkataba huo wa sulhu, na ukaandikwa mkataba huo wa sulhu ukibeba anwani isemayo: "Hivi ndivyo walivyohukumiana Ali bin Abi Talib na Muwiya bin Abi Sufyaan..".[317]

Mkataba huo ulikuwa na vipengele vifuatavyo:

1) Waamuzi wawili, Abu Musa wa Iraki na Amru bin Al-'Aas wa Sham, watafuata hukumu ya Qur-an tu:[318] (popote ilipotajwa) kuanzia mwanzo wake hadi mwisho wake.[319]
2) Watakachokikuta katika Kitabu cha Allah watakifuata; wasichokikuta basi marejeo ni katika Sunna za Mtume (s.a.w.), yaani Hadithi zake adili, zenye kuunganisha, zisizofarikisha.[320]
3) Wawakilishi wawili, Abu Musa na Amru bin Al-'Aas, wanachukua ahadi kutoka kwa Ali na Mu'awiya, kwamba wako katika amani pamoja na watu wao na mali zao na

315 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 5. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 670.

316 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 116, Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 48.

317 - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 14-15. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 671.

318 - Watafuata hukumu ya Qur-ani vipi na hukumu ya Qur-ani tangu mwanzo wameshaipinga kwa kukubali kufanya sulhu kinyume na Qur-ani ilivyosema!

319 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 5-6. Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 15. Al-Mas'udi *Al-Muruj* j. 2, uk. 526. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 671. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 108.

320 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 15. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 6. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 671. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 108,103. Maneno "Sunna za Mtume (s.a.w.) yaani Hadithi zake adili, zenye kuunganisha, zisizofarikisha" hayana maana kwamba kuna Sunna nyengine si adili na zinafarikisha, *laa* (sio hivyo), bali maana yake ni kuwa hio ndio sifa ya Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w.) kwamba zinakuwa na sifa hio ya uadilifu na kuwaunganisha Waislamu. Mfano wake ni kama Aya zisemazo: **"Wanawaua Mitume bila ya haki"** hii haina maana kuwa kuna Mitume wengine imeuliwa kwa haki, bali maneno "Bila ya haki" ni sifa mbaya inayokilazimu kitendo hicho cha kuwaua Mitume, kwamba hicho si kitendo cha haki.

Umma uwatetee kwa mujibu wa kile wanachohukumiana (katika mkataba huo).[321]

4) Hukumu ya Wawakilishi wawili, Abu Musa na Amru bin Al-'Aas, imewalazimu Waumini wote.[322]
5) Wawakilishi wawili, Abu Musa na Amru bin Al-'Aas, watahukumu katika Umma huu wala hawataurudisha tena katika vita na mfarakano.[323]
6) Wawakilishaji wawili, Ali na Mu'awiya, wataifuata natija ya hukumu itakayotolewa na waamuzi wawili hao.[324]
7) Ahadi kwamba (Waislamu) wote wataridhika na kilichomo katika mkataba huu.[325]
8) Watu wa Iraki warudi kwao Iraki; na watu wa Sham warudi kwao Sham.[326]
9) Hukumu itafanyika mwezi wa Ramadhan katika mji wa Dumat Al-Jandal au Adhruh.[327]
10) Mahakimu wawili watachukua kutoka kwa kila mmoja – Ali na Mu'awiya – mashahidi wanaotaka wenyewe.[328]

Baada ya kuandikwa mkataba huo, Al-Ash'ath bin Qais akauchukua na akawa anapita nao (mkataba huo) na kuwasomea makabila tafauti yaliokuwemo katika jeshi la Al-Imamu Ali.[329] Lakini mengi[330] katika makabila hayo yakawa yanaupinga mkataba huo. Pia Al-Ashtar, mtu muhimu sana kwa Al-Imamu Ali – alitoa upinzani wa wazi kwa mkataba

321 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 6. Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 4, uk. 15. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 671. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 108.
322 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 6. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 108.
323 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 6. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 109.
324 - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 108.
325 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 15.
326 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 15.
327 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 7. Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 671. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 109. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 15. Na inasemakana kwamba walikutana katika sehemu inayoitwa Al-balqaa. Tazama Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 498,526.
328 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 108.
329 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 6. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 526. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 672. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 110.
330 - Mengi lakini si kwamba ni mengi zaidi ya walioukubali, bali waliokubali ni wengi zaidi kama riwaya nyengine kadha wa kadha zinavyonena.

huo hata ikafika kutupiana maneno makali baina yake na Al-Ash'ath bin Qais.[331] Baada ya Al-Ash'ath bin Qais – ambaye alikuwa akipita na mkataba huo na kuyasomea makabila yaliokuwemo katika jeshi la Ali – kufika nao mkataba huo katika kabila la Banii Tamimi, mtu mmoja anayeitwa Ur-wa bin Udeyyat Al-Tamimi akaupinga vikali akisema:

> Munawafanya watu wahukumu katika kitu ambacho Allah mwenyewe ameshahukumu? Kwani masharti (yenu) ni madhubuti zaidi kuliko Kitabu cha Allah na masharti yake?[332] Kwani nyinyi mulikuwa na shaka pale mwanzo mulipopigana nao? ***"Hakuna hukumu ila ya Allah."***[333]

Makusudio ya Ur-wa bin Udeyyat – naye ndiye mtu wa mwanzo kutoa wito huo[334] – aliposema: "Munawafanya watu wahukumu katika kitu ambacho Allah mwenyewe ameshahukumu," ni kuwa suala hili ni suala ambalo Allah mwenyewe ameshaliamua katika Kitabu chake aliposema:

> **Na ikiwa makundi mawili ya Waislamu yatapigana, basi fanyeni sulhu baina yao, ikiwa moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah.**[335]

Kwa hivyo, kazi ya Ali – na Waislamu wengine – ilikuwa ni kuitekeleza hukumu hii ya Allah iliotajwa katika Aya hii: si kutoa hukumu nyengine kutoka katika ijtihadi zao.

(Basi) wito huo wa Ur-wa ukapata muitiko mkubwa katika jeshi la Al-Imamu Ali (k.w.), hasa hasa wale ambao tangu mwanzo hawakukubaliana na fikra ya kusimamisha vita. Sauti zikapaa kutoka kila sehemu **"Hakuna hukumu ila ya Allah"."** Kikundi cha jeshi la Ali kikamuendea ili waanze

---

331 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 6. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 671-672.

332 - Al-Shahrastani, *Al-Milalu Wa Al-Nihal* j. 1, uk. 134. Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 587.

333 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 110. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 6-7. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 672. Al-Mas'udi ,*Al-Muruj* j. 2, uk. 526. Riwaya hii inapinga dai kwamba watu wa Nahrawaan ndio waliotaka sulhu. Vipi iwe hivyo, na huyu hapa mmoja wao anapinga katika hatua za mwanzo kabisa za tokeo hilo.

334 - Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 587. Na kuna kauli nyengine. Tazama Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 592.

335 - Sura ya 49, Aya 9. Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 122, ili uone kwamba waliopinga sulhu walipinga kwa mujibu wa Aya hii.

vita upya lakini naye akatoa udhuru kwa kusema: "Tumeshafanya baina yetu na baina yao hukumu ya Qur-an, si halali tena kupigana nao mpaka tutazame Qur-an itahukumu nini.[336]

KURUDI KWA ALI AL-KUFA, KUJITENGA KWA *AL-QURRAA* NA MJADALA WAO NA IBN ABBAAS

Hapo jeshi la Iraki la Ali likarudi Al-Kufa hali ya kuwa – kama inavyosema riwaya ya Al-Tabari – "Wamekwenda hali ya kuwa ni wenye kupendana, marafiki; na wamerejea hali ya kuwa ni wenye kuchukiana, maadui"[337] na kama alivyosema Al-Mas'udi: "Watu wakachukiana na ikawa wanatengana; ndugu anajitenga na ndugu yake na mwana akajitenga na baba yake..".[338] Walipofika Al-Kufa, idadi kubwa ya jeshi la Ali likajitenga naye[339] na kukimbilia katika mji wa Al-Harauraa,[340] ulioko karibu na Al-Kufa (Iraki)[341] hali ya kuwa wameshikamana na msimamo wao kwamba: **"Hakuna hukumu ila ya Allah".**[342] Wakakaa hapo – Al-Harauraa – idadi ya watu elfu kumi na mbili.[343] Kisha – kama

336 - Al-Sabi'i, *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. 69-70.

337 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 11. Na mfano wake ni katika Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 673. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 114.

338 - Al-Mas'udi,*Al-Muruj* j. 2, uk. 527.

339 - Al-Mas'udi ,*Al-Muruj* j. 2, uk. 527. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 673-676-678. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 89. Ibn Kathir, *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya* j. 7, uk. 276. Soma vizuri ufahamu: kundi hili ndilo kundi linaloitwa Muhakkima na ndilo linaloitwa Watu wa Nahrawaan (Ahlu Nahrawaan) na ndilo linaloitwa Watu wa Harauraa (Al-Harauriyya), na ndilo linaloitwa Khawarij na ndilo chimbuko la fikra ya Kisiasa ya Kiibadhi, nalo ndilo kundi la Masahaba wa awali na Masahaba Wanavyuoni kama tutakavyoona baadae maneno ya Ibn Abbaas (r.a.) *Inshaa Allah.* Ama huko kuitwa Khawarij ni kama leo Waislamu Mujahidina kuitwa magaidi; hii ndio Sunna ya Mwenyezi Mungu kwa kila anayepigania haki.

340 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12. Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 89. Al-Mas'udi ,*Al-Muruj* j. 2, uk. 527-528. Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 676-678. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 114.

341 - Yaqut Al-Hamwi, *Mu'ujamu Al-Buldan* j. 3, uk. 138.

342 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 89.

343 - Al-Shahrastani, *Al-Milalu Wa Al-Nihal* j. 1, uk. 131. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 678. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 526. Ama Al-Mubarrad, yeye anasema: "Walikuwa idadi yao ni watu elfu sita". Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 591. Na hii inawafikiana na riwaya ya Al-Bayhaqi katika *Al-Kubra* j. 12, uk. 343, riwaya na. 17208. Na Al-Baladhiri anasema walikuwa watu elfu tano. Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 126, na

riwaya Al-Tabari na Al-Baladhiri inavyosema kwamba – baada ya hapo:

> Mmoja wao akanadi akisema kwamba: 'Kiongozi wa vita ni Shabath bin Rib'iy Al-Tamimi na kiongozi wa Sala ni Abdullahi bin Al-Kawaai Al-Yashkuri na jambo (la Ukhalifa) litakuwa la mashauriano baada ya ushindi, na uchaguzi (wa Khalifa utafanyika) kwa ajili ya (dini ya) Mwenyezi Mungu tu, na kuamrisha mema na kukataza mabaya.[344]

Al-Imamu Ali alitaka kujua sababu: kwanini kikundi hicho kimejitenga naye: nini hoja yao? Hapo Ali akamtuma Ibn Abbaas ili aende akafanye nao mdahalo (mjadala) juu ya sababu zao.[345] Ibn Abbaas alipofika huko – kwa mujibu wa riwaya ya Ibn A'atham – alijadiliana na mtu aitwaye 'Attaab bin Al-A'awar Al-Tha'alabi ambaye alikuwa bingwa wa Qur-ani, kama riwaya inavyomsifu kwamba: "Kana kwamba Qur-ani iko mbele ya macho yake".[346] Ufupisho wa mjadala huu ni kuwa baada ya 'Attaab

---

katika sehemu nyengine akataja riwaya nyengine isemayo kuwa walikuwa watu elfu kumi na mbili na inasemekana ni watu elfu sita. Tazama Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 126. Ama katika *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 279, Al-Mas'udi yeye anasema kwamba watu hao walikuwa ni idadi ya watu 4000 tu na baadae wakafarikiana wakabakia 1800 na ikasemwa kwamba walibakia – baada ya kufarikiana – idadi ya watu 1500. Lakini hatimae nikaona katika kitabu *Al-Futuh* cha Ibn A'atham j. 4, uk. 89 maneno haya: "..Kilipoondoka kikundi cha watu walio karibu zaidi naye (waliokaribu zaidi na Ali) nao ni (idadi ya watu) elfu nne wa jeshi la farasi, nao ni katika wale waliokuwa wakiabudu sana, watu wa *Baranis* (Wavaao kofia refu) wakajiunga pamoja nao kiasi cha watu elfu nane (wengine) waliokuwa wakikubaliana nao". Kwa hivyo, inaonesha watu elfu nne aliowataja Al-Mas'udi ni wale wanavyuoni wakubwa tu waliokuwa wakiitwa *Qurraau* ambao ndio waliokuwa wakiabudu sana, na watu elfu nane aliowataja Ibn A'atham ndio watu wengine waliokuwa wakikubaliana nao katika rai. Ukichanganya wote utapata watu elfu kumi na mbili aliowataja Al-Shahrastani na kama alivyosema Ibn A'atham mwenyewe.

344 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 114. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 687.

345 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 90. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 122.

346 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 89. Riwaya ya Ibn Abi Shaiba inasema kuhusu mtu huyo aliyejadiliana naye Ibn Abbaas: "Kana kwamba anatoa hoja yake (labda sahihi ni hoja yake) ndani ya Qur-ani katika Sura moja. Ibn Abbaas akasema (kumwambia mtu huyo): 'Mimi kwa hakika nakuona ni msomi wa Qur-ani, mjuzi ,wa yaliopambanuliwa na yasiyopambanuliwa**".** Tazama Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 727, riwaya na. 37.

kusema ayatakayo, Ibn Abbaas akamwambia mimi nina mifano ninataka nikupigie. 'Attaab akamwambia: 'Sema'. Hapo Ibn Abbaas akampa mifano ya miji ya Kiislamu kwamba ni ya Allah na kwamba kawaamrisha Mitume wake – akiwemo Mtume Muhammad (s.a.w.) – waiimarishe nao wakafanya hivyo. Akauliza Ibn Abbaas: "Je Mtume Muhammad (s.a.w.) aliacha wa kuisimamia miji hii baada yake?" 'Attaab akajibu "Ndio: alikuwa na Masahaba na watu wa nyumba yake (Ahlu Al-Bait) na *wasii* (wake) na kizazi chake". Ibn Abbaas akamuuliza je miji hii iko kama ilivyoachwa na Mtume (s.a.w.) au imebomolewa. 'Attaab akajibu kwamba imebomolewa. Ibn Abbaas akamuuliza je walioibomowa ni kizazi chake au Umma wake. Akamwambia: "Umma wake". Ibn Abbaas akamuuliza je wewe ni katika kizazi au ni katika Umma? Akajibu "Ni katika Umma". Ibn Abbaas akamwambia: "Ewe 'Attaab unatarajia kuokoka nawe ni katika Umma umebomoa mji wa Allah na mji wa Mtume…" Hatimae – kwa mujibu wa riwaya hii – mjadala ukaishia kwa 'Attaab kakubali kuwa Ali ndiye mtu pekee anayestahiki – kwa wakati huu – kuiamirisha miji ya Kiislamu, lakini kakosea kwa kumfanya Abu Musa kuhukumu katika haki ambayo Allah ameshampa yeye (Ali)![347] Baada ya hapa ndipo Ibn Abbaas akatoa hoja zake kutoka katika Qur-ani nao wakatoa jawabu zao kama tutavyobainisha baadae *Inshaa Allah.*

Baada ya haya utaona kwa uwazi ukweli wa yale yaliyosemwa na wataalamu kwamba Ibn A'atham ni "Sunni mwenye kumili katika Ushia" kama Sheikh Al-Sabi'i alivyomnukuu Shakir Mustafaa akisema hivyo katika kitabu chake "*Al-Taarikh Wa Al-Muarrikhun"*[348] na Faruq Umar katika kitabu chake "*Tabi'atu Al-Da'awa Al-'Abbaasiyya";*[349] na kwamba Ibn A'atham "Anakusudia kuandika makosa"[350] bali imesemwa kuwa: "Anasema uwongo, na ni mwenye uchache wa maarifa".[351] Riwaya hii iko wazi kwamba ama kaifinyanga yeye au imefinyangwa mjini kwake Al-Kufa, naye akaiokota na kuitumbukiza katika kitabu

347 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 90-93.

348 - Shakir Mustafaa, *Al-Taarikh Wa Al-Muarrikhun* j. 2, uk. 43.

349 - Faruq Umar, *Tabi'atu Al-Da'awa Al-'Abbaasiyya* uk. 33.

350 - Aliyesema hivyo ni aliyetia maelezo kitabu chake *Al-Futuh* j. 4, uk. 8-9.

351 - Aliyesema hivyo ni aliyetia maelezo kitabu chake *Al-Futuh* j. 3, uk. 70, baada ya Ibn A'atham kuandika kwamba Busr bin Abi Artaa alikufa katika vita vyake na Ubaidi-Lahi bin Abbaas kabla Busr hajaingia Sham alipokuwa akirudi Al-Yaman.

chake, na hili liko wazi katika kudai kwamba jambo hili (la Ukhalifa) baada ya Mtume (s.a.w.) ni la: "Masahaba na watu wa nyumba yake (Ahlu Al-Bait) na wasii na kizazi chake", nayo – kama unavyoona – ni maneno ambayo hayakubaliki kwa Sunni wala kwa Shia wala kwa Ibadhi na watangulizi wao, Watu wa Nahrawaan. Ama Sunni na Ibadhi wao hawakubaliani na suala la kwamba Ukhalifa baada ya Mtume ni wa "Watu wa nyumba yake (Ahlu Al-Bait) na wasii (Ali) na kizazi chake"; ama Shia hawakubali kwamba Ukhalifa baada ya Mtume ni wa "Masahaba". Ama Watu wa Nahrawaan wao – katika suala hili – fikra yao ni sawa na Sunni kwamba Ukhalifa unathibiti kwa njia ya Shura, na walipofika tu huko Al-Harauraa walichagua viongozi wao kwa njia ya Shura, sasa vipi tena Ibn A'atham amnukuu mmoja wao akisema maneno yanayothibitisha uhalali wa shura na uhalali wa wasia kwa Ali na kizazi chake[352] wakati mmoja?.

Tukirudi katika mjadala wa Ibn Abbaas na watu hao wa Nahrawaan. Tunasema kwamba, kwa ufupi ni kuwa hapa riwaya zinagongana – je Ibn Abbaas aliwashinda watu hao kwa hoja na kwa hivyo kusababisha wengi wao kurejea tena katika mji wa Al-Kufa na kuingia katika utawala wa Ali au wao waliziporomoa hoja za Ibn Abbaas na wakamkinaisha kwamba wao ndio waliokuwa katika haki? Lakini pamoja na mgongano huu wa riwaya, riwaya zenye kusema kwamba watu wa Harauraa (ambao baadae ndio Watu wa Nahrawaan) waliziporomoa hoja za Ibn Abbaas na wakamkinaisha ndio riwaya zenye uzito, kwa sababu:

1) Riwaya zote zinakubaliana kwamba Al-Imamu Ali (k.w.) mwenyewe baadae alikwenda kujadiliana nao baada ya kuwa ameshampeleka Ibn Abbaas.[353] Ni wazi kwamba kama Ibn Abbaas aliweza kuwashinda kwa hoja na kuwafanya warejee katika jeshi la Al-Imamu Ali, basi hapakuwa na haja tena ya Ali kwenda huko.

352 - Maana ya maneno: "Wasia kwa Ali na kizazi chake" ni kuwa Mtume (s.a.w.) kausia kuwa Ali bin Abi Talib na kizazi chake wawe ndio Makhalifa baada ya Mtume (s.a.w.), mmoja baada ya mwengine, nao ni idadi ya watu kumi na mbili akiwemo Al-Mahdi Al-Muntadhar. Na itikadi hii ya "Wasia" ni itikadi ya Kishia, nayo haina ushahidi sahihi katika Qur-ani wala katika Sunna iliothibiti. Rejea kitabu chetu *Ukhalifa* j. 1.

353 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 95. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 133.

2) Ibn Abbaas mwenyewe baadae alithibitisha kwamba watu wa Al-Harauraa (baadae ndio Watu wa Nahrawaan) ndio waliokuwa katika haki kama ilivyobainishwa katika kitabu *Al-Musannaf* cha Ibn Abi Shaiba na wengine kama tutavyonukuu maneno yao baadae *Inshaa Allah*.

HOJA ZA IBN ABI AL-HADID

Lakini Ibn Abi Al-Hadid anasisitiza kwamba kushindwa kwa Ibn Abbaas kihoja kumetokana na kitendo chake cha kutofuata wasia aliopewa na Al-Imamu Ali (k.w.), ambapo Ali alimwambia:

> Usijadiliane nao kwa Qur-ani hakika ya Qur-ani inabeba maana nyingi; wewe utasema nao watasema; bali jadiliana nao kwa Sunna (Hadithi), hakika yao hawatopata pakukimbilia![354]

Kisha, akisherehesha maneno yake hayo, Ibn Abi Al-Hadid Al-Mu'utazili, anasema:

> Ikiwa utasema: 'Je (Ibn Abbaas) alijadiliana nao (Watu wa Harauraa) kwa (mujibu wa) wasia wake (Ali)? Nitasema: 'Hapana: bali alijadiliana nao kwa Qur-ani mfano wa kauli yake (Allah isemayo): **"Basi pelekeni muamuzi kutoka upande wake (mume) na muamuzi (mwengine) kutoka upande wake (mke)…."**.[355] Na mfano wa kauli yake (Allah isemayo): **"Wahukumu kwaye (watu) wawili wenye uadilifu miongoni mwenu"**.[356] Na kwa hivyo, hawakurejea (watu hao katika uongozi wa Ali) na (badala yake) vita vikapamba moto; bali – kwa hoja zake (Ibn Abbaas r.a.) – walirejea watu (wachache tu) miongoni mwao.[357]

Hivyo ndivyo alivyosema Ibn Abi Al-Hadid, lakini maneno haya ya Ibn Abi Al-Hadid ni maneno yaliyombali sana na ukweli, kwani Sunna (Hadithi) sahihi ya Mtume (s.a.w.) haipingani na Qur-ani: bali Sunna

354 - Sh. Muhammad Abduh ,*Sharhu Nahji Al-Balagha* j. 3, uk. 358 Hutuba na. 309.
355 - Sura 4, Aya 35.
356 Sura 5, Aya 95.
357 - Ibn Abi Al-Hadid, *Sharhu Nahji Al-Balagha* j. 17, uk. 245.

huwa inaifasiri na kuibainisha maana ya Qur-ani. Ibn Abi Al-Hadid – kwa kuyasema haya – kana kwamba anaona kuwa Hadithi na Qur-ani zinagongana: ukitoa hoja kwa moja, basi ya pili uiwache! Pia alisahau Ibn Abi Al-Hadid kwamba Qur-ani haigongani bali inajifasiri yenyewe kwa yenyewe. Bila shaka ikiwa tutachukua mantiki hio ya Ibn Abi Al-Hadid, basi mtu atakayesema kuwa zina ni haramu itambidi asitoe ushahidi kwa Aya isemayo: **"Wala usiikurubie zina"**[358] na badala yake atoe ushahidi wa Hadithi isemayo: "Watu wa motoni wataudhika kwa harufu ya wazinifu"[359] ili iweze kuthibitisha uharamu wa zina! Lakini labda jawabu ya kufurahisha kwa maneno hayo ya Ibn Abi Al-Hadid ni ile aliyoitoa Sheikh Nassir Al-Sabi'i aliposema:

> Na haya ni maneno ya ajabu, hasa hasa kutokana kwake na Mu'utazili (mtu wa madhehebu ya Mu'utazila) ambaye anajenga (madhehebu yake) kwa akili; kwa sababu njia ambayo ilitakiwa kufanywa sulhu kwayo na uhalali (legitimacy) wa sulhu yenyewe, yamechukuliwa (mambo mawili hayo) kutoka katika Aya mbili hizi na zilizo mfano wake. Kwa hakika, yametangulia (huko nyuma) maneno ya Mu'awiya baada ya kunyanyuliwa Misahafu (kwamba alisema): 'Ili sisi na nyinyi turejee katika kile Allah alichokiamrisha katika Kitabu chake: toeni mtu munayemridhia miongoni mwenu; na sisi tutoe mtu miongoni mwetu…..[360]

<u>*Ninasema:*</u> bali hata Ali mwenyewe – katika mkataba wa sulhu – alisisitiza kuwa ifuatwe Qur-ani: "Kiuliwe kile ambacho Qur-ani imekiua na kihuishwe kile ambacho Qur-ani imekihuisha". Na baada ya kutokea yaliyotokea huko kwenye mkutano wa sulhu kila mtu – akiwemo Ali mwenyewe – alisema kwamba waamuzi wawili hawakuhukumu kwa mujibu wa Qur-ani. Ni wazi kwamba Qur-ani – kama ilivyo katika mas-ala yote ya Kisharia – ilikuwa ndio msingi mkuu ambao ulitarajiwa kutatua migogoro yote iliyojitokeza katika suala hili. Sasa vipi Ibn Abi Al-Hadid ategemee riwaya ya *Nahju Al-Balagha,* na aseme kwamba Ibn Abbaas kashindwa kwa hoja na Watu wa Al-

358 - Sura 17, Aya 32.

359 - Al-Rabi'u bin Habib, *Al-Jami'u Al-Sahih* j. 3, uk. 295, Hadithi na. 767. Anasema mtiaji maelezo: "Na akaitaja mtunzi wa *Kanzu Al-'Ummaal* j. 1, uk. 559, 636.

360 - Al-Sabi'i, *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. 94.

Harauraa kwa sababu alitumia hoja za Qur-ani: hakutumia hoja za Hadithi!

Lakini Ibn Abi Al-Hadid anaendelea kutetea msimamo wake kwa kusema:

> Ikiwa utasema: 'Ni Sunna (Hadithi) zipi hizo ambazo (Ali) alimuamuru Ibn Abbaas ajadiliane nao kwazo?' Nitasema: '…Hakika yake (Ali) alitaka (Ibn Abbaas) awaambie (watu wa Al-Harauraa kwamba) Mtume (s.a.w.) kasema: 'Ali yuko pamoja na haki na haki iko pamoja na Ali inazunguka pamoja naye popote pale anapokwenda', na kauli yake Mtume(s.a.w.) aliposema: 'E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adui wa aliye adui yake; na umnusuru amnusuruye; na muache mkono amuachaye mkono' na Hadithi zilizo mfano wa hizo. [361]

Nasi tunaweza kuyajadili maneno haya ya Ibn Abi Al-Hadid kama ifuatavyo:

Mosi: ni kuwa hizi si Hadithi sahihi. Na inatosha kuonesha kuwa hizo ni Hadithi za kutunga ukweli kwamba Ali mwenyewe – alipokwenda kujadiliana na watu hao baada ya kushindwa Ibn Abbaas kwa hoja – hakuzitaja Hadithi hizo kamwe, wala hakuna yeyote wakati wa mizozo hio aliyezitaja Hadithi hizo, bali Ali mwenyewe alijadiliana nao kwa hio hio Qur-ani: yeye alisema kwamba ameshaahidiana na Mu'awiya na akatoa Aya kwamba kuvunja ahadi haijuzu; na wao Watu wa Harauraa wakatoa Aya kwamba sulhu hio ni kinyume na Qur-ani. Ni wazi kwamba kama ilikuwa kweli Hadithi hizo zilikuwepo wakati huo na kama kweli Ali alimtaka Ibn Abbaas ajadiliane nao kwazo basi angelizitumia yeye mwenyewe Al-Imamu Ali alipokwenda huko. Vipi amuamuru mtu kutumia hoja kadha halafu yeye mwenyewe asizitumie? Na vipi katika mizozo yote hio – tangu *Siffin* – Ali asiwaambie watu kwamba mimi ni *Ma'asum*[362] sikosei na haki "Iko pamoja nami daima inazunguka pamoja nami popote ninapokwenda" kwa hivyo musiende kinyume na nikisemacho?

---

[361] - Ibn Abi Al-Hadid, *Sharhu Nahji Al-Balagha* j. 17, uk. 245.

- M[362]

Pili: ni kuwa hata kama kweli Hadithi hizo ni sahihi, basi bado hazijaleta maana kuwa Ali hakosei, hasa hasa katika mambo kama haya ya kidunia ya kivita, kwani ikiwa Ali "Yuko pamoja na haki na haki iko pamoja na Ali inazunguka pamoja naye popote pale anapokwenda" basi – bila shaka – Mtume (s.a.w.): "Yuko pamoja na haki na haki iko pamoja na Mtume (s.a.w.) inazunguka pamoja naye popote pale anapokwenda" na pamoja na yote hayo, Mtume (s.a.w.) kawacha mambo yaliyobora katika baadhi ya vita na Allah akamu'atibu.[363] Kwa mfano, Aya isemayo: **"Allah kakusamehe! Kwanini umewaruhusu,"**[364] imeteremka kumu'atibu Mtume (s.a.w.) kwa sababu ya kuwapa ruhusa baadhi ya watu waliotoa nyudhuru za uwongo ili wasiende vitani.[365] Kwa hivyo, ikiwa Mtume (s.a.w.) ni kigezo bora na Allah akamu'atibu, vipi Ali asikosee (katika vita hivyo) naye hapati wahyi? Au Ali ni bora zaidi kuliko Mtume (s.a.w.)?

Tatu: ni kuwa kama vile ambavyo kuna riwaya inayomnukuu Mtume (s.a.w.) akisema kuhusu Ali kwamba: "Yuko pamoja na haki na haki iko pamoja na Ali inazunguka pamoja naye popote pale anapokwenda" basi pia kuna riwaya inayomnukuu Mtume (s.a.w.) akisema: "Ammar (bin Yasir) yuko pamoja na haki na haki iko pamoja na Ammar inazunguka pamoja naye popote pale anapokwenda";[366] bali kuna riwaya inayomnukuu Ali mwenyewe akisema kuhusu Ammar bin Yasir – baada ya kupigwa katika vita vya *Siffin* – kwamba "Ammar yuko pamoja na haki na haki iko pamoja na Ammar inazunguka pamoja naye popote pale anapokwenda";[367] na bila shaka maneno haya hayajakusudiwa kwamba Ammar hakosei, bali – ikiwa riwaya hio imethibiti kutoka kwao, basi – wanakusudia kusema kwamba Ammar ni mtu wa haki: hakusudii kufanya isipokuwa haki.

Ama Hadithi isemayo: "E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adui wa aliye adui wake; na umnusuru amnusuruye; na muache mkono

363 - Kusema "Akamuatibu" ni kama kusema: "Akamlaumu," lakini neno "Lawama" ni zito zaidi, kwa hivyo aghlabu ya wanavyuoni huwa hawalitumii kwa Mitume (a.s.).
364 - Sura 9, Aya 43.
365 - Al-Sabuni, *Saf-Watu Al-Tafasir* j. 1, uk. 368.
366 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 269.
367 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 129, na uk. 269. Na imepokewa mfano wake na Al-Hakim katika *Al-Mustadrak* j. 2, uk. 162, Hadithi na. 2652, kutoka kwa Hudhaifa.

amuachaye" ni sehemu ya Hadithi isemayo: "Yule ambaye mimi ni *Maula*[368] wake basi na Ali ni *Maula* wake". Nayo ni Hadithi yenye tafauti juu ya kuthibiti kwake na kutokuthibiti kwake,[369] lakini hata wanaoona kuwa hii ni Hadithi sahihi, basi aghalabu yao wanasema kwamba maneno: 'E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adui wa aliye adui yake…." ni ziada iliyotungwa na kuongezwa katika Hadithi hio.[370] Kwa hali yoyote ile, hata ikiwa Hadithi hii ni sahihi, basi:

a) Maana ni kuwa atayemchukia Ali bure bure tu bila ya kuwepo sababu ya Kisharia ambayo ni wajibu wa Muislamu – kwa mujibu wa sababu hio – kumchukia, basi Allah naye atamchukia. Tunasema hivyo, kwa sababu hii ndio hukumu ya Uislamu kwa watu wote kwamba Allah ni adui wa yeyote anayemchukia Muislamu mcha Mungu bila ya sababu inayokubalika Kisharia, kama Hadithi *Qudsi* inavyosema: **"من عاد لي وليا فقد آذنته في الحرب"** (Atayemfanya kipenzi changu kuwa ni adui (wake) basi nimemtangazia vita).[371] Ama ikiwa kuna sababu ya Kisharia ya

368 - Neno *Maula* linakuwa na maana ya rafiki na kipenzi; na linakuwa na maana ya msimamizi wa mambo. Katika Hadithi hii *Jumhur* imechukua maana ya kwanza na Shia wamechukua maana ya pili.

369 - Mimi ninakubaliana na waliosema kuwa Hadithi hii imethibiti bila ya nyongeza isemayo: "E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adui wa aliye adui wake; na umnusuru amnusuruye; na muache mkono amuachaye".

370 - Miongoni mwa waliosema hivyo ni Al-Imamu Ahmad bin Hanbal, kama alivyomnukuu Ibn Kathir katika *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya* 7, uk. 348. Na pia kaikataa Hadithi hii Ibn Taymiya katika *Minhaju Al-Sunna* j. 4, uk. 86 kwa mujibu wa alivyonukuliwa na Al-Sayyid Al-Saqqaf katika *Al-Salafiyya Al-Wahabiyya* uk. 65. Pia kaikataa Hadithi hio Ibn Hazm kwa mujibu wa alivyomnukuu Al-Sayyid Al-Saqqaf vile vile katika kitabu chake hicho na ukurasa huo. Na hawa wawili wameikataa Hadithi hii nzima ambayo kiukamilifu inasema: "Yule ambaye mimi ni Maula wake basi na Ali ni Maula wake" hio ni sehemu ya kwanza ya Hadithi hio; kisha – katika baadhi ya mapokezi yake – yakaja maneno: "E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adua wa aliye adui wake". Na ukweli ni kuwa sehemu hii ya pili – kama Alivyosema Al-Imamu Ahmad – ndio ziada iliotungwa na kuchomekwa katika Hadithi hii; ama sehemu ya kwanza wengi katika wanavyuoni wameikubali lakini pamoja na hayo Hadithi hio ina maana tafauti na wanavyodhania ndugu zetu wa Kishia. Rejea katika kitabu chetu *Ukhalifa* j. 1, uone maelezo juu ya Hadithi hio na maelezo zaidi yatakuja katika juzuu ya pili *Inshaa Allah.*

371 - Kaipokea Al-Bukhari na akaitaja Al-Imamu Al-Nawawi katika *Riyadhu Al-Salihin* uk. 135, Hadithi na. 387, *Babu 'Alaamati hubbi Allahi lil-abdi.*

kumchukia mtu yeyote awaye, basi kumchukia ni wajibu. Soma – ukipenda – pamoja nami Hadithi isemayo: **"أوثق عرى الإسلام الولاية في الله والبغض في الله"** "Kishiko madhubuti chao cha Uislamu ni kupenda kwa ajili ya Allah na kuchukia kwa ajili ya Allah".[372] Na hii ni kanuni adili kwa watu wote: ni sawa mbele ya kanuni hii mimi na wewe; Abu Bakr na Umar; Uthman na Ali na wengine wote: kila ambaye atakhalifu Kitabu cha Allah au Sunna ya Mtume (s.a.w.) basi ni wajibu wetu kutokumuunga mkono katika hilo hata akiwa bin au bint Rasuli, na atakayetekeleza Kitabu cha Allah au Sunna ya Mtume (s.a.w.) basi ni wajibu wetu kumuunga mkono hata akiwa ni mtu wa tabaka inayodharauliwa kabisa na walimwengu wote. Huu ndio uadilifu wa mbinguni. Kwa hivyo, hata ikiwa Hadithi hio 'E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adua wa aliye adui yake…." ni sahihi, basi ni lazima ifungamanishwe na maandiko mengine ili kufikia tafsiri sahihi, na kwa kufanya hivyo, basi maana ni kumchukia Ali bila ya kosa, na hii ni hukumu ya wote.[373]

b) Ni kuwa Hadithi hii: "E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adui wa aliye adui yake…." hata ingelikuwa sahihi, isingeliwezekana kuwatolea hoja kwayo watu hao waliojitenga na Ali, kwani wao hawakujitenga kwa kuwa wakimchukia bali wao walikuwa wanamsisitiza – tangu mwanzo asisimamishe vita, na baadae – baada ya kusimamisha na kutiliana mkataba na Mu'awiya – wakawa wanamtaka Ali autupilie mbali mkataba huo ili warudi kuwa pamoja naye. Haya yote yanaonesha kwamba wao walikuwa wakimpenda Ali na wakitaka aendelee kuwa Khalifa wao, lakini wao walipojitenga naye, waliona kwamba kitendo chake cha kukubali sulhu na kutiliana mkataba na Mu'awiya ni kinyume na Qur-ani, na kwa sababu Mtume (s.a.w.) kasema: "Hakuna kumtii kiumbe ukamuasi Muumba", basi wao hawakuweza tena kushirikiana naye katika hilo, kwani wao wamembaii (wametoa ahadi ya kumtii) ili aitekeleza Qur-ani na

372 - Al-Tabarani, *Al-Kabir* j. 10, uk. 220, Hadithi na. 10531. Al-Hakim, *Al-Mustadrak* j. 2, uk. 523, Hadithi na. 3790. Na pia wameipokea wegine.

373 - Bali Hadithi hii ina sababu yake ya kutamkwa, na maelezo yake tumeyatoa katika kitabu chetu tulichokiita *Ukhalifa*, rejea huko.

Sunna (Hadithi); akienda kinyume na kimoja ya hivyo, basi Khalifa wa Kiislamu anatakiwa atubie na akikataa basi anauzuliwa. Ali hakuitekeleza hukumu ya Aya ambayo ilimpa haki ya kumpiga Mu'awiya, kama tulivyobainisha na tutavyobainisha zaidi baadae *Inshaa Allah,* na kwa hivyo wakajitenga naye kwa sababu hio, si kwa kutokumpenda.

c) Kama vile ambavyo kuna riwaya hio 'E Allah! Mpende ampendaye (Ali) na kuwa adui wa aliye adui yake…." Pia kuna riwaya isemayo: "Atayemfanyia uadui Ammar (bin Yasir) basi Allah atakuwa adui yake na atayemchukia Ammar Allah atamchuikia".[374] Na bila shaka kama tulivyosema kabla kuwa maneno haya hayamaanishi kwamba Ammar bin Yasir hakosei.

Kwa hivyo, watu hao waliokimbilia Al-Harauraa wakawa wamejitenga na Ali kwa sababu ya kukubali kwake kufanya sulhu na Mu'awiya kinyume na Qur-an. Basi kwa sababu hio na kwa sababu ya kufuta jina lake la Ukhalifa katika mkataba wa sulhu, waliona kuwa Ali hawezi tena kuwa Khalifa wa Waislamu, na kwa hivyo, walichagua Imamu wao mpya kwa njia ya Shura. Imamu mpya waliyemchagua ni Al-Imamu Abdillah bin Wahb Al-Raasbiy[375] (r.a.), naye ni Sahaba kama vitabu vya historia vinavyosema, na tutabainisha baadae *Inshaa Allah.*[376]

Tukirudi tena katika hao waliojitenga na Ali na kuelekea Al-Harauraa, ni kuwa baada ya kukusanyika hapo Al-Harauraa na kujadiliana na Ibn Abbaas na kumshinda kwa hoja na kuchagua Imamu wao mpya, baadae wakaondoka Al-Harauraa na kuelekea katika mji wa Nahrawaan, ambapo walikaa hapo hadi vikaanza vita baina yao na Ali na wakauliwa wote ila wachache sana ndio waliobakia, *Allah awawiye radhi na awaingize katika Firdaws ya juu.*

374 - Al-Hakim, *Al-Mustadrak* j. 3, uk. 441, Hadithi na. 5674.

375 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18-19.

- Katika sura ya mwisho ya kitabu hiki.376

وَيَغْنَمُ أَهْلُ النَّـهْرَوَانِ شَـهَادَةًوَمَا هِيَ إِلاَّ طَعْنَةٌ فَالْمَغَانِمُ**[377]

Na wakafaidika watu wa Nahrawaan wakapata shahada***Na halikuwa ila ni pigo moja tu (la mkuki) tahamaki wameta ng'awira.[378]

Huu ni mukhtasari wa vita hivyo vya *Siffin*, na vipi jeshi la Ali lilifarikiana na vipi na kwanini Watu wa Nahrawaan (r.a.) walijitenga na Ali (k.w.). Kwa hivyo, tunaweza kufupisha maelezo yetu kwa kusema:

1) Vita vya *Siffin* vilipiganwa siku ya Jumatano ya Mfunguo tano mwaka 37 A.H.
2) Sababu ni kukataa kwa Mu'awiya kuingia katika kumtii Al-Imamu Ali.
3) Kisingizio cha Mu'awiya ni kudai damu ya Uthman.
4) Vita vilipopamba moto na ushindi kumuelekea Ali, Mu'awiya akataka sulhu.
5) Kutaka sulhu huko hakukuwa na ukweli wowote ule, bali ilikuwa ni mbinu ya kutaka kulivunja jeshi la Ali na kujijengea nguvu mpya.
6) Jeshi la Ali likatafautiana baina ya wenye kukubali sulhu na wenye kuipinga.
7) Wenye kuipinga sulhu wakajitenga na Ali – kwa sababu ya kukubali kwake sulhu na kufuta jina lake la Ukhalifa katika mkataba wa kusimamisha vita – na wakakimbilia katika mji wa Al-Harauraa na baadae wakaenda katika mji wa Al-Nahrawaan.
8) Watu hawa ndio walioitwa *Khawarij* na ndio chimbuko la fikra ya kisiasa ya Kiibadhi. Na Ibadhi ndio wanaoona kuwa walikuwa katika haki kati ya makundi hayo matatu – Ali, Mu'awiya na Masahaba hao wa Nahrawaan.

Sasa baada ya haya, utaona kwamba tumejua historia hii imekwenda vipi, lakini bado hatujajua haki na batili iko wapi, kwani hatujajua kwa upambanuzi hoja za kila kundi: waliojitenga na Ali walikuwa na hoja

---

377 - Ubeti huu ni katika mashairi ya Mimiyya (yaliyomalizikia vina vyake kwa mimu) ya Al-Imamu Abu Muslim Al-Bahlani, Al-Rawaahi (r.a.). Maana ya neno *ng'awira* lililomo katika ubeti huu, ni kufa shahidi.

378 - Yaani watu hao walikufa Mashahidi, na ushahidi huo ni papo hapo baada ya kupigwa mkuki, upanga au mshale tu, papo hapo wakaupata.

gani za Kisharia, na kwa upande mwengine waliomtetea Ali na kuwaponda au kuwalaumu waliojitenga naye walikuwa na hoja gani. Tumekuwa tukidokeza dokeza huko nyuma ushahidi wa huyu na yule, lakini kwa ufafanuzi wa hoja za kila upande na jawabu za wapinzani wao soma sura inayofuata.

SURA YA TATU

HOJA ZA WATETEZI WA ALI NA JAWABU ZA WATU WA NAHRAWAAN

Tumeona kwamba baada ya Ali kukubali sulhu na kurudi Al-Kufa (Iraki) sehemu ya jeshi lake ilijitenga, na tumeona kwamba sehemu hio ndio hao walioitwa Watu wa Nahrawaan na kuitwa *Al-Khawarij*. Pia tumeona kwamba Ali alimtuma Ibn Abbaas ili aende kujadiliana nao na kujua hoja zao zilizopelekea kujitenga naye. Ibn Abbaas alifanya hivyo. Lakini je Ibn Abbaas alikuwa na hoja gani[379] nao walimjibu nini; nao – kwa upande mwengine – walikuwa na hoja gani? Ibn Abbaas alipokwenda kujadiliana na hao waliojitenga na Ali, aliwajengea hoja kwamba kwa kukubali sulhu, Ali hakukosea. Inaaminika kwamba alitumia Aya kama:

1) **"Sulhu ni kheri."**[380]
2) **"Na wakielekea kwenye sulhu basi nawe elekea (huko)."**[381]
3) **"Hakika ya Waumini ni ndugu basi suluhishaneni baina ya ndugu zenu."**[382]
4) **"Kama mukihofia mzozo baina yao (mke na mume) basi pelekeni muamuzi kutoka upande wake (mume) na muamuzi (mwengine) kutoka upande wake (mke), ikiwa watataka sulhu, basi Allah atawawafikisha."**[383]
5) **"Enyi mulioamini musiue kiwindwa nanyi muko katika kuhirimia; na atakayekiua miongoni mwenu kwa**

---

379 - Tumetaja huko nyuma sehemu ya mjadala wa Ibn Abbaas na watu wa Nahrawaan, ambao umetajwa na riwaya ya Ibn A'atham, lakini mjadala huo kwa namna alivyoutaja Ibn A'atham – kama tulivyosema kabla – umejengeka katika riwaya isiokubalika Kisuni, Kishia wala Kiibadhi. Kwa hivyo, tunasema kuwa huo ni mjadala wa kutunga na kwa hali yoyote ile, huo ni mjadala ambao haujengiewi hoja za kielimu.

380 - Sura 4, Aya 128.

381 - Sura 8, Aya 61.

382 - Sura 49, Aya 9.

383 - Sura 4, Aya 35.

kukusudia, basi alipe mfano wa aliyemuua katika wanyama wanaofugwa, Wahukumu kwaye (watu) wawili wenye uadilifu miongoni mwenu."[384]

Hoja ya Ibn Abbaas katika Aya hizi – na ambayo pia ndio hoja ya watetezi wa Ali – ni kuwa Uislamu umeamuru kufanya sulhu baina ya makundi au watu waliotafautiana, na hili lililotokea baina ya Ali na Mu'awiya ni miongoni mwa tafauti ambazo zinastahiki kufanyiwa sulhu. Na kwa hivyo, Ali hakuwa na kosa kwa kitendo chake cha kukubali kufanya sulhu na Mu'awiya.

Sasa kabla ya kuendelea mbele, kwanza na-tukariri kuubainisha mgongano uliopo hapa ambao pia tuliuashiria huko nyuma! Nao ni kuwa kule Watu wa Nahrawaan wametungiwa riwaya kwamba wao ndio waliotaka sulhu na wakawa wabaya kwa sababu hio; huku Ali anatetewa kwa Aya za Qur-ani kuwa yeye hakukosea kwa kutaka sulhu – bidhaa moja yapimwa kwa mezani mbili! Sasa aliyetaka sulhu ni nani: ni Ali au ni wao? Na aliyekuwa hakukosea kwa kutaka sulhu – kwa mujibu wa Aya hizi – ni Ali au ni wao? Hadithi za kutunga maisha yote hazikai sawa: na batili haidumu milele kama vile ambavyo huna njia ya kuizuia haki isidhihiri!

JAWABU YA WATU WA NAHRAWAAN

Watu wa Nahrawaan nao wakajibu kwamba kuna tafauti kubwa baina ya Aya hizo na Aya ambayo imempa Ali haki ya kupigana na Mu'awiya. Katika Aya hizo alizozitolea hoja Ibn Abbaas, Allah hakutaja hukumu

[384] Sura 5, Aya 95. Aya tatu za mwanzo sikuona kitabu ambacho kinasema kwamba Ibn Abbaas alitoa hoja kwazo, bali nimeona katika makala za muandishi tu akitoa hoja kwazo.

gani ifanywe, bali kaiwakilisha hukumu kwa wenye kufanya sulhu.[385] Na hii ni tafauti na Aya ambayo imempa Ali haki ya kumpiga Mu'awiya ambapo Allah Mwenyewe katoa hukumu, kwa hivyo ilikuwa ni wajibu wa Ali kutekeleza hukumu ya Allah. Aya hio, iliompa Ali haki ya kumpiga Mu'awiya, inasema:

> **Na ikiwa makundi mawili ya Waislamu yatapigana, basi fanyeni sulhu baina yao, ikiwa moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah.**[386]

Utaona kwamba Aya hii ni tafauti na hizo alizozijengea hoja Ibn Abbaas. Kule Allah kaamuru sulhu kwa ujumla tu bila kutoa hukumu gani ifanyike katika sulhu: hapa katoa hukumu juu ya tukio maalamu, nalo ni pale Waislamu watapopigana na mmoja akawa ni asi kama ilivyokuwa baina ya Ali na Mu'awiya. Halkadhalika Aya yenye kuzungumzia sulhu baina ya mke na mume: hakusema Allah sulhu gani ifanywe, bali kawawakilisha wapatanishi wafanye sulhu kwa kadiri wanavyoona wao kwamba italeta maslahi. Na hii pia ni tafauti na Aya hio ambayo imempa Ali haki ya kumpiga Mu'awiya: katika Aya hio Allah Mwenyewe katoa hukumu kwa kusema: **"Ikiwa moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah."**

Watu wa Nahrawaan wakamwambia Ibn Abbaas: "Allah anasema: **"Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, wakateni mikono yao".**[387] Na anasema: **"Na mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, wapigeni kila mmoja kati yao mijeledi mia"**.[388] Je inafaa kufanya sulhu kuhusu watu hawa baada ya kuthibiti kwa ushahidi wa Kisharia kwamba mtu fulani kaiba au kazini? Ibn Abbaas akasema: (Lakini Allah anasema) **"Wahukumu kwaye (watu) wawili wenye**

---

385 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 122.

386 - Sura ya 49, Aya 9.

387 - Sura 5, Aya 38. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12-13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 122.

388 - Sura 64, Aya 2. Al-Tabari,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 12-13. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 122.

uadilifu miongoni mwenu".[389] Aya hii anayoitolea hoja Ibn Abbaas hapa – kama ulivyoona kabla kwamba – kiukamilifu inasema:

> **Enyi mulioamini musiue kiwindwa nanyi muko katika kuhirimia; na atayekiua miongoni mwenu kwa kukusudia, basi alipe mfano wa aliyemuua katika wanyama wanaofugwa, *Wahukumu kwaye (watu) wawili wenye uadilifu miongoni mwenu.***[390]

Nayo – kama unavyoona – ni Aya inayozungumzia kuhusu hukumu za mtu atayeua mnyama wa nchi kavu wakati ameherimia katika Ibada za Hijja na Umra. Watu wa Nahrawaan wakamwambia Ibn Abbaas (r.a.): "Wewe unaifanya hukumu ya kiwindwa (mnyama anayewindwa) na matokeo (yanayotokea) baina ya mtu na mke wake ni kama hukumu katika damu za Waislamu?"[391] Watu wa Nahrawaan wakasema tena kumwambia Ibn Abbaas, haya "Hii Aya (uliyoitoa) iko baina yetu sisi na wewe", yaani haya twende hivyo unavyotaka wewe; Aya hio (ulioitolea hoja) inasema kuwa wahukumu watu wawili waadilifu, "Je huyo Amru bin Al-'Aas – katika uoni wako – ni muadilifu na jana alikuwa akituua

---

389 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679. Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 727-728, riwaya na. 37.

390 - Sura 5, Aya 95.

391 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Dhahir ni kuwa Ibn Abbaas kafanya *Qiyas* kwamba ikiwa mtu na mke wake wakigombana basi tunatakiwa tufanye sulhu basi vipi itakuwa wakigombana Waislamu hadi kufikia kumwaga damu? Pia mwenye kuhirimia akiua mnyama basi wanatakiwa waadilifu wawili wapitishe hukumu sasa itakuwaje damu za watu? Dhahiri huu ndio mtazamo wa Ibn Abbaas. Wakati ukitazama jawabu hio ya watu wa Nahrawaan inayosema: "Wewe unaifanya hukumu ya kiwindwa (mnyama anayewindwa) na matukio (yatokeayo) baina ya mtu na mke wake ni kama hukumu katika damu za Waislamu?" utaona kwamba dhahiri ni kuwa wao wanaona kuwa hiki alichokifanya Ibn Abbaas hapa ni *Qiyas* batili kwani kimejengeka katika mambo tafauti **(الْقِيَاسُ مَعَ الفَارِقِ).** Na hii ni kwa sababu inavyofahamika katika mjumuiko wa maandiko yote haya ni kuwa Allah kawawakilisha watu wafanye sulhu katika mambo madogo madogo na makubwa akayatolea hukumu yeye mwenyewe. Na hili ni sahihi kabisa. Wala haiwezekani kusema kwamba *Qiyas* cha Ibn Abbaas ni katika mlango wa **قياس الأولى**, kwa sabu hio tuliyoitanguliza kwamba Allah anawawakilisha watu kutoa hukumu ya mambo madogo madogo; lakini mambo makubwa akayatolea hukumu mwenyewe. Kwa hivyo, mtazamo wa Watu wa Nahrawaani ni wa ndani sana na unaungwa mkono na ukweli kwamba hicho cha Ibn Abbaas ni **قياس مع النص** ***Qiyaasu ma'a Al-Nassi*** yaani ni kufanya *Qiyas* kilicho dhidi ya andiko, nacho ni *Qiyas* batili.

na kumwaga damu yetu?"[392] Ikiwa (unasema kwamba) yeye ni muadilifu, basi sisi (tuliokuwa pamoja na Ali) si waadilifu kwani tumempiga vita (yeye Amru bin Al-'Aas)".[393] Na mumewafanya watu wahukumu kitu ambacho Allah mwenyewe ameshakihukumu;[394] na Allah ameshapitisha hukumu yake kwa Mu'awiya na kundi lake kwamba wauliwe au warejee (katika haki); na kabla ya hapo tuliwalingania katika Kitabu cha Allah Mtukufu wakakataa….".[395] Hio ndio jawabu ya Watu wa Nahrawaan kwa Ibn Abbaas.

Lakini tukirudi katika maneno ya Watu wa Nahrawaan walipomwambia Ibn Abbaas:

---

392 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13.

393 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 122. Lakini maneno haya: "Je huyo Amru bin Al-'Aas – katika uoni wako – ni muadilifu na jana alikuwa akituua na kumwaga damu yetu?" Ikiwa (unasema kwamba) yeye ni muadilifu, basi sisi (tuliokuwa pamoja na Ali) si waadilifu kwani tumempiga vita (yeye Amru bin Al-'Aas ", tunaweza tukayajadili maneno haya kwa kusema kwamba si wakati wote anapokuwa mtu mmoja ni muadilifu mpinzani wake huwa si muadilifu kwani kuna wakati ambapo watu wawili hupambana kwa sababu kila mmoja anadhania kuwa yeye yumo katika haki na kwa hivyo wote huwa wanapigania haki lakini mmoja huwa kakosea bila kujua. Katika hali kama hii mtu huyo huwa hawezi kutolewa kutoka katika uadilifu. Kisha nasi tunaweza kujibu hoja hio kwamba uadilifu unaozungumziwa ni uadilifu katika elimu ya dhahiri ambayo Allah katutaka sisi viumbe tuhukumiane kwayo: si uadilifu katika elimu ya ghaib ambayo si kazi yetu sisi viumbe. Ikiwa mtu nia yake ilikuwa ni nzuri lakini kakosea, basi sisi tunachoweza kukijua ni lile kosa lake lililotokana na matendo yake na kwalo ndio tunamuhukumu; ama nia yake sisi hatuioni wala hatuna uwezo wa kuijua, ila kuwe kuna *Qarain* (ushahidi) za wazi kwamba nia yake ilikuwa ni mbaya au nzuri. Ninasema: ushahidi wa wazi upo tena kwa maelfu kwamba Mu'awiya na Amru bin Al-'Aas – mbali ya kuwa wamekwenda kinyume na Sharia kwa mujibu wa عِلْمُ الظَّاهِرِ *elimu ya dhahir* basi pia – hawakuwa ni watu wenye nia nzuri kamwe. Na lau kama hapakuwa na ushahidi wowote ila Hadithi isemayo: "Ammar atauliwa na kikundi cha waasi" basi ingelitosha kuwatia hatiani Mu'awiya na Amru bin Al-'Aas . Ukiniambia kwamba kabla yaAmmar kuuliwa , Mu'awiya na Amru bin Al-'Aas hawakuwa wakijua atauliwa na nani. Ukiniambia hivyo nitakujibu kwamba je baada ya kuuliwa Ammar pia hawakujua kauliwa na nani? Je walisimamisha vita na kukiri kwamba – kwa mujibu wa Hadithi hio ambayo hata wao hawakuipinga – wao ndio waliokuwa katika makosa ili tujue kwamba kumbe mwanzo walikosea lakini nia zao zilikuwa nzuri?

394 - Hii ni hoja sahihi na ya haki ambayo ni wajibu wa kila Muislamu anayemuamini Allah, Mtume (s.a.w.) na siku ya mwisho asalim amri mbele yake.

395 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13.

> Aya hio (ulioitolea hoja) inasema kuwa wahukumu watu wawili waadilifu, Je huyo Amru bin Al-'Aas – katika uoni wako – ni muadilifu na jana alikuwa akituua na kumwaga damu yetu.

Tukirudi katika maneno haya, tunamkuta Ibn A'atham ananukuu jawabu ya Ibn Abbaas juu ya maneno haya. Anasema Ibn Abbaas katika riwaya hio ya Ibn A'atham: "Enyi watu! Amru bin Al-'Aas hakuwa hakimu, basi munatutolea hoja kwa yeye? Bali yeye alikuwa hakimu wa Mu'awiya".[396] Hii ndio jawabu ya Ibn Abbaas kwa mujibu wa riwaya ya Ibn A'atham, nayo – bila shaka – ni jawabu ya ajabu na ni vigumu kuikubali kuwa inatokana na mtu kama Ibn Abbaas! Labda tujiulize suali iwe ndio jawabu: nalo ni kuwa Aya aliyoijengea hoja Ibn Abbaas inasema: **"Wahukumu kwaye (watu) wawili wenye uadilifu miongoni mwenu"**[397], na waliohukumu katika kesi hio ni Abu Musa na Amru bin Al-'Aas. Kuhusu Amru bin Al-'Aas, Ibn Abbaas anasema: "Si hakimu" sasa kama Amru bin Al-'Aas si hakimu hao mahakimu wawili waliotajwa katika Aya wako wapi? Je Ibn Abbaas anajenga hoja kwa Aya ambayo wao wenyewe hawakuifuata? Na tukisema kuwa Amru bin Al-'Aas alikuwa ni hakimu, basi suali la Watu wa Nahrawaan walipouliza "Je huyo Amru bin Al-'Aas kwako ni muadilifu" litakuwa ni suali lenye muelekeo wa nguvu. Kwa hali zote mbili, Aya hii haiwezi kuwa hoja: tukijaalia kuwa Amru bin Al-'Aas alikuwa ni hakimu basi yeye hakuwa muadilifu na kama hakuwa hakimu basi hakimu alikuwa ni mmoja na yote ni kinyume na Aya.

MSIMAMO WA IBN ABBAAS BAADA YA KUPATA HOJA ZA WATU WA NAHRAWAAN

Huo ndio mjadala wa Ibn Abbaas na Watu wa Nahrawaan, na hizo ndio hoja za Watu wa Nahrawaan kwa Ibn Abbaas, nazo – kama unavyoona – si hoja bali ni majabali ambayo yalimfanya Ibn Abbaas abadilishe msimamo wake na kuona kuwa haki ilikuwa ni ya watu hao. Vinaeleza vitabu vya historia na riwaya, kwamba Ibn Abbaas – baada ya mjadala

396 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 94.

397 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679.

huo – alisema kwamba Watu wa Nahrawaan: "Wameisibu njia (ya haki)."[398] Na riwaya nyengine inauelezea mdahalo huo wa Ibn Abbaas na Watu wa Nahrawaan ikisema kwamba Ibn Abbaas: "Hakuweza kuwajibu (hoja zao)."[399] Na riwaya nyengine inasema kwamba Ibn Abbaas alirejea wala: "Hakuweza kufanya kitu."[400] Na riwaya nyengine inasema: "Hakuweza kuwathibitishia."[401] Na riwaya nyengine inasema wao Watu wa Nahrawaan: "Walimsimamishia hoja (Ibn Abbaas)."[402] Hizi ni riwaya za wanavyuoni tafauti, zenye lafdhi tafauti lakini maana ni moja nayo ni kuwa Ibn Abbaas alishindwa kuwasimamishia hoja watu hao waliojitenga na Ali na – kinyume chake – wao ndio waliomsimamishia hoja. Na kwa sababu hii ndio maana Ibn Abbaas alikataa kushiriki katika vita dhidi ya ya watu hao wa Nahrawaan na akasema baada ya kutafautiana na Ali:

> Wallahi ni bora nikutane na Allah pamoja na yaliyo katika tumbo la ardhi miongoni mwa dhahabu zake na fedha zake pamoja na vilivyojaa mgongoni kwake[403] kuliko kukutana naye na mimi nimemwaga damu ya Umma huu ili nipate ufalme au Uamiri (uongozi).[404]

Na akasema pia Ibn Abbaas: "Na lau kama kuchukua kwangu mali ilikuwa ni batili, basi (hilo) lingekuwa jepesi kwangu kuliko kushiriki katika (kumwaga) damu ya Muumini."[405]

Hayo ni maneno ya Ibn Abbaas, pamoja na kuyasema maneno hayo, lakini Ibn Abbaas alikuwa mstari wa mbele katika vita vya Ali dhidi ya Mu'awiya huko *Siffin* kama alivyokuwa pamoja na Ali katika vita vya Ali dhidi ya Talha na Zubair huko Basra. Ni wazi kwamba hapa – katika vita hivi vya Ali dhidi ya Watu wa Nahrawaan – Ibn Abbaas alimtia

398 - Al-Shammakhi, *Al-Siyar* j. 1, uk. 72.
399 - Abu Qahtaan, *Al-Siyar* j, uk . 107.
400 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18, na Al-Barrad *Al-Jawaahir* uk. 122.
401 - Ibn Abi Shaibah, *Al-Musannaf* j. 15, uk. 312.
402 - Al-Ya'aqubi, *Al-Taarikh* j. 2, uk. 191.
403 - Mgongoni mwa ardhi, yaani juu ya ardhi.
404 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 2, uk. 398. Ibn Abd Rabbi, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 326. Na mfano wake imo katika *Al-Futuh* j. 4, uk. 75, cha Ibn A'atham.
405 - Al-Qalhati, *Al-Kashf* j. 2, uk. 251. Ibn Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 331.

makosani Ali kwa kuwapiga vita Masahaba[406] hao watukufu wa Nahrawaan, kwani alipojadiliana nao aliona kwamba msimamo wa haki ulikuwa ni msimamo wao, kwani kipimo ni Qur-an na Hadithi sahihi: si fulani na fulani.

IBN ABBAAS AJITENGA NA ALI

Jambo jengine la kuzingatia ni kuwa Ibn Abbaas, baada ya tukio hilo na kupingana na msimamo wa Ali, alijitenga na alikunja virago vyake na kuelekea Makka.[407] Na ingawa kuhama kwa Ibn Abbaas Basra na kwenda Makka kimsingi kulitokana na tafauti zake na Ali juu ya ***beitlmali***; lakini tafauti baina ya Ibn Abbaas na Ali haikuwa katika suala la ***beitilmali*** tu, bali ilikuwa pia ni tafauti iliyotokana na misimamo yao kuhusu Watu wa Nahrawaan. Kama zinavyobainisha riwaya hizo tulizozinukuu, hasa hasa riwaya isemayo: "Na lau kama kuchukua kwangu mali ilikuwa ni batili, basi (hilo) lingekuwa jepesi kwangu kuliko kushiriki katika (kumwaga) damu ya Muumini." Kwa hivyo, kwa kuwa Ibn Abbaas alijitenga na Ali sawa na Watu wa Nahrawaan walivyojitenga naye na kwa sababu zilizo sawa au zenye kukaribiana, Ibn Abbaas – kwa mtazamo wa wafuasi wa Ali na wafuasi wa Mu'awiya – basi naye alitakiwa awe ni miongoni mwa *Khawarij!* Kwa bahati mbaya husikii kusemwa kuwa Ibn Abbaas alikuwa katika *Khawarij* kama ulivyokuwa husikii kuitwa hivyo Talha, Zubair na Mu'awiya – kesi moja hukumu tafauti![408]

406 - Watu wa Nahrawaan ambao ndio chimbuko la fikra ya kisiasa ya Kiibadhi – kama tulivyosema kabla – ni Masahaba, bali wao ndio Masahaba wa awali na Masahaba wanavyuoni kama tutavyobainisha baadae *Inshaa Allah.*

407 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 20.

408 - Na hili ndio tatizo la watu wengi: uadilifu unawashinda: hawauwezi. Kosa lile lile nikilifanya mimi nitaitwa kafiri; lakini akilifanya Sahaba ataitwa mujtahid (kajitahid) kakosea! Mu'awiya kajitenga na Ali na kampiga vita hakuwa mbaya bali ni mujatahid; Watu wa Nahrawaan wamejitenga na Ali tena kwa hoja madhubuti za Kisharia lakini wao ni Makhawarij! Halkadhalika wale wenye kufuata Ahlu Al-Bait, Ali au Al-Hasan au Al-Husain wakikosea si kosa; Pandu na Makame wakikosea, basi huwa wamefanya kufuru! Huu ni Uislamu wa wapi?

Kwa hivyo, hapo – baada ya mjadala huo – Ibn Abbaas ndipo alipoona uzito wa hoja za Watu Nahrawaan. Na vipi asione hivyo na Qur-an inasema kwa uwazi:

> **Na ikiwa makundi mawili ya Waislamu yatapigana, basi fanyeni sulhu baina yao, ikiwa moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah.**

Halafu Qur-ani ikatubainishia katika Aya nyengine kadha wa kadha kwamba: **"Hakuna hukumu ila ya Allah"**[409] na ikasema: **"Basi hukumu baina yao kwa alivyoteremsha Allah,"**[410] na ikasema: **"Na kwamba uhukumu kwa alivyoteremsha Allah,"**[411] na ikasema **"Na wasiohukumu kwa alivyoteremsha Allah hao ni makafiri**[412]**….Hao ni madhalimu**[413]**…..Hao ni mafasiki."**[414] Na kwa hivyo, halkadhalika pale Allah aliposema: **"Ikiwa moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah"** huwezi tena kusema kwamba "Subiri tufanye sulhu" madamu Allah ameshatoa hukumu yake.

MJADALA WA ALI NA WATU WA NAHRAWAAN

Maelezo yaliyotangulia yalikuwa kuhusu mjadala wa Ibn Abbaas na Watu wa Nahrawaan. Sasa na-tutazame mjadala wa Ali na Watu hao wa Nahrawaan.

Hapa kuna riwaya nyengine inayosema – kama tulivyoashiria kabla – kwamba baadae Ali mwenyewe alikwenda huko ili kujadiliana na watu hao. Na hapa pia riwaya zinagongana: je Ali aliwashinda kwa hoja na kusababisha wote kurudi katika kumtii yeye au walirejea baadhi yao tu. Riwaya ya Abi Mikhnaf katika masimulizi ya Al-Tabari –

---

409 - Sura 12, Aya 40-67.
410 - Sura 5, Aya 48.
411 - Sura 5, Aya 49.
412 - Sura 5, Aya 44.
413 - Sura 5, Aya 45.
414 - Sura 5, Aya 47.

akifuatiwa na Ibn Al-Athir – inaeleza kwamba: "Walirejea wote".[415] Lakini Ibn A'atham anasema kwamba waliorudi kwa Ali baada ya mjadala huo ni watu elfu nane na elfu nne wakabakia kuwa dhidi yake. Anasema: "Akawapa amani miongoni mwao watu elfu nane, na wakabakia katika kumpiga vita watu elfu nne".[416] Lakini baina ya kuwepo usemi huu na ule na riwaya hii na ile, unakuta kwamba bado kuikubali riwaya hii ni kitu kigumu. Na hili linabainika baada ya kuutazama mjadala wenyewe na kuzisoma hoja ambazo inaaminika kuwa Ali aliwashinda Watu wa Nahrawaan kwazo. Mjadala huo – na uchambuzi wake kwa ufupi – ni kama unavyofuata:

Ali – baada ya kwenda mwenyewe huko kwa hao waliojitenga naye – alisema:

> Kwanini mumetoka dhidi yetu (mumetoka katika kunitii mimi)? Wakasema: '(Kwa sababu ya) Hukumu (sulhu) yenu siku ya (vita vya) *Siffin*'. (Ali) akasema: 'Nakuulizeni kwa jina la Allah: 'Munakumbuka wakati waliponyanyua Misahafu mukasema: 'Tukiitike Kitabu cha Allah, nikakwambieni: 'Mimi nawajua zaidi watu hawa: hakika wao si watu wa dini wala si watu wa Qur-ani….mukaipinga rai yangu?[417]

Hii ndio hoja ya kwanza ya Ali kwa mujibu wa riwaya hii. Lakini kwa bahati mbaya au nzuri, Watu wa Nahrawaan hawakunukuliwa hapa wakijibu chochote, bali riwaya inaonesha kuwa walikubali na kusalim amri. Lakini, bila shaka utunzi wa riwaya hii ni jambo lililowazi kabisa. Na hii ni kwa kutazama mambo yafuatayo:

Moja: ni – kile tulichokieleza kabla – kwamba riwaya zote zimekubaliana kwamba Watu wa Nahrawaan walipinga sulhu hapo hapo *Siffin* mara tu baada ya Al-Ash'ath bin Qais kuwasomea mkataba, huku wakisema: **"Hakuna hukumu ila ya Allah".** Sasa vipi tena riwaya idai kwamba wao ndio waliotaka sulhu?[418]

---

415 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 679.

416 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 125.

417 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679-680.

418 - Na hili tumelibainisha kwa urefu katika sura 8 hatuna haja ya kulikariri isipokuwa kwa ufupi kiasi cha haja tu ili hoja na jawabu yake iwe na mshikamano.

Pili: ni – kile tulichokieleza kabla vile vile – kwamba baada ya kumalizika mkataba wa *Siffin* na Ali kurudi Al-Kufa, ikawa wanajeshi wake njia nzima wanagombana na kupigana mijeledi: walioitwa *Khawarij* wakawa wanasema kuwambia waliokuwa chini ya utawala wa Ali: "Enyi maadui wa Mwenyezi Mungu, nyinyi mumepaka mafuta kwa nyuma ya chupa[419] katika jambo la Mwenyezi Mungu".[420] Na katika riwaya ya pili:

> Mumepaka mafuta kwa nyuma ya chupa katika jambo la Mwenyezi Mungu na mumewafanya (watu) wahukumu katika (jambo alilokwisha kulihukumu katika) Kitabu chake, na mukafarikiana na jamaa.[421]

Na wale waliokubali sulhu wakawa wanasema: "Nyinyi mumefarikiana na Imamu wetu na kuusambaratisha mkusanyiko wetu".[422] Ni wazi kwamba waliokubali sulhu ni waliokuwa chini ya uongozi wa Ali.

Tatu: ni kuwa riwaya hio inagongana pia na riwaya nyengine ambayo tunapata ndani yake kwamba Ali aliambiwa na Watu wa Nahrawaan kuhusu kukubali sulhu kwamba: "Hio ilikuwa ni dhambi ambayo unatakiwa utubie kutokana na hio",[423] Ali akajibu: "Hio si dhambi".[424] Sasa tazama jinsi riwaya hizi za Al-Tabari zinavyogongana! Kule Ali anawakumbusha Watu wa Nahrawaan kuwa wao ndio waliompinga, yaani kwa kitendo chao cha kukubali sulhu; ikimaanisha kwamba hilo ni kosa lakini yeye Ali siye mtendaji wa kosa hilo. Huku alipoambiwa atubie kutokana na dhambi hio alijibu kuwa: "Hio (kukubali sulhu) si dhambi!"

Nne: ni kuwa juhudi zote zilizofanywa na wanaomtetea Ali katika jambo hili tangu zama za Ibn Abbaas hadi leo, basi zitakuwa hazina maana. Na hii ni kwa kuzingatia ukweli kwamba wote wanaomtetea Ali kwamba kwa kitendo chake cha kukubali sulhu, Ali hakufanya kosa, basi wanategemea Aya kama **"Sulhu ni kheri"** na zilizo mfano wake**.** Sasa Ali kwa mujibu wa riwaya hii – *anakubali kwamba sulhu ni kheri lakini* – anasema kwamba yeye siye aliyetaka sulhu, bali yeye alitaka vita

---

419 - Mumefanya khiyana.
420 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 673.
421 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 114.
422 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 673.
423 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 18.
424 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 18.

viendelee na Watu wa Nahrawaan ndio waliotaka sulhu, na kwa hivyo natija – kwa mujibu wa Aya hizo zilizotumika kumtetea Ali – ni kuwa Watu wa Nahrawaan walitaka kheri na Ali hakuitaka! Hii ndio natija ya kutunga riwaya ili kuuficha ukweli: mwisho wake zakugeukia mwenyewe!

Naturudi katika mjadala wa Ali na Watu wa Nahrawaan. Mjadala unaendelea, na Ali anasema:

> Mulipokataa isipokuwa kufanya mkataba, basi mimi nikawashurutisha mahakimu wawili wafuate hukumu ya Qur-ani: wakiue kilichouliwa na Qur-ani na wakihuishe kilichohuishwa na Qur-ani. Wakihukumu kwa mujibu wa Qur-ani basi haitufalii kumpinga hakimu aliyehukumu kwa mujibu wa Qur-ani, na wakikataa basi sisi tuko mbali na hukumu yao.[425]

Watu wa Nahrawaan – kwa mujibu wa riwaya hii – wakajibu: "Hebu twambie inajuzu kuwafanya watu mahakimu katika (umwagaji wa) damu".[426] Ninasema: jawabu hii ingeelekea lau ingelikuwa katika watu hao hakuna ajuae hata Alifu! Kwa hali yoyote ile, jawabu sahihi ni ile ile waliyomjibu Ibn Abbaas kwayo, nayo ni kuwa "Ni hukumu gani ya Qur-ani uliyowashurutisha waamuzi wawili hao waitekeleze, ilhali kwa kitendo cha kukubali sulhu tu basi umeshaiwacha hukumu ya Quir-ani!" Qur-ani inasema: **"....Ikiwa (kundi) moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah."** Na hii – kama walivyosema Watu wa Nahrawaan – ni sawa na Allah aliposema**: "Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, wakateni mikono yao".**[427] Na aliposema: **"Na mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, wapigeni kila mmoja miongoni mwao mijeledi mia"**.[428] Je inafaa kufanya sulhu kuhusu watu hawa baada ya kuthibiti kwa ushahidi wa Kisharia kwamba mtu fulani kaiba au kazini? Kwa hivyo, ni wazi kwamba tunachoweza kufanyiana sulhu ni kile kitu ambacho Allah na Mtume wake hawakukitolea hukumu. Ama katika

425 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 680.
426 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 680.
427 - Sura 5, Aya 38. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12-13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679.
428 - Sura 64, Aya 2.

suala hili, baada ya kuwa Allah ameshasema: **"…Ikiwa (kundi) moja litaasi dhidi ya jengine basi lipigeni lile lenye kuasi mpaka lirejee katika amri ya Allah,"** na Ali mwenyewe – katika barua yake kwa Mu'awiya – kasema:

> ..Shura (kushauriana juu ya nani awe Khalifa) ni ya Muhajirina na Ansaar pasina wengine. Wakikubaliana juu ya mtu wakamchagua kuwa ni Imamu basi hilo limekuwa ni lenye kumridhisha Allah. Akitoka katika jambo lao mwenye kutoka kwa kuponda au kwa bidaa basi wanamrejesha katika kile alichotoka kutoka katika hicho. Na akikataa basi wamuue kwa sababu ya kufuata njia isio ya Waumini.[429]

Na katika vitabu vya Kishia kuna riwaya isemayo:

> Atayekujieni anataka kuufarikisha mkusanyiko (wenu) na kuupokonya Umma jambo lake (la Ukhalifa) na kutawala bila ya Shura basi muuweni. Hakika ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ameamuru hivyo.[430]

Baada ya kuwepo kwa maandiko haya na yaliyo mfano wa haya, basi elewa kwamba hakuna tena nafasi ya sulhu, bali ama ni kurejea katika Ukhalifa wa haki au upanga na kwa leo ni bunduki, mizinga au mabomu.

Jambo jengine tunalolipata katika riwaya hio ya Al-Tabari kuhusu mjadala wa Ali na Watu wa Nahrawaan, ni kuwa riwaya hio kama tulivyobainisha kabla inasema kwamba "Walirejea wote"[431], yaani watu wote wa Nahrawaan walirejea katika utawala wa Ali baada ya mjadala huo na kushindwa kwa hoja. Ninasema: dai hili linagongana na dai jengine muhimu kwa wale wapinzani wa Watu wa Nahrawaan, nalo ni dai kwamba Ali alikwenda huko ili kuwataka watu hao wawatoe waliomuua Ibn Khabbab. Sasa vipi alikwenda kwa lengo hilo, kisha alipofika – kwa mujibu wa riwaya hii – asilitaje kabisa jambo hilo, bali alitaka watu hao warejee kwake tu, na wakarejea wote na akawapokea!

---

429 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 374. Ibn Abdi Rabih ,*Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 309.

430 - Ahmad Al-Kaatib, *Tatawuru Al-Fikri Al-Siyasi Al-Shii* uk. 444, naye kainukuu kutoka katika kitabu kinachoitwa *Uyunu Al-Akhbaari* cha Al-Sadduuq, j. 2, uk. 62.

431 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 13. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 679.

Sasa kuko wapi huko kudai damu ya Ibn Khabbab hapa?[432] Na zaidi ya hayo, ni kuwa ikiwa watu hao wote walirejea katika utawala wa Ali, vita vya Nahrawaan baina ya Ali na watu hao vilitoka wapi au – kwa lugha nyengine – Ali alipigana na nani kule Nahrawaan na watu hao wote wako chini ya taa (kumtii) yake? Hii ndio natija inayopatikana kutoka katika riwaya hizi zenye mgongano zilizotungwa ili kumtoa fulani katika makosa na kuwatia wengine katika makosa.

Hayo yaliyotangulia ni kuhusu *matn (text)* ya riwaya hio ya Al-Tabari inayohusu mjadala wa Ali na Watu wa Nahrawaan. Ama tukirudi katika *sanad* ya riwaya hio, tunakuta kwamba kuna msimulizi wetu yule yule Abu Mikhnaf, Lut bin Yahya, naye ni dhaifu sana kama tulivyomuelezea kabla.[433] Kwa hivyo, riwaya hii ni dhaifu katika *sanad* yake na *matn* yake.

MAELEZO YA AL-MUBARRAD

Ama Al-Mubarrad, yeye ameuelezea mjadala wa Ali na Watu wa Nahrawaan kwa namna ambayo mwenye kutazama kwa jicho la upekuzi au mwenye kusikiliza kwa sikio sikivu na msomaji kwa kisomo cha kutafakari anaona kwa uwazi ubatili wa riwaya hio, kwani kichwa cha riwaya kinagongana na miguu yake – mwanzo ni maji mwisho ni moto![434] Anasema Al-Mubarrad:

> (Ali) aliwaambia (Watu wa Nahrawaan): 'Hamujui nyinyi kwamba watu hawa (Mu'awiya na kundi lake) waliponyanyua Misahafu nilikwambieni kuwa: 'Hii ni mbinu na udhaifu, na kwamba kama kweli wao walikuwa wanataka hukumu ya Misahafu (walioinyanyua) basi

---

432 - Kwa ufupi ni kuwa riwaya zote *taqriban* juu ya maudhui hii zinagongana. Na hii ni alama ya kuwa aghlabu ya riwaya hizi ni za kutunga.

433 - Tazama maelezo ya chini nambari 24.

434 - Nimepekua vitabu mama vya historia vyote nilivyonavyo juu ya maudhui hii, lakini kwa hakika sijapata kuona ghushi na uwongo kama niliouona katika maudhui hii, na hili liko wazi kwa kila atakayetumia wakati wake kwa kufanya upekuzi wa *matn* za riwaya tafauti ambapo ataona msimulizi mmoja anajigonga katika masimulizi yake mgongano wa ajabu, sikwambii mgongano uliopo baina ya msimulizi mmoja na mwengine!!!

> wasingelinijia kisha wakanitaka tufanye sulhu? Munajua kwamba alikuwepo mmoja wenu akilichukia hilo zaidi kuliko mimi?'[435] Wakasem: 'Ndiyo'. Je munajua kwamba nyinyi mulinilazimisha juu ya hilo mpaka nikakukubalieni, nikashurutisha kwamba hukumu yao (waamuzi wawili, Abu Musa na Amru bin Al-'Aas) itapita (itatekelezwa) madamu wamehukumu kwa (mujibu wa) hukumu ya Allah Mtukufu, na watakapokwenda kinyume basi mimi na nyinyi tuko mbali nao, na nyinyi munajua kwamba hukumu ya Mwenyezi Mungu mimi hainipiti?' Wakasema: 'Ndiyo'. Wakasema (kumwambia Ali): '(Sasa wewe) umewafanya (watu) wahukumu katika dini ya Allah kwa sababu ya rai yetu? Basi (kama ni hivyo) sisi tunakiri kwamba tumekufuru na sisi (sasa) tunatubia, basi kiri kama tulivyokiri sisi na utubie (kama tulivyotubia sisi) tuondoke pamoja nawe kwenda Sham (kupigana na Mu'awiya)'. (Ali) akasema kuwambia wao: "Hamujui kwamba Allah – Sifa zake zimetukuka – kaamuru kuwafanya watu wahukumu katika ugomvi baina ya mtu na mke wake, akasema Allah Mtukufu: **"Basi pelekeni muamuzi kutoka upande wake (mume) na muamuzi (mwengine) kutoka upande wake (mke)…."**,[436] na kuhusu kiwindwa kilichopigwa katika Eneo Tukufu kilicho sawa na robo dinari, akasema Allah Mtukufu: **"Wahukumu kwaye (watu) wawili wenye uadilifu miongoni mwenu.**[437] *Misho wa kunukuu.*[438]

Sasa zingatia vyema mjadala huu: Ali mwanzo kawalaumu Watu wa Nahrawaan kwamba wao ndio waliomlazimisha kukubali kufanya sulhu na kwamba yeye jambo hilo alikuwa analichukia. Lakini mara alipoambiwa:

> Umewafanya (watu) wahukumu katika dini ya Allah kwa sababu ya rai yetu? Basi sisi tunakiri kwamba tumekufuru na sisi tunatubia, basi kiri

---

435 - Maneno haya: "Munajua kwamba alikuwepo mmoja wenu akilichukia hilo zaidi kuliko mimi" ni makosa ama ya mpokezi au ya mchapishaji; na usahihi wake ni: "Munajua kwamba hakukuwa na yeyote katika nyinyi aliyelichukia hilo zaidi kuliko mimi?" kama ilivyo katika kitabu hicho hicho cha Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 605 na kitabu cha Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 122. *Wallahu A'alam.*

436 - Sura 4, Aya 35.

437 - Sura 5, Aya 95.

438 - Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 588. Kisha Al-Mubarrad akaisimulia tena riwaya hii katika sehemu nyengine ya kitabu chake, lakini maelezo ya sehemu ya pili tafauti na hayo ya hapa, jambo ambalo linathibisha hayo niliyokwambia kabla ya kuwepo mgongano mkubwa wa riwaya hizi. Tazama Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 605.

> kama tulivyokiri sisi na utubie tuondoke pamoja nawe kwenda Sham (kupigana na Mu'awiya).

Ali akatoa hoja kwa Aya hizo tulizozinukuu kuonesha kwamba hilo la kukubali sulhu si kosa, bali ni jambo jema lenye kuamrishwa na Aya za Qur-ani! Sasa vipi mwanzo awalaumu kwamba wao ndio waliomlazimisha naye alikuwa jambo hilo analichukia kisha mwisho alitetee kwa Aya za Qur-ani kwamba hilo ni jambo jema. Sasa kama ni jambo jema lenye kuamrishwa na Allah katika Qur-ani na waliolitaka ni walioitwa *Khawarij,* kwanini tena awalaumu kwalo? Ni wazi kwamba yote haya yalitungwa ili kuufunika ukweli, na kwa hivyo, natija ni kuwepo kwa mgongano huu unaouona. Na ukiifungamanisha riwaya hio iliyotangulia na riwaya inayomnukuu Ali akisema:

> Amesema uwongo aliyedai kwamba mimi nimeghairi kuikubali sulhu. Basi (ninasema kwamba) atakayeiona (hio sulhu) kuwa ni upotovu, basi yeye ni mpotovu zaidi.[439]

Ukiifungamanisha riwaya ya mwanzo ya Al-Mubarrad na riwaya hii, bila shaka utaona jinsi gani riwaya hii ya pili inavyogongana na kitendo cha Ali cha kuwalaumu Watu wa Nahrawaan kwa kukubali sulhu, kwani kule anawalaumu kwa hilo na huku anasema "…Atakayeiona (hio sulhu) kuwa ni upotovu, basi yeye ni mpotovu zaidi". Hii ina maana kwamba yeye ndiye aliyetaka sulhu, na kwamba wao hawakutaka, wakati kule wao ndio waliotaka yeye hakutaka! Changanya riwaya hio na riwaya ya Ali alipoambiwa kwamba Al-Ashtar hakuridhika na mkataba wa sulhu, Ali alijibu: "Hata mimi sikuridhika lakini kurejea baada ya mkataba haifai,"[440] utapata mgongano mkubwa wa riwaya hizi, jambo ambalo linaeleza ukweli kwamba riwaya zote hizi au asilimia kubwa ya riwaya hizi zinatokana na utunzi wa watu.

Baada ya yote hayo, na baada ya kutazama matukio yalivyokwenda na misimamo ilivyokuwa, basi itakubainikia kwamba lafdhi sahihi ya riwaya hio ya Ali alipojadiliana na Watu wa Nahrawaan, ni lafdhi isemayo:

---

439 - Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 605.

440 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 110.

> Je munajua kwamba mimi nilikuwa ndiye mwenye kuchukia zaidi sulhu na kusimamisha vita miongoni mwenu; (nilichukia kusimamisha vita na kufanya sulhu) baina yetu na watu hao na nikakujuilisheni kwamba wao hakika wameinyanyua Misahafu kwa hadaa na mbinu tu, **basi rai yangu ikapingwa**.[441]

Hii – kwa kutazama matukio yote na kulifungamanisha kila tukio moja na jengine, basi inaonesha kuwa – ndio lafdhi sahihi ya riwaya hii. Lakini wapinzani wa Watu wa Nahrawaan, wamebadilisha maneno **"Ikapingwa"** yenye kumaanisha kwamba walioipinga rai hio si Watu wa Nahrawaan, na badala yake wakaweka maneno: **"Mukaipinga"** ili kuonesha kuwa walioipinga rai hio ni Watu wa Nahrawaan. Lakini baada ya kuwa riwaya zote zimekubaliana kwamba:

1) Walioipinga rai ya Ali ni wale waliokuwa wengi.
2) Watu wa Nahrawaan walitangaza upinzani wao hapo hapo *Siffin* mara tu baada ya kuandikwa mkataba.

Basi – baada ya hayo – elewa kwamba maneno **"rai yangu ikapingwa"** ndio sahihi na maneno **"rai yangu mukaipinga",** ama ni kosa la wasimulizi au ni utunzi wao.

MAELEZO YA AL-SHAHRASTANI

Ama Al-Shahrastani, yeye katika kuutetea kwake msimamo wa Ali katika tukio hilo la kuwafanya watu wahukumu katika tafauti hizo ziliotokea baina yake na Mu'awiya, ana hiki cha kutueleza: "Pili ni kuwa kuwafanya watu wahukumu inajuzu, kwani watu ndio wenye kuhukumu katika mas-ala haya".[442] *Mwisho wa kunukuu.* Hivyo ndivyo alivyosema, nayo ni maneno ya ajabu kutoka kwa mtu mwanachuoni! Kwani lawama ambazo Watu wa Nahrawaan walimlaumu Ali kwazo, si kitendo chake cha "Kuwafanya watu wahukumu" tu; bali ni "Kuwafanya watu wahukumu katika jambo ambalo Allah mwenyewe ameshahukumu", na wakatoa mfano wa mzinifu na mwizi ambao hukumu zao Allah ameshazitaja: je Ali ana mamlaka ya kuleta sulhu kwa watu hao?

---

441 k.h.j, uk. 122.

442 - Al-Shahrastani, *Al-Milalu Wa Al-Nihal* j. 1, uk. 132.

Baada ya haya, utaona kwamba hoja za Ali kwa Watu wa Nahrawaan, katika mjadala huu, ni hoja zenye udhaifu sana na pia ni zenye kugongana na hoja zilizomo katika riwaya nyengine. Na kwa ufupi, ni kuwa tukichukulia kwamba yaliyosemwa katika mjadala huo ni sahihi kuhusishwa kwake na Ali, basi Ali atakuwa hakutoa hoja sahihi iliyojengeka juu ya misingi ya Qur-ani au Hadithi sahihi ya Mtume (s.a.w.): hakuweza kutoa hoja ambayo iliweza kuthibitisha kwamba yeye alikuwa yuko katika msimamo sahihi na Watu wa Nahrawaan walikuwa wamekosea; bali kinyume chake wao ndio walioweza kutoa hoja sahihi kutoka katika Qur-ani zenye kuonesha kwamba wao ndio waliokuwa katika msimamo sahihi.

NATIJA NA MUKHTASARI WA SEHEMU HII

Baada ya haya, tunachoweza kukisema ni kuwa, kwa mkusanyiko wa Aya zote tulizozinukuu katika mjadala wa Ibn Abbaas na Watu wa Nahrawaan na mjadala wa Ali na watu hao, nazo ni Aya zenye kuhimiza sulhu kama alivyozitolea hoja Ibn Abbaas na Aya walizozitolea hoja Watu wa Nahrawaan kumjibu Ibn Abbaas, zina maana kuwa:

1) Sulhu ni kheri pale ambapo Allah hakutaja hukumu.
2) Alipotaja hukumu, sulhu ni batili, na badala yake ni lazima itekelezwe hukumu ya Allah. Na kwa hivyo katika Aya hizo walizozitegemea watetezi wa Ali katika tukio hilo[443] kama ni hoja kwamba Ali alisibu na Watu wa Nahrawaan walikosea, tunaona kwamba Aya ndizo lakini hoja yao ni batili kwani:
    a) Aya hizo hazikutaja hukumu gani.
    b) Aya ambayo Watu wa Nahrawaan waliitolea hoja dhidi ya Ali, ndani yake Allah katoa hukumu yake.
    c) Ali kwa bahati mbaya sana ilimpita hukumu ya Allah iliyomo katika Aya hio, na badala yake akawafanya watu wawe mahakimu katika jambo ambalo Allah mwenyewe ameshalitolea hukumu.
    d) Na kwa hivyo wanaofuata haki (nayo ni Qur-an na Sunna: sio fulani na fulani), wakaamua kujitenga na Ali, kwa sababu

[443] - Sote ni watetezi wa Ali, lakini kila mtu apewe haki yake, kwani kutetea maana yake si kuwadhulumu wengine.

ya kwenda kwake kinyume na Qur-an (Si kwa uovu, lakini kwa kukosea kama binaadamu yeyote): Qur-an inasema **"Wapigeni mpaka warejee katika amri ya Allah."** Je Ali alifanya hivyo? Kwa hivyo, hio ndio sababu iliyowapelekea Watu wa Nahrawaan kujimegua kutoka katika jeshi la Ali. Na hizo ndizo hoja zao. Je enyi wenye kusoma kitu kwa kufahamu na kutumia bongo zenu vyema hapo kosa lilikuwa ni la nani? Hukumuni kwa uadilifu, na huo ndio wajibu wa kila Muislamu: kufanya uadilifu katika hukumu na kumpa haki mwenye haki yake na kumtetea aliyedhulumiwa hata akiwa Yahudi au Nasara na kutokukubaliana na aliyedhulumu hata akiwa ni mtoto wa Nabii. Huu ndio Uislamu aliokujanao Mtume Muhammad (s.a.w.).

SURA YA NNE

KUFUTWA JINA LA UKHALIFA: JAMBO LA PILI LILILOWAPELEKEA WATU WA NAHRAWAAN KUJITENGA NA ALI NA KUCHAGUA IMAMU WAO

Tumeona – katika maelezo yaliyotangulia – kwamba jambo moja ambalo lilileta mzozo mkubwa baina ya wafuasi wa Ali wenyewe kwa wenyewe kwa upande mmoja; na wao pamoja na wafuasi wa Mu'awiya kwa upande wa pili, ni suala la kufutwa kwa jina la Uamiri (Uongozi wa Waislamu) wa Al-Imamu Ali bin Abi Talib katika mkataba huo wa sulhu. Tumebainisha huko nyuma kisa chenyewe kwamba baada ya Mu'awiya na wafuasi wake kufanya mbinu ya kunyanyua Misahafu juu ya mikuki ikiwa kama ni ishara ya kutaka vita visitishwe, kilichofuatia ni kutiliana mkataba wa kusimamisha vita hadi itapofika tarehe na mwezi walioahidiana ambapo itafanyika sulhu baina ya pande mbili hizo. Ali akawa katumia – katika maandiko yake – kipengele kinachomtaja yeye kuwa ni Amiri. Upande wa Mu'awiya ukapinga Ali kutumia kipengele hicho katika uandishi wa mkataba wa amani na akasema Mu'awiya: "Ikiwa unataka sulhu, basi jina la Uamiri lifute".[444] Na katika riwaya nyengine Mu'awiya akasema: "Hakika yangu lau niliridhia kuwa wewe ni *Amiri Al-Mu-uminin* (Kiongozi wa Waislamu) basi nisingelipigana na wewe".[445] Ama Amru bin Al-'Aas – kwa upande wake – yeye (katika uandishi huo wa mkataba) alimwambia muandishi aliyekuwa katika wafuasi wa Ali: "Andika jina lake na jina la baba yake; yeye ni Amiri wenu; ama sisi si Amiri wetu".[446] Na hatimae – baada ya vuta-nikuvute – Ali akaamuru kufutwa jina lake la Ukhalifa.

444 - Al-Sabi'i, *Al-Khawarij* uk. 103, naye kainukuu kutoka kwa Al-Iraqiy, *Al-Mustafaad* j. 3, 1589.

445 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 197. Ibn Kathir, *Al-Bidayah Wa Al-Nihayah* j. 7, uk. 278. Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 116.

446 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 3, uk. 103.

Lakini jambo la kusikitisha ni kuwa Al-Imamu Ali alikwishakupewa tahadhari tangu mwanzo kwamba asikubali kulifuta jina la "Ukhalifa". Al-Ahnaf bin Qais – mmoja wa wafuasi wake ambao baadae walijitenga na Ali – kama tulivyonukuu maneno yake kabla, alimshikilia sana kwamba asikubali kulifuta jina la 'Ukhalifa', akamwambia:

> Wewe na Mtume (s.a.w.) wapi na wapi?! *Wallahi* sisi tulipokubaii hatukukupendelea na hakika yetu lau tulimjua yeyote miongoni mwa watu anastahiki zaidi kwa jambo hili la(ukhalifa) kuliko wewe basi tungelimbaii kisha tukapigana na wewe. Na mimi naapa kwa (jina la) Allah kwamba ikiwa utalifuta jina hili ambalo umeahidina na (Waislamu) juu yake na ukapigana nao (Mu'awiya na wafuasi wake kwalo),basi(jina hilo) halitorudi kwako milele.[447]

Na akamwambia: "Hakika yenu nyinyi hamuna (haki au sifa sawa na) za Mtume (s.a.w.)".[448] Lakini baada ya yote hayo, hatima ni kuwa Ali alilifuta jina lake la Ukhalifa katika mkataba huo wa amani, na badala ya kuandika "Amiru Al-Mu-uminin" akakubali kuandika "Ali bin Abi Talib" tu. Na kwa hivyo, katika mkataba huo wa amani Ali alikubali kuuvua Ukhalifa. Anasema Al-Sabi'i akimnukuu Jueit kutoka katika kitabu chake *Al-Fitnah*[449]

> Na kwa kufanya hivyo, ikawa Ali kajiweka katika nafasi ya usawa na Mu'awiya na hakuwa tena isipokuwa ni Kiongozi wa Wairaki kama vile ambavyo Mu'awiya ni kiongozi wa wafuasi (wake) wa Sham (Syria).[450]

Na kwa hivyo, Ali hapa hakuwa tena Amiri wa Umma wa Kiislamu, bali ni Amiri wa Wairaki![451] Na hili ni jambo jengine ambalo liliwapelekea wale waliokuwa wakipinga sulhu kujitenga na Ali na kuchagua kiongozi wao, kwani kwa kitendo hicho cha kufuta jina la Ukhalifa Ali hakuwa Khalifa tena ila ikiwa atachaguliwa tena mara ya pili. Na – kwa bahati mbaya au nzuri – hakuchaguliwa tena na Umma.

---

447 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 5.

448 - Al-Baradi, *Al-Jawahir* uk. 116. Al-Shammakhi, *Al-Siyar* j. 1, uk. 48.

449 - Jueit, *Al-Fitnah* uk. 212.

450 - Al-Sabi'i, *Al-Khawarij* uk. 103.

451 - Kumbuka kwamba huu ni mkataba na Waislamu: hakuna mchezo wala maskhara ndani yake: utalokubali kulinena au kiliandika basi linazingatiwa.

Lakini pamoja na yote hayo, Ali na watetezi wake hawakuacha kuutetea msimamo wao kwa hoja japokuwa ni dhaifu kama nyumba ya buibui! Hoja kubwa wanayoitegemea ni *Qiyas* cha (kulinganisha) kitendo hicho cha Ali cha kufuta jina lake la Ukhalifa na kitendo cha Mtume (s.a.w.) cha kufuta jina lake la Utume katika mkataba wa Hudaibiyah ujulikanao kwa jina la *Sulhu Hudaibiyah*. Sulhu hii ilifanyika baada ya Mtume (s.a.w.) na Masahaba wake kuzuiwa na makafiri wasiingie Makka kufanya ibada ya Umra. Pakatokea mizozano ya hapa na pale na hatimae pakafanyika sulhu baina ya Waislamu na makafiri, na Ali bin Abi Talib akawa ndiye muandishi wa Mtume (s.a.w.). Mtume (s.a.w.) akamwambia Ali andika: "Hii ndio sulhu aliofanya Muhammad, Mjumbe wa Allah".[452] Kipengele "Mjumbe wa Allah" makafiri wakakataa kukitambua na muwakilishi wao akasema:

> Lau tunajua kuwa wewe ni Mjumbe wa Allah tusingelikuzuia (usiingie katika) Nyumba (Takatifu, yaani Al-Ka'abah) wala tusingelipigana nawe, lakini andika: 'Muhammad bin Abdillahi.[453]

Hapo Mtume (s.a.w.) akamuamuru Ali aandike: "Muhammad bin Abdillahi" na afute jina "Mtume wa Allah". Ali akakataa; Mtume (s.a.w.) akalifuta kwa mkono wake.[454]

Hoja yao hapa ni – kama tulivyotangulia kusema – kwamba Mtume (s.a.w.) mwenyewe kakubali kufuta jina la Utume katika mkataba wa amani, basi nini kosa la Ali kufuta jina la Uamiri katika mkataba kama huo.

Ama wasiokubaliana na kitendo hicho, ni kama tulivyoona katika maneno na tahadhari aliyoitoa Al-Ahnaf bin Qais alipomwambia Ali kwamba: "Hata kama watu watauana (usikubali kulifuta)"[455] na akamwambia "Wewe na Mtume (s.a.w.) wapi na wapi?!"[456] Na akamwambia: "Hakika yenu nyinyi hamuna (haki au sifa sawa na) za

452 - Al-Mubarakfuri, *Al-Rahiqu Al-Makhtum* uk. 284.
453 - Al-Mubarakfuri, *Al-Rahiqu Al-Makhtum* uk. 284.
454 - Al-Mubarakfuri, *Al-Rahiqu Al-Makhtum* uk. 284.
455 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 3, uk. 103.
456 - Tazama lugha ya watu walioufahamu Uislamu.

Mtume (s.a.w.)".[457] Kwa hivyo, waliokipinga kitendo hicho cha Ali cha kufuta jina la Ukhalifa walikuwa wanaona kwamba hizi ni kesi mbili tafauti zimetafautika kwa kutafautika wahusika na kwa hivyo huwezi kuzifanyia *Qiyas* (kuzilinganisha).

Labda maelezo ambayo yameweza kutoa picha ya wazi zaidi juu ya tafauti ya kesi ya Ali na Mu'awiya kwa upande mmoja; na ile ya Mtume (s.a.w.) na makafiri wa Makka kwa upande wa pili, ni kama alivyoelezea Al-Imamu Nuru Al-Din Al-Salimi (r.a.). Anasema Al-Imamu Al-Salimi maneno yenye maana kwamba:

> Tafauti iliopo baina ya Utume na Uimamu au Ukhalifa ni kuwa Utume mfano wake ni kama mtu na mama yake: akimkubali kuwa ni mama yake basi ni mama yake; akimkataa na kusema kuwa si mama yake basi bado ni mama yake vile vile – akamtaka asimtake. Halkadhalika Utume: Mtume (s.a.w.) ukimkubali au ukimkataa yeye ni Mtume; halkadhalika hata yeye akifuta jina la Utume bado ni Mtume vile vile, wala hawezi kujiuzulu akasema mimi Utume basi na hata akisema hivyo basi bado ni Mtume vile vile. Ama Khalifa au Amiri yeye mfano wake ni kama mtu na mke wake. Akimwambia: "talaka" basi si mke wake tena. Halkadhalika Khalifa atakapojiuzulu au kukubali kufuta Ukhalifa wake basi huwa si Khalifa tena.[458]

Hii ni kusema kwamba kuna tafauti kubwa baina ya Mtume na asiyekuwa Mtume. Mtume kachaguliwa na Allah wakati asiyekuwa Mtume kachaguliwa na watu kwa njia ya shura na mikataba.[459] Na kwa

---

457 - Al-Baradi, *Al-Jawahir* uk. 116, Al-Shammakhi, *Al-Siyar* j. 1, uk. 48.

458 - Al-Salimi ,*Jawabatu Al-Salimi* j. 6, uk. 21-22.

459 - Labda jawabu hii inawafaa wale wanaona kwamba Ukhalifa hupatikana kwa njia ya shura nao ni Jumhuri (majority) ya Waislamu. Ama Shia wao wanasema kwamba Makhalifa au Maimamu wao kumi na mbili kuanzia Ali walichaguliwa na Allah na Mtume wake. Kwa hivyo, wao jawabu hii hapa haiwafaii. Lakini kwa hapa tunasema kwamba dai hilo halina ushahidi sahihi. Kwa hali yoyote ile Ali kafikia cheo hicho cha ukhalifa kwa njia ya shura, hii ni kusema kwamba kafikia cheo cha ukhalifa kwa kuchaguliwa na watu na kwa hivyo, akijiuzulu basi anakuwa si Khalifa tena wa watu. Na lau kama yeye anaona kwamba shura ni batili, basi kwanini tena akubali kuchaguliwa kwa njia batili? Sikusudii kubaiiwa: yeye kachaguliwa kwa shura kama wenzake na akabaiiwa kama wenzake. Maelezo hapa ni marefu, unaweza kurejea sura ya saba ya kitabu chetu"*Mezani Ya Haki* "na pia rejea kitabu chetu "*Ukhalifa"* ili kuweza kujua maudhui hii kwa upana zaidi.

hivyo, Mtume hata akisema mimi si Mtume tena bado anaendelea kuwa Mtume wakati Amiri akisema mimi si Amiri tena basi huwa Uamiri wake umefutika. Hii ndio tafauti ya Mtume (s.a.w.) na Ali bin Abi Talib. Na kwa hivyo, *Qiyas* hicho cha kulinganisha kitendo cha Mtume (s.a.w.) cha kufuta jina lake la Utume katika Sulhu ya Hudaibiyah na kitendo cha Ali cha kufuta jina lake la Uamiri katika sulhu ya *Siffin*, ni *Qiyas* batili kwani kimejengeka katika mambo tafauti **(الْقِيَاسُ مَعَ الفَـارِقِ),** wakati sharti ya msingi na ya lazima ya *Qiyas* ni: **""ُوجُوْدُ الْمُسَاوَاةِ بَيْنَ الأَصْلِ وَالْفَرْعِ** kuwepo usawa baina ya Shina na Tawi, jambo ambalo kwa hapa limekosekana kabisa.

Na miongoni mwa mambo yenye kubainisha zaidi kwamba jambo la kufuta uongozi katika mkataba ni mahususi kwa Mtume (s.a.w.) na kwamba Mtume (s.a.w.) alifanya hayo kwa Wahyi, ni yale aliyoyaeleza Sheikh Nasir Al-Sabi'i katika kitabu chake "*Al-Khawarij Wa Al-Haqiqtu Al-Ghaiba.* Anaeleza kwamba, Masahaba waliupinga mkataba huo wa Hudaibiya na waliona kwamba yaliyomo katika mkataba huo ni kuwanyima Waislamu haki zao. Na kwa hivyo, Ali alikataa kulifuta jina la Utume; Umar bin Al-Khattab (r.a.) naye alimg'ang'ania Mtume (s.a.w.) huku akisema:

> Ewe Mtume wa Allah! Kwani sisi si tumo katika haki na wao wamo katika batili? Akasema: 'Ndio'. Akasema: 'Kwani si watakaouliwa kwetu wako peponi na watakaouliwa kwao wako motoni?' Akasema: 'Ndio'. Akasema : 'Basi kwanini tutoe *dania*[460] katika dini yetu.[461]

Lakini jawabu ya Mtume (s.a.w.) kwa Umar, ilikuwa ni tangazo la wazi kwamba yeye kalifanya alilolifanya kwa sababu ya Utume wake. Na hiki ndicho alichokisema Mtume (s.a.w.) – ikiwa kama ni jawabu kwa Umar – kwamba: **"(..إنـي رسـول الله ولـن يضـيعني أبدا)** *Innii Rasulu L-llahi walan yudhiiani abadan.* (..Kwani mimi ni Mtume wa Allah na hatonitupa milele)". Anasema Sheikh Al-Sabi'i maneno yenye maana kwamba katika kauli hii ya Mtume (s.a.w.) aliposema: "..Kwani mimi ni Mtume

460 - *Dania* ni kitu kidogo sana na dhalili. Na makusudio ni kuwa kwanini tunakubali kuwapa hata kitu kidogo na kujitoa katika haki yetu *(kutanazal)* na sisi ndio tulio katika haki!

461 - Al-Mubarakfuri, *Al-Rahiqu Al-Makhtum* uk. 284.

wa Allah na hatonitupa milele" kuna ubainifu wa wazi kwamba jambo hilo ni mahususi kwa Mtume (s.a.w.), na ni ubainifu wa ahadi ya Allah kwa Mtume wake kwamba katika mkataba huo wa Hudaibiya hatima njema itakuwa ni ya Waislamu. Na hatimae hali ikawa hivyo – natija ya sulhu ya Hudaibiyah ni ufunguzi wa Makka wakati hatima ya sulhu ya *Siffin* ni kumuuzulu Ali kutoka katika cheo cha Ukhalifa.[462]

Ninasema tukirudi nyuma kidogo katika maneno ya Mtume (s.a.w.) aliposema: **"إني رسول الله ولن يضيعني أبدا)** *Innii Rasulu L-llahi walan yudhiiani abadan.* (Kwani mimi ni Mtume wa Allah na hatonitupa milele)", ni kuwa lafdhi hii **إني** *Innii* ambayo Mtume (s.a.w.) kaitumia katika kumjibu Umar (r.a.), ni lafdhi yenye maelezo marefu katika lugha ya Kiarabu na Usuli-l-fiqhi.[463] Ufupisho wake ni kuwa, herufi hii inapokuja katika mfumo kama huu wa maneno huwa inaonesha sababu.[464] Na kwa hivyo, sababu ya Mtume (s.a.w.) kufanya aliyoyafanya ni kuwa yeye ni Mtume. Na bila shaka kuwa yeye ni Mtume tu bado haijamaanisha kuwa afanye hivyo, kwa hivyo ni wazi kwamba kafanya hivyo kutokana na Wahyi alioupata,[465] na kule kusema kwamba (kafanya hivyo) kwa sababu yeye ni Mtume ni kwa kuwa hakuna njia ya kupata Wahyi ila njia ya Utume, na ili ajue Umar na wenzake kwamba yeye analolifanya ni kwa amri ya Allah. Hii ndio maana inayoletwa na herufi hio katika maneno hayo ya Mtume (s.a.w.) aliposema: "**(إني رسول الله ولن يضيعني أبدا)** *Innii Rasulu L-llahi walan yudhiiani abadan.* (Kwani mimi ni Mtume wa Allah na hatonitupa milele)". Na kwa hivyo, kumlinganisha Ali na Mtume (s.a.w.) katika tukio hilo ni makosa kwani kule *Illa* (sababu) imetajwa nayo ni

462 - Al-Sabi'i ,*Al-Khawarij* uk. 104-105.

463 - Tumeielezea lafdhi hii kwa urefu katika sura ya tatu ya kitabu chetu *Mezani Ya Haki* chini ya anwani: *Ahlu Al-Bait Ni Nani: Je Wake Wa Mtume (S.A.W.) Ni Ahlu Al-Bait?* Rejea huko.

464 - Ndio maana nimeifasiri herufi hio hivi *"Kwani"* kwa sababu hapa imetumika herufu hio kumaanisha "Sababu" ya Mtume (s.a.w.) kafanya hivyo.

465 - Na kwa hivyo, tunamkuta mwanachuoni Al-Imamu Al-Salimi (r.a.) anasema: "Na Masahaba (r.a) walirejea (kwa Mtume (s.a.w.)) katika sulhu ya siku ya Hudaibiya, (ili abadilishe msimamo wake) mpaka akawaambia kwamba (alivyofanya yeye kunatokana na) Wahyi". Tazama Al-Imamu Al-Salimi, *Sharhu Tal'ati Al-Shams* j. 2, uk. 4. Al-Imamu Al-Salimi kayasema hayo pamoja na kuwa maneno "Kwamba (alivyofanya yeye kunatokana na) Wahyi" hayamo katika riwaya lakini bila shaka Imamu huyu katazama maana inayoletwa na herufi **(إني)** *Innii* iliomo katika riwaya hio.

Utume, jambo ambalo huku kwa Ali halipo na kwa hivyo hicho ni ***Al-Qiyaas ma'a Al-Fariq*** **(الْقِيَاسُ مَعَ الفَارِقِ)** (kulinganisha mambo yenye sababu tafauti).

Nukta nyengine ya kuzingatiwa – ambayo pia kaileta Sheikh Al-Sabi'i – ni kuwa:

> Uislamu katika zama za Mtume (s.a.w.): katika wakati wa sulhu hio ya Hudaibiya ulikuwa ndio unaanza, wakati katika zama za Ukhlifa wa Ali, ulikuwa umeshakamilika na kufikia ukomo. Na huenda yakasamehewa mwanzoni kwa ajili ya kuulea (Umma) mambo ambayo hayasamehewi mwishoni.[466]

Na hili pia linajenga tafauti baina ya matukio hayo mawili.

MUKHTASAR NA NUKTA MUHIMU

1) Tulichokisoma hapa ni suala la Ali kufuta jina lake la Uamiri (uongozi) katika mkataba wa kusimamisha vita uliofanyika huko *Siffin*.
2) Jambo hilo lilileta mzozo mkubwa baina ya wafuasi wa Ali, wakasisitiza baadhi yao, hasa hasa wale waliopinga sulhu tangu mwanzo, kwamba Ali asikubali kufuta jina la Uamiri na kwamba hata watu wakiuana basi asifanye hivyo na kwamba akikubali kulifuta jina hilo basi halitorejea kwake milele.
3) Waliojitenga na Ali na kuchagua Imamu wao mpya (ambao ndio Watu wa Nahrawaan na ambao ndio walioitwa *Khawarij)* waliona kwamba kitendo cha Ali kukubali kufuta jina lake la Ukhalifa au Uamiri basi kimemvua nafasi yake hio na kwamba hakuwa tena Amiri. Ukichanganya kitendo hicho na kitendo cha kukubali kwake kufanya sulhu kinyume na Aya ya Qur-ani – nao wamemchagua kwa sharti kwamba atekeleze Qur-ani na Sunna – na ukichanganya kwamba katika sulhu iliyofanyika huko Daumat Jandal – kama tutakavyoona baadae – Ali aliuzuliwa na muwakilishi wake, tunapata kwamba Ali hakuwa tena Khalifa

[466] - Al-Sabi'i *Al-Khawarij* uk. 103.

wa Waislamu hadi hapo atakapochaguliwa tena upya. Sasa wapi Umma ulimchagua tena Ali ili aliyejitenga naye aitwe asi *(baghi)* au aitwe *Khawarij* (mwenye kutoka) katika kumtii Imamu?

4) Watetezi wa Ali wanadai kwamba kwa kufuta jina la Uamiri, Ali hakukosea, na wanajenga hoja kwa kukilinganisha kitendo chake hicho na kitendo cha Mtume (s.a.w.) kufuta jina la Utume katika mkataba wa sulhu ya Hudaibiya iliyofanyika baina yake na makafiri wa Makka.
5) Waliopinga sulhu wanaona kwamba kitendo hicho ni mahususi kwa Mtume (s.a.w.). Na hili tunaweza kulipatia ushahidi kwa sababu ambayo yeye mwenyewe Mtume (s.a.w.) aliitoa katika kumjibu Umar kwamba: **"(إني رسول الله)** (Kwani mimi ni Mtume wa Allah)", yaani sababu ya mimi (Muhammad) kufanya hivyo ni Utume wangu kwa maana kwamba mimi ninapata Wahyi. Sasa je Ali naye alikuwa Mtume wa Allah au alikuwa akipata Wahyi ili *Qiyas* – baina ya kesi ya Mtume (s.a.w.) na kesi ya Ali – kiwe kimesalimika?

SURA YA TANO

SULHU YA "DUMAT AL-JANDAL" NA NATIJA YAKE

Tumeona kwamba Masahaba wanavyuoni wa Nahrawaan – ambao ndio chimboko la fikra ya kisiasa ya Kiibadhi – hawakukubaliana na mkataba wa kusimamisha vita. Na waliona kwamba hilo ni kinyume na Aya iliyompa Ali haki ya kupigana na Mu'awiya. Kama vile ambavyo hawakukubaliana na kitendo cha Ali cha kufuta jina lake la Uamiri.[467] Na kwa hivyo, wakajimegua na kuchagua Imamu mpya wa Waislamu na kujitenga na Ali. Tumeeleza huko nyuma kwamba mkataba wa kusimamisha vita ulioandikwa huko *Siffin* baina ya Ali na Mu'awiya, haukuwa ndio sulhu yenyewe, bali ulikuwa ni mkataba uliotoa masharti ya sulhu itayofanyika mwezi wa Ramadhani katika sehemu iitwayo Dumat Al-Jandal au Adhruh. Sasa Ali na waliopamoja naye wamekubali sulhu, na wakati wa sulhu umefika, je nini kiletendeka katika sulhu hio na nini natija yake?

Baada ya kufika wakati wa maahidiano, Ali akamtuma Abu Mussa Al-Ash'ari kwenda kukutana na Amru bin Al-'Aas kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya sulhu ya kudumu baina ya Ali na Mu'awiya. Siku zikapita ikawa hakuna kilichofanyika isipokuwa Abu Musa kukutana na Amru bin Al-'Aas na kuzungumza wao watu wawili tu hadi watu wa Ali wakawa na wasi wasi kwamba Abu Musa kamuuzulu Ali,[468] na pia Mu'awiya akawa na wasi wasi kwamba Amru bin Al-'Aas anataka

---

467 - Basi baada ya yote haya watu hawaoni kwamba wanadanganywa? Hawaoni kwamba watu hawa wakimtakia kheri Ali: wakitaka aendelee kuwa Khalifa wa kisharia na wao waendelee kumlinda kwa damu zao. Bado munadanganywa tu mukiambiwa kwamba hawa ni khawarij walimpinga Ali, ilhali wao ndio waliokuwa mstari wa mbele kumtetea! Lakini alipokubali kusitisha vita na kufanya mkataba wa amani na kukubali kufuta jina la Ukhalifa, basi vipi baada ya hayo watamlinda na kupigana kwa ajili yake na yeye ameshafuta jina la ukhalifa: si Khalifa tena! Mwenye akili na afahamu!

468 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 25.

kumpindua.[469] Mu'awiya bin Abi Sufyaan – kwa mujibu wa riwaya ya Ibn A'atham – akamtuma mtu aitwaye Al-Mughira bin Shu'uba, ambaye alikuweko Sham kwa ziara tu, aende kupeleleza ukweli wa mambo. Al-Mughira bin Shu'uba akaenda hadi Dumat Al-Jandal mahali walipokutana watu wawili hao, Abu Musa na Amru bin Al-'Aas. Alipofika hapo akaingia kwa Abu Musa na kumuuliza: "Unaonaje kuhusu wale ambao wamejitenga na jambo hili na wakachukia umwagaji wa damu wasiwe na Ali wala Mu'awiya?" Abu Musa akajibu: "Hao *Wallahi* ndio watu bora kuliko yule aliyeutwika mgongo wake na dhulma za waja".[470] Kisha akamuendea Amru bin Al-'Aas akamuuliza suali hilo hilo. Akamjibu: "Hao ndio viumbe waovu wa Mwenyezi Mungu; hawaijui haki wala hawaikatai batili".[471] Hapo Al-Mughira alirudi kwa Mu'awiya na kumwambia kwamba hakuna shaka Abu Musa atamuuzulu sahibu yake Ali; ama kuhusu Amru nimemsikia akisema maneno yanayoonesha kwamba jambo hili (la Ukhalifa) ajitakia yeye. Hio ni riwaya ya Ibn A'atham.[472] Ama Ibn Al-Athir, yeye hakutaja kwamba Al-Mughira bin Shu'uba alitumwa na Mu'awiya kwenda kupeleleza, bali – dhahir – ni kuwa Al-Mughira bin Shu'uba mwenyewe alitaka kujua tu je watu hao wataafikiana au *laa?* Na baada ya kusikiliza maoni ya pande mbili akasema: "Hawa hawakubaliani milele".[473]

Baada ya kuwa siku zimepita bila ya sulhu kufanyika watu wakaanza kuwapigia kelele Abu Musa na Amru bin Al-'Aas: "Mumelichelewesha jambo hili tunahofia muda kwisha nanyi hamujafanya kitu vita vikarejea kama vilivyokuwa".[474] Na ikawa Waislamu wa kila upande wamehudhuria hapo – upande wa Ali na upande wa Mu'awiya.[475] Hio ni riwaya moja; na riwaya ya pili ni kuwa watu wa upande wa Ali hawakuhudhuria,[476] na hili – kama ilivyoelezwa katika riwaya hio – ni

469 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 26.
470 - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 26.
471 - k.h.j., uk. 26-27.
472 - k.h.j, uk. 27.
473 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 682.
474 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 28.
475 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 528. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 14. Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 680-681. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 120.
476 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 8.

moja kati ya mambo yaliomfanya ‘Amru bin Al-’Aas amuhadae Abu Musa.

Lakini je kweli Amru bin Al-’Aas – muwakilishi wa Mu’awiya – alimfanyia ujanja Abu Musa – muwakilishi wa Ali – ambapo ‘Amru bin Al-’Aas alimrairai Abu Musa ili amuuzulu Ali na baada ya Abu Musa kufanya hivyo, Amru bin Al-’Aas akamtawalisha Mu’awiya? Au mahakimu wawili hao, Abu Musa na Amru bin Al-’Aas, walikubaliana kwamba wawauzulu wote Ali na Mu’awiya na kuliwacha jambo kuwa ni la kushauriana? Moja ya riwaya inaeleza kwamba Amru bin Al-’Aas alimuhadaa Abu Musa kwa kumrairai wala haikutaja riwaya hio makubaliano ya kuwauzulu wote.[477] Na riwaya nyengine zinaeleza kuwa ‘Amru bin Al-’Aas na Abu Musa waliamua kwa pamoja kuwauzulu wote wawili ili ushauriano[478] mpya uanze.[479] Lakini kwa hali yoyote ile, katika riwaya zote tunaona kwamba hadaa ilipita, kwani hata riwaya zenye kusema kwamba Amru bin Al-’Aas na Abu Musa walikubaliana kwa pamoja kuwauzulu wote wawili (ili pafanywe ushauriano), tunakuta kwamba riwaya hizo zinasema kwamba baada ya Abu Musa kutangaza kumuuzulu Ali na Mu’awiya, Amru bin Al-’Aas alimtangaza Mu’awiya kuwa ni Khalifa.[480] Hatimae ni kuwa riwaya zote zinaeleza kwamba hatima ya jambo hilo ni kutokuwepo kwa maafikiano yaliyofikiwa katika jaribio hilo la sulhu.

477 - Kama riwaya ya Al-Tabari katika *Al-Taarikh* j. 6, uk. 8. Labda iko riwaya nyengine ilio kama hio, lakini hio ndio nina kumbukumbu nayo.

478 - Kama riwaya ya Al-Tabari katika *Al-Taarikh* j. 6, uk. 16. Al-Mas’udi *Al-Muruj* j. 2, uk. 530. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 124. Na Ibn A’atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 28-31.

479 - Na hili linathibitisha kwamba ukhalifa unathibiti kwa Shura, vyenginevyo Masahaba wote waliohudhuria hapa wangesema tu kwamba Ali kachaguliwa na Allah kwahivyo hakuna haja ya kushauriana; na Ali mwenyewe angesema hivyo. Lakini hakuna hata mmoja aliyedai hivyo, kwa hivyo ilikuwa ni jambo lenye kueleweka kwa wote kwamba Khalifa huchaguliwa kwa mashauriano ya Waislamu.

480 - Al-Tabari katika *Al-Taarikh* j. 6, uk. 16. Al-Mas’udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 530. Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 125. Na Ibn A’atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 28-31.

ALI AKUSANYA JESHI UPYA ILI KUMPIGA MU'AWIYA; NA WATU WA NAHRAWAAN WAKATAA KUJIUNGA NA ALI

Baada ya kuwa sulhu haikufikiwa, hapo Al-Imamu Ali akaanza kukusanya jeshi lake tena kuelekea Sham ili kuanza upya vita na Mu'awiya.[481] Ali akatuma ujumbe kuwapelekeya wale Watu wa Nahrawaan, (ambao ndio walioitwa kuwa ni *Khawarij)* waliojitenga naye kwa sababu ya kukubali kwake sulhu na kufuta kwake jina la Ukhalifa, ili sasa wajiunge naye tena kwenda kumpiga Mu'awiya, lakini nao sasa wakakataa: wakamtaka yeye ajiunge na Imamu mpya waliyemchagua.[482] Na katika riwaya nyengine tunapata kwamba Watu wa Nahrawaan (r.a.) walimjibu Ali hivi: "Na imetufikia barua yako (ambayo) umetaja ndani yake kwamba mahakimu wawili (Abu Musa na Amru bin Al-'Aas) wamekitupilia mbali Kitabu cha Allah nyuma ya migongo yao na wakahukumu kinyume na alivyoteremsha Allah, na sisi tulilijua hilo, basi *Alhamdu Lillahi* (Sifa zote zilo njema ni za Allah) kwamba jambo lao tangu mwanzo lilikuwa kinyume na haki, nawe kwa kuwafanya wao wahukumu (basi) ni mwenye jarima kubwa zaidi kuliko wao".[483] Na riwaya nyengine inasema kwamba wao walimjibu Ali kwamba: "Ukijishuhudia kwa ukafiri na kuielekea toba, basi tutatazama baina yetu na wewe".[484] Ali – baada ya hapo – aliamua kuachana nao watu hao na kuelekea Sham[485] ili kwenda kupambana tena na Mu'awiya.[486] Alipofika

481 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 20. Al-Mas'udi, *Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 532-534.

482 - Hii ndio riwaya ya Kiibadhi kuhusu jawabu ya watu hao kwa Al-Imamu Ali, nayo ni jawabu ya Al-Imamu 'Abdullah bin Wahb Al-Rasibi (r.a.) kama ilivyo katika Al-Kashf cha Al-Qalhati. Ama riwaya za kumkafirisha Ali hazikuthibiti kamwe kwa Maibadhi na hata kama zilikuwepo basi maana yake ni kama tulivyozieleza humu.

483 - Al-Qalhati, *Al-Kashf* j. 2, uk. 241, naka kutoka katika kitabu *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba cha* Al-Sabi'i uk. 114.

484 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 20. Lakini hii pia ni riwaya ya Abu Mikhnaf ambaye ni dhaifu sana. Kwa hali yoyote ile ikiwa riwaya hii itasihi, basi itakuwa maana ya neno "Kufuru" ni ile iliyotajwa katika Aya kadha wa kadha na Hadithi kadha wa kadha ambazo limetajwa neno hilo ndani yake kumaanisha maasi tu: si kufuru kama ya Abu Jahl, Yahudi na Mkiristo, kama tutavyoelezea kwa urefu baadae.

485 - Kwa hivyo, natija ni kwamba hatima ya sulhu haikuwa ni jambo la maslahi kwa Al-Imamu Ali (k.w.) na vile vile haikuwa ni jambo la maslahi kwa Waislamu. Na kuanzia hapa inabainika – kwa kila mwenye kutumia bongo yake vizuri – kwamba wale ambao tangu mwanzo walipinga sulhu ndio waliokuwa katika msimamo sahihi.

njiani akapewa habari kwamba watu wa Nahrawaan wamemuua Sahaba aitwaye Abdillahi bin Khabbaab. Hapo baadhi ya watu waliokuwa katika jeshi la Ali wakashauri kuwa warudi kwenda kuwauwa Watu wa Nahrawaan kwanza kisha ndio waende kwa Mu'awiya. Ali akatuma mtu kwanza kwenda kufatilia na kuchunguza juu ya habari hio: je ni kweli watu hao wamemuua Sahaba Abdillahi bin Khabbaab? Riwaya inasema kwamba mtu huyo aliyetumwa kufanya uchunguzi naye pia wakamuua. Hapo Ali aligeuza jeshi lake na – badala ya kwenda Sham kupambana na Mu'awiya – akaelekea Nahrawaan kwenda kuwaua watu hao waliojitenga naye.[487] Lakini je ni kweli watu hao walimuua Abdillahi bin Khabbab au zilikuwa ni propaganda zilizofanywa na majasusi wa Mu'awiya waliokuweko huko Iraki ili kuudhoofisha upinzani dhidi yake?[488] Sura inayofuata inajadili suala hilo la kifo cha Abdillahi bin Khabbaab.

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

---

486 - Al-Mas'udi, *Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 534.

487 - Al-Mas'ud,i *Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 534. Hapa Ibn A'atham kisa chote kakipotoa kama kawaida yake. Yeye kaeleza kwamba baada ya Ali kufikiwa na habari ya kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbab alikuwa yuko nyumbani kwake Al-Kufa na akakusanya watu na kutoa khutuba kali ili watu waende kuwaua watu wa Nahrawaan lakini ikawa hakuna aliyemuitika. Akatoa khutuba ya pili kali mpaka akawaapiza watu wa Al-Kufa, ndio tena wakaanza kujikusanya kidogo kidogo kisha akatoa khutuba ya tatu wakamuitika watu kwa wingi. Nayo ni riwaya isiyo na kichwa wala miguu, kwani khutuba ya tatu ukiitazama utajua kwamba ni ya kutungwa kwani muna maneno ambayo mcha Mungu hayasemi. Kwa mfano Ali kasema: "*Wallahi* mukinitii mimi hamutopotoka na mukiniasi hamutoongoka". Tazama Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4 uk. 98-106. Bali mcha Mungu husema: "Nikienda sawa nifateni na nikenda kombo ninyoosheni" kama alivyosema Abu Bakr. Tazama Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 3, uk. 266-267. Ibn Abi Al-Hadid, *Sharhu Nahji Al-Balagha* j. 17, uk. 110. Pia khutuba hio ina mambo mengine yasiokubalika kiakili.

488 - Mu'awiya alikuwa na majasusi wake huko Iraki. Anasema Ibn Al-Athir: "Al-Ashtar akajiandaa kwenda Misri, na majasusi wa Mu'awiya wakamjia na (habari) hio". Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 704. Tazama pia Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 32. Halkadhalika katika zama za utawala mfupi wa Al-Hasan bin Ali, Mu'awiya alikuwa akituma majasusi wake waeneze propaganda za uwongo huko Iraki. Tazama Al-Ya'aqubi *Al-Taarikh* j. 2, uk. 214.

1) Tulichokizungumzia hapa ni suala la sulhu ya kudumu iliotarijiwa kufanywa huko Dumat Al-Jandal baina ya Ali (akiwakilishwa na Abu Musa) na Mu'awiya (akiwakilishwa na Amru bin Al-'Aas).
2) Tumeona kwamba maafikiano hayakupatikana juu ya sulhu hio.
3) Hatima ya sulhu hio ilikuwa ni Ali kuuzuliwa kutoka katika nafasi yake ya Ukhalifa.
4) Hukumu hio Ali hakuikubali kwa kuwa ni kinyume na Qur-ani. Lakini sababu hii ilitakiwa aitumie tangu mwanzo kwani masharti katika mkataba wa mwanzo yalikuwa pia ni kinyume na Qur-ani.
5) Pamoja na hayo, riwaya zinagongana juu ya kwamba je Amru bin Al-'Aas alimuhadaa Abu Musa kwa kumrairai ili amuuzulu Ali au alimuhadaa kwa kukubaliana naye kuwa wawauzulu wote wawili kisha yeye akafanya khiyana?
6) Ukizitazama riwaya zote mbili hata zinazotolewa ushahidi wa kuwa watu wawili hao walikubaliana juu ya kuwauzulu Ali na Mu'awiya, (ili kuliwacha jambo kuwa ni la Shura) basi bado unaona kwamba hadaa ilipita.
7) Kwa hivyo, mukhtasari wa sehemu hii ni kuwa sulhu baina ya Ali na Mu'awiya haikuwa na maslahi kwa Ali wala kwa Umma wa Kiislamu, na hapa unadhihiri uoni wa mbali wa Watu wa Nahrawaan au hao walioitwa kuwa ni Khawarij.
8) Baada ya kufeli kwa sulhu hio, Ali aliandaa jeshi upya kwenda kumpiga Mu'awiya; na hapo Ali aliwaandikia barua Watu wa Nahrawaan ili wajiunge pamoja naye, lakini nao sasa wakakataa – kwa mujibu wa baadhi ya riwaya – ila kwa masharti maalumu ambayo Ali naye hakuyakubali.
9) Riwaya iliothibiti kwa Maibadhi ni kuwa watu hao walikataa kabisa kurudi kwa Ali wala hawakuwa na sharti yoyote ile ambayo kukubalika kwake kungeliwafanya wao warudi tena kwa Ali; bali walimtaka yeye ajiunge na Imamu mpya waliyemchagua.
10) Ali akatoka na alipofika njiani akapata habari kwamba watu hao (wa Nahrawaan) wamemuua Ibn Khabbaab, na baada ya kutuma mpelelezi wake naye pia akauliwa. Hapo Ali – akishauriwa na wanajeshi wake hasa hasa Al-Ash'ath bin Qais, jasusi wa Mu'wiya katika jeshi la Ali – aliamua kugeuza jeshi na

kuwaendea Watu wa Nahrawaan badala ya kumuendea Mu'awiya.

11) Lakini je kweli Watu wa Nahrawaan walimuua Abdullah bin Khabbaab? Soma sura inayofuata kupata jawabu hio.

SURA YA SITA

KUULIWA KWA ABDULLAHI BIN KHABBAB NA KUANZA KWA VITA VYA NAHRAWAAN

Wote wanaohalalisha kitendo cha Ali cha kuwaua Watu wa Nahrawaan,[489] wanatoa sababu kwamba watu hao si kwamba walijitenga na Ali tu, bali pia walimuua Abdillahi bin Khabbaab. Na inayofuata ni riwaya yenyewe kwa ufupi:

RIWAYA YA KUULIWA KWA SAHABA ABDU-LLAHI BIN KHABBAAB

Riwaya hio inasema:[490]

> **Kikundi (*cha Makhawarij*) kilichotoka Basra** kilikuja mpaka kikakaribia walikokuweko wenzao kwenye mto (wa Nahrawaan, hapo)….wakamkuta mtu anamuendesha mwanamke juu ya punda….wakamuuliza wewe ni nani? Akasema: 'Mimi ni Abdullah bin Khabbab, Sahaba wa Mtume (s.a.w.)……..wakamwambia tusimulie ulichokisikia kutoka kwa Mtume (s.a.w.)…akawasimulia kwamba Mtume (s.a.w.) kasema (kwamba) kutakuwa na fitna mtu ataamka hali ya kuwa ni muumini; akifika jioni ni kafiri; jioni atakuwa muumini asubuhi ni kafirii…wakamwambia unasemaje….kuhusu Ali kabla ya kukubali hukumu na baada ya kukubali hukumu. Akasema yeye anamjua zaidi Allah kuliko nyinyi[491] na ni mwenye kuilinda zaidi dini yake kuliko nyinyi….wakamwambia wewe unawapenda watu kwa sababu ya majina yao: si kwa vitendo vyao….wakamchukua wakamfunga wakaenda naye chini ya mtende uliozaa sana, ikaanguka

---

489 - Vita vya Nahrawaan vilipiganwa mwaka 38 A.H. Tazama Al-Mas'udi, *Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 498.

490 - Kumbuka kwamba mimi nafanya mukhtasari tu wa riwaya hizi kwani ni refu, kwa hivyo kwa kufupisha maudhui nazikata vipande tunavyovihitaji tu.

491 - Tazama riwaya za kutunga zilivyo: kana kwamba suala ni: "Je nani mcha Mungu baina yetu na Ali?" Basi elewa ndugu msomaji kwamba tatizo si nani mjuzi au mcha Mungu, tatizo ni nani yuko sawa na nani kakosea kwa mujibu wa Qur-ani. Hata akiwa aliyeko sawa ni Myahudi basi ni lazima apewe haki yake katika hukumu.

tende, mmoja wao akaichukua akaitia mdomoni, mmoja wao (akamgomba na kumwambia unakula tende ya watu) bila ya uhalali na bila (ya kulipa) thamani (kwa mwenyewe)….kisha akapita nguruwe wa watu wa dhimma,[492] mmoja wao akamuua (yule nguruwe)....wenzake wakamwambia huu (unaofanya wewe) ni ufisadi katika ardhi. Akamuendea mwenye nguruwe akamridhisha kwa sababu ya kumuua nguruwe wake. Abdullah bin Khabbab alipoona hivyo, akawambia ikiwa nyinyi ni wakweli katika hayo ninayokuoneni, basi sitopata tabu kwenu: mimi ni Muislamu sijazua kitu katika Uislamu….basi wakamlaza na kumchinja…..kisha wakamuendea mwanamke[493]…wakampasua tumbo lake na wakawaua wanawake watatu wa (kabila la) Tayyi na wakamuua Ummu Sinan….Habari zilipomfika Ali akamtuma Al-Harith bin Murra Al-'Abdi[494] ili akatazame ukweli wa habari zilizomfikia.....(Naye pia) wakamuua..…..Habari (ya kuuliwa kwake) ilipomfikia Ali, ndio wakaamua kuwaendea Watu wa Nahrawaan kwanza na kuwaua kabla ya kumuendea Mu'awiya na jeshi lake.[495]

UCHAMBUZI WA *MATN* YA RIWAYA HIO

Maudhui ya riwaya hii ni miongoni mwa mambo muhimu ambayo kwayo Watu wa Nahrawaan wametiwa ila. Na ila yenyewe – kama unavyoona – ni kitendo cha kumuua Abdullahi bin Khabbab na mke wake na watu wengine waliokuwepo hapo. Nayo bila shaka ni ila kubwa ikiwa itathibiti. Lakini je tukio hilo lina ukweli katika kuhusishwa kwake na Watu wa Nahrawaan au ni katika jaribio la kisiasa la kuwapaka matope watu hao kwa sababu ya msimamo wao na ili kitendo cha Ali

---

492 - Mtu wa dhimma au dhimmiy ni Mkiristo au Myahudi aliyechini ya dola ya Kiislamu ambaye ameahidiana na Waislamu kutokuwapiga vita katika dini yao, naye akawa analipa jiz-ya, na kwa hivyo akapata himaya ya Waislamu na kuwa chini ya dhimma yao.

493 - Katika riwaya nyengine "Mwanamke aliyekuwa na mimba".

494 - Lakini Al-Baladhiri kaidhoofisha riwaya hii, kwani Al-Harith bin Murra Al-'Abdi aliuliwa huko Qiyqan mwaka 42 A.H. Bali – kwa mujibu wa Al-Baladhiri – aliyetumwa ni Al-Harith mwengine ambaye ni katika wafusi wa Ali. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 143.

'495 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 23. Al-Mas'udi, *Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 534. Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 690-692. Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 606-607. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 141.

cha kuwaua iwe ni halali? Nukta (points) zinazofuata zinamfanya mpekuzi mwenye kutumia akili yake vizuri au msomaji muadilifu ahoji usahihi wa habari hio:

1) Kikundi kilichomuua Abdullahi bin Khabbab kwa mujibu wa riwaya hii si wale waliojitenga na Ali baada ya kukubali sulhu na kuelekea Al-Harauraa na baadae kuelekea Nahrawaan, bali ni kikundi kilichotoka Basra ambacho kiliafiki rai ya kutokuwepo sulhu,[496] kama riwaya inavyosema: "Kikundi (cha *Makhawarij*) kilichotoka Basra…". Na kwa hivyo, hata ikiwa tukio hilo ni kweli lilitokea bado kuna kujiuliza kuhusu usahihi wa kuhusishwa kwake na Watu wa Nahrawaan. Kwa lugha nyengine, ni kuwa hata ikiwa kweli kuna watu waliomuua Abdullahi bin Khabbab, basi hawakuwa wale Watu wa Nahrawaan walioitwa kuwa ni *Khawarij* kwani Watu wa Nahrawaan wao kwanza walikusanyika Al-Harauraa na baadae wakakusanyika Al-Nahrawaan, wakati hiki ni kikundi kilichotoka Basra kikiongozwa na Mis'ar bin Fadaki. Kwa hivyo, wauwaji si *Ahlu Nahrawaan* (Watu wa Nahrawaan). Na hii ndio sababu ya Ibn Abbaas kumtuma Abu Al-As-wad Al-Diili[497] kwenda kupambana na kikundi hiki kilichotoka Basra kama inavyoeleza riwaya ya Al-Tabari,[498] wakati katika vita vya Nahrawaan Ibn Abbaas alikataa kushiriki katika vita hivyo dhidi ya watu hao wa Nahrawaan, ikimaanisha kwamba Watu wa Nahrawaan na kikundi hiki kilichomuua Abdullahi bin Khabbab kutoka Basra kikiongozwa na Mis'ar bin Fadaki, ni vikundi viwili tafauti, vilivyokuwa na siasa tafauti. Na hii ndio dhahir ya maana inayooneshwa na riwaya ya

496 - Na hili ni tatizo la waandishi wengi wa historia tangu zamani hadi leo, ikitokea kuwa vikundi fulani vimekubaliana katika kitu kimoja, basi kimoja huhusishwa na chengine japo kuwa kuna mambo kadha wa kadha wanatafautiana. Kukubaliana kwa kikundi kilichotoka Basra na Watu wa Nahrawaan katika kupinga sulhu haina maana kuwa ni wamoja, kwani wametafautiana katika misimamo mengine. Tazama ukweli kwamba kikundi hiki kilichotoka Basra kiongozi wao, Mis-ar bin Fadaki, alipewa amani na Ali, je Ali naye kawa *khawarij* kwa kukubaliana naye katika hilo. Halkadhalika vikundi vyengine vilivyoitwa kuwa ni *Khawarij* vina fikra na itikadi tafauti kabisa na watu wa Nahrawaan, isipokuwa kukubaliana kwao katika kuipinga sulhu tu.

497 - Pia huitwa "Al-Duali".

498 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 20.

Al-Baladhiri, kwamba kikundi cha Basra kilifanya mauaji hayo kabla kufika Nahrawaan,[499] bali Al-Baladhiri kasema kwa uwazi:

> Na walikuwa *Khawarij* ambao walitoka Basra pamoja na Mis'ar bin Fadaki wakihatarisha (maisha ya) watu njiani, kutahamaki wako mbele ya mtu anamuendesha mke wake juu ya punda wake..wakamwambia: 'Wewe ni nani?' …Akasema: Abdullah bin Khabbaab….[500]

2) Kikundi hicho kilimuua Abdullahi bin Khabbab – kwa mujibu wa riwaya hii – njiani kabla ya kufika Nahrawaan walikokuwa wanakwenda ili kujiunga na Watu hao walioitwa kuwa ni *Khawarij*. Na hili linaipa nguvu nukta (point) ya kwanza tuliyotangulia kuieleza.[501]

3) Baada ya kikundi hicho kufika huko Nahrawaan ambako ndiko walikokuweko watu hao waliyojitenga na Ali, tunapata mgongano wa riwaya: je Watu wa Nahrawaan walikubali kuwapokea watu wa kikundi hicho[502] au hawakukubali.[503] Hapa riwaya zinagongana.[504] Lakini pamoja na hayo riwaya zenye kusema kwamba Watu wa Nahrawaan hawakukubaliana na kikundi hicho ndio riwaya sahihi, kwani Mis'ar bin Fadaki,

---

499 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 136.

500 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 142.

501 - Dhahir utaona kuwa sehemu hii na ya kwanza ni sawa sawa lakini ukizichunguza utaona iko tafauti ya maelezo. *Nukta* (point) ya kwanza inakusudiwa kwayo kubainisha kwamba wale waliomuua Ibn Khabbaab wenyewe ni tafauti na Watu wa Nahrawaan. Ama *nukta* (point) ya pili inakusudiwa kwayo kubainisha kwamba kile kitendo chenyewe cha mauaji kilifanyika kabla hata ya wauaji kufika Nahrawaan, jambo ambalo linaonesha kuwa si kwamba Watu wa Naharawaan hawakushiriki katika kitendo hicho tu, bali hata walikuwa hawana taarifa nacho kamwe hadi baada ya kutokea kwake.

502 - Kama inavyoonesha riwaya ya Al-Tabari katika, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 24 na Ibn Abi Shaiba *Al-Musannaf* j. 8, uk. 732, riwaya na. 13, na wengine kwamba Watu hao wa Nahrawaan walimwambia Ali: "Sisi sote ni wenye kuwaua". Lakini tumeshabainisha uhakika wa riwaya hii.

503 - Kama inavyosema riwaya ya Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 50.

504 - Lakini hata kama ni kweli kwamba Watu wa Nahrawaan walikipokea kikundi hicho kilichotoka Basra, basi hili litakuwa sawa na Ali kuwapokea na kuwakumbatia waliomuua 'Uthman kwa wale wanaoona kuwa 'Uthman kauliwa kwa dhulma.

kiongozi wa kikundi hicho, baadae alijiunga na Abu Ayyub Al-Ansari katika vita vya Nahrawaan ili kuwapiga watu hao. Ni wazi kwamba lau Watu wa Nahrawaan walimkubali Mis'ar na kuwa pamoja naye, basi asingelikuwa dhidi yao.

4) Watu hawa walikerwa sana na mmoja wao kumuua nguruwe na mwengine kula kokwa ya tende ya watu kwani kufanya hivyo ni kufanya ufisadi katika ardhi, lakini walimlaza mtu wakamchinja kama kuku! Na hiki ni kitu ambacho hakuna anayekikubali ila anayefuata matamanio ya nafsi yake. Ni wazi kuwa huu ni utunzi utokanao na wapambe wa Ali au wa Muwiya au Mayahudi – kama tutakavyoona – ili kuwapaka matope watu hao waliosifika kwa elimu na ucha Mungu.

5) Ali alimtuma Al-Harith bin Murra Al-'Abdi ili kwenda kuhakikisha habari hio. Hii ina maana kwamba Ali alikuwa hana hakika kwamba je yaliyosemwa ya kuwa watu hao walimuua Abdillahi bin Khabbab ni kweli au si kweli, ndio maana akamtuma Al-Harith bin Murra Al-'Abdi kwenda kuhakikisha. Riwaya inasema kwamba Al-Harith bin Murra Al-'Abdi naye pia akauliwa. Lakini pamoja na hayo Ali aligeuza jeshi lake kutoka upande wa Sham alikokuwa Mu'awiya na badala yake kuwaelekea Watu wa Nahrawaan. Sheikh Nassir Al-Sabi'i anauliza:

> Ikiwa mpelelezi aliyemtuma Ali pia kauliwa, ni nani aliyemuhakikishia Ali kwamba Watu wa Nahrawaan wamemuua Abdullah bin Khabbab baada ya hapo?[505]

Ninasema: hatimae tunamkuta Al-Mas'udi akitwambia kwamba aliyefikisha habari hizo: "Ni Myahudi wa Al-Sawaad".[506] Myahudi atoa habari; Al-Ash'ath bin Qais – jasusi[507] wa Mu'awiya – ahimiza

505 - Al-Sabi'i ,*Al-Khawaarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. uk. 309.

506 - Al-Mas'udi, *Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 534

507 - Anasema Al-Baladhiri kwamba baada ya Al-Imamu Ali kumuuzulu Al-Ash'ath bin Qais katika Uliwali (Ugavana) wake wa mji wa Adhrabaijan, Al-Ash'ath alighadhibika na akaandikiana na Mu'awiya. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 80. Ni wazi kwamba mtu aliye katika jeshi la Ali akiandikiana na Mu'awiya atakuwa ni mtu wa Mu'awiya,

kuwaendea Watu wa Nahrawaan akijua kwamba ikiwa Ali atawaua watu hao, basi hatokuwa tena na nguvu ya kupambana na Mu'awiya! Na hivyo ndivyo ilivyokuwa – ndoto za Al-Ash'ath bin Qais zathibiti katika ulimwengu wa hakika!

MAELEZO ZAIDI KUHUSU *MATN* YA RIWAYA HII

Katika riwaya hii na nyengine[508] tunapata kwamba Abdullah bin Khabbab alijadiliana na Mis'ar bin Fadaki Al-Tamimi kuhusu Al-Imamu Ali, Mis'ar bin Fadaki akamuua Abdullah bin Khabbab. Habari za kifo cha bwana huyo zilipomfika Al-Imamu Ali, Al-Ash'ath bin Qais na wengine wakashikilia kuwa kwanza twende tukawapige hawa Watu wa Nahrawaan halafu ndio tumuendee Mu'awiya. Na hapa kuna mambo ya kustaajabisha:

Mosi: ni kuwa hata kabla ya kutokea mauaji ya Sahaba Abdillahi bin Khabbaab, tayari baadhi ya watu waliokuwemo katika jeshi la Ali walishauru kwamba kwanza wakawauwe Watu wa Nahrawaan kisha ndio wamuendee Mu'awiya na wafuasi wake. Inasema riwaya ya Al-Tabari:

---

hususan ukichukua mambo mengine mengi aliyoyafanya Al-Ash'ath kama vile kusisitiza kusimamisha vita huko Siffin au atajimegua yeye na kundi lake lote la watu wa Al-Yaman na kabila lake la Al-Kindi na kukataa kuingia katika vita dhidi ya Mu'awiya baada ya kumalizika vita vya Nahrawaan na kushirikiana na Ibn Muljam katika kumuua Al-Imamu Ali. Anasimulia Al-Baladhiri baada ya vita vya Nahrawaan kwamba: "Mu'awiya aliandikiana na viongozi waliokuwa pamoja naye (pamoja na Ali) kama Al-Ash'ath bin Qais na wengine na akawaahidi na kuwapa matumaini na kuwapa (labda pesa au ahadi) hadi akawafanya wamili upande wake na kuwafanya wafanye uzito kutoka pamoja na Ali (ili kwenda kumpiga yeye); akawa (Ali) anasema wala hakuna anayeigeukia kauli yake na analingania wala hakuna anayeusikiliza ulinganio wake". Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 156. Na hata katika vita vya Siffin, Ali alimuuzulu Al-Ash'ath katika nafasi ya uongozi kwa sababu ya habari iliyomfikia kuhusu yeye. Tazama Ibn A'atham j. 3, uk. 105.

508 - Al-Baladhiri *Ansabu Al-Ashraf* j. 3, uk. 142. Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 98, lakini yeye hakutaja kwamba mjadala ulikuwa juu ya Uimamu wa Ali.

> Na ikamfikia Ali kwamba watu wanasema: 'Lau (Ali) engetupeleka kwa hawa Harauriyya (Watu wa Nahrawaan) tukawamaliza wao kwanza kisha ndio akatupeleka kwa wavunjaji ahadi.[509]

Ali aliposikia hivyo, akawahutubia watu, akasema:

> ..Wacheni kuwataja (hao Watu wa Nahrawaan); na nendeni kwa watu wanaopigana na nyinyi ili wapate kuwa wafalme majabari na wawafanye waja wa Allah kuwa ni watumwa.[510]

Suali ni kuwa: kwanini wakawaue watu hao nao hapa ilikuwa – kwa mujibu wa riwaya hizi – hawajamuua mtu? Ni wazi kwamba baada ya majasusi wa Mu'awiya kuona kwamba ushauri huo Ali kaukataa, ndio wakazua suala la kuwa Ahlu Al-Nahrawaan wamemuua Ibn Khabbaab. Lengo lilikuwa ni kuwamaliza watu hao ambao ndio waliokuwa tishio kwa Mu'awiya, na ili kuhakikisha kwamba 'Ali kadhoofika.

Pili: ni kuwa kama kweli Ali alipigana na watu hao ili kulipiza kisasi cha kuuliwa kwa Ibn Khabbaab, mbona yule muuaji hasa, naye Mis'ar Fadaki, alimpa hifadhi: hakumuua?

Tatu: ni kuwa, wakati hapa tunajifunza kwamba sababu ya Ali kwenda kuwapiga watu hao ni kitendo chao cha kumuua au cha kumkumbatia aliyemuua Abdillahi bin Khabbab, tunaona kwamba riwaya nyengine kadha wa kadha zinasema kwamba Ali na waliokuwa pamoja naye walipofika huko walikokuweko watu hao wa Nahrawaan, walikuwa wakiwalingania kuwa watu hao warudi kuwa pamoja nao ili waende kumpiga Mu'awiya! Na hii ina maana kwamba tafauti baina ya Ali na wao haikuwa katika tukio la kuuliwa kwa Ibn Khabbab, bali ni katika kumuacha mkono Ali na kuchagua Imamu mwengine.

---

509 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 22. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 690.

510 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 22. Ni wazi kwamba Ali alikuwa akiona kuwa Watu wa Nahrawaan (r.a.) ni bora zaidi kuliko Mu'awiya na wafuasi wake. Na hii ni kinyume na wafuasi wa Mu'awiya wanavyotaka kuupindua ukweli kwamba watu hao ni Makhawaarij waliotoka katika dini na kwamba Mu'awiya ni mtu mwema mujtahid aliyekosea tu!

Kwa hivyo, ni wazi – kwa mujibu wa riwaya hizo – kwamba Ali alipofika huko hakulitaja kamwe suala la mauaji ya Abdullahi bin Khabbab, na hii ina maana kwamba kuanzisha uongozi mpya ilikuwa ndio mzozo wa Ali na watu hao. Na hili linapata nguvu kwa riwaya ya Al-Bayhaqi kwamba mtu mmoja aliwaita Watu wa Nahrawaan kuwa ni washirikina (makafiri). Ali akamwambia: "Kutoka katika ushirikina (ukafiri) wameshakimbia". Yaani musiwaite makafiri. Akamuuliza: "Je ni wanafiki?" Ali akamjibu: "Wanafiki hawamtaji Allah isipokuwa kidogo". Akauliza: "Sasa ni nani?" Ali akajibu: "Ni watu wametuasi, tukapewa ushindi juu yao".[511] Ni wazi – kwa mujibu wa riwaya hii – kwamba vita vya Ali na Watu wa Nahrawaan msingi wake haukuwa kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbaab, bali ilikuwa ni tafauti zao za kisiasa kwa sababu ya kujitenga kwao na yeye (Ali) na kitendo chao cha kuchagua Imamu wao, ndio maana Ali akasema kuhusu watu hao kwamba: "Ni watu wametuasi, tukapewa ushindi juu yao". Na hili pia ndilo lenye kuelezea kwanini Ibn Abbaas hakukubali kushiriki katika vita hivyo dhidi ya watu hao, na akaviita kuwa ni vita vya kupigania utawala, kwa sababu kama kweli watu hao walimwaga damu za Waislamu bila ya haki, basi Ibn Abbaas asingelikataa kuwa pamoja na Ali katika vita vyake dhidi ya watu hao, na badala yake Ibn Abbaas huyo huyo atume jeshi kwenda kupigana na kikundi kilichotoka Basra kwa sababu ya kufanya mauaji haramu.[512] Pia ukiyatazama yale yaliyoelezwa na Al-Baladhiri, utaona ukweli huu niliokueleza hapa kwa uwazi. Na hii ni kuwa riwaya ya Al-Baladhiri inaeleza kwamba baada ya Ali kufika huko Nahrawaan alinyanyua bendera ya amani yaani atakayekubali kurudi kwake basi yuko katika amani. Miongoni mwa waliorudi kwake – kwa mujibu wa riwaya hio – ni Mis'ar bin Fadaki na kikundi cha watu elfu moja. Sasa utakumbuka kwamba – kwa mujibu wa riwaya tuliyoinukuu kabla – Abdullah bin Khabbaab kauliwa na Mis'ar bin Fadaki na kikundi chake kilichotoka Basra. Sasa kama ni hivyo, na Ali ameshampa amani muuwaji Mis'ar bin Fadaki, kwanini tena awapige waliobaki ilhali mwenye kuuwa ameshampa amani? Ni wazi kwamba tafauti baina ya Ali na Watu wa Nahrawaan ni katika suala la uongozi. Na kwa hivyo, ndio maana Ibn Abbaas alipokataa kushiriki katika vita hivyo alimwambia Ali yale tuliyoyanukuu kabla:

511 - Al-Bayhaqi, *Al-Sunan* j. 12, uk. 334, riwaya na. 17189.

512 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 20.

> Wallahi ni bora nikutane na Allah pamoja na yaliyo katika tumbo la ardhi miongoni mwa dhahabu zake na fedha zake pamoja na vilivyojaa mgongoni kwake[513] kuliko kukutana naye na mimi nimemwaga damu ya Umma huu ili nipate ufalme au uamiri (uongozi).[514]

Bali hata riwaya zenye kusema kwamba Ali alikwenda huko walikokuweko watu hao ili kuwataka wamtoe aliyemuua Abdilahi bin Khabbaab, basi ikiwa utazitazama kwa jicho la upekuzi na akili yenye kufikiri, utaona kwamba kuna kitu mgongano. Kwa mfano, ukisoma maelezo ya Ibn A'atham katika kitabu chake *Al-Futuh*, na Al-Mas'udi katika *Muruju Al-Dhahab* utaona kwamba Ali alipofika huko alijadiliana na watu hao juu ya kwanini wamejitenga naye. Na waliokubali kurudi kwake – kama tulivyosema kabla – aliwapa amani. Anasema Ibn A'atham: "Akawapa amani miongoni mwao watu elfu nane, na wakabakia katika kumpiga vita watu elfu nne".[515] Na anasema Al-Mas'udi kuhusu mjadala wa Ali na Watu wa Nahrawaan: "Akawalingania warejee (kwake) na watubie".[516] Sasa jiulize wewe, je:

1) Kosa lao lilikuwa ni kumuua Abdillahi bin Khabbaab? Kama ndio, vipi awape amani watakaorejea kwake na awaue watakaobaki? Je kule kurejea kwao katika utawala wake ndiko kuliko halalisha damu ya Ibn Khabbaab?
2) Au kosa lao lilikuwa ni kujitenga na Ali na kujichagulia Imamu mpya, na kwa hivyo atayerejea katika utawala wake hatokuwa na hatia tena? Kama ni hivyo, basi natujiulize je hili suala la kuuliwa kwa Ibn Khabbaab na kuhusishwa kwake na Watu wa Nahrawaan limetokea wapi? Ni wazi kwamba riwaya hizi zina mgongano. Na bila shaka jambo ambalo lina ukweli ni kuwa Abdillahi bin Khabbab aliuliwa, lakini nani aliyemuua, hili ni jambo ambalo watafiti wanahitajika kuingia kazini zaidi.

---

513 - Mgongoni mwa ardhi.

514 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 2, uk. 398. Ibn Abd Rabbi, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 326. Na mfano wake imo katika *Al-Futuh* j. 4, uk. 75, cha Ibn A'atham.

515 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 2, uk. 125.

516 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 535.

Lakini, kwa hali yoyote ile, tukijaalia kuwa riwaya zenye kusema kwamba Ali alijadiliana na watu hao kuhusu waliomuua Abdillahi bin Khabbab, ni riwaya sahihi, suali muhimu la kujiuliza hapa ni lile lile tulilotangulia kujiuliza kabla: nalo ni kuwa je Watu wa Nahrawaan – kwa mujibu wa riwaya hizo – walikubaliana na kitendo hicho cha Mis'ar bin Fadaki na kikundi chake kilichotoka Basra cha kumuua Abdullah bin Khabbab au hawakukubaliana nacho? Hapa riwaya zinagongana. Moja ya riwaya[517] hizo inasema kwamba Ali alipofika huko kwa Watu wa Nahrawaan na kuwataka wamtoe aliyemuua Abdullah bin Khabbab walisema: "Sote sisi ni wenye kuwaua na sote sisi tunaihalalisha damu yao na damu yenu".[518] Wakati kuna riwaya hio, tunakuta riwaya nyengine inasema kwamba Watu wa Nahrawaan walikipinga kitedo hicho cha Mis'ar bin Fadaki – kiongozi wa kikundi kilichotoka Basra – cha kumuua Abdullah bin Khabbab, na kwa hivyo wakamfukuza kuwa pamoja nao.[519]

RIWAYA YA PILI

Hio iliyotangulia ni riwaya moja na uchambuzi wa *matn* yake. Riwaya nyengine kaisimulia tena Al-Tabari. Riwaya hio inasema:

> *Al-Khawarij* waliingia katika kijiji, akatoka Abdullahi bin Khabbab, Sahaba wa Mtume (s.a.w.) hali ya kuwa ni mwenye kufadhaika. Wakamwambia: 'Mbona umefadhaika?' Akasema: 'Wallahi mumenifadhaisha'. Wakasema: 'Wewe ni Abdullahi bin Khabbab, Sahaba wa Mtume (s.a.w.)?' Akasema: 'Ndio'.[520]

Halafu, baada ya hapo, wakamuuliza kuhusu Hadithi aliyoisikia kutoka kwa baba yake kutoka kwa Mtume (s.a.w.) akitaja (mambo ya) fitna (itayotokea kwamba itapotokea fitna hio basi): "Aliyekaa kitako katika (fitna) hio ni bora kuliko aliyesimama; na aliyesimama ni bora kuliko

517 - Yaani maelezo haya ni kujaalia tu kuwa riwaya hizo ni sahihi.

518 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 24. Ibn Abi Shaiba *Al-Musannaf* j. 8, uk. 732, riwaya na. 13, *Kitabu Al-Jamal wa Al-ssiffin wa Al-Khawarij; Babu Maa dhukira fii Al-Khawarij.* Huyu mtunzi wa riwaya hizi alikuwa hata hajui kutunga riwaya!

519 - Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 50.

520 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk.22-23.

anayekwenda…".[521] Kisha wakamchukua "Pembeni kwa mto wakamkata shingo yake…na wakalipasua tumbo la mke wake".[522]

MATN YA RIWAYA HII

Riwaya hii bila shaka ina tafauti ndogo na riwaya ya kwanza! Katika riwaya hii, tunapata kwamba Abdullahi bin Khabbab kauliwa bila ya kosa: kosa lake ni kuulizwa kuhusu Hadithi ya Mtume (s.a.w.) alioisikia kutoka kwa baba yake, naye akaisimulia kwamba Mtume (s.a.w.) kasema kwamba kuna fitna (itayotokea na kwamba itapotokea fitna hio basi): "Aliyekaa kitako katika (fitna) hio ni bora kuliko aliyesimama; na aliyesimama ni bora kuliko anayekwenda…". Katika Hadithi iliotangulia sababu ya kuuliwa Abdullahi bin Khabbab ni kitendo chake cha kumkubali Ali (na Uthman), na kwa hivyo wakamwambia: "Wewe unawapenda watu kwa sababu ya majina yao: si kwa vitendo vyao". Lakini baina ya kuwepo sababu hii na ile bado kuna kujiuliza kwamba Abdullahi bin Khabbab kauliwa kwa sababu hizo au kwa moja ya hizo, je mke wake kauliwa kwa sababu gani? Katika riwaya hii – na iliotangulia – hatuoni sababu yoyote ya kuuliwa mke wake.[523] Namna hivi riwaya zinatongoa – nguruwe ahurumiwa; mwenye kokwa ya tende alipwa; binaadamu auliwa na kupasuliwa tumbo! Asanteni wafuasi wa Mu'awiya, tupeni uhondo!

RIWAYA YA TATU

Riwaya ya tatu inasema:

> Ali aliwakataza watu wake wasiwapige *Khawarij* hadi hapo watapozua jambo. Wakapita kwa Abdillahi bin Khabbab wakamchukua. Mmoja wao akapita (sehemu) kuna kokwa ya tende imeanguka kutoka katika

521 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 23. Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 97.
522 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 23.
523 - Labda kwa sababu alikuwa anampikia Abdullah bin Khabbaab!!!

mtende akaichukua akaitia mdomoni mwake, mwenzake akasema: 'Hii ni tende ya *Mu'ahid* kwanini umeihalalisha (kuila)', basi akaitema kutoka katika kinywa chake. Kisha wakapita kwenye nguruwe, mmoja wao akampiga upanga wake, mwenzake akasema: 'Huyu ni nguruwe wa *Muahid* kwanini umehalalisha (kumuua)'. Abdullah bin Khabbab akawaambia je munataka nikuonesheni chenye utukufu zaidi ya haya? Wakasema: 'Ndio'. Akasema: 'Mimi'. Wakamtanguliza, wakampiga shingo yake (kwa upanga) . (Ali) akawatumia ujumbe kwamba tupeni aliyemuua Abdillahi bin Khabbab ili tumuue. Wakamtumia ujumbe: vipi tukupeni kisasi cha Abdillahi bin Khabbab na sisi sote ni wenye kumuua[524]….Basi (Ali) akawaamuru watu wake wawatie mikononi..basi wakawaua. (Ali) akasema: 'Mtafuteni *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu)', akaletewa. (Ali) akasema: 'nani anayemjua huyu'. Hakuna aliyemjua isipokuwa mtu mmoja, akasema nilimuona (huyu huko) Al-Hayawa…… (Ali) akasema: 'Kasema kweli! Huyu *(Dhu Al-Thudaiyya* Mwenye kichuchu), ni miongoni mwa majini'![525]

MATN YA RIWAYA

Tunachokiona kwa uwazi katika *matn* za riwaya hizi ni hii migongano iliyokuwepo baina ya riwaya moja na nyengi au riwaya moja yenyewe kwa yenyewe. *Matn*[526] ya riwaya hii ina vipengele sawa na vipengele vya riwaya ya kwanza tuliyoinukuu kutoka kwa Al-Tabari, hatuna haja ya kuvirejea. Lakini kuna mambo mawili, matatu, ya ziada ya kuzingatiwa katika riwaya hii:

Jambo moja lililomo katika riwaya hii ni kuwa: "Ali aliwakataza watu wake kwamba wasiwapige *Khawarij* mpaka watapozua jambo".[527] Kwa hivyo, kwa mujibu wa riwaya hii, Ali hakupewa amri na Mtume (s.a.w.) ya kuwapiga watu hao na kwa hivyo alisubiri wafanye kosa. Na hii ni

524 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 119.

525 - Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 732, Hadithi na. 13. Al-Daraqutni *Al-Sunan* j. 3, uk. 131-132, riwaya na. 156. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 141. Al-Bayhaqi ,*Al-Kubra* j. 12, uk. 356-357, riwaya na. 17237.

526 - Sijanukuu riwaya kamili kwani maana ya riwaya nyengine ni sawa na zilizotangulia, na pia ili tufupishe kadiri inavyowezekana.

527 - Tazama marejeo hayo niliyoyatoa ya riwaya hii.

tafauti na riwaya nyengine za kutunga zinavyosema kwamba Ali kapewa amri ya kuwapiga watu hao, kama vile riwaya isemayo:

> Nimeamrishwa kuwapiga vita *Annakithin* (Wenye kuvunja ahadi)[528] na *Al-Qaasitin* (Waovu, wenye kukengeuka kotokana na haki)[529] na *Al-Mariqiin*[530] (Wenye kutoka, yaani Khawarij).[531]

Na riwaya isemayo:

> …Popote mutapowakuta waueni, hakika kuwaua wao ni ujira mkubwa[532]…..Lau si (hofii) kuja mukafanya israfu (mukachupa mipaka) basi ningewasimulia kile alichokiahidi Allah kupitia katika kinywa cha Muhammad kwa wale watakaowapiga[533]….Lau linajua jeshi litalowapata kile walichopewa na Allah kupitia katika kinywa cha Nabii wao (s.a.w.) basi wangeacha kufanya (mambo mengine yote).[534]

Sasa cha kujiuliza hapa ni kuwa, ikiwa Ali kapewa amri ya kuwapiga, kwanini tena asiwapige watu hao mara tu baada ya kujitenga naye, akasubiri mpaka wakaua watu? Hio ikiwa tutaichukulia riwaya inayohusu kuuliwa Abdullah bin Khabbaab kuwa ni sahihi, na tukichukua riwaya kwamba Ali aliwapiga bila ya wao kuua mtu, itabidi tujiulize riwaya zote hizi zilizojaa katika vitabu kwa kapu na kwa magunia (kuwa wao walimuua Ibn Khabbaab) zimetoka wapi? Tena kwa mara ya pili, tukichukua riwaya kwamba Ali kupewa amri basi itabidi tujiulize kwanini Ali akasema baadae kwamba: "Musiwaue

528 - Wenye kuvunja ahadi ni Talha na Zubair aliopigana nao katika vita vya Jamal.

529 - Al-Qaasitin (Waovu, wenye kukengeuka kotokana na haki) ni Mu'awiya na kundi lake.

530 - Al-Mariqiin (Wenye kutoka) ndio hao waliyoitwa kuwa ni Khawarij, yaani Watu wa Nahrawaan. Nayo riwaya hii ni uwongo mtupu uliyotungwa na Shia wa Iraki, katika *sanad* yake kumejaa Mashia ambao wanavyuoni wa wapokezi wanatwambia kuwa ni waongo, watunzi wa riwaya kama tutavyobainisha katika juzuu ya pili *Inshaa Allah*.

531 - Nayo ni riwaya maudhui (ya kutunga) kama tutakavyoibainisha katika juzuu ya pili *Inshaa Allah*.

532 - Al-Bayhaqi: *Al-Kubra* j. 12, uk. 323, riwaya 17164.

533 - Al-Bayhaqi: *Al-Kubra* j. 12, uk. 323, riwaya 17166.

534 - Al-Bayhaqi: *Al-Kubra* j. 12, uk. 323, riwaya 17167.

Makhawarij tena baada yangu, aliyeitafuta haki akakosea si kama aliyeitafuta batili (kwa kukusudia)".[535] Na akasema Al-Tabari:

> Katika mwaka huu, walifanya harakati *Makhawarij* ambao walijitenga na (wenzao) waliojeruhiwa huko Nahrawaan na (pia walijitenga na) wale waliopona miongoni mwa majeruhi wao huko Nahrawaan, wakapona, basi Ali (r.a.) akawasamehe.[536]

Vipi Ali anasema: "Musiwaue *Makhawarij* tena" na vipi anawasamehe wakati Mtume (s.a.w.) kamuamuru awauwe na akaahidi – kwa mujibu wa riwaya tulizozinukuu kabla – ujira usio na kifani kwa atakayewaua: vipi mtu huyu kapewa amri na Mtume (s.a.w.) ya kufanya kitu kisha haitekelezi, bali – kinyume chake – anakataza kufanywa kitu hicho? Je riwaya hizi zina ukweli?

Jengine: tunalolipata katika riwaya hii, ni kuwa kule kujitenga kwao na Ali tu, siko kulikosababisha vita hivyo, jambo ambalo pia ni tafauti na riwaya nyengine ambazo zinasema kwamba kitendo chao cha kumuasi Ali ndio sababu ya Ali kuwapiga watu hao; na bila shaka hili ni jambo lenye mantiki kabisa, kwani ikiwa Ali kafunga safari kutoka Al-Kufa kwenda kumpiga Mu'awiya Sham[537] kwa sababu hakumtambua, vipi asifunge safari kwenda mahala pa meli mbili, tatu, kupambana na watu wengine ambao walimuacha mkono na kuchagua Amiri wao? Wala haiwezekani kusema kwamba amri aliyopewa Ali imefungamanishwa na pale watu hao watakapofanya mauaji, kwani baada ya kufanya mauaji bila haki basi hukumu zake zimeshatajwa katika Qur-ani na Sunna: hakuna haja ya utabiri wala kuambiwa mtu kuwa awaue kwani muuaji hukumu yake inajulikana.

---

535 - Ifahamike kwamba neno: "Al-Khawarij" katika kitabu hicho *Nahju Al-Balagha* cha khutuba za Ali, halikutamkwa na Ali mwenyewe, bali ni katika usarifu wa waandishi, kwani Ali (k.w.) kafa mwaka wa 40 wakati neno "Al-Khawarij" kwa maana ya waliyomuacha mkono Ali lilitumika kuanzia mwaka wa 60. Neno lililokuwa likitumika katika zama za Ali kumaanisha watu hao ni "Al-Harauriyyah" (Watu wa Al-Harauraa) au "Al-Nahrawaaniyyun" (Watu wa Nahrawaan).

536 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 79.

537 - Bali unaweza ukasema kwamba Ali alifunga safari kutoka Madina, kwani kwanza Ali alikuwa akijiandaa kutoka Madina kwenda kumpiga Muawiya Sham baadae ndio akapata habari ya matatizo ya Talha na Zubair huko Iraki akaamua kwenda Iraki kwanza. Tazama Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 582.

Jambo jengine: ambalo limo katika riwaya hii ni maelezo kuwa katika watu hao (*Khawarij*) kuna alama; na alama yenyewe ni *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu), yaani mtu mwenye kikono chenye maumbile kama chuchu ya mwanamke.[538] Hio ndio alama ambayo kwayo watu hao watajulikana, lakini pamoja na yote hayo cha kustaajabisha ni kuwa – kwa mujibu wa riwaya hii na nyengine zote – Ali aliwapiga watu hao bila ya kuiyona alama aliyopewa, baada ya kuwaua ndio akasema: "Mtafuteni *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu)", ambaye ndiye alama! Sasa vipi Ali kaua watu kwanza bila kujua kuwa ndio waliyokusudiwa katika maelekezo ya Mtume (s.a.w.).? Huku ni kumfanya Ali kuwa hajui alifanyalo![539]

La mwisho ni kuwa, Ali alipouliza kuhusu mtu huyo mwenye kikono chenye maumbile kama chuchu ya mwanamke, ikawa hakuna aliyemjua isipokuwa mtu mmoja ambaye alieleza kwamba alimuona sehemu kadhaa, kisha Ali akasema: "Kweli; yeye (huyu mwenye kichuchu) ni katika majini!" Kwa hivyo, kumbe mtu huyo aliyetajwa na Mtume (s.a.w.) kama ni alama ya kuwajua *Khawarij* hakuwa mtu bali ni jini! Tutakuwa na maelezo ya ziada kuhusu riwaya hii tukifika mahala pake *Inshaa Allah*. Kwa haya machache yenye kuihusu *matn* ya riwaya hii yanatosha kuonesha kuwa hizi ni riwaya zilizokuwa zikitungwa na watu ili kuwapaka matope watu waliokuwa na msimamo wa haki.

TAKHRIJ NA UCHAMBUZI WA *SANAD* ZA RIWAYA HIZO

Baada ya kuzitazama *mutun (texts au maneno)* za riwaya hizo, sasa na-tutazame *sanad* zake:[540]

538 - Tutaielezea riwaya hii katika juzuu ya pili *Inshaa Allah*.

539 - Riwaya hii ya mwenye kichuchu au mwenye kikono ina maelezo marefu yatakuja *Inshaa Allah* katika juzuu maalumu ya utafiti kuhusu riwaya za Khawarij.

540 - Cha kufahamu ni kuwa hapa kuna riwaya nyengine sikuzinukuu ambazo zina maelezo sawa na hizo nilizozinukuu. Nimeziwacha kwani maneno yaliomo katika

Riwaya ya kwanza tuliyoinukuu kutoka kwa Al-Tabari, kaisimulia pia Al-Bukhari.[541] Al-Khatib Al-Baghdadi,[542] Ahmad,[543] Al-Tabarani,[544] Ibn Sa'ad,[545] Abu Ya'ala,[546] Ibn Abi A'asim,[547] Ibn Abi Shaiba,[548] Al-Daraqutni kwa *sanad* mbili,[549] Abdul-Razzaaq,[550] na Al-Baladhiri.[551]

Riwaya ya Al-Bukhari, Ahmad, Al-Tabarani, Ibn Sa'ad, Abu Ya'ala, Ibn Abi A'asim, Ibn Abi Shaiba, na Al-Baladhiri, *sanad* yake ni: "Kutoka kwa Ayyub kutoka kwa Humaid bin Hilal kutoka kwa mtu katika (watu wa kabila la) Abdil-Qais". Nayo – kama unavyoona – ni *sanad* yenye mpokezi asiyejulikana, *sanad* inasema: "Kutoka kwa ***mtu*** katika (watu wa kabila la) Abdil-Qais" basi ni hivyo tu "Mtu wa kabila la Abdil-Qais": hajulikani ni nani, na kwa hivyo riwaya hii ni dhaifu sana.

Ama Al-Imamu Al-Tabari mwenyewe, yeye kaisimulia riwaya hio kwa *sanad* hii: "Kasema Abu Mikhnaf kutoka kwa Ataa bin 'Ajlaan kutoka kwa Humaid bin Hilal".[552] Abu Mikhnaf, naye ni Lut bin Yahya, sifa yake ni mbaya sana kama tulivyombainisha kabla.[553] Ama Ataa bin 'Ajlaan, naye pia ni dhaifu sana bali kaitwa muwongo, msimulizi wa Hadithi za kutunga.[554] Na msimulizi wa riwaya hio – sawa na riwaya

---

riwaya hizo ni sawa na maneno yaliyomo katika riwaya hizi , na kwa hivyo, nitaelezea *sanad* tu za riwaya hizo, yaani nitaelezea *sanad* za riwaya nilizozinukuu na *sanad* za riwaya nisizozinukuu.

541 - Al-Bukhari , *Al-Taarikh Al-Awsat* j. 1, uk. 175, *tarjama* na. 267.

542 - Al-Khatib, *Taarikh Baghdad* j. 1, uk. 220, *tarjama* na. 46 na j. 12, uk. 286, *tarjama* na. 6733.

543 - Ahmad, *Al-Musnad* j. 7, uk. 69, riwaya na. 21378.

544 - Al-Tabarani ,*Al-Kabir* j. 4, uk. 3629-3630-3631.

545 - Ibn Sa'ad, *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 5, uk. 189-190, *tarjama* na. 783.

546 - Abu Ya'alaa, *Al-Musnad* j. 13, uk. 176, riwaya na. 7215.

547 - Ibn Abi Asim, *Al-Ahadi Wa Al-Mathani* j. 1, uk. 215.

548 - Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 732, riwaya na. 16, *Kitabu Al-Jamal wa Siffin wa Al-Khawarij.*

549 - Al-Daraqutni, *Al-Sunan* j. 3, uk. 132, riwaya na. 157.

550 - Abdul-Razzaaq *Al-Musannaf* j.

551 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 142, na 143-144.

- Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 6, uk. 23. 552

553 - Tazama maelezo nambari 24.

554 - Anasema Ibn Ma'in: "Si mwenye kuaminika….mwongo mkubwa…alikuwa hana maana: anatungiwa Hadithi kisha yeye anazisimulia". Anasema Asid bin Zaid kutoka

iliyotangulia – ni Humaid bin Hilal naye hakuyashuhudia matukio hayo bali ni mambo ya kusimuliwa na watu tu – kake kannena kake kantongoa *Wallahu Al-musta'an.*

Ama Al-Khatib Al-Baghdadi – katika moja ya *sanad* zake mbili – na Al-Daraqutni – pia katika moja ya *sanad* zake mbili[555] – wao wameipokea riwaya hii kutoka kwa….Ahmad bin Muhammad bin Rishdain[556]…kutoka kwa…Humaid bin Hilal kutoka kwa Abu Al-Ahwas akisema: "...Tulikuwa pamoja na Ali siku ya (vita vya) Nahrawaan"…kisha inafuata riwaya. Abu Al-Ahwas huyu ni Awf bin Malik bin Nadhlah Al-Jushami Al-Kufi, naye kuna khilafu juu ya kuwa je kapata kusikia riwaya kutoka kwa Ali au hakusikia.[557] Lakini kwa hali yoyote ile, Abu Al-Ahwas huyu ni mwenye kuaminika wala hakuna aliyemtia ila.[558] Hata hivyo, tatizo bado liko katika *sanad* hii ambayo inatufikisha huko kwa Abu Al-Ahwas. Katika *sanad* hii – kama unavyoona – kuna Ahmad bin Muhammad bin Rishdain, naye ni dhaifu. Anasema Ibn Adaeiy: "Walimkadhibisha (Walisema kuwa ni mwongo) na wakamkanushia mambo mengi (Wakazipinga Hadithi zake nyingi)".[559]

---

kwa Zuhair bin Mu'awiya: "Sikumtuhumu (mtu yeyote yule kwa uwongo) isipokuwa Ataa bin Ajlan, na akamtajia hayo Hafs bin Ghiyaath akamsadiki (kuwa anavyosema ni kweli)". Anasema Amru bin Ali: "Mwongo mkubwa". Anasema Abu Zur'a kwamba (Ataa bin Ajlaan ni): "Dhaifu". Anasema Abu Hatima: "Hadithi zake ni dhaifu; Hadithi zake ni munkar sana…naye Hadithi zake zinaachwa". Anasema Al-Bukhari: "Hadithi zake ni munkar." Anasema Abu Daud: "Hana maana". Anasema Al-Nasai: "Si mwenye kuaminika". Anasema Al-Tirmidhi: "Ni dhaifu; Hadithi zake hazina maana". Anasema Al-Juzjaani: "Ni mwongo mkubwa". Wanasema Ali bin Junaid, Al-Daraqutni na Ibn Shahin: "Ni mwenye kuachwa". Anasema Al-Tabarani: "Ni dhaifu". Anasema Ibn Hibbaan: "…Anasimulia Hadithi za kutunga kutoka kwa wapokezi wenye kuaminika; si halali kuandika Hadithi zake". Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7, uk. 186-187, *tarjama* na. 388.

555 - *Sanad* ya pili ya riwaya ya Al-Daraqutni tutaielezea katika maelezo yetu juu ya riwaya ya tatu.

- Wengine humtamka "Rashdain".[556]

557 - Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 150, *tarjama* na. 305.

558 - Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 150, *tarjama* na. 305.

559 - Ibn Hajar, *Lisanu Al-Mizan* j. 1, uk. 280, *tarjama* na. 805.

Ama katika *sanad* ya pili ya Al-Khatib, Ahmad bin Muhammad bin Rishdain hayumo, lakini katika *sanad* hii ya pili ya Al-Khatib pamoja na *sanad* ya Al-Daraqutni, aliyeisimulia riwaya hio kutoka kwa Abu Al-Ahwas, ni Al-Hakam bin 'Abda Al-Shaibani, naye ni dhaifu.[560] Bila kusahau kwamba katika *sanad* hii ya pili ya Al-Khatib yumo Abu Khaithama, Ali bin Amri bin Khalid, dhahir ni kuwa huyu ni mpokezi asiyejulikana. [561] Kwa hivyo, kwa hali yoyote ile hii pia ni riwaya dhaifu.

Riwaya ya pili ya Al-Tabari *sanad* yake ni sawa na riwaya ya Al-Bukhari, Ahmad, Al-Tabarani, Ibn Sa'ad, Abu Ya'ala, Ibn Abi A'asim, Ibn Abi Shaiba, na Al-Baladhiri, ambayo tumeielezea katika riwaya ya kwanza katika *Takhrij* hii: *sanad* yake ni: "Kutoka kwa Ayyub kutoka kwa Humaid bin Hilal kutoka kwa mtu katika (watu wa kabila la) Abdil-Qais". Nayo tumeshaibainisha udhaifu wake.

Riwaya ya tatu kaipokea Ibn Abi Shaiba,[562] Al-Daraqutni,[563] Al-Bayhaqi[564] na Al-Baladhiri[565] kwa njia ya Sulaiman Al-Taymi kutoka kwa Abu Mijlaz. Riwaya hii katika *sanad* zake zote msimulizi wake ni mmoja naye ni Abu Mijlaz, naye ni Lahiq bin Humaid bin Said Al-Sadusi, naye ni mwenye kuaminika kwa mujibu wa wote isipokuwa Ibn Mai'n anasema: "Hadithi zake zinagongana".[566] Kwa hali yoyote ile tatizo la Abu Mijlaz katika riwaya hii hususan, ni kuwa riwaya yake hii ni *mursala* kama Al-Daraqutni alivyoitia kasoro kwa kusema kwamba riwaya hii: "…Kaisimulia Abu Mijlaz hali ya kuwa ni riwaya mursala",[567] na riwaya *mursala* – kwa wanavyuoni wa Hadithi – ni dhaifu.[568] Kwa hivyo

560 - Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 2, uk. 372, *tarjama* na. 755.

561 - Katajwa katika baadhi ya vitabu nilivyovitazama lakini sikuona alipotajwa kuwa ni *thiqa* (mwenye kuaminika) au kuwa ni dhaifu. Huenda ikawa viko vitabu vilivyomuelezea lakini hilo si muhimu kwani sanad tayari ina kasoro nyengine kama ulivyoona, kwa hivyo, sikufanya bidii ya kumpekuwa sana.

562 - Ibn Abi Shaiba *Al-Musannaf* j. 8, uk. 732, riwaya na. 13, *Kitabu Al-Jamal wa Al-ssiffin wa Al-Khawarij; Babu Maa dhukira fii Al-Khawarij.*

563 - Al-Daraqutni ,*Al-Sunan* j. 3, uk. 131-132, riwaya na. 157.

564 - Al-Bayhaqi ,*Al-Sunan Al-Kubra* j. 12, uk. 356, riwaya na. 17237.

565 - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 141.

566 - Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 151, *tarjama* na. 293.

567 - Al-Daraqutni, *Al-Ilalalu Al-Waarida* j. 4, uk. 101.

568 - Tena *mursala* hii si ile ambayo inasimuliwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.) ambayo kuna uwezekano mkubwa msimulizi ikawa labda kaisikia kutoka kwa Sahaba: hii

riwaya hii pamoja na mgongano uliyomo katika *matn* yake, vile vile ina udhaifu katika *sanad* yake.

Riwaya ya nne kaisimulia Abdul-Razzaq kutoka kwa Ma'amar kutoka kwa Ayyub kutoka kwa Humaid bin Hilal.[569] Ma'amar alikuwa Shia, na Shia – kama tulivyosema – hata kama si mwongo basi akisikia riwaya inayounga mkono *Ahlu Al-Bait* au inayowaponda waliokuwa hawakukubaliana na Ali, basi hana haja hata ya kuihakikisha na kumchunguza msemaji aliyemwambia. Bali Ibn Ma'in anasema:

> Ma'amar akikusimulia kutoka kwa Wairaki basi usimkubalie ila kutoka kwa Al-Zuhri na Tawus, ama akikuhadithia kutoka kwa watu wa Al-Kufa na Basra basi usizikubali (riwaya zake).[570]

Na riwaya hii Ma'amar kaisimulia kutoka kwa Ayyub bin Abi Tamima, mtu wa Basra huko Iraki, na kwa hivyo kwa mujibu wa Ibn Main hii ni riwaya ya uwongo. Hatimae tunamkuta msimulizi wa riwaya hio ni Humaid bin Hilal Al-'Adawi, naye – kama tulivyosema kabla – hakuyashuhudia matukio hayo bali kasikia watu tu: kake kannena na yeye akanena!

Lakini Abdul-Razzaaq kaisimulia riwaya hii tena kwa *sanad* isemayo:

> Kutoka kwa Ma'amar kasema kaniambia zaidi ya mmoja miongoni mwa watu wa (kabila la) Bani Abdil-Qais kutoka kwa Humaid bin Hilal kutoka kwa baba yake…[571]

Lakini kama unavyoona kwamba *sanad* hii ina wasimulizi *Majhulun* (Wasiojulikana): *sanad* inasema: "Zaidi ya mmoja miongoni mwa watu wa (kabila la) Bani Abdil-Qais"; basi ni hivyo tu: hawajulikani ni nani. Kwa hivyo, hii pia ni *sanad* dhaifu. Na msimulizi wa riwaya hii ni Hilal

---

inasimuliwa kuhusu matukio yaliyotokea zama za Ali, na kwa hivyo, uwezekano mkubwa ni kuwa aliyeisimulia si Sahaba kamwe bali inawezekana ikawa ni maneno ya kusikia mitaani tu hasa hasa tukichukua kauli iliyomo katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 151, *tarjama* na. 293, yenye kuashiria kwamba Abu Mijlaz ni Shia.

569 - Abdul-Razzaaq, *Al-Musannaf* j. 9, uk. 439, riwaya na. 18900.

570 - Tazama: *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 10, uk. 218-220, *tarjama* na. 440.

571 - Abdul-Razzaaq, *Al-Musannaf* j. 9, uk. 439, riwaya na. 18901.

bin Suwaid bin Hubaira, baba yake Humaid bin Hilal, dhahir ni kwamba naye pia hajulikani.[572]

Riwaya ya tano kaisimulia Al-Bukhari katika kitabu chake kiitwacho *Al-Taariikh Al-Awsat*[573] kutoka kwa Aamir Al-Sha'abi. Lakini Al-Sha'abi pia hakuyashuhudia hayo bali kasimuliwa tu na watu wala hakusema ni nani hao. Kwa hivyo, riwaya hii pia bado haijawa hoja inayokubalika katika uwanja wa elimu.

UCHAMBUZI WA UJUMLA WA SANAD YA RIWAYA HII

Kwa ujumla ni kuwa riwaya ya kuuliwa kwa Ibn Khabbaab na kuhusishwa kwake na Watu wa Nahrawaan (r.a.), imekuja kwa njia tatu:

Moja: ni njia ya Abu Miljaz ambayo Al-Daraqutni kaidhoofisha – kama tulivyotangulia kumnukuu – kwa sababu ya kuwa kwake ni riwaya *mursala* – Abu Mijlaz hakuyaona matukio hayo wala hakusema ni nani aliyemwambia: bali ni masuala ya kusikia mitaani tu; na masimulizi kama haya huwa hayana kima (thamani) katika uwanja wa elimu.

Pili: ni njia ya Hilal bin Humaid, nayo – kama ulivyoona kwamba – katika *sanad* zote zinazotuchukua hadi kwa bwana Hilal mwenyewe ni *sanad* dhaifu. Jengine lililomo katika *sanad* hizo ni mgongano wa *sanad*: riwaya hio – katika baadhi ya mapokezi yake – Hilal bin Humaid anaisimulia kutoka kwa mtu asiyejulikana wa kabila la Abdil Qais; wakati

---

572 - Isipokuwa ikiwa ni Hilal bin Suwaid Al-Ahmari aliyemtaja Ibn Hajar katika *Lisanu Al-Mizan* j. 6, uk. 201, *tarjama* na. 716-717, na Al-Dhahabi katika *Al-Mizan* j. 5, uk. 439, *tarjama* na. 9269. Kama huyu ndiye aliyekusudiwa katika *sanad* hiyo tunayoizungumzia, basi ni dhaifu sana. Rejea marejeo hayo tulioyataja. Vyenginevyo, atakuwa ni mpokezi asiyejulikana. Ninasema: na hata akijulikana yeye, wapokezi wengine wasiojulikana waliomo katika sanad hio wanaifanya *sanad* iporomoke. Hata hivyo, nimepekuwa vya kutosha sikuona alipotajwa mpokezi huyu pamoja na jina la babu yake "Hubaira" isipokuwa pale alipotajwa mwanawe Humaid bin Hilal bin Hubaira au bin Hilal bin Suwaid bin Hubaira kama ilivyo katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* cha Ibn Hajar j. 3, uk. 45, tarjama na. 87. *Wallahu A'alam.*

573 - Al-Bukhari, *Al-Awsat* j. 1, uk. 190, *tarjama* na. 309.

katika riwaya nyengine watu wa kabila hilo ndio waliyoisimulia riwaya hio kutoka kwa Hilal bin Humaid na Hilal mwenyewe kaisikia kutoka kwa baba yake, isitoshe baba yake mwenyewe ni *Raawin Majhul* (Mpokezi asiyejulikana);[574] na katika masimulizi mengine Hilal bin Humaid kaipokea kutoka kwa Abu Al-Ahwas, Awf bin Malik bin Nadhlah Al-Jushami Al-Kufi. Na bila shaka huu ni mgongano wa wazi wa *sanad* ambao haukubaliki katika elimu ya Hadithi.

Tatu: ni njia ya Al-Sha'abi, lakini Al-Sha'abi naye pia hakuyashuhudia matukio hayo na hakusema nani aliyemwambia, na kwa maana hio riwaya yake hapa haikubaliki.

Hizo ndizo riwaya zenye kusimulia suala la kuuliwa kwa Sahaba Abdillahi bin Khabbab na kuyahusisha mauaji hayo na Watu wa Nahrawaan, nazo kama unavyoona ni riwaya ambazo hazijengi hoja sahihi: si katika *mutun (texts)* zake wala si katika *sanad* zake – zote **كَسَرَابٍ بِقِيعَةٍ يَحْسَبُهُ الظَّمْآنُ مَاءً حَتَّى إِذَا جَاءَهُ لَمْ يَجِدْهُ شَيْئاً ni kama mazigazi**[575] **(mirage) katika ardhi tambarare, mwenye kiu hudhani ni maji hata akiyajia hakuti kiti.**

UCHAMBUZI WA SHEIKH NASSIR AL-SABI'I WA RIWAYA YA KUULIWA KWA ABDILLAHI BIN KHABBAB

Sheikh Nassir Al-Sabi'i – katika maudhui hii – ana hiki cha kutueleza:

> Tunakuta katika baadhi ya riwaya kwamba Ali alipowataka (Watu wa Nahrawaan kwamba wawatoe) wauaji (waliomuua Abdillahi bin Khabbab), alitoka mtu.[576] Je ni mtu gani huyu? Na kwanini atoke

- Au ni dhaifu sana ikiwa aliyekusudiwa ni yule aliyetajwa na Ibn Hajar katika *Lisanu* [574] *Al-Mizan* na Al-Dhahabi katika *Al-Mizan* kama maelezo yalivyotangulia katika maelezo na. 571.

[575] - Mazigazi ni mmeremeto au mng'aro wakati wa jua kali ambao unamfanya mtu aone kama ni maji kumbe ni mng'aro au mmeremeto wa mwanga ulioakisiwa katika ardhi.

[576] - Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 3, uk. 1105. Ibn Abdi-Rabbih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 2, uk. 94.

wakati huo? Na wanasimulia Al-Baladhiri na Al-Ash'ari kwamba Mis'ar bin Fadaki Al-Tamimi[577] alijiunga na bendera ya Abi Ayyub Al-Ansari katika jeshi la Ali kabla ya kuanza vita vya Nahrawaan.[578] Bali anasimulia Al-Ash'ari vile vile, na Al-Maqdisi kwamba Mis'ar alijiondoa kuelekea Basra kabla ya kuanza vita (vya Nahrawaan).[579] Na hii inakubaliana na riwaya ya Al-Shammakhi yenye kusema kwamba Mis'ar bin Fadaki alipofika kwa Watu wa Nahrawaan waliyapinga yale aliyoyatenda na wakataka kumuua akakimbia, nao wakajitenga naye, basi akatoka (Mis'ar) akawa anaua watu ovyo ovyo.[580] Kama anavyosimulia Ibn Hazm – akiafikiana na Al-Shammakhi – kwamba Mis'ar alikuja kwa Al-Imamu Ali akaomba apewe amani kisha akatubia. Kasema Ibn Hazma: "Na alikuwa akifanya wizi wa njiani na kuhalalisha kuingilia (wanawake)".[581]

Haya yote yanathibitisha kutokuhusika kwa Watu wa Nahrawaan na matendo maovu ya Mis'ar, vile vile yanathibitisha kutokukiridhia kwao (Watu wa Nahrawaan, kitendo cha) kuuliwa kwa Ibn Khabbaab na kwamba wao walimbebesha jarima hio Mis`ar. Na kwa sababu hii, Al-Ash'ari anasema – baada ya kuyasimulia aliyotenda Mis'ar -: "Na baadhi ya *Khawarij* wanasema kwamba Abdullah bin Wahb[582] alikuwa akiyachukia yote hayo halkadhalika wafuasi wake".[583] Na kilicho mbali zaidi kuliko haya ni kile kinachosemwa na baadhi ya riwaya (kwamba):

> Wakenda mpaka wakafika Nahrawaan, basi kikatoka kikundi miongoni mwao wakawa wanawatishia watu kwa kuwaua, wenzao wakawambia: "Wele wenu! Haya sio ambayo juu yake tulifarikiana na Ali.[584]

Na kwa msingi huu na kwa ajili ya kuziowanisha riwaya zote hizi, basi inawezekana kuwa maneno "Sote ni wenye kumuua" – tukijaalia kuwa yamethibiti – (basi yatakuwa) yametokana na kikundi hiki ambacho

---

577 - Ambaye ndiye aliyeongoza kikosi kilichotoka Basra kilichomuua Abdillahi bin Khabbab.

578 - Al-Baladhiri „*Al-Ansab* j. 3, uk. 146. Al-Ash'ari *Al-Maqalat* uk. 43.

579 - Al-Ash'ari *Al-Maqalat* uk. 43. Al-Maqdisi, Tahir *Al-Bad-U Wa Al-Taarikh* Jalada la 2, j. 5, uk. 137.

580 - Al-Shammakhi ,*Al-Siyar* j. 1, uk. 50.

581 - Ibn Hazm, *Al-Muhalla* j.11, uk. 301-302. Al-Shammakhi, *Al-Siyar* j. 1, uk. 50.

582 - Imamu wa Waislamu wa Nahrawaan (r.a.).

583 - Al-Ash'ari, *Al-Maqalat* uk. 43.

584 - Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 15, uk. 31. Abu Ya'ala *Al-Musnad* j.1, uk. 366.

(kilitoka Basra) kikiongozwa na Mis'ar kabla ya kufika Nahrawaan, ambapo walimuua mjumbe wa Ali. Na baada ya kufukuzwa kutoka Nahrawaan wakawaua wengine mbali na Abdillah bin Khabbaab na mkewe; kwani riwaya ya Al-Shammakhi inaonesha kwamba Mis'ar alimuua Ibn Khabbaab tu kabla ya kufika Nahrawaan; alipofika kwao (Watu wa Nahrawaan) wakamfukuza akatoka akawa anaua watu na akawakuta Mahujaji akawakata shingo zao.[585] Na labda aliposikia kwamba Ali kanyanyua bendera ya amani alikwenda ili apate msamaha. Na ili asalimike na adhabu alikuja hali yakuwa ni mwenye kujibadilisha sura yake kama ilivyo katika (kitabu cha) Ibn Hazm (kwamba):

Alikuja Mis'ar bin Fadaki naye ni mwenye kujibadilisha sura mpaka akaingia kwa Ali bin Abi Talib, basi hakuacha Aya ya Qur-ani yenye kushadidia ila alimuuliza (Ali) kuhusu (Aya) hio na huku anasema: 'Je (mtu atayefanya hivyo) ana toba?'[586] 'Hata akiwa Mis'ar bin Fadaki?' Akasema (Ali): 'Hata akiwa Mis'ar bin Fadaki'. Akasema: (Mis'ar bin Fadaki kumwambia Ali): 'Mimi ni Mis'ar bin Fadaki nipe amani'. Akasema (Ali): 'Uko katika amani'. Anasema (Ibn Hazm): 'Na alikuwa akifanya wizi wa njiani na kuhalalisha kuingilia (wanawake).[587]

Pili: kuna jambo jengine – mbali na hilo liliotangulia – lenye kuunga mkono kutokuhusika kwa Watu wa Nahrawaan na njia ya kufanya mauaji na kuhatarisha maisha ya watu, na kwamba matukio ya mauaji yaliyotajwa hayakuvuka kuwa ni utokaji wa kibinafsi katika mzunguko huu.[588] Alikuwa Abu Bilal Mirdas bin Udaiyya Al-Tamimi ni miongoni mwa waliohudhuria *Siffin* pamoja na Ali na akapinga kufanywa kwa sulhu kisha akajitenga na akaenda Al-Harauraa pamoja na waliopinga sulhu hio. Na ni miongoni mwa (watu) mia nne waliojeruhiwa katika vita (lakini) akanusurika kufa na alibakia hadi zama za Ziad bin Abihi, Liwali wa Mu'awiya wa Al-Kufa na Al-

585 - Al-Shammakhi, *Al-Siyar* j. 1, uk. 50.

586 - Yaani Mis'ar akawa anamuuliza Al-Imamu Ali kuhusu zile Aya zenye kutaja adhabu kwa watu wenye kufanya makosa kisha anamuuliza je mtu mwenye kufanya makosa hayo ana toba? Akimwambia ndio humuuliza tena: 'Hata akiwa Mis'ar bin Fadaki?' Anauliza hivyo naye kajibadilisha sura ili akiambiwa Mis'ar hana toba akimbie asijeakauliwa na Al-Imamu Ali.

587 - Ibn Hazm, *Al-Muhalla* j. 11, uk. 301-302. Al-Shammakhi, *Al-Siyar* j.1, uk. 50.

588 - Yaani habari zilizotajwa kuhusu mauaji ya Abdillahi bin Khabbaab ni mauaji yaliofanywa na mtu binafsi: hayahusiani na harakati kamili au madhehebu kamili ya Watu wa Nahrawaan.

Basra. Na Ziad alikuwa aondokapo Al-Basra, humfanya Samura bin Jundub Al-Fazaari kuwa ndiye Khalifa wake. Ziad na Samura – wote kwa pamoja – walikuwa na siasa ya kijeuri kwa wapinzani wa utawala (wao) mpaka hali ikawa mbaya sana, jambo ambalo liliwapelekea baadhi ya wapinzani wao nao kufuata siasa kali, basi likatokea tukio la Qarib bin Murra Al-Azdi Al-Iyadi na Zahhaf bin Zuhar Al-Tai (ambao walikuwa mama zao ni ndugu) kuua watu wengi. Abu Bilal[589] akasema: "Qarib, Allah asimkurubishe na kila kheri na Zahhaf Allah asimsamehe; kwa hakika wameingia katika kiza".[590] (Abu Bilal) kayasema hayo kwa sababu ya (Qarib na Zahhaf) kuua kwao bila ya haki. Na katika riwaya nyengine (Abu Bilal kasema): "Qarib Allah asimkurubishe na kheri yoyote, naapa kwa (jina la) Allah kuanguka mimi kutoka kwenye mbingu ni bora zaidi kwangu kuliko kuyafanya waliyoyafanya wao" yaani (kwa jarima lao la) kuua watu bila ya haki.

Na alitoka Mirdas (Abu Bilal) pamoja na watu arobaini katika zama za Ziad – ambaye alikwenda mwenendo mbaya zaidi kuliko wa baba yake – kuelekea Al-Ahwaz huku akisema:

> Wallahi – kwa hakika – hatuwezi kukaa pamoja na madhalimu hawa, wanatupitishia hukumu zao nao ni wenye kuuepuka uadilifu; wenye kuliacha kila lenye fadhila;[591] Wallahi, kusubiri juu ya haya ni vigumu, na kuunoa upanga na kuwatia watu hofu (pia) ni (jambo) zito, lakini sisi tunawaachilia mbali wao na wala hatuunoi upanga wetu wala hatupigani ila na atayetupiga.[592]

Na miongoni mwa aliyoyasema (Abu Bilal ni):

> Hakika ya sisi hatukutoka ili kufanya ufisadi katika ardhi wala kumtia hofu mtu yeyote, lakini (tumetoka) kwa ajili ya

589 - Aliyeongoza harakati baada ya kuuliwa kwa Al-Imamu Abdullahi bin Wahb Al-Rasibi (r.a.).

590 - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 5, uk. 183, Al-Ya'aqubi ,*Al-Taarikh* j. 2, 232, Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 3, uk. 1169.

591 - Lakini katika riwaya ya Al-Mubarrad limetumika neno "Al-Faslu" lenye kumaanisha "Hukumu au Upambanuzi". Inawezekana ikawa ni kosa la chapa au ikawa ndio neno sahihi, na maana yake ni: "Wenye kuiacha kila hukumu iliyopambanuliwa katika Qur-ani na Sunna".

592 - Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 628. Ibn Abdi Rabbih,, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 1, uk. 178.

kukimbia dhulma, na hatupigani ila na atakayetupiga wala hatuchukui ngawira isipokuwa *ataya*[593] zetu.[594]

Na vitabu vyengine vinathibitisha kwamba yeye (Abu Bilal) hakuua (mtu) wala hakuhatarisha amani ya njia,[595] na kwamba "Alikuwa haitakidi (uhalali wa) kuua bila haki".[596]

…..Mwenendo (huu) wa Abu Bilal uko wazi kwamba hahalalishi kumpiga mtu yeyote ila kwa ajili ya kujilinda, na hili linatupa picha ya tabia ya Watu wa Nahrawaan kwamba wao walikuwa hawahalalishi damu ya yeyote, kwani Abu Bilal ni mmoja wao, na hakuna shaka kwamba alisimama msimamo wa kiuadui dhidi ya Qarib (bin Murra) na Zahhaf kwa sababu ya waliyoyafanya (ya kuua watu bila haki), wakati Abdillahi bin Wahb – naye ndiye nembo ya Watu wa Nahrawaan – aliridhika naye;[597] (na hili) linatubainishia picha ya uhakika wa mwenendo wao (Watu wa Nahrawaan) katika muamala[598] wao na wapinzani wao. Anasema Abu Bilal:

أبعد ابن وهب ذي النزاهة والتقى ... ومن خاض في تلك الحروب المهالكا
أحب بقاءً أو أرجّي سلامة ... وقد قتلوا زيد بن حصن ومالكا
فيا ربِّ سلِّم نيَّتي وبصيرتي ... وهب لي التقى حتى ألاقي أولئكا[599]

Baada ya Ibn Wahb mwenye mtakasiko na taquwa,
Na ambaye kajimwaga katika vita vile vyenye kuua.
Nipende salama au nitarajie bakia,
Na Zaid bin Hisn na Malik wamewaua.
E Mola! salimisha wangu uoni na yangu nia,

---

593 - Ataya zao ni fungu lao wanalostahiki kutoka katika beitil mali.

594 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 5, uk. 190, Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 3, uk. 1178.

595 - Ibn Al-khayyaat, *Al-Taarikh uk*. 159.

596 - Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 5, uk. 189.

597 - Yaani Abu Bilal, mmoja wa Watu wa Nahrawaan, aliridhika na Abdullah bin Wahb, Imamu wa Watu wa Nahrawaan (r.a.), wakati Qarib (bin Murra) na Zahhaf aliwachukia kwa sababu ya kuuwa watu. Ni wazi kwamba kuuwa watu bila haki haikuwa tabia ya watu hao wa Nahrawaan, ndio maana Abu Bilal alijitenga na akina Qarib (bin Murra) na Zahhaf Na kwa hivyo, ni kosa la kihistoria kukinasibisha kifo cha Ibn Khabbaab kwa watu hao.

598 - *Mu'amala* yaani ni maingiliano na ushirikiano wa pamoja.

599 - Al-Mubarrad, *Al-Kaamil* j. 3, uk. 1176. Ibn 'Abdi- Rabih, *Al-'Iqd* j. 2, uk. 99.

.

Mpaka nikutane na hao (Mola) nipe taquwa.[600]

> Kwa hivyo, ni wazi kwamba mwenendo wa Watu wa Nahrawaan haukuwa wa kuua na kuhatarisha maisha ya watu, kwani Abu Bilal – mmoja wao aliyesalimika katika vita hivyo – alikuwa akijitenga na kuwalaani Qarib na Zahhaf na kujitenga na Ziad kwa sababu ya kufanya mauaji, wakati Watu wa Nahrawaan alikuwa akiwasifu kwa ucha Mungu na kuwaombea dua na kumuomba Allah amkutanishe nao huko akhera). *Mwisho wa kunukuu kutoka katika kitabu cha Sh. Al-Sabi'i.*[601]

TANBIHI

Baada ya kuona hayo; tuliyoyanukuu kutoka kwa Sheikh Al-Sabi'i, ni vyema kujiuliza suali moja lenye kuhusiana na kipengele alichokitaja katika riwaya inayonukuu majibu ya Watu wa Nahrawaan kwa Ali, pale alipowataka wamtoe muuaji wa Abdullahi bin Khabbaab, watu hao walisema: **"Sote ni wenye kumuua"** yaani ni wenye kumuua Abdillahi bin Khabbab. Kipengele hiki ndicho kilichochukuliwa na kuhalalisha damu za Watu wa Nahrawaan.[602] Lakini hata hivyo, tukirudi katika vitabu vya historia tunakuta kwamba wakati Mu'awiya alipodai damu ya 'Uthman; na baada ya Abu Huraira na Abu Al-Dardaai kumuendea Mu'awiya na kumnasihi ili aingie katika kuukubali Ukhalifa wa Ali, Mu'awiya alijibu kwamba yeye anachokitaka ni waliomuua Uthman watolewe awaue kisha naye atakubali ombi hilo.[603] Abu Huraira na Abu Al-Dardaai wakatoka kumuendea Ali na kumtaka awatoe waliomuua Uthman, na baada ya hapo ikiwa Mu'wiya ataendelea na vita basi

---

600 - Ni taq-wa lakini nimeongeza "u" ili ilete sauti nzuri katika utenzi. Na maneno ya Mashairi haya nimeyapanga tafauti kwa lengo hilo hilo: maneno ni yale yale lakini upangaji ni jaribio langu.

601 - Nayo ni maneno ambayo lau hatukusema chochote ila kuyanukuu maneno haya basi yangetosha kubainisha haki ni ipi na batili ni ipi, Allah amzidishie Sheikh Al-Sabi'i elimu na nuru. Tazama *Al-Khawaarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. 127-131.

602 - Nacho – kama alivyosema Al-Sabi'i – ikiwa kitathibiti kipengele hicho, basi waliokisema ni watu wa kile kikundi kilichotoka Al-Basra kabla ya kufika huko Al-Nahrawaan.

603 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 93-94.

"Tutajua kwamba kweli yeye ni dhalimu, mwenye kufanya uadui".[604] Ali akawajibu kwamba: "Alipouliwa 'Uthman mimi sikuhudhuria:[605] lakini je munawajua waliomuua?"[606] Wakasema: "Imetufikia kwamba ni: Ammar bin Yasir, Al-Ashtar, 'Adey bin Hatim, 'Amru bin Al-Hamaq na fulani na fulani".[607] Akawambia: "Nendeni mukawachukue".[608] Abu Huraira na Abu Al-Dardaai wakaenda na walipofika huko ili kuwachukua watuhumiwa, "Kelele zikapaa katika jeshi la Ali kwa kufika habari hio na wakasimama zaidi ya watu elfu kumi katika jeshi la Ali nao wanasema: 'SISI SOTE TUMEMUUA 'UTHMAN".[609] Na akasema mshairi kuwajibu Abu Huraira na Abu Al-Dardaai:

إِنْ كُنْتُمَا أُمِرْتُمَا بِدَمِ الْقَا**تِلِ فَالنَّاسُ كُلُّهُمْ قَتَّالُ

Kama mumeamrishwa (kumleta) muuaji,
Basi watu wote (hawa) ni wauaji (waliomuua Uthman).

Na akasema Ammar bin Yasir kumwambia Amru bin Al-'Aas huko *Siffin*: "Mimi niko pamoja na waliomuua na leo nawapigania waliomuua kwani yeye alitaka kuiua dini". [610] Bali Ali mwenyewe katika barua zake alizokuwa akimpelekea Mu'awiya kakiri kwamba waliomuua Uthman anawajua lakini hataki kuwatoa.[611] Anasema:

> Ama kuwataja kwako waliomuua Uthman na kutaka nikupe wewe….hakika mimi nimelifikiria jambo hili lakini (naona) halinipi nafasi kuwatoa nikakupa wewe wala asiyekuwa wewe.[612]

---

604 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 95.

605 - Riwaya kuhusu Ali alikuwa wapi alipouliwa Uthman zinagongana. Kuna riwaya kwamba Ali alikuwa msikitini; nyengine inasema alikuwa nyumbani kwake na nyengine inasema kwamba alikuwa katika ardhi yake iliyokuwa maili 24 kutoka Madina. Labda itakuwa kuna riwaya nyengine tafauti na hizi.

606 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 95.

607 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 95.

608 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 95.

609 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 95.

610 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 125.

611 - Bali Ali aliwafanya ndio vipenzi kuliko watu wote, kama vile Muhammad bin Abi Bakr, mtoto wa Sayyidna Abu Bakr Al-Siddiq (r.a.), ambaye Ali alikuwa akimwita mwanawe kwa jinsi ilivyokuwa akimpenda; na Sahaba Ammar bin Yasir.

612 - Ibn Abdi Rabih *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 311.

Na baada ya kufika risala ya Mu'awiya kwa Ali – iliyofikishwa na Abu Muslim Al-Khawlani – risala ambayo Mu'awiya alimtaka Ali awatoe waliomuua 'Uthman, Ali aliwakusanya washauri wake Msikitini na kuwasomea risala hio, nao wakajibu: "Sote sisi ni wenye kumuua Uthman na sote ni wenye kuyapinga matendo yake".[613]

Suali ni kuwa je:

1) Kuna tafauti gani baina ya ibara iliyotamkwa na jeshi la Ali kuhusu damu ya 'Uthman na ibara iliyotamkwa na walioitwa Khawarij[614] kuhusu aliyemuuwa Ibn Khabbab wakati wote – kwa mujibu wa riwaya hizo – wamesema: "Sote ni wenye kumuua"? – Huku 'Uthman na kule Ibn Khabbaab.
2) Ali alichukua hatua gani baada ya watu hawa kukiri kwamba wote wameshiriki katika kumuua 'Uthman?
3) Damu ya Ibn Khabbab ni bora zaidi kuliko damu ya 'Uthman au huu ni ushahidi wa kuwa Ali naye kashiriki katika kumuua 'Uthman au kwa uchache karidhia? Kwani tunaona Ali alipokuwa Khalifa alitaka kumuua mtoto wa Sayyidna Umar, Ubaidi-Lahi bin Umar bin Al-Khattab, kwa sababu ya kitendo chake cha kamuua Hurmuzan, Mfursi, kwa dhulma,[615] sasa kwanini hawa asiwaue kama hakushiriki au hakuridhika?

---

613 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 67. Bali kuna riwaya kwamba Amru bin Al-'Aas ni miongoni mwa waliohimiza kuuliwa kwa Uthman na hii ni baada ya Uthman kumuuzulu Amru katika Ugavana wa Misri. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 70. Lakini *sanad* ya riwaya hii – kwa mapokezi ya Al-Baladhiri – ni dhaifu sana, na hivyo ndivyo zilivyo aghlabu ya riwaya za historia. Lakini Al-Baladhiri kaisimulia tena habari hio katika uk. 73-74, kwa *sanad* nyengine.

614 - Yaani sisi hapa tunajaalia tu kuwa riwaya ya kuuliwa kwa Abdullahi bin Khabbaab na kuhusishwa kwake na watu wa Nahrawaan ni sahihi, kama ni hivyo basi tumebakiwa na suala hili, vyenginevyo tumeona kwamba riwaya hio ni dhaifu katika *sanad* na *matn*, na kwamba muuaji alikuwa ni Mis'ar bin Fadaki na kikundi chake cha Basra.

615 - Na – ikiwa masimulizi ya Al-Mas'udi yamethibiti, basi – huyu Ubaidi-Lahi alikuwa na vumbi la kijahili sana. Eti Abu Lu-u-lu-a, Muirani, kamuua baba yake, naye akatafuta Muirani mwengine akamua na akaahidi kumuua kila Muirani atayemkuta Madina. Sasa imehusu nini kosa la mtu mmoja kumpachika nalo mwengine. Tazama Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 517. Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 78.

4) Ikiwa Masahaba Muhajirina na Ansar waliridhia na mamia ya Masahaba waliokuwa katika jeshi la Ali walikiri kwamba wao ndio waliomuua 'Uthmam, nini dhambi ya wale waliokuja baadae ambao waliridhia kama walivyoridhia Masahaba.[616] Kama kuridhia huku ni kosa kwanini liwe ni kosa la hawa wa mwisho lisiwe kosa la watangulizi wao ambao ndio vigezo vikuu vya Umma huu?

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

1) Tulichokitafiti hapa ni suala la kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbab.
2) Tukio hili ndilo linalotajwa kuwa ni kosa kubwa ambalo watu wamelichukua na kuwapaka matope kwalo Watu wa Nahrawaan; na bila shaka ni kosa kubwa ingelikuwa kweli watu hao wamelitenda.
3) Lakini tunaona kwamba kwa mujibu wa riwaya zilizosimulia tukio hilo, waliomuua Abdillahi bin Khabbab ni kikundi kilichotoka Basra kikiongozwa na Mis'ar bin Fadaki, kabla hata kikundi hicho hakijafika huko Nahrawaan.
4) Lakini je Watu wa Nahrawaan walikubaliana na kitendo hicho cha Mis'ar bin Fadaki na kikundi chake cha kumuua Abdillahi bin Khabbab au walikipinga?
   a) Baadhi ya riwaya zinasema kuwa watu hao walikiridhia kitendo hicho, na kwa hivyo Ali alipowataka wamtoe muuaji walisema: **"Sisi sote ni wenye kumuua".** Lakini riwaya hii inajibika kwamba Mis'ar bin Fadaki mwenyewe, ambaye ndiye muuaji, alikwenda kwa Ali kutangaza toba na kuomba amani na Ali akampokea. Sasa vipi Ali awatake wamtoe aliyemuua Abdillahi bin Khabbab na ilhali aliyemuua anaye mikononi?
5) b) Riwaya nyengine zinakataa, na zinasema kwamba watu hao hawakukiridhia kitendo cha Mis'ar bin Fadaki cha kumuua Abdillahi bin Khabbab, na kwamba walimfukuza kuwa pamoja nao na wakataka kumuua, akakimbia, na hapo ndipo alipokuwa akipita na kuua watu ovyo ovyo. Na hiki ndicho kilicho sahihi

616 - Hata maneno ya Aisha siku ya vita vya Jamal, yanaonesha kwamba waliomuua Uthman ni Masahaba waliokuwa pamoja na Ali.

kwa ushahidi mwingi ambao tumeunukuu kutoka katika utafiti wa Sheikh Nasir Al-Sabi'i. Katika utafiti wake ametueleza kwamba Abu Bilal Mirdas alikuwa ni mmoja wa Watu wa Nahrawaan ambaye aliokoka katika vita hivyo, naye alijitenga na kuwalani sana Qarib (bin Murra) na Zahhaf kwa sababu ya vitendo vyao vya kuua watu bure wakati Watu wa Nahrawaan (Abu Bilal) alikuwa akiwasifu kwa ucha Mungu na kuwaombea dua na kumuomba Allah amkutanishe nao huko Akhera. Na haielekei kuwa mtu amlani muuaji kwa kosa hilo kisha amuombe Allah amfufue pamoja na mwengine, mwenye kufanya kosa hilo hilo, siku ya Kiyama. Pia Mis'ar bin Fadaki, kiongozi wa kikundi kilichotoka Basra, baadae alijiunga na Abu Ayyub Al-Ansari katika vita vya Nahrawaan ili kuwapiga watu hao. Ni wazi kwamba lau Watu wa Nahrawaan walimkubali Mis'ar na kuwa pamoja naye, basi asingelikuwa dhidi yao.

c) Baada ya hayo, utaona kwa uwazi kwamba kosa hilo lilikuwa ni la Mis'ar na kikundi chake ndio maana akaenda kutangaza toba yake kwa Ali, bila shaka hili ni baada ya Watu wa Nahrawaan kumfukuza kukaa pamoja nao.

6) Pamoja na yote hayo, riwaya hizi zote ambazo zimekihusisha kitendo cha kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbab na Watu wa Nahrawaan, bado ni riwaya dhaifu sana zenye *mutun (texts)* zenye kugongana zenyewe kwa zenyewe na pia zenye kugongana na riwaya nyengine kadha wa kadhaa ambazo zinategemewa na watetezi wa Ali katika suala hili, na pia ni riwaya zenye *sanad* dhaifu sana.

7) Kwa hivyo, natija ni kuwa Watu wa Nahrawaan hawakuhusika kamwe na damu ya Ibn Khabbaab wala ya mwengine yeyote, na tunayoambiwa na Mashekhe na wanahistoria ni habari zisizo sahihi (wrong information) zilizotolewa katika mtazamo wa kisiasa ili kuficha ukweli wa uovu wa Banii Umayya na kuwapaka matope watetezi wa haki –Watu wa Nahrawaan (r.a.).

SURA YA SABA

ITIKADI WALIZOHUSISHWA NAZOWALIOITWA KHAWARIJ

Baada ya hayo ni vyema kutazama rai ambazo kwazo walioitwa *Khawarij* wametiwa ila.[617] Mambo hayo ni:

1) Kujitenga na Ali.
2) Kukataa Sulhu.
3) Kuanzisha Uimamu kwa asiyekuwa Quraish.
4) Kuua bila ya haki.
5) Kuwakafirisha Waislamu (kuwaita makafiri).
6) Kujuzisha kufanya mapinduzi dhidi ya kiongozi jeuri (asiyehukumu kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna).

MJADALA WA RAI HIZI

Kujitenga na Ali. Ama kuhusu suala la kujitenga na Ali, tumeshalijadili na kubainisha nini hoja za Watu wa Nahrawaan: kwanini walimuunga mkono walipomuunga na kwanini walimuacha mkono walipomuacha. Kama tulivyoona kwamba ikiwa kujitenga na Ali ndio *Ukhawarij* wenyewe, basi Mu'awiya, Talha na Zubair pia walijitenga naye na kupigana naye vita. Bali Ibn Abbaas pia alijitengana naye. Haya tumeshayaeleza hatuna haja ya kuyarejea.

Kukataa Sulhu. Pia kuhusu kwanini watu hao walikataa sulhu, hilo pia tumeshalizungumza na kubainisha nini hoja yao katika Qur-ani.

---

617 - Rai na itikadi ambazo zimehusishwa na makundi yote yanayoitwa kuwa ni *Khawarij* ziko nyingi na tutazijadili *Inshaa Allah* katika juzuu nyengine za kitabu hiki; kwa hapa tunajadili mambo yaliohusishwa na watu wa Nahrawaan tu, yaani wale waliojitenga na Ali.

Kuanzisha Uimamu kwa asiyekuwa Quraish. Pia hoja za kwamba kauli ya haki ni kuwa Imamu au kiongozi wa Dola ya Kiislamu anakuwa mtu wa kabila na tabaka yoyote ile ilimradi awe na sifa za Uimamu au uongozi, tumezieleza kwa urefu katika kitabu chetu "*Mezani Ya Haki",* rejea huko utazame.[618]

Kwa hivyo, hapa tumebakiwa na kutoa ufafanuzi zaidi juu ya suala la kwamba watu hao walikuwa wakiua watu bila haki, japokuwa suala hili tayari tumeshalizungumzia na kulibainisha kwamba ni suala walilozushiwa Watu wa Nahrawaan. Pia kuna tukio maalumu na muhimu ambalo tunaweza kulihusisha hapa, nalo ni kuuliwa kwa Al-Imamu Ali: je aliuliwa na walioitwa *Khawarij* kama tunavyodanganywa au aliuliwa kwa njama za Mu'awiya? Tutalizungumzia hili mahala pake *in shaa Allah*. Ama suala la kujuzisha kufanya mapinduzi dhidi ya kiongozi jeuri (asiyehukumu kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna), hili tutazungumzia katika juzuu ya tatu ya kitabu hiki *in shaa Allah*.

KUUA BILA YA HAKI

Hii ndio ngoma maarufu inayopigwa na waandishi wa makala na historia na watu – bila kujua ukweli wake – wakaicheza na kuisherehekea. Tumeona katika sehemu zilizotangulia kwamba mfano mkubwa na mashuhuri unaotolewa ni tukio la kuuliwa kwa Sahaba Abdillahi bin Khabbab. Lakini kama tulivyoona kwamba suala hilo la kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbab na kuua watu bila ya haki, si sahihi kuhusushwa kwake na Watu wa Nahrawaan. Lakini suali ni kuwa: tukiijaalia habari hio ya Watu wa Nahrawaan kumuua Abdillahi bin Khabbab kuwa ni kweli, je hilo linawafanya watu hao kuwa ndio wametoka katika dini? Au tukijaalia kuwa jambo hilo ni la kweli, je jambo hilo limewafanya wao kuwa ndio *Khawarij* na kwamba ndio tayari limeshaupaka matope uongozi wao? Je wengine hawakufanya kama na kuliko hayo?

618 - Tazama *Mezani Ya Haki* sura ya tano, kuanzia uk. 116-171.

Tukirudi kuyatazama matukio ya historia, tunakuta kwamba **MU'AWIYA NA DOLA YAKE:** walifanya mauaji na dhulma ambazo mbingu na ardhi zinakaribia kupasuka, lakini husikii watu kumsema Mu'awiya kwa ubaya bali wanamsifu na kumtetea na kumuombea dua! Mifano ifuatayo inatosha kukupa picha ya wazi ya namna gani vikundi vyengine vilifanya:

1) Alikuwa Abdul-Rahman bin 'Udais Al-Balawi ni miongoni mwa wale ambao Mu'awiya kawaweka rumande, akawafunga Palestina wakakimbia, basi askari wa farasi (wa Mu'awiya) akamkuta (Abdul-Rahman) Ibn 'Udais akataka kumuua. Akasema Ibn 'Udais kumwambia yule askari: 'Wele wako, mche Mungu kutokana na damu yangu hakika ya mimi ni katika watu waliombaii (walioahidiana na Mtume (s.a.w.)) chini ya mti', akamwambia: 'Miti kwenye milima iko mingi', akamuua.[619]
2) Baada ya Amru bin Al-'Aas kuingia Misri, Mu'awiya bin Hudaij Al-Sakuni alimuua Muhammad bin Abi Bkar (Al-Siddiq), kisha akamtupa katika mwili wa punda (mfu) kisha akamchoma moto, (habari) ilipomfikia Aisha alifadhaika mfadhaiko mkubwa na akawa anamuombezea (anamlani) Mu'awiya na Amru (bin Al-'Aasi) baada ya kila sala.[620]
3) Mu'awiya alimtuma Al-Dhahhak bin Qais na akamuamuru apite (sehemu ya) Waaqisa ya chini na amvamie kila atayempitia ambaye anamtii Ali (bin Abi Talib) miongoni mwa Mabedui….basi Al-Dhahhak akafika Tadmur akaua miongoni mwao watu kumi na tisa.[621]
4) Mu'awiya bin Abi Sufyaan – baada ya kumfika (habari ya) hukumu ya waamuzi wawili[622] – alimtuma Busr bin Abi Artaa (na wenzake), wakaenda kutoka Sham mpaka wakaja Madina. Na Liwali (Gavana) wa Ali hapo alikuwa ni Abu Ayyub Al-Ansaari, basi akawakimbia….Busr akaingia Madina…Kisha akasema: 'Enyi watu wa Madina! Lau si wasia wa Mu'awiya kwangu, nisingeacha yeyote aliyefikia baleghe ila ningemuua…na Busr akabomoa majumba

619 - Tazama Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 4, uk. 335. Masahaba waliombaii Mtume (s.a.w.) chini ya mti ni wale waliotajwa kwa ujumla katika Sura ya 48, Aya ya 10 na Aya ya 18.
620 - Ibn Khayyat, *Al-Taarikh* uk. 116. Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 3, uk. 132. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 709. Tazama pia *Ali Bin Abi Talib Minal Milaad Ilaal Istish'haad* cha Dr. Ya'aqub Al-Rifaai, uk. 490.
621 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 3, uk. 150.
622 - Ambapo Ali aliuzuliwa, na Mu'awiya akathibitishwa katika Ukhalifa!

huko Madina, kisha akaenda Makka. Na Abu Musa kabla ya hapo aliandika (risala kuipeleka kwa watu wa) Al-Yaman (akiwaambia kwamba): "Hakika kuna jeshi limetumwa kutoka kwa Mu'awiya linaua watu: linamuua kila mwenye kukataa kuikubali hukumu". Kisha akatoka Busr kuelekea Al-Yaman na alikuwa (Liwali) wa Ali huko ni Ubaidi-Llahi bin Abbas, akakimbia kwenda Al-Kufa (Iraki), na akamfanya Ubaidi-Llahi bin Abdil-Mudaan Al-Harithi kuwa ni Khalifa wa Al-Yaman, basi Busr akamjia akamuua na akamuua mwanawe, na akakuta Busr familia ya Ubaidi-Llahi bin Abbas na kati yao walikuwemo watoto wake wawili, basi akawachinja. Na inasemekana kwamba (Busr) aliwakuta (watoto wawili hao) kwa mtu wa kabila la Banii Kinana katika watu wa ubeduini, alipotaka kuwaua, Bin Kinana akasema: "Kwanini unawaua (watoto) wawili hawa wala hawana kosa, ikiwa unawaua basi niue na mimi". Akasema (Busr): "Nitafanya (hivyo)". Basi akamuanza Bin Kinana akamuua kisha akawaua wao…Na akaua Busr katika safari yake hio kundi kubwa la wafuasi wa (Al-Imamu) Ali (bin Abi Talib) huko Al-Yaman.[623]

5) (Mu'awiya alimtuma) Abdullahi bin Mas'ada Al-Fazari pamoja na watu 1,700 kwenda Taymaa, na akamuamuru kuchukua zaka kutoka kwa mabedui ataowapitia na amuue atayekataa kumpa zaka ya mali yake kisha aje Makka na Madina na Hijaz na afanye hivyo hivyo".[624] *Mwisho wa kunukuu.*

Hizo ni nakala tano nilizozinukuu kutoka kwa Sh. Al-Sabi'i,[625] na tunaongeza yafuatayo:

6) Katika mwaka wa 41 A.H., Mu'awiya alimpeleka Busr bin Artaa, na akadai kwamba katumwa na Mu'awiya awaue Banii Ziad.[626]
7) Mu'awiya alimtuma Dhahhak bin Qais akaenda akaivamia miji ya Iraki na akamuua mtu katika wafuasi wa Ali.[627]
8) Mu'awiya alimtuma Sufyaan bin 'Awf Al-Ghamidi aivamie Iraki ya chini na kumuua atayeweza katika wafuasi wa Ali….[628] Akamuua

623 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 3, uk. 153. Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 3, uk. 1385.
624 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 3, uk. 150.
625 - Nakala hizi nimezinukuu kutoka katika *Al-Khawarij Wa Al-Haqitul Ghaiba* cha Sh. Nassir Al-Sabi'i, uk. 122-123, na hayo ndio marejeo aliyotupa.
626 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 76.
627 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 37-38.
628 - Ibn A'atham,, *Al-Futuh* j. 4, uk. 47.

Ashras bin Hassan Al-Bakri na kuua kundi kubwa la wafuasi wake.[629]

9) Mu'awiya alimtuma Busr bin Abi Artaa kwenda Al-Yaman, kupitia Madina na Makka, na kumuamuru kwamba asipite mji wowote ambao watu wake wanamtii Ali ila awalinganie kumtii yeye (Mu'awiya) na atayekataa atumie upanga.[630] … Naye alipoingia Madina alizichoma nyumba za Masahaba wa Kiansar na akataka kumuua Sahaba Jabir bin Abdillahi….[631] Kisha akaenda Makka akafanya vitisho na kumua Qutham bin Ubaidillahi bin Abdil-Muttalib na ndugu yake…[632] Kisha akaenda katika mji wa Qibala[633] uliokuwa na wafuasi wa Ali akawaua wote….[634] Kisha akaenda katika mji wa Najran akamuua Sahaba na mwanawe…[635] Kisha akaenda katika miji ya kabila la Hamdhan, na mji wa Jayshaan na San'aa na Hadharamaut, akaua humo kila aliyemkuta ambaye anamtii Ali bin Abi Talib,[636] inasemekana kwamba katika msafara wake huo aliua watu wasiopungua elfu thalathini na …[637]

10) Ubaidillah bin Ziyad alimkata Al-Baljaa[638] miguu na mikono kisha akamtupa sokoni![639] Al-Baljaa huyu ni mwanamke aliyesifika kwa ucha Mungu na juhudi katika ibada.

---

629 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 4, uk. 48-49.

630 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 56.

631 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 57.

632 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 59. Lakini katika riwaya ya Ibn 'Asaakir katika *Taarikh Dimashq* j. 10, uk. 133, na riwaya ya Al-Tabari katika *Taarikh* j. 6, uk. 60, mauaji hayo ya Qutham bin Ubaidillahi bin Abbas na ndugu yake (Abdul-Rahman bin Ubaidillahi bin Abbas) yalifanyika Al-Yaman. Na dhahir ni kuwa hii ndio kauli sahihi, kwani Al-Hafidh Ibn Hajar, naye ni miongoni mwa marejeo makuu katika elimu ya Hadithi na wapokezi, kainukuu riwaya hio kutoka katika *Al-Taarikh Al-Saghir* cha Al-Bukhari na wala hakusema kwamba ni dhaifu. Tazama Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1, uk. 381, *tarjama* na. 801.

633 - Katika *Mu'ujamu Al-Buldan* cha Yaqut Al-Rumi sikuona mji wenye jina hili bali nimeona katika j. 7, uk. 16, mji wenye jina "Qibal". Sasa sijui kama ndio huo huo unaitwa hivi na hivi au ni kosa la chapa au ni miji miwili tafauti.

634 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 62.

635 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 4, uk. 62-63.

636 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 4, uk. 63-65.

637 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 69. Rejea pia kaika Ibn 'Asaakir ,*Al-Taarikh* j. 10, uk. 127-135, *tarjama* na. 1090.

638 - Katika riwaya ya Al-Baladhiri – kwa kopi nilionayo – mwanamke huyo jina lake ni Al-Thabjaa. Sijui nani katika hawa kamtaja kwa jina lake sahihi. Tazama Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 5, uk. 189.

11) Ubaidillah bin Ziyad alituma jeshi la watu elfu nne likamrudishe Abu Bilal, Mirdas (r.a.) na kikundi chake cha watu arubaini waliokuwa wakihama kukimbia fitna zake, jeshi hilo lilichapwa vibaya sana na kikundi hicho kidogo…..basi ikafika wakati wa sala ya Ijumaa wakakubaliana wasimamishe vita ili kusali Ijumaa, basi wakati Abu Bilal, Mirdas na kundi lake wamo katika kurukuu na kusujudu, jeshi la Ubaidillahi bin Ziyad liliwavamia Abu Bilal na wenzake na wakawaua wote![640]

12) Jeshi la Yazid bin Mu'awiya lilipoingia Madina katika vita vya Al-Harra na kushinda vita hivyo, walikaa hapo siku tatu: "Wanaua watu na kuchukua vitu na mali, basi wakawafadhaisha Masahaba kwa kufanya hivyo ".[641] "Na Muslim (amirijeshi wa Yazid bin Mu'awiya) akawataka watu wambaii Yazid kwa sharti kwamba wao ni watumwa wake: ahukumu katika damu zao na mali zao na amtakaye katika watu wao, na aliyekataa hayo akamuua.[642]….na wakaletwa hapo watu wawili ambao wameshapewa amani wakaambiwa wambaii Yazid kwa masharti hayo. Wakasema: "Tunambaii kwa sharti (ya kuwa afuate) Qur-ani na Sunna (za Mtume (s.a.w.)), basi akawakata shingo zao".[643] …na akamuua Yazid bin Wahb kwa sababu hio hio na akamuua Ma'qil bin Sinan,[644] naye ni Sahaba.[645]

---

639 - Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 627.

640 - Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 627-630. Je hili linakubalika kiislamu? Mwanzo Abdullah bin Ziada alituma jeshi la watu elfu mbili kuwashika watu hao arubaini, lakini jeshi hilo lilichapwa vibaya sana. Ubaidillah bin Ziyad akaghadhibika akaongeza jeshi likawa ni jeshi la watu elfu nne, nao pia hawakuliwezi jeshi la watu arubaini, ndio hatimae wakatumia mbinu hio isiyokubalika katika Uislamu. Tazama maelezo hayo katika Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 2, uk. 627-630. Abu Bilal, Mirdas huyu ni mmoja wa watu wa Nahrawaan waliosalimika. Anasimulia Al-Mubarrad kwamba Abu Bila kabla ya kutoka alinyanyua mikono yake akaomba dua akasema: "E Mwenyezi Mungu ikiwa hivi tulivyo sisi ndio haki, basi tuoneshe ishara, basi nyumba ilitetemeka, na wengine wanasema paa la nyumba lilifunuka". Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 2, uk. 631. Na njiani ndio hivyo waliweza kulipiga jeshi la watu elfu nne nao ni watu arubaini tu, *Allah amuwiye radhi Abu Bilal na waliokuwa pamoja naye. Ammin.* Tazama pia Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 5, uk. 191-193. Tazama pia maneno ya Abu Bilal yalionukuuliwa na Al-Imamu Munir bin Al-Niyar Al-Ja'alani (r.a.) katika *Al-Siyar* j. 1, uk. 236, uone alikuwa Abu Bilal (r.a.) anasema nini anapotoka jihadi.

641 - Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 3, uk. 216. Hakuna shaka yoyote ile kwamba hawa ndio Makhawarij wenyewe. Na wapi umesikia kwamba mali ya mtu wa *tauhid* ni halali? Hata ikiwa damu yake ni halali, bado mali yake si halali.

642 - Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 3, uk. 217.

643 - Ibn Al-Athir, ,*Al-Kamil* j. 3, uk. 217. Watu wamekatwa shingo kwa sababu wao wametaka Yazid afuate Qur-ani na Sunna. Haya! Enyi walimwengu wenzangu! Hebu

Hayo ni baadhi tu ya mauaji yaliofanyika chini ya utawala na amri ya Mu'awiya pamoja na warithi wake. Na mwaka wa sitini A.H., Mu'awiya akaondoka duniani na wakashika utawala kizazi chake, nao wakafanya maovu na maasi na mauaji yasio na kifani. Yazid bin Mu'awiya, alikuwa muuaji kama baba yake. Ibn Zubair alikuwa akimwita mlevi na fasiki.[646] Na Yazid huyu alituma jeshi kwenda kupigana na Ibn Zubair huko Makka akianzia Madina, na akamuusia Amiri-Jeshi wake kwamba awaue majeruhi na watakaokimbia awatafute na kuwaua.[647] Na hili ni kinyume na Sunna ya Mtume (s.a.w.). Basi aliwaua Masahaba wengi wa Mtume (s.a.w.) miongoni mwa Muhajirina na Ansar.[648] Na inasemekana kwamba baada ya vita hivi vya Madina – vijulikanavyo katika historia kuwa ni vita vya ***Al-Harra*** – ambapo Banii Umayya waliingia huko kwa dhulma – waliwaingilia wanawake bikira wengi na wakachukua mimba.[649] Na jumla ya waliouliwa miongoni mwa Maquraish[650] na Ansar ni watu mia tatu na sita na miongoni mwa *Mawali* na wengineo ni nyongeza juu ya nyongeza ya hao".[651] Na wengine wanasema: "Waliouliwa miongoni mwa wakuu wa Kiquraish (tu) ni mia saba; mbali na Ansar".[652] Na wengine wanasema: "Waliuliwa siku ya vita vya Al-Harra watu elfu sita na mia tano".[653] Anasema Al-Mas'udi: "Na alikuwa (Yazid bin Mu'awiya) akidhihirisha maasi, na makosa yake anayafanya kuwa ni mambo mazuri yenye kupendeza, na akiyachukulia mambo ya

---

niambieni kwa uadilifu, ni nani hasa anayestahiki kuitwa Khawarij aliyetoka katika dini?! Ahlu Nahrawaan katika historia yao yote walikuwa wakihimiza kufuatwa Qur-ani na Sunna; wakati hawa Banuu Umayya ugomvi wao ni kuwatajia kufuata Qur-ani na Sunna! Lakini baada ya yote hayo, wao walikuwa wakijiita *Ahlu Al-Sunna Wa Al-Jamaa* na kuwaita wapinzani wao kuwa ni *Ahlu Al-Bidaa!*

644 - Ibn Al-Athir ,*Al-Kamil* j. 3, uk. 217.

645 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 3, uk. 214. Ibn Hajar, *Al-Isaba* j. 6, uk. 182, *tarjama* na. 8142.

646 - Al-Mas'udi ,*Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 279.

647 - Al-Mas'udi, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 279.

648 - Al-Mas'udi,, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 279.

649 - Al-Ya'aqubi *Al-Taarikh* j. 2, uk. 250.

650 - Dhahir ni kuwa anakusudia kwa kusema "Maquraish" Masahaba Muhajirin (r.a.).

651 - Ibn Abdi Rabbih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 364.

652 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 5, uk. 351.

653 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 5, uk. 351. Kumbukumbu yangu ni kuwa pia kuna riwaya inayosema kuwa waliokufa ni watu elfu kumi. *Wallahu A'alam.*

dini yake kuwa ni rahisi kwa maslahi ya dunia yake."[654] Na miongoni mwa mambo makuu alioyafanya ni kumuua Al-Husain bin Ali, mjukuu wa Mtume (s.a.w.)[655] kifo kibaya sana na wakamkata kichwa na ikawa wanamkejeli.[656] Anasema Al-Ya'aqubi: "Alikuwa Sa'id bin Al-Musayyib anaiita miaka ya Yazid bin Mu'awiya kuwa (ni miaka ya) nuhusi: katika mwaka wa mwanzo aliuliwa Al-Husain bin Ali na watu wa Nyumba ya Mtume (s.a.w.), (*Ahlu Al-Bait);* mwaka wa pili ikavunjiwa heshima sehemu tukufu ya Mtume (s.a.w.) na kuvunjiwa heshima ya utukufu wa Madina; mwaka wa tatu ikamwagwa damu katika eneo Takatifu (la Makka) na kuunguzwa Al-Ka'aba"![657]

Na hivyo, ndivyo walivyokuwa kizazi chote cha Banii Umayya, hakusalimika na uovu isipokuwa Al-Imamu Al-'Adil, Umar bin Abdil-Aziz (r.a.). Na kama hawakufanya Banii Umayya uovu wowote ila kumfanya Hajjaj bin Yusuf kuwa ndiye Liwali wao huko Basra basi lingetosha hilo kuwatia kasoro. Hajjaj alikuwa muuaji ambaye hajatokea mfano wake katika historia ya Uislamu. Na lau kama hakumuua ila Said bin Jubair, Imamu mkubwa wa Umma huu, basi lingetosha hilo kuwachafulia historia yao hapa duniani na kuwaweka pabaya huko akhera.[658] Na alikuwa Umar bin Abdil-Aziz anasema: "Lau ulikuja kila Umma na muovu wao, nasi tukaja na Hajjaj, basi tungeliwashinda".[659]

Na miongoni mwa watu muhimu katika Dola ya Banii Umayya, ni Samura bin Jundub.[660] Samura bin JundubJundub alikuwa ni miongoni mwa Masahaba wa Mtume (s.a.w.). Lakini alijiunga na kambi ya Mu'awiya akafanya mauaji na udhalimu ambao hausemeki, hadi naye

654 - Al-Mas'udi, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 279.
655 - Al-Mas'udi, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 278.
656 - Al-Ya'aqubi, *Al-Taarikh* j. 2, uk. 245.
657 - Al-Ya'aqubi, *Al-Taarikh* j. 2, uk. 253.
658 - Wala usinipinge kwa kusema: "Vipi uwaingize wote kwa kosa alilolifanya Hajjaj baada ya kauli ya Allah: **وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَى (Wala (nafsi) haibebi mzigo wa (nafsi) nyengine),** kwani ninasema: "Wanaoingia ni wale waliomtawalisha Hajjaj na wote wale ambao waliyaridhia matendo yake pamoja na kuiridhia dola hio ".
659 - Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 2, uk. 184-185, *tarjama* na. 388.
660 - Na pia huitwa "Jundub".

akafa kifo kibaya kilioje![661] Anasimulia Al-Tabari, kutoka kwa Sulaiman bin Muslim kutoka kwa baba yake, akisema kwamba:

> Nilipita Msikitini akaja mtu akatoa zaka ya mali yake, kisha akaingia (msikitini) akaanza kusali. Akaja mtu akampiga shingo yake (kwa upanga), ikawa kichwa chake kiko msikitini na kiwiliwili kiko upande mwengine…..Nimelishuhudia hilo. Basi Samura hakufa ila alishikwa na baridi kali akafa kifo kibaya sana. Na nimemshuhudia na waliletwa watu wengi na watu (wengine) wako mbele yake, basi humuuliza mtu: 'Nini dini yako'. Basi hujibu: 'Nashuhudia kwamba hakuna Mola isipokuwa Allah peke yake: hana mshirika; na Muhammad ni Mjumbe wake nami najitenga na Harauriyya,[662] basi humchukua akamkata shingo yake hata wakazidi (watu) ishirini na...[663]

Hio ni riwaya moja, na riwaya nyengine:

> Kutoka kwa Abu Sawwar Al-'Adawi kwamba: "Samura aliwaua katika kaumu yangu asubuhi moja watu arubaini na saba ambao walikuwa wamehifadhi Qur-ani.[664]

Na riwaya nyengine inasema:

> ....Nilimuuliza Anas bin Siyrin:[665] 'Je Samura aliwahi kumuua mtu yeyote?' Akasema: 'Kwani aliowaua Samura wanahesabika? Ziyad alimfanya kuwa ni Khalifa wake wa Basra akaja Al-Kufa, basi alikuja akaua watu elfu nane. Akamwambia: 'Huhofii kuwa umemuua asiye na hatia? Akasema: 'Lau niliwaua pamoja nao mfano wao (mara mbili) basi nisingelihofu...au kama alivyosema (maneno yenye maana hio).[666]

---

661 - Alipigwa na baridi kali ilioje! Akawa anaweka maji ya moto ili kujitibu akaanguka humo akafa humo humo. Tazama Al-Dhahabi *Al-Siyar* j. 4, uk. 333, *tarjama* na. 257.

662 - Wengine huwaita Haruriyya.

663 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 147-148.

664 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 114.

665 - Katika Taarikh ya Al-Tabari – chapa nilio nayo – kaandikwa "Sayrin" na jina maarufu ni Siyrin, na kwa hivyo katika kitabu *Asmaau Man Yu'urafu Bi-Kun-yatih* cha Abu Al-Fa-hi Al-Azdi *tarjama* na.64, katajwa kwa jina la "Anas bin Siyrin".

666 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 114.

Anasema Al-Dhahabi: "Na Samura aliua watu wengi".[667]……."Waliuliwa huko watu elfu sabiini. Nikamuuliza Yunus, akasema: 'ndio, baina ya waliouliwa na waliokatwa'[668], ikaulizwa: 'nani aliyefanya hivyo?' Akasema: 'Ziyaad, na mwanawe na Samura'. [669]

Hio ni Dola ya Banii Umayya na hayo ndio baadhi tu ya waliyoyatenda. Kisha baada ya Dola ya Banii Umayya ikaja Dola ya Abbasiyyin (Banuu Abbas), ikafanya mauaji na maovu hadi ikawa inawafukuwa maiti wa Banii Umayya na kuwachoma moto![670]

Hayo ni sehemu ndogo sana[671] ya maovu na mauaji yaliofanywa na Mu'awiya na Dola yake pamoja na Abbasiyyin. Sasa je hawa wao si *Khawarij*? Watu wa Nahrawaan wameenezewa kuwa ni waovu katika vitabu vyote vya historia na kwamba wao ni *Khawarij* waliotoka katika dini. Ukiuliza kwanini watu hao ni *Khawarij* na vipi wamekuwa waliotoka katika dini? Utaambiwa wamemuacha mkono Ali na wamemuua Abdillahi bin Khabbab, na yote – kama tulivyoona – ni maneno yasiyo na msingi: kumuacha kwao mkono Ali ni kwa hoja za Kisharia za Qur-ani na Sunna kama tulivyobainisha, na suala la kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbab hawakuhusika nalo, bali walilichukia kama tulivyobainisha. Hawa Banii Umayya walikuwa wauwaji, walevi, wabadilishaji wa Sunna ya Mtume (s.a.w.), na watunzi wa Hadithi za uwongo ndio Waislamu *Ahlu Sunna*! Basi huo ndio Uislamu wao na huko ndiko kufuata Sunna kwao, na waliokwenda kinyume na wao ndio *Khawarij* wenyewe walitoka katika dini! *Wallahu Al-musta'aan!*

667 - Al-Dhahabi *Al-Siyar* j. 4, uk. 332, *tarjama* na. 257.

668 - Dhahir ni waliokatwa mikono au miguu au yote kwa pamoja.

669 - Al-Dhahabi *Al-Siyar* j. 4, uk. 333, *tarjama* na. 257.

670 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 3, uk. 256.

671 - Kuzungumzia maovu na mauaji ya Banii Umayya na Abbasiyyin kiukamilifu kunahitaji kitabu chenye juzuu nyingi, kwa hapa tunatoa mifano miwili mitatu kiasi cha kubainisha ukweli tu.

WALIOKUJA BAADAE: HARAKATI ZA SHEIKH MUHAMMAD ABDIL-WAHHAB NA WAFUASI WAKE

Hayo tulioyazungumzia ni mambo yaliofanywa na Mu'awiya na dola yake.[672] Nyakati zilipopita, duniani kukawa kunazidi kutokea harakati za kisiasa na za kidini. Mapinduzi au majaribio ya mapinduzi yakafanyika katika sehemu tafauti za ulimwengu wa Kiislamu, na mauaji kwa misingi ya kimadhehebu na kikabila yakafanyika kwa wingi katika sehemu tafauti, kiasi cha kwamba lau tutajaribu kuyakusanya matukio hayo itatubidi tufanye kitabu maalumu. Kwa hapa – na ili kujirahisishia kazi mimi mwenyewe – nakukumbusha baadhi ya yale nilioyazungumzia katika barua yangu kwa Sheikh X, ya jinsi gani wale wanaojiita *Salafiyya* na ambao watu wanawaita Mawahabi walivyofanya katika kuua Waislamu wasio na hatia yoyote. Tunanukuu kutoka katika kitabu chao wenyewe mambo yafuatayo. Anasema muandishi:

1) Kisha Sheikh (Sheikh ni Muhammad Abdul-Wahhab) akaamrisha jihadi na kuwahimiza (watu) juu ya hilo... wakawavamia nadhani (walikuwa) mabedui (basi) wakateka ngawira na wakarejea kwa Salama![673]

2) Kisha akaenda Abdul-Aziz na jeshi lenye kupata ushindi mpaka (mji unaoitwa) Al-Ahsaa…..akawaua wanaume wengi kiasi cha watu sabiini, na akachukua mali nyingi! Kisha akauvamia (mjia wa) Al-Mubarraz[674] akawaua wanaume katika watu wake (watu

672 - Tumesema kwamba migawanyiko ya kisiasa ya mwanzo ilitokana na wafuasi wa Ali, ambao ndio baadae waliunda harakati za Kishia; wafuasi wa Mu'awiya, ambao ndio chimbuko la fikra ya Kisuni; na Watu wa Nahrawaan ambao ndio chimbuko la fikra ya Kiibadhi. Cha muhimu kukifahamu ni kuwa wote hawa walikuwa wanatafautiana katika fikra za kisiasa tu: ama dini na ibada zote wakati huo zilikuwa hazina tafauti: tafauti zilitokea baadae kwa sababu mbaya na nzuri. Mbaya ni sababu za utunzi wa Hadithi za uwongo; na nzuri ni sababu za ijtihadi za wanavyuoni.

673 - Uthman bin Bishr Al-Najdi, *Unuwaan Al-Majd Fii Ta'arikh Najd* uk. 15, kilichochapishwa na *Maktaba Al-Riyaadh Al-Hadithiyya* huko Riyaadh, Su'udia. Nimetoa marejeo hapa kwa namna hii, kwani nasikia kwamba kitabu hicho sasa wamekichapisha tena lakini mambo yote yale walioyafanya kuhusu mauaji wameyatoa!

674 - Mji huu haukuandikwa kwa irabu, inawezekana ikawa jina lake ni hivyo na inawezekana ikawa ni: Al-Mubarriz, Al-Mubriz au Al-Mubraz; majina yote haya

wa mji huo).[675]

3) Basi akaziteketeza mali zao zote na akawaua kiasi cha watu thalathini![676]

4) Basi akawavamia watu (wa mji wa) Al-Dhabia kijiji maarufu katika (mji wa) Al-Kharaj na wakachukua baadhi ya wanyama wao na wakaua katika watu (wa mji huo) watu kumi na mbili na wakaikata mitende ya mji huo na baadhi ya konde zao.[677]

5) Basi akawaendea wakati wa asubuhi na akaua watu miongoni mwa viongozi wao na jeshi lao la farasi na akachukua ngamia wao na mbuzi na kondoo wao![678]

6) Akawavizia Su'ud ukaja msafara na walikuwa na kiu na wakenda kwenye maji hali ya kuwa (wengine) wamepanda na (wengine) wanakwenda kwa miguu. Basi Su'ud akawavamia akawaua.[679]

7) Na Su'ud akakombakomba ngamia na mbuzi na kondoo na vyombo ambavyo havina idadi wala havihisabiki na kuwaua (watu) wengi.[680]

8) Na vikatokea baina yao vita vikali basi wakashindwa wale Mabedui na wakauliwa miongoni mwao wengi miongoni mwa jeshi lao la farasi na viongozi wao…….na akachukua …….ngawira nyingi miongoni mwa (ngawira hizo walikuwemo) ngamia, na mbuzi na kondoo na fanicha na vitu (vyengine) na wakakaa katika kuwafuatilia kiasi cha siku mbili au tatu wanachukua mali na kuwaua wanaume na Su'ud akachukua

---

kilugha yanawezekana. Lakini kujua ni jina lipi hasa linaitwa mji huo ni lazima uwasikie wenyewe.

675 - Uthman bin Bashir Al Najdi,*Unuwaan Al Majd Fii Ta`arikh Najd* uk. 46.

676 - k.h.j uk. 47.

677 - k.h.j uk. 63.

678 - k.h.j uk. 77.

679 - k.h.j uk. 79.

680 -k.h.j uk. 85.

ngawira zote: ngamia kiasi cha elfu kumi na moja (11,000) na zaidi na kondoo na mbuzi zaidi ya laki moja –(100,000.).[681]

9) Na akawaua katika wao idadi kubwa ya wanaume zaidi ya mia nne (400) na akachukua mali nyingi![682]

10) Na akaelekea Qatar (hii ilio) maarufu (iliopo) baina ya Oman na Bahrein basi wakapigana nao, na Sulaiman (kiongozi wa jeshi la Abdul-Aziz) akawashinda akawaua isipokuwa wachache tu na akachukua vipandwa vyao (ngamia).[683]

11) Basi Su'ud akawavamia na akawachukua kikundi (akawateka nyara idadi kubwa) na akakombakomba (akasomba) kutoka kwao mali nyingi ngamia zaidi ya elfu nane (8,000) na akachukua kondoo na mbuzi wao wote na makazi yao na vyombo vyao na zaidi ya farasi ishirini na akawaua idadi (kubwa) ya wanaume.[684]

12) Basi akawavamia kutoka hapo Mabedui katika (kabila la) Sabii na wengineo na akawachukulia ngamia wengi basi Su'ud alipozikuta athari zao akawafuata……(wakawa) wanaua na kuchukua ngawira wakayaangamiza makundi hayo kwa kuyaua na kuyanyanganya……..na wakaangamia Banu Khalid katika tukio hili kwa kuuliwa na kwa kiu makundi mengi inasemekana ni zaidi ya watu elfu moja na inasemekana kuhusu waliokufa ni karibu ya watu elfu mbili na akachukua ngamia wao wote na farasi wao wote na hakiba zao na vyombo vyao na magodoro yao na kila walicho nacho inasemekana farasi ni zaidi ya mia mbili (200) basi Su'ud akahodhi ngawira zote hizo.[685]

13) Na akaelekea upande wa Al-Ahsaa walipopanda vipandwa vyao (ngamia) na wakapiga risasi zao kwa pamoja basi zilitia kiza angani na kutetemesha ardhi na moshi ukafanya kiwingu katika

---

681 - k.h.j uk. 87.
682 - k.h.j uk. 88.
683 - k.h.j uk. 88-89.
684 - k.h.j uk. 89.
685 - k.h.j uk. 97-98.

anga na wanawake wengi waliokuwa na mimba waliharibu (mimba zao) katika mji wa Al-Ahsaa.…na akawaamuru (watu wa Al-Ahsaa) watoke waende kwake wakatoka basi akakaa katika makazi hayo muda wa miezi (kadha) anamuua anayemtaka kumuua na anamtoa (katika mji) anayetaka kumtoa na anamfunga anayetaka kumfunga na anachukua mali na anabomoa makazi na anabomoa majumba na alikithirisha Su'ud mauaji kwao![686]

14) Basi wengine wakauliwa katika mji na wegine wakawatoa kuwapeleka kwenye mahema na kukatwa shingo zao katika hema la Su'ud mpaka akawamaliza ila wachache na Su'ud akakombakomba katika vita hivyo mali ambazo hazina idadi wala hazihisabiki![687]

Hayo ni baadhi ya yaliyofanywa na watu wa madhebu nyengine[688] na hadi leo yanaendelea kufanywa. Iraki Shia na Sunni wanauana. Tumeshuhudia katika T.V. huko Iraki watu wa madhehebu moja wanawachoma moto watu wa madhehebu nyengine wakiwa hai na wengine wamewaua kisha wanawaburura njiani, kama vile ambavyo Maimamu wengi wa Misikiti wameuliwa katika nchi hio. **Suali tunalojiuliza hapa:** ni kuwa ikiwa tutazingatia kosa la kitendo cha mauaji kuwa ndio *Ukhawarij* wenyewe, je ni nani anayestahiki zaidi kuitwa *Khawarij*: ni hawa au ni Watu wa Nahrawaan?

686 - k.h.j uk. 105-106.

687 - k.h.j uk. 106. Asili ya nakala hizi nimezinukuu kutoka katika kitabu *Wasaqata Al-Qina'u* cha Al-Imamu Badru Al-Din Sh. Al-Khalili alichokitoa ili kumjibu Dr. Al-Tahhaan. Na nimekirejea kitabu hicho *'Unuwaan Al-Majd Fii Ta'arikh Najd* chenye maelezo hayo. Na nikaona kwamba hakuna tafauti hata ya herufi moja katika yaliyomo humo na aliyotunukulia Sheikh Al-Khalili katika *Wasaqata Al-Qina'u.* Hata hivyo, kumekuwa na funu – *Wallahu A'alam* – kwamba kitabu hicho Mawahabi wamekitoa upya na wamezitoa sehemu hizo ambazo zinawapiga wenyewe. Lakini nakala za asili tunazo na hayo yote yamo.

688 - Kwa hapa ni wale wajiitao *Al-Salafiyya* au *Ansar Al-Sunna.*

KUWAITA WAISLAMU MAKAFIRI

Kuwaita Waislamu makafiri au kuwakafirisha Waislamu ni jambo jengine ambalo kwalo wametiwa aibu walioitwa *Khawarij*. Na bila shaka hii ni dhimma kubwa kwa mtazamo wa Sharia Tukufu ya Kiislamau. Anasema Mtume (s.a.w.): "**Kumtukana Muislamu ni ufasiki na kumpiga ni ukafiri."**[689] Na akasema: **"Atayemwita mwenzake: 'Ewe kafiri; (naye) akamwambia wewe ndio kafiri, basi mmoja wao amestahikiwa na ukafiri, na aliyeanza ndiye dhalimu zaidi".**[690]

Ukweli ni kuwa vilikuweko vikundi[691] vilivyoitwa kuwa ni *Khawarij* – vilivyokuja baada ya kuwa Watu wa Nahrawaan hawapo tena – ambavyo vilikuwa vikiwaita baadhi ya Waislamu kuwa ni makafiri, lakini hivi havihisabiwi kuwa ni katika Watu wa Nahrawaan wala kuwa ni warithi wa sira ya Watu wa Nahrawaan, bali wao wameafikiana na Watu wa Nahrawaan katika kitu kimoja tu, nacho ni kutokukubaliana na sulhu baina ya Ali na Mu'awiya: si katika Fiq-hi ya siasa na itikadi. Ama Watu wa Nahrawaan hawakuwa wakiwakafirisha Waislamu. Waandishi wanaonadai kuwa watu hao "Walijitenga na Ali na kumkafirisha",[692] wametegemea riwaya zenye kuwanukuu watu hao wakisema kumwambia Ali na waliobakia pamoja naye kwamba: "Nyinyi na watu wa Sham mumeshindana (katika) kuukimbilia ukafiri".[693] Na riwaya inayomnukuu mtu mmoja akimwambia Ali: "Watu wanazungumza

---

689 - Al-Bukhari, *Al-Sahih* Hadithi na. 48-6044-7076, na katika kitabu chake chengine *Al-Taarikhu Al-Saghir* j. 1, uk. 263, na katika *Al-Adabu Al-Mufrad* Hadithi na. 436. Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 116-117.

690 - Al-Rabi'u, *Al-Jami'u Al-Sahih* uk. 45, Hadithi na. 65. Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 6103,6104. Muslim *Sahihu Muslim* Hadithi na. 212,213.

691 - Tutavizungumzia katika juzuu nyengine ya kitabu hiki *Inshaa Allah.*

692 - Haya yako katika vitabu vingi mmno. Kwa sasa unaweza kutazama Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7, uk. 297, *tarjama* na. 566, na Ibn Uthaimin, *Sharhu Riyadhu Al-Salihin* j. 4, uk. 308, katika sherehe ya Hadithi na. 1732,1733. Lakini Sheikh huyu anaonesha hakujilazimisha kusema ukweli. Haya ndio matatizo ya Umma huu; mtu akiwapinga watu huona bora awazulie jambo wasilolisema wala kuliitakidi ili awakimbize watu kutokana na fikra zao, hatima imekuwa ni kudanganywa kila siku. Nitayanukuu maneno yake yasiyo na ukweli na kuyabainisha katika juzuu zinazofuata *Inshaa Allah.*

693 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 12. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 122.

kwamba umerejea kutokana na ukafiri wako".[694] Na riwaya inayosema kwamba Watu wa Nahrawaan: "Wakawakafirisha walioiridhia sulhu".[695] Na riwaya inayowanukuu watu hao wakimwambia Ali: "Mpaka uishuhudie nafsi yako kwa ukafiri".[696] Na riwaya zilizo mfano wa hizo. Na makusudio ya ukafiri wenyewe ambao umetajwa katika riwaya hizi ni kile kitendo cha Ali cha kukubali sulhu na Mu'awiya. Lakini tatizo ni kuwa kama vile ambavyo kuna riwaya hizo zinazowanukuu Watu wa Nahrawaan wakisema hivyo, halkadhalika kuna riwaya nyengine zinazomnukuu Ali mwenyewe alipoambiwa na mmoja wa wafuasi wa Mu'awiya kwamba:

> ..Na tumeona ewe Aba Al-Hasan (Al-Imamu Ali) kwamba uondoke (hapa vitani *Siffin*) wewe na walio pamoja nawe, tukuachie Iraki yako na Hijaz yako na utuachie Sham yetu..[697]

Ali alijibu:

> Jambo hili limenitia majonzi sana na limenikesesha na nikalitafakari sana, lakini sikuona isipokuwa (kupigana) vita (na Mu'awiya) au (vyenginevyo) ***nikikufuru kile alichokiteremsha Allah"***.[698] Na katika riwaya nyengine akasema: "Jambo hili nimelitafakari sana, lakini sikuona isipokuwa (ama) vita au ***nikikufuru kile alichokuja nacho Muhammad (s.a.w)***..[699]

Kwa hivyo, kwa mujibu wa riwaya hizi, utaona kwamba kama vile ambavyo Watu wa Nahrawaan walikuwa wakiona kwamba kukubali sulhu ni ukafiri kwa maana kwamba ni kwenda kinyume na Qur-ani,

694 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 18.
695 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 134.
696 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 135,141.
697 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 286.
698 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 265. Na riwaya kama hii, kaisimulia Al-Baladhiri katika *Al-Ansab* j. 3, uk. 33, katika vita vya Al-Jamal.
699 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 287. Na hii inatosha kutoa jawabu kwa wale waliosema kuwa watu wa Nahrawaan walimkafirisha Ali kwa sababu ya kusimamisha kwake vita hivyo na kukubali sulhu. Kwa hivyo, tukijaalia kuwa hayo ni kweli, basi elewa kwamba – kwa mujibu wa riwaya hizi – Ali ndiye wa mwanzo aliyesema kuwa kusimamisha vita hivyo na kukubali sulhu ni kukikufuru Kitabu cha Allah na Sunna ya Mtume wake. Na mfano wa maneno hayo, Ali aliyasema katika vita vya Jamal. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 33.

vivyo hivyo ndivyo Ali alivyokuwa akiona. Na labda riwaya mbili hizo zinazomnukuu Ali akisema maneno hayo, ndizo tunazoweza kuzichukua na kwazo kuifasiri riwaya ya Al-Mubarrad iliyotumia neno "Kukiri ukafiri", aliposema akiwanukuu walioitwa *Al-Khawarij* wakisema kumwambia Ibn Abbaas kuhusu Ali: "Na-atubie baada ya kukiri kwake kukufuru."[700]

Lakini tukijaalia kwamba riwaya zenye kuwanukuu Watu wa Nahrawaan na zenye kumnukuu Ali, ni riwaya zilizothibiti, suali ni kuwa je ukafiri huu unaokusudiwa katika riwaya hizo ni ukafiri wa aina gani? Ukafiri unagawika sehemu mbili kubwa:

1) Ukafiri unaomtoa mtu katika Umma wa Kiislamu na kumfanya yeye kuwa si mfuasi wa Umma huu tena. Huu unawaingiza wote wale ambao hawafuati dini ya Kiislamu.

2) Ukafiri unaoitwa "Kufru Al-Ni'ima" (Kuikufuru neema ya Allah).[701] Huu ni ukafiri wa kutenda dhambi kubwa yoyote na kutokutubia. Ukafiri wa mwanzo hauhitaji elimu: kila mtu anaujua. Ama ushahidi wa ukafiri wa aina ya pili tunaupata ndani ya Hadithi kama: "Kumtukana Muislamu ni ufasiki na kumpiga ni ukafiri."[702] Na Hadithi: "Atayemwita mwenzake: 'Ewe kafiri; (naye) akamwambia wewe ndio kafiri, basi mmoja wao amestahikiwa na ukafiri, na aliyeanza ndiye dhalimu zaidi".[703] Hizo ni Hadithi ambazo tumezinukuu kabla. Ushahidi mwengine juu ya ukafiri wa namna hio ni Hadithi kama: "Musije mukarejea kuwa makafiri baada yangu,

---

700 - Al-Mubarrad ,*Al-Kamil* j. 2, uk. 578.

701 - Al-Imamu Al-Nawawi (Shafi), kama ilivyo katika *Yaliyomo* (Table of contents) ya kitabu chake *Shrhu Sahihi Muslim* j. 2, uk. 364 ambapo anasema: "Mlango (kuhusu): ubainifu wa kupungua imani kwa kupungua ta'a (kutii), na kubainisha utumiaji wa neno *Ukafiri* kwa ukafiri usio wa kumkufuru Allah, kama *Kufru al-nni'ima wa Al-huquq* (kuikufuru neema na haki (za watu)". Pia kauli hii imekuja katika kitabu *Majmu'a Al-Tawhid* chenye mafunzo ya Ibn Taymiyya na Muhammad bin Abdil-Wahaab uk. 10, ambapo imeandikwa hivi: "Na kufuru ndogo haimtoi (mtu) katika mila (Uislamu), nayo ni Kufru Al-Ni'ima (kuikufuru neema ya Allah)."

702 - Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 48-6044-7076, na katika kitabu chake chengine *Al-Taarikhu Al-Saghir* j. 1, uk. 263, na katika *Al-Adabu Al-Mufrad* Hadithi na. 436. Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 116-117.

703 - Tumeshaitolea marejeo kabla kidogo.

mukapigana shingo zenu wenyewe kwa wenyewe."[704] Na Hadithi: "Hakuna baina ya mtu na ukafiri ila kuacha kwake Sala."[705] Na Hadithi: "Musiwakatae baba zenu: atayemkataa baba yake basi kakufuru."[706] Na Hadithi: "Mambo mawili katika Umma wangu ni ukafiri: kuitukana nasaba na kumuombolezea maiti."[707] Na Hadithi: "Hakuna mtu atayedai kwa asiye baba yake (akadai kuwa ni baba yake) ila huwa amekufuru. Na atakayedai kwamba (yeye ni mtu anayetokana na) kaumu (fulani, wala) hana nasaba nao, basi na-ajiandaliye makazi yake motoni."[708] Na Hadithi "Atayedai baba katika

---

[704] - Kaipokea Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 4403-6166-6785-6868-7077. Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 220/65. Na pia wameipokea wapokezi wengine wengi. *Na bila shaka Masahaba hawakukusudiwa kwamba watarudia dini zao za kijahilia: za kuabudu masanamu.*

[705] - Kaipokea Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 242/82. *Jumhuri* ya wanavyuoni wameufasiri ukafiri wa mtu kuacha sala ikiwa anakubali kwamba Sala ni wajibu, kuwa ukafiri huo si ule ukafiri unaomtoa mtu katika Umma. Ama wanavyuoni wengine wakiwemo wanavyuoni wa sasa wa Su'udia kama Ibn Baz katika *Fatawa Ulamai Al-Haram* uk. 171-175, na Ibn Uthaimin katika kitabu hicho hicho uk. 158-161, na pia katika Sherehe yake ya *Riyadh Al-Salihin* j. 3, uk. 280, hawa wao wanaona kwamba kuwacha kusali ni ukafiri mkubwa ambao unamtoa mtu katika mila ya Kiislamu na hukumu yake ni *murtadi!* Bali Ibn Uthaimin katika Sherehe yake ya *Riyadh Al-Salihin* j. 3, uk. 280, anasema kwamba Yahudi na Nasara ni bora zaidi kuliko Muislamu asiyesali! Na lau si kuogopa kuathirika jamaa zake basi tungelisema aachwe juu ya ardhi aliwe na mbwa!

[706] - Kaipokea Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 6768. Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 215/62. Na pia wameipokea wapokezi wengine.

[707] - Kaipokea Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 224/67. Na pia wameipokea wengine.

[708] - Kaipokea Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 3508. Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 214/61. Na pia wameipokea wapokezi wengine. Hapa kuna tahadhari kubwa sana kwa wale watu ambao wamebadilisha nasaba zao na kabila zao. Kwanza inawapasa watu wajue kwamba kabila ni baba. Ukisema kwamba mimi ni Rawahi basi elewa kwamba unasema kwamba mimi natokana na au ni mtoto wa mtu anayeitwa "Rawaha bin 'Adnan". Ukisema mimi ni Hashimi basi jua kwamba unasema kuwa wewe ni mtoto wa au baba yako ni mtu anayeitwa "Hashim bin Abddi Manaf". Ukisema mimi ni Mauli basi huwa unasema kuwa mimi ni mtoto wa au baba yangu ni "Ma'awala bin Shams". Sasa ikiwa wewe siye basi huwa umemkana baba yako na umejinasibisha na kaumu ambayo wewe si katika wao, na kwa hivyo umeikufuru neema ya Allah na kuingia katika mambo mawili makuu yenye kuangamiza: kumkana baba na kujinasibisha na kaumu ambayo huna nasaba nayo. Kuna watu ambao wamejipachika Kabila za Kiarabu nao baba zao si Waarabu bali ni Wazungu, Wahindi, Washirazi, Waafrika n.k. Huu ni ukafiri wa neema ya Allah aliyemuumba mtu huyo kuwa ni Mzungu au Mshirazi au Muafrika au Muhindi. Nalo ni jarima kubwa sana mbele ya

Uislamu asiyekuwa baba yake, (naye) anajua kuwa si baba yake basi Pepo imemuharamikia".[709] Na Hadithi: "Nimeoneshwa moto! Basi kutahamaki watu wake wengi ni wanawake wanaokufuru. Ikasemwa (kuulizwa Mtume (s.a.w.)): 'Je wanamkufuru Mwenyezi Mungu? Akasema: 'Wanamkufuru mume na wanaikufuru ihsani, lau utamfanyia mmoja wao ihsani dahari (nzima) kisha akaona kitu (kisichompendeza kwako siku moja) basi husema: 'Sijapata kuona

---

Allah linaweza kumuweka mtu pabaya kwani ni kuipinga hukumu ya Allah aliyemuumba hivyo. Na kwa hivyo, Mtume (s.a.w.) hapa katoa tahadhari hii. Na kuna wengine walikuwa matajiri, basi wakawa wanakwenda kwa Waarabu wajinga wanawambia tuuzie kabila, na asili mia kubwa ya Waarabu waliokuja Zanzibar wakati huo walikuwa hawajui dini yao, basi wakawa wanawauzia. Kwa hivyo, ni wajibu wa kila anayejijua kwamba wazee wake wamefanya jarima hilo kurudi haraka katika kabila yake ya asili. Na tujue kwamba Allah hatazami Mwarabu wala Muhindi wala Muafrika, wala mweupe wala mweusi bali anatazama uchaji tu. Anasema Allah:

"يا أيها الناس إنا خلقناكم من ذكر و أنثى و جعلناكم شعوبا وقبائل لتعارفوا إن أكرمكم عند الله أتقكم إن الله عليم خبير." الحجرات 13

"Enyi watu hakika Yetu Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume (mmoja, Adam) na mwanamke (mmoja, Hawaa) na tukakujaaliyeni (kuwa) mataifa (mbali mbali) na makabila (mbali mbali) ili mupate kujuana, hakika ya mbora wenu kwa Mwenyezi Mungu ni mcha Mungu wenu (zaidi), hakika ya Allah ni Mjuzi, Mwenye habari (ya kila kitu)." Sura ya 49, Aya ya 13. Basi kuna haja gani tena kwa mtu kujinasibisha na watu ambao hana nasaba nao? Allah amehimiza kwamba watu waitwe kwa (majina na nasaba za) baba zao akasema katika Sura ya 33 Aya 5 **"Waiteni kwa baba zao."** Yaani majina yao na ya baba zao na babu zao na kabila na nasaba zao. Hii ni hadhari, nimeielezea kwa sababu watu wengi wanaona labda hili la kubadili kabila ni kitu chepesi mbele ya Allah, kumbe ni jambo kubwa ambalo Mtume (s.a.w.) anasema – katika riwaya zake nyengine kadha wa kadha – kwamba atakayelifanya basi "Pepo kwake ni haramu." Na labda sababu ya watu kudhania kuwa hilo ni jambo jepesi ni kuwa wengi wao hawajui kabila ni nini: wao hudhania kwamba kabila mtu hujichagulia tu, kumbe kabila ni baba na ni nasaba. **Tanbihi ya kwanza:** Mtu akisilimu basi anaruhusiwa kugeuza jina lake tu, ama baba na kabila haruhusiki kubadilisha na akifanya hivyo basi kaingia katika onyo kali lililomo katika Hadithi hizo, na kenda kinyume na Aya: **"Waiteni kwa baba zao."** Tazama kwamba Allah hakusema **"Waiteni kwa majina ya baba zao"** bali kasema: **"Waiteni kwa baba zao"** ili yaingie majina na kabila au ukoo wa baba; mtoto hunasibishwa na baba yake na kabila au ukoo wa baba yake. Hii ndio kauli sahihi yenye ushahidi wa Qur-ani na Hadithi, atayekwambia kinyume na hivyo basi kakupoteza. **Tanbihi ya pili:** jua kwamba kama ilivyokatazwa mtu kujinasibisha na nasaba ambayo si yake, basi pia imekatazwa mtu kuikataa nasaba yake.

[709] - Muslim ,*Al-Sahih* Hadithi na. 216.

kheri kwako katu."[710] Na Hadithi ya mke wa Thabit bin Qais ambaye alimuendea Mtume (s.a.w.) akamwambia: "Ewe Mjumbe wa Allah, Thabit bin Qais simlaumu kwa tabia wala dini, lakini mimi nachukia *kukufuru ndani ya Uislamu."*[711] Zingatia maneno "Kukufuru ndani ya Uislamu," halafu jiulize wewe vipi mtu anakufuru ndani ya Uislamu? Maana ya kukufuru ndani ya Uislamu ni kufanya maasi ilhali wewe ni Muislamu. Naye – mwanamke huyo – kayasema haya kumwambia Mtume (s.a.w.), wala Mtume (s.a.w.) hakumwambia kwamba hakuna kukufuru ndani ya Uislamu.[712]

Huo ni kwa upande wa Hadithi zenye kuonesha kuwepo kwa "Kufru Al-Ni'ima" (Kuikufuru neema ya Allah). Ama kwa upande wa Aya za Qur-ani zilizoonesha ukafiri huu ambao si ukafiri unaomtoa mtu katika mila ya Uislamu ni Aya kama: **"Na wale ambao hawakuhumu kwa alivyoteremsha Allah basi hao ni makafiri."**[713] Na Aya: **"Na Mwenyezi Mungu amewawajibishia watu wafanye hija katika Nyumba (yake) hio. Na atayekufuru (asifanye hija naye ana uwezo) basi (jueni kwamba) Allah hawahitaji walimwengu (wote na vilimwengu vyote).**[714] Na Aya inayomnukuu Nabii Sulaiman akisema: **"….Ili (Allah) anijaribu (kwa hizo neema alizonipa) je nitashukuru au nitakufuru."** Na bila shaka Nabii Sulaiman hakusudii ukafiri kama ule wa kiyahudi, bali ni ukafiri wa kuzitumia neema za Allah kinyume na maamrisho yake.[715]

Kwa hivyo, baada ya haya utaona kwamba tukijaalia kwamba riwaya hizo zenye kusema kuwa Watu wa Nahrawaan walimkafirisha Ali na riwaya kwamba Ali alisema kwamba akikubali sulhu atakuwa

---

710 - Kaipokea Al-Bukhari – *Na lafdhi ni yake* – *Al-Sahih* Hadithi na. 29-1052-5197. Muslim – *Na lafdhi yake ni tafauti kidogo na ina ziada* – *Al-Sahih* Hadithi na. 238/79. Na pia wameipokea wapokezi wengine wengi.

711 - Hadithi hio kaipokea Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 5273. Ibn Majah *Al-Sunan* Hadithi na. 2056. Na pia wameipokea wapokezi wengine.

712 - Hadithi kama hii kitaalamu huitwa *A-ssunnatu Al-taqririyya.* Nayo ni Hadithi ambayo Mtume (s.a.w.) anaona au anasikia kitu na akakinyamazia naye ana uwezo wa kukikataza.Hii ina maana kwamba kilichofanywa au kilichonenwa ni sahihi.

713 - Sura, 5 Aya 44.

714 - Sura, 3 Aya 97.

715 - Sura, 27 Aya 40.

ameyakufuru yale aliyoyateremsha Allah na aliyokuja nayo Mtume (s.a.w.), tukijaalia kuwa riwaya hizo zote ni sahihi basi elewa kwamba ukafiri wenyewe uliokusudiwa katika riwaya hizo si ule ukafiri unaomtoa mtu katika Umma wa Kiislamu, bali ni ukafiri kwa maana ya maasi makubwa. Na bila shaka – hakuna haja ya kupingana – Watu wa Nahrawaan wakimuona Ali kuwa kafanya kosa kubwa kwa kukubali sulhu; na Ali naye akiwaona wao wamefanya makosa makubwa kwa kumuacha mkono na kujichagulia uongozi mpya. Kwa hivyo, ukafiri katika riwaya hizo, maana yake ni maasi makubwa na haya yanaweza kumtokezea Muislamu yeyote akiwa Sahaba au Muislamu wa kawaida. Ama kusema kuwa Watu wa Nahrawaan wamemwita Ali kafiri kwa maana ya kuwa Ali si Muislamu: hayumo kabisa katika Umma huu, hili halikuthibiti kamwe. Na ingelikuwa hakuna ushahidi wowote ule isipokuwa kitendo cha wafuasi wa madhehebu ya Kiibadhi – ambao ndio warithi sahihi wa siasa ya Watu wa Nahrawaan – kuwa wao wanamuombea dua Ali kwa kusema: *"Karrama Allahu wajhahu"* basi ungetosha ushahidi huu kubatilisha riwaya hizo, kwani dua kama hii haijuzu kuombewa kwa asiyekuwa Muislamu.

Na kwa hivyo, Sheikh Nassir Al-Sabi'i anaeleza kwamba riwaya zenye kusema kuwa wao walimwita Ali mshirikina, zinatokana na ubadilishaji wa lafdhi za riwaya hizo, kwa maana kwamba msimulizi alikuwa akiitakidi kwamba Watu wa Nahrawaan walipotumia neno *ukafiri* walikuwa wakikusudia kuwa Ali ni kafiri mshirikina, na kwa hivyo msimulizi huyo aliposimulia riwaya badala ya kutumia neno *"Kufru"* (ukafiri) ambalo lina maana ya ukafiri wa ushirikina unaomtoa mtu katika Umma; na pia lina maana ya ukafiri wa kuikufuru neema, nao ni ukafiri ambao haumtoi mtu katika Umma; basi wasimulizi walilibadilisha neno hilo na badala yake wakatumia neno *"Shirk"* ambalo halina maana isipokuwa ya ukafiri wa kutoka katika Umma.[716] Na jambo hili la kuwa wao walimwita Ali kafiri mshirikina haliwezekani kwa sababu tatu:

[716] - **Ninasema:** na hii ni kawaida ya wasimulizi katika asilimia kubwa ya riwaya wamezisimulia kimaana. Lakini tatizo linakuja katika sehemu ambazo wahusika wana fikra nyengine na msimulizi ana fikra nyengine kama ilivyo hapa.

Mosi: Riwaya inayowanukuu watu hao wakimwambia Ibn Abbaas maneno hayo kuhusu Ali: "Inawasifu (watu hao wa Nahrawaan) kuwa ni wenye uwezo (mkubwa) wa kutoa ushahidi kutoka katika Qur-ani na kumuathiri muhubiriwa, kama vile ambavyo inamsifu msemaji wao kwamba ni msomi wa Qur-ani, mjuzi wa yaliyopambanuliwa na yasiyopambanuliwa.

Pili: Ni kwa sababu katika riwaya hii, wao (wameitwa): 'Jino la mwanzo la Masahaba wa Muhammad" yaani wao ni watangulizi katika Masahaba wa Muhammad.

Tatu: Ni kwa sababu kuwaita (Waislamu kuwa ni) washirikina kumeanza na Nafii bin Al-Azraq mwaka wa migawanyiko[717]. *Mwisho wa kunukuu.*[718]

Ninasema: Lakini maneno hayo ya Sheikh Nassir Al-Sabi'i yanaweza kupata upinzani kwamba riwaya inayosimuliwa na Al-Tabari katika *Taarikh*[719] na Ibn Abi Shaiba katika *Al-Musannaf*[720] na Al-Baladhiri katika *Al-Ansab*[721] inaeleza kwamba wakati Ali yupo Al-Kufa anawahutubia watu, basi mmoja wa Watu wa Nahrawaan alisimama akatia vidole vyake masikioni kisha akapaza sauti yake na kumsomea Ali Aya isemayo:

لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ

Ukimshirikisha (Mwenyezi Mungu) basi matendo yako (mema) yataanguka na utakuwa katika waliohasirika.[722]

Mpinzani anaweza akasema kwamba ni wazi – kwa mujibu wa riwaya hii – kwamba watu hao walikuwa wakimkafirisha Ali ukafiri wa ushirikina. Nasi tunaweza kujibu kwa hoja mbili:

---

717 - Itikadi za Nafi'i ndio itikadi za *kikhawarij* kama maelezo yatavyokuja *Inshaa Allah* katika juzuu nyengine za kitabu hiki.

718 - Nassir Al-Sabi'i , *Al-Khawarij Wa Al-Qiqitu Al-Ghaiba* uk. 136.

719 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 6, uk. 18.

720 - Ibn Abi Shaiba, *Al-Musannaf* j. 8, uk. 733-734, riwaya na. 20.

721 - Al-Baladhir,i *Al-Ansab* j. 3, uk. 128.

722 - Sura 39, Aya 65.

Moja: ni kile kilichotangulia katika maneno ya Sheikh Nassir mwenyewe cha kuwepo utunzi na ubadilishaji wa lafdhi za riwaya hizi kwa sababu tatu alizozitoa.

Pili: ni kuwa riwaya hio inasema kwa uwazi kwamba aliyefanya hivyo ni mtu mmoja katika wao. Na bila ya shaka kosa la mtu mmoja hatuwezi kuwapachika nalo watu wote. Vyenginevyo itabidi tuseme kwamba wale waliobakia katika uongozi wa Ali walikuwa nao wakiwaita Watu wa Nahrawaan kuwa ni makafiri washirikina kwani mmoja wao alimwambia Ali: "Nani anayemkumbuka nyumbu[723] siku waliyouliwa washirikina, yaani Watu wa Nahrawaan?"[724] Kwa hivyo, ikiwa kauli hio ya mtu mmoja katika Watu wa Nahrawaan imeweza kuchafua saffu nzima ya Watu hao, basi saffu ya Ali nayo na ichafuliwe na maneno haya ya mfuasi wake mmoja ya kuwaita watu wa Nahrawaan washirikina ilhali Ali mwenyewe alikuwa akiona kwamba hao si Washirikina. Na bila shaka hio si hukumu adili, basi uadilifu unatutaka kwamba na Watu wa Nahrawaan tusiwatupie lawama kwa kosa la mtu mmoja tukijaalia kuwa riwaya hio ni sahihi. Wala tusipingwe kwamba katika riwaya hio hio isemayo: "Nani anayemkumbuka nyumbu siku waliyouliwa washirikina…" kwamba Ali alimkataza mtu huyo kusema hivyo, wakati aliyesoma Aya **"Ukimshirikisha (Mwenyezi Mungu) basi matendo yako (mema) yataanguka na utakuwa katika waliohasirika"** kumwambia Ali, hakuna yeyote katika watu hao aliyemkataza mtu huyo, kwani tunasema:

a) Kutokupokewa kwa riwaya nyengine sahihi inayosema kuwa miongoni mwa Watu wa Nahrawaan walitoa ushahidi wa Aya hio **"Ukimshirikisha (Mwenyezi Mungu) basi matendo yako (mema) yataanguka na utakuwa katika waliohasirika"** ili kuthibitisha kuwa Ali ni kafiri,[725]

---

723 - Dhahir inaonesha kwamba walikuwa wakikumbushana matukio ya Nahrawaan na kwamba labda siku hio kulikuwa na nyumbu.

724 - Al-Bayhaqi *Al-Sunan* j. 12, uk. 334, riwaya na. 17189.

725 - Isipokuwa riwaya ya Al-Baladhiri imesema kwamba wakasema kwamba watu hao wakasema: **"Ukimshirikisha (Mwenyezi Mungu) basi matendo yako (mema) yataanguka".** Lugha hii "Wakasema" inamaanisha kwamba waliosema ni wote, lakini kama unavyoona kwamba riwaya ya Al-Tabari na Ibn Abi Shaiba ina uzito zaidi kwa sababu ya kupokewa na waliowengi zaidi, na kwa sababu katika *sanad* ya riwaya ya Al-Baladhiri kuna Wahb bin Jarir naye ni muaminifu lakini anakosea katika Hadithi.

inamaanisha kuwa ima watu hao hawakukubaliana na msomaji wa Aya hio au tukio hilo lote halikuwepo kabisa, bali lilitungwa kama alivyosema Sheikh Al-Sabi'i.

b) Halkadhalika kama vile Ali – kiongozi wa upande mmoja – alivyopinga kuitwa Watu hao wa Nahrawaan kuwa ni makafiri washirikina, tunamkuta kiongozi wa watu wa Nahrawaan – naye ni Abu Bilal – kwamba historia yake nzima inaonesha kuwa hakuwa akiwakafirisha watu wengine ambao – kwa mtazamo wake – wamekosea zaidi kuliko Ali, nao ni wale waliokuwa upande wa Mu'awiya na warithi wake. Kwa hivyo, yaliyotokea ya kuitana kafiri mshirikina – tukijaalia kuwa riwaya hizo ni sahihi basi – yametokea kutoka kwa wafuasi wa pande mbili: si upande mmoja, tena hayo yametokea kwa nadra ambapo kila upande aliyeyasema hayo ni mtu mmoja tu. Na kwa hivyo, hakuna maana ya kulihusisha jambo hilo na Watu wa Nahrawaan.

Lakini cha kujiuliza ni kuwa je ikiwa Watu wa Nahrawaan wametoka katika Uislamu kwa sababu wamemwita Ali kafiri; tukijaalia kuwa hilo ni kweli, je makundi mawili yaliyobaki – kundi la Ali na kundi la Mu'awiya – yalikuwa hayaitani makafiri na kulaaniana? Vitabu vya historia na riwaya kama vile ambavyo vinabeba riwaya hizo, kwamba Watu wa Nahrawaan walimkafirisha Ali na wafuasi wake, vivyo hivyo ndivyo vinavyobeba riwaya kadha wa kadha za Waislamu wengine kuwakafirisha Watu wa Nahrawaan na kukafirishana wenyewe kwa wenyewe:

1) Banuu Umayya walieka sunna ya kumlani Ali katika membari. Anasema Ibn Kathir:

> Na katika mwaka huu (wa 90 H.) alikufa Muhammad bin Yusuf Al-Thaqafi ndugu yake Al-Hajjaj na alikuwa ni Amiri wa Al-Yaman na alikuwa akimlani Ali juu ya mebari.[726]

Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 11, uk. 142, *tarjama* na. 273. Na Wahb bin Jarir kaipokea riwaya hio kutoka kwa baba yake Jarir bin Hazim bin Abdillahi, naye alichanganyikiwa na alikuwa akikosea, akisimulia Hadithi munkar na pia akasemwa kwa kughushi. Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 2, uk. 60-62, *tarjama* na. 111.

[726] - Ibn Kathir, *Al-Bidaya wa Al-Nihaya* j. 9, uk. 83, katika matukio ya mwaka 90.

2) Anasema Ibn Taymiyya:

> **وممن قاتله ولعنه (أي عليا) من أصحاب معاوية وبني مروان**
> "Katika wale waliopigana naye (yaani Ali) na kumlaani miongoni mwa wafuasi wa Mu'awiya na Banii Mar-waan".[727]

Mbona hatusikii vitabu kupiga kelele kwamba "Banii Umayya walimkafirisha Ali na kumuombezea laana", na wakalaumiwa kwalo?

2) Mfuasi wa Ali aitwaye Sa'asa'a bin Suhaan alimwambia mfuasi wa Mu'awiya kabla ya kuanza vita vya maji huko *Siffin*: "Hakika Allah atawanyima maji siku ya kiama makafiri (na) mafasiki mfano wako na walio mfano wako",[728] na katika riwaya nyengine: "Hakika Allah atawanyima (maji) waovu na wanywaji wa pombe, Allah akulani na amlani fasiki huyu".[729] Na kuna sehemu tafauti katika vitabu tafauti vya historia ambapo upande wa Ali na Mu'awiya huitana "Mbwa"[730] na "Adui wa Allah"[731] na mengineo. Na Al-Najashi, mshairi wa Ali kamwita Mu'awiya katika mashairi yake kuwa ni mnafiki.[732] Na kuna riwaya inayomnukuu Ali akiwasema wafuasi wa Mu'awiya kuwa "…Yeye anawalingania katika uongofu na dini ya haki; wao wanamlingania (yeye) katika ibada ya masanamu" na kwamba wao ni "Mafasiki".[733] Na akasema Ali: "Aliyemua Ammar (bin Yasir) hana Uislamu kitu".[734] Na pia kuna riwaya inayomnukuu Ali akiwaita watu wa Nahrwaan kuwa ni: "Mafasiki, waliotoka (katika dini)…".[735] Mu'awiya siku ya vita vya *Siffin* alimuandikia

---

727 - Ibn Taymiyya, *Minhaju Al-Sunna* j. 3, uk. 3. Na haya yako mengi yameelezwa katika vitabu vingi tunayawacha kwa kufupisha.
728 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 3.
729 - Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 635.
730 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 41, na uk. 187.
731 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 233.
732 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 23.
733 - Ibn A'atham ,*Al-Futuh* j. 3, uk. 235.
734 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 268.
735 - Ibn A'atham,, *Al-Futuh* j. 4, uk. 100.

Qais bin Sa'ad bin 'Ubada barua akamwambia: "Baada ya hayo, wewe ni yahudi mwana wa yahudi",[736] na Qais naye akamuandikia Mu'awiya akamwambia: "Wewe ni muabudu sanamu mwana wa muabudu sanamu".[737] Ali – baada ya sulhu ya Dumat Al-Jandal – alikuwa kila akisali anamlani Mu'awiya na viongozi wenzake.[738] Anasimulia Ibn A'atham kwamba mtu mmoja aliyekuwa katika jeshi la Mu'awiya alitokana naye baada ya haki kumbainikia na akajiunga na kambi ya Ali na akatoa mashairi yake yenye ubeti usemao: "Ewe Dhu Al-Kalaa'i achana na watu waliokufuru (yaani Mu'awiya na wafuasi wake)".[739] Na katika vita vya *Siffin*, Hammam bin Al-Aghfal, mmoja wa wafuasi wa Ali, baada ya kuona watu wengi wa Sham waliokufa alitoa shairi akisema: "Macho yamefurahi kutokana na (kuuliwa) mafasiki; na kutokana na (kuuliwa) viongozi wa ukafiri na unafiki".[740] "Viongozi wa ukafiri na unafiki" anaowakusudia ni wale waliokuwa katika jeshi la Mu'awiya. Baada ya Al-Husain bin Ali kutakiwa ambaii Yazid bin Mu'awiya na Al-Husain kukimbia kwenda Makka, kuna riwaya inayomnukuu Ibn Abbaas akisema kuhusu watawala wa Banii Umayya kwamba: "Hakika wao wamemkufuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake…".[741] Na haya na mfano wa haya katika vitabu ni mengi mno. Kwa hivyo, suala la kukafirishana halikuwa ni suala mahususi kwa kikundi fulani, bali ni suala ambalo walikuwa nalo watu wa makundi tafauti, ndio maana Ibn Taymiyya akasema: "Na (suala la) kuombeana laana lilitokea pande zote mbili (upande wa Ali na upande wa Mu'wiya)".[742]

736 - Ibn 'Abdi Rabih *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 315.

737 - Ibn 'Abdi Rabih, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 315. Na bora mtu umwite kafiri kuliko kumwita Yahudi au muabudu sanam, kwani kafiri ikiwa umekusudia kafiri wa neema kama Hadithi na Aya tulizozinukuu zinavyosema, basi ni neno jepesi kuliko Yahudi na muabudu sanamu. Ama Yahudi na muabudu sanamu huwa wametoka katika Uislamu moja kwa moja.

738 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 116-17. Ibn Al-Athir, *Al-Kamil* j. 2, uk. 684. Al-Baladhir,i *Al-Ansab* j. 3, uk. 126.

739 - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 129-130.

740 - Ibn A'atham „*Al-Futuh* j. 3, uk. 218.

741 - Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 3, uk. 5, uk. 40.

742 - Ibn Taymiyya, *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 204.

Bali hao wanaozuliwa kuwa na sifa hii (yaani Watu wa Nahrawaan) – ukirejea vitabu tafauti – utaona kuwa wao ndio waliojiweka mbali na suala hili.

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

1) Utakumbuka kwamba katika sura iliyokabla ya hii tulizungumzia suala la kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbab na kuthibitisha kuwa hakuna ushahidi unaowahusisha Watu wa Nahrawaan na kitendo hicho kiovu, bali hicho kilikuwa ni kitendo cha Mis'ar bin Fadaki na kikosi chake cha Basra, na Watu wa Nahrawaan hawakukubaliana naye, kwa hivyo wakamfukuza.
2) Hapa tumesema kwamba hata tukijaalia kuwa tukio hilo ni sahihi kuhusishwa na Watu wa Nahrawaan, je watu wa madhehebu mengine hawakufanya kama hivyo au zaidi kwa kutumia jina la Uislamu?
3) Tumeona jinsi Mu'awiya na warithi wake walivyoua maelfu – kama si malaki – ya Waislamu bila ya haki. Na tumeona pia riwaya nini zinasema kuhusu mauaji yaliyofanywa na Samura bin JundubJundub, na pia jinsi Abbasiyyin walivyoua na kufanya ufisadi hadi kufikia kuyafukua makaburi na kuwatoa maiti na kuwachoma moto!
4) Tumetazama pia dai kwamba Watu wa Nahrawaan walikuwa wakimkafirisha Ali.
5) Tumesema kuwa riwaya hizo hazikuthibiti lakini tukijaalia tu kuwa zimethibiti basi ukafiri unaokusudiwa ni kuikufuru neema kwa maana ya maasi makubwa.
6) Pia tumesema kwamba kama vile ambavyo kuna riwaya zenye kuwanukuu watu hao wakimkafirisha Ali kwa sababu ya kukubalikwake sulhu, vivyo hivyo kuna riwaya zinazomnukuu Ali mwenyewe – alipoombwa kusimamisha vita – akisema kwamba akifanya hivyo atakuwa kakikufuru kile alichokiteremsha Allah na alichokuja nacho Muhammad. Sasa nini ubaya wa watu hao hata ikiwa riwaya hizo ni sahihi?
7) Pia tumeona namna gani watu wa upande wa 'Ali, na watu wa upande Mu'awiya walivyokuwa wakikafirishana. Sasa kwa nini

hawa wasiwe nao *Makhawarij*, kwa kufanya kwao kosa lile lile ambalo limewapatia wale jina la *Ukhawarij*?

8) Pia tumeona katika zama za karibuni na hizi tulizonazo jinsi gani Mawahabi walivyowaua Waislamu kwa maelfu. Kama vile ambavyo katika sehemu mbali mbali za ulimwengu wa Kiislamu, kwa jina la Uislamu, Waumini waliuliwa na Wanauliwa bila haki. Na wauaji ni viongozi na wafuasi wa hizo madhehebu zenyekuwaita wenzao kuwa ndio *Khawarij!*

Sasa baada ya haya utaona kwamba:

a) Muawiya kampinga Ali na kupigana naye vita.
b) Kaua maelfu ya Waislamu bila haki.
c) Lakini Mu'wiya ni Muslamu mwema akitajwa tunamuombea dua!
d) Na mfano wa kitendo cha mauaji ya Mu'awiya ni mauaji yaliofanywa na Muhammad bin Abdil-Wahhab na wafuasi wake.
e) Watu wa Nahrawaan wametafautiana na Ali nao walikuwa na ushihidi madhubuti wa Qur-ani ambao hata Ibn Abbaas – kama tulivyobainisha – hatimae alikubaliana nao.
f) Hawakumuua mtu yeyote, isipokuwa yale yaliosemwa kuhusu kuuliwa kwa Ibn Khabbaab. Lakini tumeonesha kwamba tukio hilo si sahihi kuhusishwa kwake na Watu wa Nahrawaan. Bali ni mauaji binafsi yaliotendwa na Ibn Fadaki na kikosi chake kilichotoka Basra.
g) Pamoja na hayo, pasemwa kuwa Watu wa Nahrawaan ni *Khawarij* waliotoka katika dini; ama Mu'awiya na watu wake wao ni *Ahlu Sunna* waliohifadhi sira ya Mtume (s.a.w.); na Muhammad bin 'Abdil-Wahhab ni *Sheikh Al-Islam*!

Kuanzia hapa utaanza kujua kwamba kutumiwa jina *Khawarij* kwa watu wa Nahrawaan ni sawa na leo kutumiwa kwa jina magaidi (*terorrists)* kwa Waislamu wanaotetea au kutafuta haki zao. Watu wa Nahrwaan ndio waliokuwa Masahaba wa awali, wanavyuoni na ndio wacha Mungu wao na ndio waliokuwa na msimamo thabiti katika kuondoa dhulma. Na kwa hivyo, wapambe wa Ali na watawala wa Banii Umayya wakawabandika jina hilo, kwani watawala wa Banii Umayya – pamoja

na mwenendo wao ambao haukuwapendeza Waislamu – walikuwa wakijiita Ma-Amiri Al-Mu-uminin!

SURA YA NANE

KUULIWA KWA AL-IMAMU ALI

Al-Imamu Ali aliuliwa na mtu anayeitwa Abdul-Rahman bin Muljam Al-Muradi huko Iraki katika siku ya Al-Khamisi kuamkia Ijumaa[743] tarehe kumi na tatu [744] ya mwezi wa Ramadhani mwaka 40 A.H.[745] Hakuna khilafu kwamba aliyemuua Al-Imamu Ali ni Ibn Muljam, lakini je waliopanga njama hizo ni nani? Sheikh Nasir Al-Sabi'i ananukuu[746] maneno ya Al-Ustadh Ahmad bin Sulaiman Ma'aruf akisema:

> Je kweli upanga uliomuua Ali ni upanga wa *Kikhawarij*? Au lilikuwa ni jambia la kisasi cha kibinafsi cha baadhi ya waliouliwa Nahrawaan: hakihusiki na *Makhawarij* wote ndani yake? Au alikuwa ni mjumbe mwenye shauku na mahaba ya mwanamke wa *Kikhawarij* jina lake Qatam? Au lilikuwa ni pigo la uuaji wa kisiasa uliotekelezwa – kupitia kwa *Makhawarij* – na mkono wa mjanja wa Sham (Mu'awiya) na mshauri wake mwerevu Amru bin Al-'Aas?[747]

Masuali haya ni masuali ya kimaumbile na ya lazima kwa kila atakayefuatilia na kuisoma historia nzima ya vita vya *Siffin* hadi kufikia kuuliwa kwa Al-Imamu Ali. Lakini – kwa maajabu – utaona kwamba waandishi wengi wa historia, makala na wanavyuoni wakubwa

---

743 - Bali ni siku ya Ijumaa kwani alfajiri ilikuwa imeshaingia. Lakini hii si siku ya kifo chake, labda ni siku aliyopigwa upanga tu, ama siku ya kifo chake ni usiku wa Jumatatu, kwa mujibu wa riwaya ya Ibn Sa'ad katika *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 27. Hata hivyo, wengine wengi husema kuwa Ali kafa siku ya Ijumaa, wakimaanisha kwamba alipigwa upanga kabla ya siku hio. Na hivi ndivyo alivyonena Al-Mas'udi katika *Al-Muruj* j. 2, uk. 212 kwamba: "Na aliishi siku mbili (baada ya kupigwa upanga) na akafa usiku wa Ijumaa".

744 - Tarehe nyengine zilizotajwa ni 16-17-20-21.

745 - Ibn Hajar ,*Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7, uk. 297, *tarjama* na. 566. Ibn Sa'ad, *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 27.

746 - Nassir Al-Sabi'i , *Al-Khawarij Wa Al-Qiqitu Al-Ghaiba* uk. 164.

747 - Ma'aruf Ahmad, *Qiraatu Jadida Fii Mawaqifi Al-Khawarij* uk. 59.

wanawasukumizia Watu wa Nahrawaan kadhia ya kuuliwa kwa Ali! Wakati ukifuatilia historia yenyewe unakuta kwamba kuna muelekeo wenye nguvu sana unaoonesha kuwa njama za kumuua Al-Imamu Ali zilipangwa na Mu'awiya bin Abi Sufyaan. Lakini hili la kufanya kitu halafu akawasukumizia watu wengine, halikuwa geni katika siasa ya Mu'awiya. Ammar bin Yasir (r.a.), aliuliwa na Mu'awiya, yaani na jeshi lake katika vita vya *Siffin*: hakuna khilafu juu ya hilo katika Umma; lakini Mu'awiya alipokumbushwa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo: "Ammar atauliwa na kundi la waasi", basi alimtupia jukumu Al-Imamu Ali kwamba yeye ndiye aliyemuua kwani yeye ndiye aliyemleta vitani! Kwa hivyo, usione ajabu kwamba Mu'awiya afanye kitu kisha awasukumizie watu wengine ili kuwapaka matope wao na kujitoa hatiani yeye hapa duniani. Hali inakuwa mbaya zaidi na kusikitisha pale waandishi wanapokombakomba kila walisikialo na kuliweka katika vitabu na watu wakajisomea na kusadiki. Waandishi wa Banii Umayya waliyaandika hayo na watu wakayapokea kwa mikono miwili.[748] Lakini – kama

[748] - Miongoni mwa watu walioandika mambo ya uwongo na watu wakayapokea ni Ibn Hazm. Anasema: "Na akasema Abu Ismail na wafuasi wake kuwa nao (Maibadhi ni katika Makhawarij, na wanasema) kwamba hakuna Sala ya wajibu isipokuwa rakaa moja asubuhi na rakaa moja jioni na wanaona (kwamba inajuzu kufanya) Hijja katika miezi yote ya mwaka. Na wanaharamisha kula samaki mpaka achinjwe. Na wanaona (kwamba haijuzu) kuchukua jiz-ya kutoka kwa majusi. Na wanamwita mwenye kutoa khutba siku ya Idi Al-fitri na Idi Al-adh-ha kuwa ni kafiri. Pia wanasema kuwa watu wa motoni wamo katika raha!" *Mwisho wa kunukuu.* Tazama: Ibn Hazm *Al-Faslu Fii Al-Milal Wa Al-Ahwai Wa Al-Nnihal* j. 5, uk. 51-52. Sasa maneno haya waliyoyasema wameyapata wapi katika vitabu vya Kiibadhi vya tangu karne ya kwanza hadi leo! Cha kustaajabisha ni kuwa hadi zama hizi watu bado wanawazulia Ibadhi uwongo sawa na huo waliozuliwa Watu wa Nahrawaan katika zama za Mu'awiya. Mutakumbuka kwamba katika miaka ya nyuma kuna kikundi ambacho kiliuvamia Msikiti Mtukufu wa Makka. Basi watu ili kutaka kuficha upinzani wanaopata nchini kwao, walizua kwamba waliovamia Msikiti huo ni Ibadhi! Lilisema garzeti la Jordan liitwalo *Jaridatu Al-Dustur* toleo na. 4412, tarehe 22-2-1979, likinukuu chanzo (Source) cha Su'udia kwamba: "Wanachama wa kikundi kilichouvamia Msikiti Mtakatifu alfajiri ya mwanzo wa mwezi wa mwaka 1400 A.H, ni kikundi cha *Khawarij*. Na kikundi hiki ni chenye kasumba na siasa kali…nao ni katika Maibadhi wanakaa Algeria, Maskati, Afrika (ya Mashariki), Tunis, Libya na Oman". *Mwisho wa kunukuu.* Anasema Sheikh Al-Khalili: "Na-tuutazame huu uzishi mkuu! Je kuna hata mtu mmoja miongoni mwa Ibadhi katika waliovunja heshima ya Msikiti Mtukufu? Je yumo katika kikundi hiki kilichovamia Msikiti Mtukufu katika zama hizo mtu japo mmoja katika Ibadhi? Hakika hakuna miongoni mwa hawa hata Muomani mmoja wala Mualjeria hata mmoja wala Muafrika Mashariki hata mmoja wala yeyote kutoka Tunis wala yeyote kutoka Libya,

Waswahili wasemavyo – ukweli haujifichi na njia ya mwongo fupi. Ushahidi ambao wanautoa watu hao katika kuwasukumizia Watu wa Nahrawaan jarima hilo la kumuua Ali, ni ushahidi wenye mashaka sana: si rahisi kwa msomaji mwenye tabia ya kuhoji usahihi wa kitu na kujiuliza na kutafakari kuweza kuukubali.

Waliosema kuwa Ali kauliwa kwa njama za Watu wa Nahrawaan au kwa njama za *Khawarij* wanategemea riwaya isemayo:

> Ilikuwa hadithi (story) ya Ibn Muljam na wenzake, kwamba Ibn Muljam na Al-Burak bin Abdillah na Amru bin Bakr Al-Tamimi walikusanyika wakazungumzia mambo ya watu (yalivyo) na wakamtia kasoro Ali, kisha wakawataja Ahlu Al-Nahri (Watu wa Nahrawaan) wakawaombea dua ya kuwatakia rehema. Na wakasema: 'Hawa waliobakia baada yao hatuwafanyi kitu'?
>
> Wakasema: 'Tuziuze nafsi zetu na tuwajie viongozi wa upotovu tutafute (njia za) kuwaua, ili tuipumzishe miji kutokana na wao, na tulipize kisasi cha ndugu zetu. Akasema Ibn Muljam – na alikuwa ni mtu wa Misr -: 'Mimi wangu Ali bin Abi Talib, akasema Al-Burak bin Abdillah: 'Mimi wangu Mu'awiya bin Abi Sufyaan; akasema Amru bin Bakr: 'Mimi wangu Amru bin Al-'Aas'.

Kisha riwaya – nayo ni refu – ikataja kisa cha vichekesho kwamba:

> Ibn Muljam alikutana na mwanamke mzuri jina lake anaitwa Qatam, akamrusha akili kwa uzuri wake akataka kumuoa akamwambia yeye mahari yake ni Elfu tatu (labda dirham au dinar) na mtumwa

---

bali (walikuwa wavamizi) ni kutoka Su'udia yenyewe na walioambatana nao kutoka nje ya Su'udia ni Mawahabi wenye siasa kali, basi vipi tuhuma hii wanabandikwa nayo Ibadhi". Tazama Sheikh Al-Khalili: *Nabdhu Al-Ta'assubi Al-Madh-Habi* uk. 41-42. ***Ninasema:*** sisi kule kwetu Zanzibar tulikuwa tunadanganywa kwamba waliouvamia Msikiti ni Mashia wa Iran! Hivi ndivyo, uwongo hadi leo unavyoendelezwa kuzuliwa madhehebu fulani kwa sababu za Kisiasa! Basi elewa kwamba hivi unavyoona leo ndivyo hivyo hivyo ilivyokuwa katika zama hizo za Sheikh Mu'awiya na Al-'Allama Amru bin Al-'Aas.

mwanamume na mtumishi mwanamke na kumuua Ali. Ibn Muljam akakubali.[749]

MATN YA RIWAYA

Riwaya hii ni riwaya ya vichekesho! Silaumu riwaya hii kupata soko na muitiko kutoka kwa watu wa kawaida kwani wao hawana vipimo vya kutosha vya kuweza kujua udhaifu na usahihi wa riwaya, lakini inastaajabisha kuona kwamba watu wenye elimu na akili zao katika Umma huu kuwa wamekikubali kisa hiki! Kisa hiki ni batil kwa *matn (text)* na *sanad* (wapokezi). Ama *matn* (*text*) ni kuwa, ikiwa watu watatu hawa waliyapanga haya kwa siri ni nani aliyeweza kujua yote haya kwa ufafanuzi wa kutosha namna hii[750] kama hiki si kisa cha uwongo na cha kutungwa?[751] Hasa hasa ukizingatia kwamba katika riwaya hii – nayo ni refu hapa tumeikata – kuna maelezo haya: "Akaja Ibn Muljam Al-Kufa (Iraki) akawakuta wenzake *Makhawarij*, akawaficha kile

[749] - Al-Tabari katika *Taarikh* j. 6, uk. 62. Al-Tabarani katika *Al-Mu'ujam Al-Kabir* j. 1, uk. 97, Hadithi na. 168. Ibn Sa'ad *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 25-26. Al-Mas'udi *Al-Muruj* j. 2, uk. 539.

[750] - Hatimae nikakuta katika *Muruju Al-Dhahab* j. 2, uk. 543, kwamba Zaadawaihi au Amru bin Al-Burak Al-Tamimi ambaye ndiye aliyejitwika jukumu la kumuua Amru bin Al-'Aas ndiye aliyemuelezea kisa hiki Amru bin Al-'Aas. Ninasema: ikiwa masimulizi ya kisa hiki yamepatikana kwa njia ya Amru bin Al-'Aas na kundi lake basi sina cha kukwambia ewe Al-Mas'udi pamoja na waandishi wa historia isipokuwa nakupeni mkono wa pole! Hii inathibitisha wazi kwamba hiki ni kisa kilichotungwa na kundi la Mu'awiya na Amru bin Al-'Aas ili kuficha jarima la aliyemuua Ali! Tanbihi: Katika *Al-Kamil* cha Al-Mubarrad j. 2, uk. 600, imeandikwa Zadhawaihi badala ya Zaadawaihi.

[751] - Wala usiniambie kwamba *"Hio si hoja madhubuti kwani katika historia kumejaa mifano kama hii, utakuta kikundi fulani kinakutana kwa siri kuzungumzia mikakati yao lakini yote hayo yamerikodiwa katika historia kuwa walizungumza kadha na kadha"* kwani ninasema kwamba: "Yote hayo yalioandikwa kwa njia kama hizo si hoja sahihi dhidi ya mpinzani ila yawe maandiko hayo yamepata nguvu kwa njia nyengine inayokubalika, kwani historia – kama tulivyosema – imeandikwa kwa matamanio ya nafsi na kwa hamasa na uwongo mwingi. Na kwa kawaida ni kuwa kilichozungumzwa kwa siri huwa hakijulikani na wengine, kwa hivyo anayedai kuwa kakijua ni lazima atupe ushahidi wa njia aliyojulia. Katika suala hili – kama tulivyoona – njia ya kulijua ni taarifa ya Amru bin Al-'Aasi!

alichokikusudia".[752] Ni wazi – kwa mujibu wa riwaya hii – kwamba Ibn Muljam aliyafanya hayo kwa siri, sasa sijui ufafanuzi wa namna hii umepatikana wapi. Ni wazi – kwa mtu mwenye akili yake – kwamba kisa hiki ni kisa cha kutunga ili kuwapaka matope Watu wa Nahrawaan na kumficha muuaji wa kweli aliyemuua Ali.

Pili – kama alivyosema Al-Sabi'i – ni kuwa jambo lenye kustaajabisha ni kuwa walioandaliwa kuuliwa ni Ali, Mu'awiya na Amru bin Al-'Aas; Ali akauliwa lakini Mu'awiya na Amru hawakuuliwa. Hapa kuna wasi wasi mkubwa wa kuwa Mu'awiya na Amru ndio waliopanga njama hizo za kumuua Ali kisha wakazifunika kwa njia ya waandishi wao wa historia na ukipenda sema waandishi wao wa habari!

Tatu: ni kuwa kiini cha kisa hiki kina aina fulani ya mgongano. Kisa hiki kinakusudiwa kuonesha kwamba Ibn Muljam kamuua Ali kwa msukumo wa mwanamke mzuri; wakati mwanzoni mwa kisa chenyewe hali inaonesha kwamba lengo la kumuua Ali ni kuwapumzisha watu na fitna zilizotokea na kulipiza kisasi cha waliouliwa huko Nahrawaan na kwa hivyo njama zilipangwa Makka kwa siri baina ya watu watatu.

Nne: ni mgongano uliokuwepo katika maneno haya: "Akaja Ibn Muljam Al-Kufa (Iraki) akawakuta wenzake *Makhawarij*, akawaficha kile alichokikusudia".[753] Na akaongeza Al-Tabari: "….Kwa kuchukia (watu) wakajakudhihirisha chochote katika jambo lake".[754] Ni wazi – kwa mujibu wa maneno haya – kwamba Ibn Muljam alilificha jambo lake hilo kwa kuhofia lisije likadhihiri na kwa hivyo aliwaficha hata wale waliokuwa na msimamo mmoja pamoja naye. Sasa soma sehemu ya pili ya riwaya hio hio yenye kusema:

> Na Ibn Muljam akamjia mtu katika (watu wa kabila la) Ashja'u anayeitwa Shabib bin Bajara[755] akamwambia: 'Je uko tayari kujipatia utukufu wa dunia na akhera? Akasema: 'Ni upi huo'. Akasema (Ibn Muljam): 'Kumuua Ali'.[756]

---

752 - Ibn Sa'ad, *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 26. Al-Tabari *Al-Taarikh* j.6, uk. 62.

753 - Ibn Sa'ad, *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 26. Al-Tabari *Al-Taarikh* j.6, uk. 62.

754 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 62. Al-Mas'udi *Al-Muruj* j. 2, uk. 540.

755 - Kwa mujibu wa riwaya ya Al-Mas'udi jina lake ni "Shabib bin Najda". Al-Mas'udi *Al-Muruj* j. 2, uk. 539.

756 - Al-Tabari „*Al-Taarikh* j. 6, uk. 63.

Na katika riwaya ya Ibn Sa'ad: "Na Abdul-Rahman bin Muljam akamkuta Shabib bin Bajara Al-Ashja'i akamjuilisha kile alichokikusudia na akamtaka wawe wote".[757] Mgongano huu uliokuwemo ndani ya riwaya moja unaonesha kwamba kisa hiki ni kisa cha kupanga au kimezidishwa mambo ya ziada ili kutaka kuiharibu sura ya kikundi fulani.

Tano: kwanini Ibn Muljam akamatwe na kuuliwa lakini mwanamke aliyepanga naye njama, Qatam, asiuliwe wala kupitishiwa hukumu yoyote, ikiwa kweli kulikuwa na mwanamke huyu na alifanya hivyo?

SANAD YA RIWAYA

Ama kuhusu *sanad* ya riwaya hii – chambilecho Warabu *Fas-al wala haraj* (uliza wala hakuna ubaya)! Msimulizi wa riwaya hii ni Uthman bin Abdil-Rahman Al-Taraaifi Al-Khuzaai Abu Abdil-Rahmaan. Anasema Al-Bukhari: "Anasimulia (riwaya) kutoka kwa watu madhaifu". Anasema Abu 'Aruba *"Layyin"*. Anasema Al-Saji: "Ana (Hadithi) nyingi *munkar"*. Anasema Al-Imamu Ahmad: "Simjuzishi (kupokea riwaya zake)". Anasema Al-Azdi: "Ni mwenye kuachwa". Anasema Ibn Numair: "Mwongo mkubwa". Anasema Ibn Hibban: "Anasimulia kutoka kwa watu madhaifu mambo anayaghushi; haijuzu kumfanya kuwa ni hoja".[758] Baada ya maelezo haya ya wanavyuoni wataalamu wa fani ya Hadithi na wapokezi wake, je bado kuna hoja sahihi katika kisa hiki dhidi ya walioitwa kuwa ni *Khawarij* enyi walimwengu wenzangu?

USHAHIDI WA WANAOSEMA KUWA ALI KAULIWA KWA NJAMA ZA MU'AWIYA

Kwanza cha kufahamu ni kuwa wakati huu alipouliwa Ali ilikuwa hakuna tena Watu wa Nahrawaan: Ali ameshawaua wote. Waliobaki wachache ni kama Abu Bilal, Mirdas bin Hudair (r.a.). Na hakuna

757 - Ibn Sa'ad *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 26.

758 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7, uk. 123, *tarjama* na. 280.

ushahidi wowote wa kihistoria, sahihi wala dhaifu, kwamba hawa wachache walishiriki katika kumuua Ali au walipanga njama hizo.[759] Bali waandishi wa historia wengine wameeleza kwamba Watu wa Nahrawaan – yaani wachache waliobaki – hawakukiridhia kitendo cha Ibn Muljam cha kumuua Ali. Anasema Al-Mas'udi: "Na wengi katika *Khawarij* hawampendi Ibn Muljam, kwa sababu ya kumuua kwake kwa kumdoea".[760] Kwa hivyo, kuhusishwa mauaji ya Ali na watu hao ni kosa la kihistoria.

Ama ushahidi wanaoutegemea Ibadhi na watetezi wengine wa Watu wa Nahrwaan (r.a.) – pale waliposema kuwa kuna muelekeo mkubwa wa kuwa Mu'awiya ndiye aliyekuwa mpangaji wa mauaji hayo – ni kama ilivyo katika maelezo ya Sheikh Nassir Al-Sabi'i katika kitabu chake.[761] Kwa kuanzia ni kuwa Ibn Muljam kabla ya kumuua Ali, alifanya mkutano na Al-Ash'ath bin Qais Al-Kindi.[762] Na Al-Ash'ath huyu alikuwa katika jeshi la Ali, lakini je Al-Ash'ath alikuwa nani? Huyu alikuwa ni jasusi wa Mu'awiya aliyechomekwa katika jeshi la Ali. Bali historia yake tangu zamani ilikuwa ni historia mbovu kwani:

> Alirtadi pamoja na waliortadi katika zama za Abu Bakr kisha akasilimu tena[763] na Abu Bakr mwenyewe alijuta kwanini hakumuua kwa jinsi alivyokuwa mtu muovu. Anasema Abu Bakr: 'Natamani siku niliyoletewa Al-Ash'ath bin Qais ningeikata shingo yake: hakika inanijia fikra kwamba yeye haoni shari ila huikimbilia na kuipalilia'.[764] Na labda kilichochochea ghadhabu za Al-Ash'ath dhidi ya Ali ni kwamba yeye (Ali) alimuuzulu (Al-Ash'ath katika Ugavana wa) Adhrabaijan[765] baada ya kuwa Uthman bin Affaan alimpa nafasi hio.[766] Na imepokewa kwamba Ali alimwambia katika barua ya kumuuzulu: 'Hakika umeghururika kutokana na nafsi yako kwa

759 - Na mwenye ushahidi naatuletee.
760 - Al-Mas'udi *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 273.
761 - Nassir Al-Sabi'i *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. 170-175.
762 - Kama tutavyotoa ushahidi katika kurasa zinazofuata.
763 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 156.
764 - Al-Baladhiri, *Fat-Hu Al-Buldan* uk. 112.
765 - Nilivyoona katika vitabu viwili vitatu nilivyovipitia ni kuwa mji huu unatamkwa hivyo. Lakini Yaqut Al-Hamwi kautaja kwa jina la *Adhrabijan* na pia akataja matamshi mengine yanaoitwa mji huo. *Mu'ujamu Al-Buldaan* j. 1, uk. 109.
766 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 80.

sababu Allah kakupuruzia; ukawa unakula riziki zake (anazokupa) na unajifurahisha kwa neema zake na unayamaliza mazuri yako katika siku (hizi) za uhai wako (wa kidunia: akhera huna kitu); basi njoo nawe umezichukua ngawira zilizo kabla yako wala usijifanyie njia (ya kujiingizi katika lawama yaani usijitie mashakani)".[767]

Na hiki ndicho ambacho kilimpelekea Al-Ash'ath – kama inavyosimuliwa – kuandikiana na Mu'awiya.[768] 'Na kwa hivyo, itakuwa Al-Ash'ath kaanza maisha yake na Ali kwa mwanzo usio wa kimapenzi wala wa ikhlas, basi akawa (Al-Ash'ath bin Qais) anamsubiria (Ali) mambo yamgeukie na kusubiri fursa ili ajilipize kutoka kwake na akafanya hivyo.[769]

Hayo – kama tulivyosema ni maelezo ya Sheikh Al-Sabi'i – na baada ya hapo Sheikh akatoa ushahidi wenye kuonesha kwamba Al-Ash'ath kweli alikuwa ni jasusi wa Mu'awiya. Miongoni mwa mambo yenye kuonesha hivyo ni:

1) Kushikilia kwake kwamba vita (vya *Siffin*) visitishwe.

3) Kushikilia kwamba muwakilishi wa Ali – katika kufanywa sulhu – awe Abu Musa.Kupitisha mkataba wa sulhu katika jeshi la Ali (akiwashawishi wana jeshi wa Ali waukubali mkataba huo).

4) Kumshikilia Ali kuachana na ahadi yake aliyowapa watu wa Harauraa (Watu wa Nahrawaan) kwamba hatompeleka tena Abu Musa huko Adhruh.[770]

5) Kumshikilia kwake Ali huko Al-Nukhaila kwamba wageuke kuwaendea Watu wa Nahrawaan badala ya (kuwaendea) watu wa Sham, na hayo ni baada ya kudhihiri natija ya hukumu.

6) Kuwaacha mkono watu wa Ali baada ya (kumalizika vita vya) Nahrawaan, asiwanusuru ili kuwapiga watu wa Sham.[771]

---

767 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 388.

768 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 80.

769 - Ma'aruf, Ahmad ,*Qiraatu Jadida Fii Mawaqifi Al-Khawarij* uk. 70, nakala kutoka katika kitabu *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* cha Al-Sabi'i.

770 - Nadhani katika baadhi ya vitabu wanaliandika jina la sehemu hii kuwa ni *Al-Adhrah,* lakini Yaqut Al-Rumi anasema ni *Adhruh*. Tazama Yaqut Al-Rumi *Mu'ujamu Al-Buldan* j. 1, uk. 110.

Na kwa hivyo, si ajabu (kwa) Ibn Abi Al-Hadid kusema: 'Uharibifu wote katika Ukhalifa wa Ali (k.w.) na migogoro yote iliyotokea, asili yake ni Al-Ash'ath"[772] na Al-Shahrastani akamuhisebu Al-Ash'ath: "Kuwa ni miongoni mwa waliotoka zaidi dhidi ya Ali na walitoka zaidi katika dini (yaani ndio *Khawarij* mkubwa)'.[773]

…….Na kwa hakika Mu'awiya alimtuma Utbat bin Abi Sufyaan – wakati wa vita vya *Siffin* – kwenda kwa Al-Ash'ath akimwambia: "Mwambie Al-Ash'ath maneno laini, kwani akiridhia yeye sulhu basi wote wataridhia.[774]

…..Na inaonesha kwamba Ali alikuwa katika orodha ya jumla ya watu ambao (Mu'awiya) alipanga kuwaua. Na ikiwa Muhammad bin Abi Bakr na Al-Ashtar Al-Nakha'i – nao ni wasaidizi wa Ali – ni shabaha ya mwanzo ya njama hizo (za Mu'awiya), ambapo Amru bin Al-'Aas alimuua Muhammad (bin Abi Bakr)[775] na akamtilia sumu Al-Ashtar, hadi Mu'awiya akasema: "Ali alikuwa na mikono miwili ya kuume (Wasaidizi wawili wa nguvu); mmoja nimeukata siku ya (vita vya) *Siffin*, yaani Ammar bin Yasir,[776] na mmoja nimeukata leo, yaani Al-Ashtar"[777], basi ni jambo la kiakili kabisa kwamba Ali atakuwa ndiye mlengwa wa uhakika; na vipi Mu'awiya amuache mgonvi (wake ambaye) alikuwa akiwahimiza watu kumpiga vita miaka miwili[778] (halafu amuache) bila ya kumkusudia kumuua au kumfanyia njama?

---

771 - Yaani miadi ilikuwa ni kwanza wakapigane na watu wa Nahrawaan wakimaliza vita hivyo ndio waende Sham kupigana na Mu'awiya. Kumbe hii ilikuwa ni njama tu iliofanywa na Al-Ash'ath na Mu'awiya ili kumdhoofisha Ali. Baada ya kumalizika vita vya Nahrawaan na kuuliwa kwa watu hao wa Nahrawaan na Ali kudhoofika kwa sababu ya kuwauwa watu hao waliokuwa tishio kwa Mu'awiya; Al-Ash'ath na walio pamoja naye wakakataa kwenda kumpiga Mu'awiya!

772 - Ibn Abi Al-Hadid ,*Sharhu Nahji Al-Balagha* j. 2, uk. 279.

773 - Al-Shahrastani, *Al-Milalu Wa Al-Nihal* j. 1, uk. 114.

774 - Ibn Qutaiba, *Al-Imama Wa Al-Siyasa* (kilichonasibishwa naye), uk. 102-103.

775 - Al-Tabari ,*Al-Taarikh* j. 3, 132.

776 - Tazama maneno ya Mu'awiya yasivyokuwa na tawfiq ya Allah; alipouliwa Ammar huko Siffin akamrushia mzigo Ali baada ya kukumbushwa Hadithi sahihi ya Mtume (s.a.w.) juu ya jambo hilo; hapa anajisifu kwamba kamuua Ammar!

777 - Al-Tabari,„ *Al-Taarikh* j. 3, 133. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 705.

778 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 4, uk. 570.

Na la kustaajabisha ni kuwa kifo cha Al-Hasan bin Ali pia ni kwa kutiliwa sumu na mke wake, Ja'ada bint Al-Ash'ath bin Qais![779]

Na kwa hivyo, ni katika jambo la kawaida kuwakuta miongoni mwa wafuasi wa Ali (wa zama hizo) kwamba walikuweko waliomtuhumu Mu'awiya kwa uwazi kuwa (ndiye aliyepanga njama za) kumuua Al-Imamu Ali. Anasema Abu Al-As-wad Al-Dili.[780]

ألا أبلغ معاوية بن حربفلا قرت عيون الشامتينا**
أفي شهر الصيام فجعتمونابخير الناس طرا أجمعينا**

E! Mfikishie Mu'awiya bin Harb, [781]Yasifurahi macho ya watutakiao shari.
Katika mwezi wa siamu mumetuumiza, Kwa (kumuua) mbora wa watu wote![782]

Na ni sawa tu: ikiwa Abdul-Rahman bin Muljam kumuua kwake Al-Imamu Ali ni kwa msukumo wa Mu'awiya au wa Al-Ash'ath au kwa kutekeleza matakwa ya mwanamke mzuri au ikiwa ni kisasi binafsi cha baadhi ya walioliwa Nahrawaan, basi ufupisho wa yote hayo ni kuwa *Al-Khawarij* hawana hatia ya damu ya Al-Imamu Ali na mikono yao iko safi kama alivyosema Al-Ustadh Ahmad Sulaima Ma'aruf.[783] Na makusudio ni kuwa, pamoja na kunasibika Abdul-Rahman bin Muljam na Muhakkima (Watu wa Nahrawaan), basi hakika kitendo chake hakihusiani kabisa na wao madamu hawakusaidiana naye wala kumuunga mkono katika kumuua Al-Imamu Ali.[784]

Kwa hali yoyote ile, tukio hili mfano wake ni kama tukio la kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbab; alichokifanya Abdulrahman bin Muljam (kumuua Al-Imamu Ali) ni kama alichokifanya Mis'ar bin Fadaki (kumuua Abdillahi bin Khabbab). Na ikiwa (kitendo) hiki (cha

779 - Ibn Hajar, *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 23, uk. 274, *tarjama* na. 1331.
780 - Pia huitwa *Al-Duali.*
781 - Harb ni jina la Abu Sufyaan, baba yake Mu'awiya.
782 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 625, Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 160, Al-Mubarrad *Al-Kamil,* j. 3, 1169. **Tanbihi:** kilichosahihi katika marejeo ya Al-Baladhiri aliyotupa Sheikh Nassor ni j. 3, uk. 265: si uk. 625, wala juzuu hio haina idadi hio ya kurasa, ni wazi kwamba hilo ni kosa la chapa.
783 - Ma'aruf, Ahmad ,*Qiraatu Jadida Fii Mawaqifi Al-Khawarij* uk. 76.
784 - Bali walikichukia na kukipinga.

> kumuua Abdillahi bin Khabbab) ndio sababu ya kuwamaliza Watu wa Nahrawaan, basi (kitendo) hicho (cha Abdulrahman bin Muljam cha kumuua Al-Imamu Ali) kinatosha kuipa sura mbovu sauti ya Muhakkima (Watu wa Nahrawaan) na kuwafanya wapinzani wao wawapakazie (uovu), pamoja na kuwa Muhakkima (Watu wa Nahrawaan) hawabebi jukumu la alichokifanya Ibn Muljam hata tukijaalia kuwa naye ni mwenye rai kama zao, basi vipi kama hakuwa hivyo. *Mwisho wa kunukuu.*[785]

Baada ya *bahthi* (utafiti) hii ya Sheikh Nassir, tunapata – kutoka katika maelezo yake – kwamba walioitwa *Khawarij* hawakuhusika na kitendo cha Ibn Muljam cha kumuua Al-Imamu Ali, bali hicho kilikuwa ni kitendo cha Ibn Mujam mwenyewe. Na hili – ukiachilia mbali hayo yaliyotangulia kutoka katika uchambuzi wa Sheikh Al-Sabi'i – hata hio riwaya ambayo inasema:

> Ilikuwa hadithi (story) ya Ibn Muljam na wenzake, kwamba Ibn Muljam na Al-Burak bin Abdillah na Amru bin Bakr Al-Tamimi walikusanyika wakazungumzia mambo ya watu (yalivyo) na wakamtia kasoro Ali, kisha wakawataja Ahlu Al-Nahri (Watu wa Nahrawaan) wakawaombea dua ya kuwatakia rehema. Na wakasema: 'Hawa waliobakia baada yao hatuwafanyi kitu?.....Akasema Ibn Muljam……: 'Mimi wangu Ali bin Abi Talib….

Tunakuta katika riwaya hii – kama tulivyosema kabla – kwamba kuna maneno yasemayo: "Akaja Ibn Muljam Al-Kufa (Iraki) akawakuta wenzake *Makhawarij*, akawaficha kile alichokikusudia".[786] Ni wazi – kwa mujibu wa riwaya hii ambayo ndio inayotegemewa katika suala hili – kwamba kitendo hicho hawahusiki nacho walioitwa *Khawarij,* vyenginevyo Ibn Muljam hakuwa na haja ya kuwaficha wenzake.

Pia tunapata kwamba Al-Ash'ath bin Qais Al-Kindi – ambaye alikuwa katika jeshi la Ali – alikuwa akitumiwa na Mu'awiya, kwa ushahidi ambao tumeunukuu kutoka katika maneno ya Sheikh Nassir. Pili ni kuwa Al-Ash'ath huyu hakuwa na mapenzi na Ali tangu mwanzo kwa

785 - Sheikh Nassir Al-Sabi'i ,*Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* uk. 170-174.
786 - Ibn Sa'ad, *Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 26.

sababu ya kumuuzulu kwake kutoka katika Ugavana wa Adhrabaijan.[787] Tumeona pia kwamba Mu'awiya kajisifu kwa kumuua Al-Ashtar – mtu muhimu kwa Ali – kwa kutiliwa sumu na mshauri wa Mu'awiya, Amru bin Al-'Aas. Pia mtoto wa Sayyidna Ali, Al-Hasan bin Ali, alitiliwa sumu na mkewe ambaye ni mtoto wa Al-Ash'ath bin Qais, jambo lenye kuonesha kuwepo kwa msukumo wa kufanya hivyo utokao kwa Al-Ash'ath mwenyewe, na hatimae kuonesha chuki za Al-Ash'ath kwa Al-Imamu Ali. Ni wazi kwa haya, kwamba Mu'awiya na Al-Ash'ath bin Qais wote walikuwa wakimsubiria Ali kumuondoa duniani kama walivyowaondoa Al-Ashtar na (dhahir) kumuondoa Al-Hasan bin Ali.

Sasa – kwa ufupi – ni kuwa ikiwa Watu wa Nahrawaan hawakuhusika na damu ya Ali kwa hali yoyote ile na kwa makadirio yoyote yale; na Mu'awiya alijenga uadui na Ali; na Al-Ash'ath bin Qais alikuwa akitumiwa na Mu'awiya na alikuwa na chuki za wazi dhidi ya Ali; bado tuna suali la kujiuliza nalo ni kuwa ni kitu gani kinachotupa ushahidi kuwa mauaji ya Ali yalifanyika kwa mbinu za Mu'awiya na Al-Ash'ath bin Qais? Ushahidi tunaupata katika riwaya ya Ibn Sa'ad isemayo:

> ...Na akalala Abdul-Rahman bin Muljam usiku huo ambao katika huo aliazimia kumuua Ali asubuhi yake, (ikawa) anazungumza na Al-Ash'ath bin Qais Al-Kindi msikitini kwake mpaka alfajiri ikakaribia kuchomoza. Al-Ash'ath akamwambia (Ibn Muljam): 'Asubuhi itakufedhehesha simama'. Akasimama Abdul-Rahman bin Muljam na Shabib bin Bajara wakachukua panga zao kisha wakaja mpaka wakakaa mukabala (opposite) na mlango ambao Ali hupitia….[788]

Na katika riwaya ya Al-Baladhiri:

> Hakuacha Ibn Muljam usiku huo kuwa kwa[789] Al-Ash'ath bin Qais anazungumza naye mpaka Al-Asha'th akamwambia: 'Simama hakika asubuhi itakufedhehesha'. Na akaisikia kauli yake hio Hujr bin Adey

- Wengine wanaitamka *Adharbijan.* [787]

[788] - Ibn Sa'ad ,*Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 26. Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 540.

[789] - "Kuwa kwa Al-Ash'ath" ni kuwa pamoja naye ama nyumbani kwake au Msikitini.

> Al-Kindi, alipouliwa Ali, Hujr akamwambia (Al-Ash'ath bin Qais): 'Ewe chong'o wewe ndiye uliyemuua.[790]
>
> Na akasema Al-Madaini, kasema Maslama bin Muhaarib: 'Aliyesikia maneno (hayo: simama hakika asubuhi itakufedhehesha) ni (mtu aitwaye) Afif, ami yake Al-Ash'ath. Alipouliwa Ali, Afif akasema (kumwambia Al-Ash'ath bin Qais): 'Hiki ni kitendo chako na njama zako ewe chongo'.[791]

Kwa hivyo, kwa mujibu wa riwaya hizi, ni wazi kwamba Al-Ash'ath bin Qais na Ibn Muljam ndio waliomuua Al-Imamu Ali, jambo ambalo linathibitishwa zaidi na riwaya ya Al-Mas'udi katika *Al-Muruj* aliposema: "(Abdul-Rahman bin Muljam) akafikia kwa Al-Ash'ath bin Qais Al-Kindi, akakaa kwake muda wa mwezi mmoja ananoa upanga wake".[792] *Mwisho wa kunukuu.* Na tutakapojua kwamba Al-Ash'ath alikuwa ni jasusi wa Mu'awiya, na Mu'awiya ndiye hasimu mkubwa wa Ali, ukichanganya na ukweli kwamba hata walioishi katika zama hizo miongoni mwa wafuasi wa Ali wako waliomtuhumu Mu'awiya kwa kumuua Ali, basi ni wazi kwamba muaelekeo uliyo mkubwa zaidi kuhusu mauaji ya Ali ni kuwa yalitokana na njama za Mu'awiya zilizotekelezwa na jasusi wake, Al-Ash'ath bin Qais, akishirikiana na Ibn Muljam kisha wakatupiwa mzigo wa mauaji hayo wale walioitwa *Khawarij* ilhali hakuna uthibitisho wowote wa kihistoria kwamba wao walihusika. Bali kinyume chake, uthibitisho wa kihistoria unaonesha kinyume na hivyo, kwani Al-Mas'udi – kama tulivyosema kabla – anaeleza kwamba: "Na wengi miongoni mwa *Khawarij* wanajitenga na Ibn Muljam kwa sababu ya kumuua kwake (Ali) kwa kumdoea".[793]

---

790 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 254. Ama Ibn A'atham – kama kawaida yake – kisa hiki kakipotosha na akasema kwamba Ibn Muljam usiku huo alilala nyumbani kwa Qatam. Ibn A'atham, *Al-Futuh* j. 4, uk. 139, na kuna mambo mengi ya ajabu ajabu katika masimulizi yake. Lakini pia inawezekana kuwa kachanganyikiwa kwa sababu ya riwaya inayosema kuwa Qatam usiku huo alifanya itikafu katika msikiti huo aliouliwa Ali, na kwamba Ibn Muljam na Shabib walikwenda hapo. Al-Mas'udi *Al-Muruj* j. 2, uk. 539.

791 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 254. Na Al-Mubarrad, *Al-Kamil* j. 2, uk. 624, kwa mukhtasari sana. Al-Mas'udi *Al-Muruj* j. 2, uk. 540. Ibn Sa'ad ,*Al-Tabaqatu Al-Kubra* j. 3, uk. 25-26.

792 - Al-Mas'udi, *Al-Muruj* j. 2, uk. 212.

793 - Al-Mas'udi, *Al-Tanbihu Wa Al-Ishraf* uk. 273.

Anasema Sheikh Al-Sabi'i: "Na ikiwa ibara hii (Isemayo: kwa sababu ya kumuua kwake (Ali) kwa kumdoea) itamaanisha kwamba *Al-Muhakkima* au *Al-Khawarij* waliridhika kwa kuuliwa Al-Imamu Ali lau hayakuwa mauaji hayo ni ya kumdoea, basi msimamo wa pili hauungi mkono (ibara) hio, nayo ni kauli ya Abi Sufyaan, Mahbub bin Ruhail Al-Qurashi – miongoni mwa Maulamaa wakubwa wa Kiibadhi mwishoni mwa karne ya pili A.H. – alipoulizwa kuhusu Ibn Muljam, alisema: "Sikupata kumsikia yeyote akimsifu wala akimponda, na hakikunifikia chochote kuhusu yeye. Akaambiwa: 'Labda ni kwa sababu ya kuumua (Ali) kwa kumdoea. Akasema *"Laa"* (si hivyo)".[794]

Ninasema: bali maneno yasemayo: "Kwa sababu ya kumuua kwake (Ali) kwa kumdoea" yanaonesha pia kutokuwepo kushirikiana baina ya Ibn Muljam na Watu wa Nahrawaan, kwani hakukuwa na njia nyengine ya kumuua Ali isipokuwa hio, sasa kama hio hawakuridhika nayo basi ni wazi kwamba wao hawakushiriki katika tukio hilo.

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

1) Tulichokitazama hapa ni suala la kuuliwa kwa Al-Imam Ali (k.w.).
2) Aliyemuua ni mtu aitwaye Abdul-Rahman bin Muljam Al-Muradi.
3) Waandishi wengi wanadai kuwa Ali kauliwa na *Khawarij*.
4) Lakini wakati huo huo riwaya wanazozitegemea waandishi hao zinaonesha kwamba njama hizo za kumuua Ali zilipangwa kwa siri baina ya watu watatu tu. Na hili linatufanya tujiulize:
   a) Vipi watu waliweza kukijua kisa hicho kwa ufasaha wa kutosha namna hio kama njama hizo zilipangwa kwa siri. Maelezo ya Al-Mas'udi katika *Muruju Al-Dhahab* yanasema kwamba yule ambaye alikusudia kumuua Amru bin Al-'Aas huko Misri ndiye aliyeshikwa na kutoa siri hio. Ninasema: hii ina maana kwamba kisa hiki kimepatikana kwa njia ya Amru bin Al-'Aas. Na kama ni hivyo, basi huu ni ushahidi

794 - Al-Barraadi, *Al-Jawahir* uk. 145.

tosha kwamba hiki ni kisa cha uwongo kilichotungwa ili kuufunika ukweli wa aliyemuua Ali. Na hili lilikuwa ni jambo rahisi kwa mtu kama Amru bin Al-'Aas na Mu'awiya kwani dola ilikuwa mikononi mwao; chochote wanachokitaka kukieneza basi wanakieneza kiurahisi kabisa.[795]

b) Hii ina maana kwamba hata kama kweli Ibn Muljam alikuwa ni mwenye fikra na itikadi sawa na za Watu wa Nahrawaan basi bado kitendo hicho cha kumuua Ali kilikuwa ni kitendo chake binafsi, ndio maana akafanya aliyoyafanya kwa siri na akawaficha hata hao walioitwa kuwa ni *Khawarij* wenzake kama riwaya inavyosema. Kwa hivyo, kwa makadirio yoyote yale utayoyakadiria katika kisa hiki, natija utakayoibuka nayo ni kuwa Watu wa Nahrawaan wako mbali na jukumu la damu ya Ali. Na ndio maana ikawa vitabu vinaeleza kwamba Abu Bilal – miongoni mwa waliosalimika katika vita vya Nahrawaan – na wengine walioitwa kuwa ni *Khawarij* walikuwa wakijitenga na Ibn Muljam, yaani wakimchukia.

5) Dalili nyengine zinaonesha kuwa kuna muelekeo mkubwa kwamba Ali kauliwa kwa njama za Mu'awiya, kwani usiku aliouliwa Ali, Al-Ash'ath bin Qais alikuwa pamoja na Ibn Muljam na ilipoingia alfajiri akawa anamuhimiza akimwambia: "Asubuhi itakufedhehesha simama". Na Al-Ash'ath bin Qais huyu alikuwa ni jasusi wa Mu'awiya kwa ushahidi ambao tumeuelezea kabla.
6) Na kwa hivyo, utaona kwamba dai la kuwa Ibn Muljam alikuwa miongoni mwa watetezi wa Watu wa Nahrawaan, si dai sahihi. Na hili liko wazi, kwani kushirikiana kwake na Al-Ash'ath bin Qais kunalifanya dai hilo lisiwe na muelekeo kabisa. Utakumbuka kwamba Al-Ash'ath bin Qais alikuwa pamoja na Ali katika vita dhidi ya Watu wa Nahrawaan. Hii ina maana kwamba Al-Ash'ath bin Qais alikuwa ni adui wa Watu wa

795 - Kumbuka tuliyoyasema huko nyuma kwamba katika zama za utawala mfupi wa Al-Hasan bin Ali, Mu'awiya alikuwa akituma majasusi wake waeneze propaganda za uwongo huko Iraki. Tazama Al-Ya'aqubi, *Al-Taarikh* j. 2, uk. 214. Kwa hivyo, uenezaji wa propaganda za uwongo halikuwa jambo geni katika siasa ya Mu'awiya.

Nahrawaan, na kwa hivyo haiwezekani tena kuwa ashirikiane na Ibn Muljam kwa chochote kile lau Ibn Muljam – kama riwaya zinavyosema – alikuwa ni mwenye msimamo na itikadi za Watu wa Nahrawaan na ni mtetezi wa Watu wa Nahrawaan. Hii ni kusema kwamba lau ilikuwa hivyo, basi Al-Ash'ath bin Qais angelikuwa ni adui kwa Ibn Muljam sawa na alivyokuwa Ali, na kwa hivyo hawawezi watu wawili hao kushirikiana bali Ibn Muljam – kama kweli alikuwa ni mmoja wa Watu wa Nahrawaan au ni mtetezi wao na kwamba kafanya hivyo ili kulipiza kisasi kwa kuuliwa watu hao – basi kwanza angelimuanza Al-Ash'ath ambaye ndiye adui mkuu wa watu hao. Lakini hatimae tunaona kwamba Ibn Muljam na Al-Ash'ath bin Qais wanashirikiana katika kumuondoa Ali duniani; ni wazi kwamba:

a) Yasemwayo kwamba Ibn Muljam alikuwa ni katika watu waliokuwa na rai za Watu wa Nahrawaan, hayana ukweli, bali ni katika kuukwepa ukweli.
b) Ibn Muljam alikuwa na msimamo sawa na wa Al-Ash'ath bin Qais, na hii ina maana kwamba wote walikuwa ni wajumbe kutoka kwa Mu'awiya, hususan utapojua ukweli kwamba miongoni mwa wafuasi wa Ali wa wakati huo wako waliomtuhumu Mu'awiya kwa mauaji hayo kama tulivyonukuu kabla; ongezea na kitendo cha kuchukizwa kwa Watu wa Nahrawaan na kitendo hicho cha mauaji ya Ali na kufurahishwa kwa Mu'awiya na kitendo hicho, utapata natija safi na iliyowazi

SURA YA TISA

MASAHABA WA NAHRAWAAN

UTANGULIZI

Ni muhimu kujua kwamba miongoni mwa Watu wa Nahrawaan – ambao historia imewapachika jina baya la *Ukhawarij* – walikuwemo Masahaba wengi wa Mtume (s.a.w.). Umuhimu huu unakuja katika kutupatia maarifa zaidi juu ya mzozo huu ambao ulikuwa baina ya Masahaba wenyewe kwa wenyewe. Kwa wale ambao wana itikadi kwamba Masahaba wote ni waadilifu au kwa uchache ni *Mujtahidun* na kwa hivyo tusiwaseme kwa ubaya katika mule walimoteleza, basi watakuwa wamejua – baada ya kugubikwa kwa muda mrefu na propaganda za Banii Umayya – kwamba kumbe katika Watu wa Nahrawaan kuna Masahaba wengi, na kwa hivyo:

Mosi: Ama iwe Watu wa Nahrawaan ndio waliokuwa katika makosa katika mizozo hio. Ikiwa ni hivyo, basi kwa uchache tuache kuwasema kwa ubaya kama misingi yetu ya itikadi inavyosema kwamba Masahaba wote ni waadilifu na ni Mujtahidun: waliokosea walikosea lakini walikusudia kutafuta kheri,[796] na kwa hivyo "Haijuzu kumtukana hata Sahaba mmoja"[797] na ni wajibu "Kuzisalimisha nyoyo na ndimi kwa Masahaba wa Mtume (s.a.w.)"[798] "Na wala hatumchukii yeyote miongoni mwao"[799] "Na kuwachukia wao (Masahaba) ni ukafiri na unafiki na kuasi".[800] "Waombee (Masahaba) rehema na utaje fadhila zao

796 - Tazama Sheikh Ibn Baz,*Al-Aqidatu Al-Sahiha Wa Nawaqidhu Al-Islam* uk. 20.
797 - Ibn Taymiyya, *Minhaju Al-Sunna* j. 2, uk. 225.
798 - Ibn Taymiyya, *Al-'Aqidatu Al-Wasatiyya* uk. 25. Na mfano wake ni maneno ya Abu Zur-a Al-Razi kama alivyomnukuu Sh. Muhammad bin Yusuf katika *Hayatu Al-Sahaba* uk. 7, kutoka katika *Al-Kifaya* cha Al-Khatib Al-Baghdadi, uk. 97.
799 - Sadru Al-Din Al-Hanafi, *Sharhu Al-'Aqidatu Al-Tahawiyya* uk. 466.
800 - Sadru Al-Din Al-Hanafi, *Sharhu Al-'Aqidatu Al-Tahawiyya* uk. 466.

na ujizuiye kutokana na (kutaja) walimoteleza. Wala hatumtaji yeyote miongoni mwao ila kwa kheri."[801]

Na hivyo ndivyo Sayyidna Ali mwenyewe alivyokuwa akiwaona watu hao wa Nahrawaan kwamba ni watu wema waliokosea;[802] wakati Ali huyo huyo akimuona Mu'awiya kuwa ni muasi na muovu, kama riwaya yake inavyosema.[803]

Pili: Au wawe wao ndio waliokuwa katika haki, basi hapa ni wajibu wetu wa Kisheria na ni jukumu letu kuwaunga mkono na kuwatangaza kuwa wao ndio waliokuwa katika haki.

Hayo ni kwa msingi wa wale wenye itikadi kwamba: "Masahaba wote ni waadilifu na ni Mujtahidun: waliokosea walikosea lakini walikusudia kutafuta kheri". Ama wale ambao hawatazami Sahaba wala asiyekuwa Sahaba, basi na-watazame tu katika mizozo hio nani alikuwa na hoja zilizokwenda sambamba na Qur-ani na Hadithi; na nani kaenda kinyume na mambo mawili hayo au kaenda kinyume na moja ya mambo mawili hayo. Aliyeifuata Qur-ani au Hadithi sahihi ndiye wakuungwa mkono yeyote yule awaye bila kutazamwa kabila, nasaba wala jengine lolote lile. Huu ndio wajibu wa kila anayetarajia rehema za Mola wake.

Ama kuhusu Masahaba ambao walimuacha mkono Ali – baada ya kukubali sulhu – na kwenda Harauraa na baadae kwenda Nahrawaan na ambao baadae waliitwa kuwa ni *Khawarij*, bila shaka – kiakili – watakuwa ni wengi. Ama kwa upande wa kiakili ni kuwa vita baina ya

---

801 - Al-Barabahari *Sharhu Al-Sunnah* uk. 68-69.

802 - Na wao wakimuona Ali kuwa ni mtu mwema aliyekosea.

803 - Kama Ali alivyosema: "Musiwaue *Makhawarij* tena baada yangu, aliyeitafuta haki akakosea si kama aliyeitafuta batili (kwa kukusudia)." Aliyetafuta haki akakosea – kwa mtazamo wa Ali – ni watu wa Nahrawaan; na aliyetafuta batili kwa kukusudia – kwa mtazamo wake – ni Mu'awiya. **Ninasema:** na watu wa Nahrawaan nao wanaona hivyo hivyo alivyokuwa akiona Ali; nao wanaona kwamba Ali ni aliyetafuta haki akakosea, na Mu'awiya ni aliyetafuta batili kwa kukusudia. Halkadhalika Al-Hasan mtoto wa Ali, alikuwa akiwaona hao walioitwa kuwa ni *Khawarij* kwamba ni bora zaidi kuliko Mu'awiya, na kwa hivyo baada ya Al-Hasan kukubali kujiuzulu na kumpa Ukhalifa Mu'awiya, Mu'awiya alimtaka Al-Hasan akapigane na walioitwa *Khawarij*, naye akamjibu: "Nipigane na watu kwa ajili yako, nawe *Wallahi* ni bora zaidi kukupiga kuliko wao". Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 2, uk. 622.

Ali na Mu'awiya vilishirikisha Masahaba wengi sana. Na wote – *taqriban* – walikuwa upande wa Ali:[804] upande wa Mu'awiya ulikuwa na Masahaba wachache sana, inasemakana kwamba upande huo haukuwa na Masahaba wa Kiansar (wa Madina) isipokuwa wawili tu: Nu'uman bin Bashir na Maslama bin Mukhallad.[805] Mizozo ilipotokea katika jeshi la Ali baada ya kuja suala la sulhu, wengi walioipinga sulhu walikuwa ni wale walioitwa kuwa ni *Quraa* (Wasomi) kama tulivyoelezea katika riwaya nyingi. *Quraa* (Wasomi) – kwa lugha ya wakati huo – ni wanavyuoni, na aghlabu yao walikuwa ni Masahaba. Na hao waliopinga sulhu ndio ambao walijitenga na Ali na kwenda Harauraa na baadae wakenda Nahrawaan. Hii ni kusema kwamba wengi wa hao waliojitenga na Ali na kwenda Harauraa na baadae wakaenda Nahrawaan walikuwa ni Masahaba au – kwa uchache – ndani yake mulikuwa na Masahaba wengi. Na hii ni tafauti kabisa na waandishi wa makala wa mrengu wa Banii Umayya na wapambe wa Ali wanavyotaka kuupotoa ukweli huu na kuonesha kuwa waliojitenga na Ali ni Mabedui wasiojua chochote. Na hili ni kama lile tukio la kuuliwa Uthman: Uthman aliuliwa na Masahaba wenzake – kama tulivyobainisha kabla – kisha watu wakalipindua tukio hilo na kudai kwamba Uthman kauliwa na

---

804 - Anasema Al-Ash'ath bin Qais katika riwaya ya Ibn A'atham: "Hakika ya Masahaba wa Muhammad (s.a.w.) wako pamoja na sisi, na katika sisi kuna Masahaba wa Badri na Masahaba wa Al-'Aqaba". Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 74. Na anasema Abu Nuh – aliyekuwa katika jeshi la Ali katika vita vya Siffin – kumwambia Amru bin Al-'Aas: "Hakika pamoja nasi kuna Masahaba wa Mtume (s.a.w.) na wote wako tayari kukupigeni nyinyi". Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 119. Na anasema Al-Ash'ath bin Qais – aliyekuwa katika jeshi la Ali – kumjibu Mu'awiya bin Khudaij – aliyekuwa katika jeshi la Mu'awiya – kuhusu Ali kwamba: "Na (Ali) wamemchagua Muhajirin na Ansar, nawe unapigana nami (ukiwa pamoja) na mtu ambaye wamemfanya Khalifa watu wa Sham: hawana haki ya (kuchagua) ukhalifa wala (ya kufanya) Shura". Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 276. Na inasema riwaya kwamba ujumbe wa Mu'awiya ulipofika kwa Ali uliikuta Majlisi yake: "Imezama (imezungukwa) kwa Muhajirina na Ansar". Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 284. 116. Anasema Abdullah bin Budail kumwambia Ali huko Siffin: "Watu wa busara na Qur-ani wako pamoja nawe". Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 105.

805 - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 180-181, na uk. 281. Lakini dhahir ya riwaya ya Al-Baladhiri katika *Al-Ansab* j. 3, uk. 76, ni kuwa Ka'ab bin 'Ujra Al-Ansari pia alikuwa katika kambi ya Mu'awiya, lakini labda yeye hakushiriki katika vita au labda hilo halikuthibiti kwani Ibn Hajar katika *Al-Isaba* na katika *Al-Tahdhib* kamtaja bila ya kutaja habari hio.

mabedui[806] na viongozi wa *Khawarij*[807] kwa njama za Ibn Saba-a![808] Wakati riwaya zinasema kwamba waliomuua Uthman ni Masahaba na

[806] - Na hili ndilo tatizo la waandishi wengi wasio na khofu ya siku ya Kiyama: wanapong`ang`ania msimamo fulani basi wao huwa hawaoni tabu kusema uwongo na kuwazulia wapinzani wao mambo ya kutunga. Kwani ukweli hautoshi kubainisha haki? Mfano mmoja ni suala la waliomuua Uthman bin Affan, Khalifa wa tatu. Watu wanatunga vitabu wakizua kwamba waliomuua ni mabedui wa miji tafauti, na wengine husimulia kisa cha uwongo cha Ibn Saba-a kilichosimuliwa na Saif bin Umar, msimulizi mwongo. Wakati Uthman kauliwa na Masahaba wenzake wa Madina kwa sababu ya baadhi ya mambo aliyoyafanya nao wakampinga kwayo na wakamtaka ajiuzulu naye asikubali. Jiulize wewe ikiwa Uthman kauliwa na Mabedui au kwa njama za Ibn Saba-a, Masahaba waongofu na wafuasi wao walikuwa wapi wakati Uthman kabla ya kuuliwa alizingirwa zaidi ya mwezi mmoja mbona hawakuja kumuokoa nao walikuwa wengi sana, na wengi wao walikuwa Madina. Anasema Abdul-Rahman bin Ghanam Al-Ash'ari kumwambia Abu Huiraira (r.a) na Abu Al-Dardai (r.a.): "Ajabu ya nyinyi! Munamjia Ali munataka akupeni waliomuua 'Uthman na tunajua kwamba Muhajirina na Ansar walikuwa wapo Madina wamehudhuria siku aliyouliwa Uthman nao hawakumnusuru wala hawakumtetea". Tazama Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 97. Na akataja Ibn A'atham katika *Al-Futuh* j. 3, uk. 123, maneno ya Ammar bin Yasir akimwambia Amru bin Al-'Aas kwamba: "Je unajua kwamba Uthman bin Affan watu wengine walimuacha mkono na wengine wakahimiza dhidi yake (ili auliwe); hakuna kati yao aliyemnusuru kwa mkono wake wala aliyekataza (watu) kutokana na yeye kwa ulimi wake, na alizingirwa nyumbani kwake siku arubaini…". Anasema Sahaba Al-Nnu'uman bin Bashir – aliyekuwa katika jeshi la Mu'awiya siku ya vita vya Siffin – kuwaambia Ansar wenzake waliokuwa katika jeshi la Ali: "…Enyi Ansar! Mumekosea kwa kumuacha mkono Uthman *Yaumu Al-ddaar* (siku aliozingirwa naye yumo katika nyumba yake)." Nao wakamjibu: "….Uthaman kaachwa mkono na waliobora zaidi kuliko wewe na baba yako……..Tazama Muhajirina na Ansar wako wapi (wako pamoja na nani (Ali au Mu'awiya)". Tazama Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 280-281. Anasema mfuasi wa Ali aitwaye Hashim kumjibu mfuasi wa Mu'wiya siku ya vita vya Siffin: "(Uthman) wamemuua Masahaba wa Mtume (s.a.w.) na watoto wa Masahaba wake na wasomi wa watu (wote) nao ndio watu wa dini na elimu". Tazama Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 665. Na katika vita vya Jamal, Ali alisema kuwa hao waliodai damu ya Uthman ndio waliomuua. Tazama Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 37. Anasema Sahibu yangu Sheikh Hafidh Al-Sawwaafi katika kitabu chake juu ya historia ya Ibadhi: "Matamanio ya nafsi yamefanya kazi kubwa, hata kutungwa kisa hiki kuwa ni mkasa ulioandaliwa na Abdullahi bin Sabai, na kuwa wao ni wafuasi wa Ibn Sabai na ndio waliokuwa *Khawarij* baadae; lakini je unawajua hao waliomuua Othman? Baadhi yao ni hawa: 1) Malik bin Harith maarufu kwa Al-Ashtar. Amemtaja Ibn Hibaan kuwa ni wa kuaminiwa katika Matabiina, na amesema Al-Imamu Ali (k.w.): *"Amrehemu Allah Malik; hakika alikuwa kwangu mimi kama nilivyokuwa kwa Mjumbe wa Allah."* 2) Thabit bin Qais bin Khatim bin Uday; amemtaja Ibn Shaahin kuwa ni katika Masahaba, na huyu alijeruhiwa siku ya Uhud majeraha 12 na akaitwa tokea siku

wafuasi wao akiwemo Ammar bin Yasir na Muhammad bin Abi Bakr Al-Siddiq.[809]

Naturudi katika suala la Masahaba waliokuwemo katika Watu wa Nahrawaan. Tunasema: Ama kuhusu riwaya zilizosema au kuonesha kuwemo kwa Masahaba miongoni mwa watu hao ni nyingi kama tutavyobainisha katika maelezo yajayo. Kwa hapa tunatoa ithbati ya hayo kutoka katika riwaya ya Ibn Abbaas ambaye anawaelezea watu wa Nahrawaan kuwa siyo tu kuwa ni Masahaba, bali ni Masahaba wa awali, Masahaba wacha Mungu, Masahaba wanavyuoni. Inasema riwaya yake: "Wao Wallahi ni jino la mwanzo katika Masahaba wa Muhammad, Wao Wallahi ni watu wa *Baranis (kofia refu)*[810] na viguzo."[811] Maneno ya Ibn Abbaas aliposema: "Wao Wallahi ni jino la mwanzo katika Masahaba" maana yake ni kuwa wao ndio Masahaba wa awali; maneno yasemayo: "Wao Wallahi ni watu wa *Baranis* na viguzo" maana yake ni kuwa walikuwa *('Ulamaa, 'Ubbad, Zuhhad)* wanavyuoni, wenye kuabudu wenye

---

hio na Mtume (s.a.w) Haasir, na Ali alimtawalisha awe Liwali (Gavana) wa Madain akaendelea mpaka akaondolewa na Mughira siku za Mu'awiyah. 3) Jundub bin Zuhair Al-Ghamidi. Huyu ni mmoja katika Masahaba wa Mtume (s.a.w). 4) Jundub bin Kaab Al-Azdi; huyu ni Jundub L-khair aliyemuua mchawi, na huyu ni katika Masahaba Muhajirina. 5) Hakim bin Jibilah Abadiy; ni katika Masahaba vile vile. 6) Hamrani bin Aban; amesema Yahya bin Ma'in: Hamran ni tabii wa watu wa Madina na muhaddithi wao. 7) Zaid bin Suhaan Abadi; ni ndugu wa Sa'a-sa'ah bin Suhaan, alisilimu wakati wa Mtume(s.a.w.) na alikuwa Sahaba. 8) Sa'a-sa'ah bin Suhaan; ni katika Masahaba wa Mtume (s.a.w). 9) Abdul-Rahman bin Udais Al-Balawi; ni mmoja katika Masahaba walioshuhudia Baiatu Ridhwaan, na yeye ndiye aliyekuwa kiongozi wa jeshi lilokuja kutoka Misri katika kumuondosha Othman. 10) Uday bin Hatim bin Abdillah Ataai; alisilimu katika mwaka wa tisa, na yeye alithibiti katika Uislamu kweli kweli. 11) Urwah bin Jaad, na wengine wanamwita Ibn Abi Jaad, na huyu ni katika Masahaba, na yeye ndiye aliyetumwa na Mtume (s.a.w) aende akamnunulie mbuzi kwa dinari moja, akanunua kwa dinari hio mbuzi wawili.

807 - Ibn Kathir *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya* j. 7, uk. 228. Ajabu ilioje hii! Wakati huo hata harakati za hao walioitwa Khawarij hazijaanza. Lakini Khawarij wenyewe ndio hao tuliowataja kabla. Huu ndio uchambuzi wa Ibn Kathir! *Wallahu Al-musta'aan.*

808 - Wakati hakuna kamwe riwaya sahihi kuhusu suala la Ibn Saba-a.

809 - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 95.

810 - Neno *baranis* ni wingi wa neno *Burnus,* nalo lina maana si chini ya tatu: 1) kofia refu 2), nguo yoyote ile ambayo imeungana na kofia yake 3), nguo za kuvaa baada ya kukoga zenye mikono mipana. Lakini dhahir ni kuwa maana ya mwanzo ndio iliokusudiwa hapa.

811 - Tazama Ibn Abi Shaiba *Al-Musannaf* j. 8, uk. 727, riwaya na. 37.

kuipuuza dunia: "Watu wa Baranis" yaani ni wenye kuvaa kofia refu ambazo ni kivazi cha watu wema. "Watu wa viguzo" yaani kila wakati wameegemea nguzo za msikiti wanasoma Qur-ani. Huu ni ushahidi kutoka kwa Ibn Abbaas, *Wamaa Adraka Maa Ibn Abbaas* (Na nini kinachokujuilisha Ibn Abbaas ni nani).[812]

Halkadhalika mmoja wa majasusi wa Mu'awiya aliyekuweko Iraki, baada ya Ali kuwapiga Watu wa Nahrawaan, alimpelekea Mu'awiya barua akimwambia: "Wametokana na Ali wafuasi wake na wale wenye kuabudu miongoni mwao, basi akawaendea akawaua, basi kwa hakika jeshi lake limemuharibikia".[813]

Baada ya haya utaona kwamba hoja za kiakili na kimaandishi zinaonesha kuwa Watu wa Nahrawaan (r.a.) walikuwa ndio Masahaba Maulamaa; na ndio Masahaba wacha Mungu. Na utakapolifahamu hili, basi utakuwa umefahamu kwamba kuitwa Masahaba hao kuwa ni Mabedui, *Makhawarij* n.k, kumetokana na sababu mbili kuuu:

Sababu ya kwanza: ni siasa za chuki za Banii Umayya na wapambe wa Ali. Banii Umayya wao walikuwa wakilinda mkate wao na kwa hivyo maslahi yao yalikuwa ni kumpiga vita kila mpinzani kwa upanga na kwa kumuenezea sumu katika jamii. Ndio maana waliwaua wajukuu wa Mtume (s.a.w.) na kuanzisha siasa ya chuki dhidi ya Ali na wakaanzisha Sunna ya kumlani katika membari.

Ama wapambe wa Ali, wao walijifunza na wanaendelea kujifunza kujenga uadui na kila asiyekubaliana na Ali katika jambo lolote lile bila

812 - Ama riwaya inayomnukuu Ibn Abbaas akisema kuwambia watu wa Nahrawaan kwamba: "Nimekujieni kutoka kwa Muhajirina na Ansar na kutoka kwa Bin-Ami yake Mtume (s.a.w.) wala hakuna yeyote miongoni mwenu" ni riwaya ya kutunga bila shaka, kwani Masahaba waliokuwa katika Watu wa Nahrawaan (r.a.) wametajwa baadhi yao kwa majina kama tutavyoeleza *Inshaa Allah*. Kwa hivyo, riwaya sahihi ya Ibn Abbaas ni hio isemayo: "Wao Wallahi ni jino la mwanzo katika Masahaba wa Muhammad, Wao Wallahi ni watu wa *Baranis (kofia refu)* na viguzo."

813 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 3, uk. 156-157. Naam! Ali baada ya kuwauwa watu hao hakuwa na nguvu tena za kijeshi, akabaki kujuta na kusema: "Wako wapi waabuduo wakati wa usiku; na simba wa mchana". Ali Yahya Muammar, *Al-Ibadhiyya Baina Al-Firaq* j. 2, uk. 211.

kutafuta na kutafakari vyema katika jambo hilo haki iko wapi. Msimamo huu uliwapelekea kuwatungia wapinzani wao maelfu ya riwaya za uzushi na pia kuzikanusha riwaya kadha sahihi za fadhila za Masahaba wengine, kama vile ambavyo msimamo huo uliwapelekea kuzua itikadi ya *'isma* ya Maimamu wao.[814]

Sababu ya pili: ni kuwa hayo makundi ya *Khawarij* wa kweli hasa – kama *Al-Azaariqa* na wengine – yalikuwa yakiafikiana na Watu wa Nahrawaan katika suala la kupinga sulhu. Kwa hivyo, watu wakachanganya baina ya hawa na wale na wakawapa wale hukumu ya hawa – wakawaita wote kuwa ni *Khawarij*. Na kukubaliana katika fikra moja juu ya maudhui fulani, hakuzifanyi madhehebu tafauti kuwa ni moja. Al-Hasan bin Abi Al-Hasan Al-Basri – kwa mfano – ni miongoni mwa wanavyuoni waliosemwa kuwa walikuwa wakiipinga sulhu, na ikawa akimtaja Ali husema: "Kwanini unafanyisha sulhu nawe ndiye mwenye haki, basi husongi mbele (ukaendelea na vita)".[815] Lakini pamoja na hayo, Al-Hasan huyu alikuwa na rai tafauti na walioitwa *Al-Khawarij*.[816] Katika Mashia kulikuwa na vikundi ambavyo vilikuwa vikisema kwamba eti Mungu ni Mtume Muhammad naye kagawika sehemu tano: Mtume Mwenyewe, Ali, Fatima, Hasan na Husain.[817] Shia wa kawaida wanakubalina na vikundi hivyo katika ubora wa Ali, lakini je vikundi hivyo baada ya kuwa na itikadi hizo wanahesabiwa kuwa ni Shia tena? Au je tutakapozungumzia Shia tutoe mifano ya watu kama hao? Ahmadiya au Kadiyani asili yao ni Sunni, lakini je baada ya kuzua waliyoyazua bado wanaendelea kuwa Sunni? Kwa hivyo, mtu kuwa ni mfuasi wa madhehebu fulani ni kitu kimoja na kuwa yeye asili yake ni madhehebu hio au kakubaliana nao watu wa madhehebu hio katika fikra fulani ni kitu chengine. Al-Azaariqa na wengine ambao waliitwa

---

814 - Yaani itikadi ya kudai kwamba Maimamu wao – kuanzia Sayyidna Ali – hawakosei wala hawatendi dhambi!

815 - Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 2, uk. 608.

816 - Ama Al-Imamu Malik yeye katajwa kuwa miongoni mwa wenye rai za walioitwa kuwa ni *Khawarij*. Inasemekana kwamba alikuwa akiwataja Uthman, Ali, Talha na Zubair kisha akisema: "Wallahi hawakupigania isipokuwa *tharid* ya paa". Tharid ni mkate uliochanganywa na nyama, yaani walikuwa wakipigania dunia. Tazama Al-Mubarrad *Al-Kamil* j. 2, uk. 608. **Ninasema:** hata Ibn Abbaas kamwambia Ali maneno hayo hayo katika vita vyake na watu wa Nahrawaan.

817 - Ahmad Al-Kaatib, *Tatawwuru Al-Fikr Al-Siyasiy Al-Shi'iy* uk. 260-261.

khawarij, walikubaliana na Watu wa Nahrawaan katika suala la kupinga sulhu, lakini walizua mambo ambayo yamewatoa katika kuzingatiwa kuwa miongoni mwa wafuasi wa Watu wa Nahrawaan au kuwa ni warithi wa fikra sahihi za Watu wa Nahrawaan.

Sasa baada ya utangulizi huu mfupi na-tutazame majina ya baadhi ya Masahaba waliokuwa miongoni mwa Watu wa Nahrawaan. Sehemu hii ya utafiti wa majina ya Masahaba hao nimeunukuu kiukamilifu kutoka katika kitabu *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* cha Sheikh wetu Nassir Al-Sabi'i.

MAJINA YA MASAHABA WA NAHRAWAAN

1) ZAID BIN HISN (AU HUSAIN) AL-TAI. Huyu katajwa na idadi kubwa ya wanahistoria kuwa ni miongoni mwa Watu wa Nahrawaan.[818] Na Abu Al-Mu-uthir na Al-Baradi wakamuhisabu kuwa ni miongoni mwa Masahaba,[819] kama vile Ibn Hajar alivyomtaja (pia) katika sehemu ya kwanza[820] ya kitabu chake *Al-Isaba* kwa kutegemea kile kilichotajwa na Al-Haitham bin Adey kwamba (Zaid bin Hisn au Husain Al-Tai huyu) alikuwa Liwali (Gavana) wa Umar bin Al-Khattab katika mipaka ya Al-Kufa (Iraki),[821] na ameyataja hayo pia Ibn Hibban katika *Al-Thiqat*[822] na Al-Baradi.[823] Amesema Ibn Hajar: "Na nimetanguliza

818 - Ibn Ghailan, *Al-Siyar* karatasi ya 161 (bado kuchapishwa). Abu Al-Mu-uthir ,*Al-Siyar* j. 2, uk. 313. Al-Baladhiri ,*Al-Ansab* j. 3, uk. 147. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 101-102-115-117-121-122-148. Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 51-53.

819 - Abu Al-Mu-uthir, *Al-Siyar* j. 2, uk 313. Al-Baradi ,*Al-Jawahir* uk. 118.

820 - Kawagawa Ibn Hajar Al-'Asqalani sehemu nne wale aliowataja katika *Al-Isaba Fii Ma'arifat Al-Sahaba*

Ya kwanza: yule ambaye Usahaba wake umepokewa au katajwa pamoja na kitu chenye kuonesha Usahaba (wake) kwa njia yoyote ile iwayo.

Ya pili: aliyezaliwa katika zama za Mtume (s.a.w.) na akawa hajafikia umri wa kupambanua mambo wakati Mtume(s.a.w.). anafariki dunia

Ya tatu: aliyewahi wakati wa kijahilia na wala haikupokewa kwamba kakutana na Mtume (s.a.w.); na hawa si Masahaba kwa makubaliano (ya wote).

Ya nne: aliyetajwa kuwa miongoni mwa Masahaba kwa njia ya dhana na makosa.

821 - Ibn Hajar, *Al-Isaba* j. 2, uk. 603.

822 - Ibn Hibban, *Al-Thiqat* j. 2, uk. 295.

823 - Al-Baradi, *Al-Jawahir* uk. 129.

(maelezo) zaidi ya mara moja kwamba katika zama hizo (za Umar bin Al-Khattab) walikuwa hawawapi uongozi ila Masahaba".[824]

2) HURQUS BIN ZUHAIR AL-SA'ADI, AL-TAMIMI: Idadi (kubwa) ya watu wa historia wamemtaja kuwa ni miongoni mwa walioiuliwa katika Watu wa Nahrawaan.[825] Lakini inafahamika kutokana na yale aliyoyanukuu Ibn Hajar kutoka kwa Al-Haitham bin Adey kwamba *Khawarij* wanadai kwamba Hurqus ni miongoni mwa Masahaba na kwamba aliuliwa siku ya (vita vya) Nahrawaan. Amesema Al-Haitham: "Basi nikaulizia hilo sikumkuta yeyote amjuae",[826] inafahamika kutokana (na maelezo) haya kwamba Hurqus bin Zuhair huyu si yule Hurqus aliyeuliwa Nahrawaan. Na kwa hivyo, Ibn Hajar amemtaja Hurqus mwengine ambaye (kabila yake ni) Ambari, na akanukuu kutoka kwa Ibn Abi Daud[827] (kauli ya) mkato kwamba yeye (Hurqus bin Zuhair) ndiye *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu) aliyeuliwa Nahrawaan,[828] jambo ambalo linapinga kwamba Hurqus (bin Zuhair) Al-Sa'adi kauliwa katika vita vya Nahrawaan. Na akamuweka Ibn Hajar Hurqus Al-

---

824 - Ibn Hajar ,*Al-Isaba* j. 2, uk. 603. Na tegemeo la Al-Hafidh (Ibn Hajar) katika kuthibitisha Usahaba kwa kidhibiti hiki, ni kile alichokinasibisha kwa Ibn Abi Shaiba kwamba yeye ametoa (riwaya) kutoka katika njia (moja) akasema: "Walikuwa wao hawamfanyi Amiri katika vita isipokuwa Sahaba". (Tazama Ibn Hajar): *Al-Isaba* j. 1, uk. 9. Na kwa hakika nimepekuwa upekuzi wa kuchokesha (nimepekuwa mpaka nimechoka) katika kitabu *Al-Musannaf* cha Ibn Abi Shaiba wala sikuweza kuligundua andiko hilo. Lakini (andiko hilo) linapata ushahidi wa Umar bin Al-Khattab wa kumfanya Abu Ubaid bin Mas'ud Al-Thaqafi kuwa ni Amiri wa vita vya Furs (Iran): Umar alipoita watu kwa muda wa siku tatu, akawa wa mwanzo kuitika ni Abu Ubaid huyu. Akaambiwa Umar: "Eh! Mfanye sahaba kuwa ndiye Amiri" akasema: "Hakika ya mimi namfanya Amiri wa mwanzo aliyeitika mwito; hakika ya nyinyi mumewatangulia watu katika kuinusuru dini hii; na hakika ya huyu ndiye aliyeitika wito kabla yenu". Ibn Kathir *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya* j. 4, uk. 25. Na faida ya tukio hili ni kuwa kwa asili ilivyo ni kuwa wao (Masahaba katika enzi ya Umar walikuwa) hawamfanyi Amiri isipokuwa Sahaba, na kwamba kumfanya Abu Ubaid Al-Thaqafi kuwa ni Amiri ni jambo la nadra (exceptional), na kwa hivyo Umar akalaumiwa (kwalo)".

825 - Ibn Khayyat *Al-Taarikh* uk. 119, Abu Al-Mu-uthir *Al-Siyar* j. 2, uk 313, Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 133-136, Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 2, uk. 497, j. 3, uk. 103-115-121-122, Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 53.

826 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 49.

827 - Ibn Abi Daud ni Abdullah bin Sulaiman bin Abi Daud Al-Sajistani mwenye kitabu *Al-Sunan*, kamtaja Ibn Hajar katika utangulizi wa kitabu chake *Al-Isaba* j. 1, uk. 2, (kuwa ni) miongoni mwa waliotunga (vitabu) juu ya Masahaba.

828 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 170.

Ambari katika sehemu ya tatu, na akataja kwamba yeye ni mwenye kuwahi (zama za Mtume s.a.w.) na kahudhuria ufunguzi (conquering) wa (mji) wa Tustar pamoja na Abu Musa Al-Ash'ari, akasema (Ibn Hajar): "Naye si Hurqus bin Zuhair Al-Sa'adi".[829] Nayo ni maneno yenye kugongana na kile kilichothibiti katika historia kwamba Hurqus aliyeuliwa Nahrawaan ndiye aliyehudhuria ufunguzi (conquering) wa (mji) wa Tustar. Wala hakuna chanzo chochote (kitabu chochote) kinachothibitisha kwamba katika ufunguzi wa Tustar kulikuwa na Hurqus wawili. Ametaja Al-Tabari kwamba 'Utbat bin Ghaz-waan[830] alimuandikia Umar bin Al-Khattab akimtaka kuongeza jeshi (reinforcement), Umar akamtuma Hurqus bin Zuhair Al-Sa'adi na akamfanya kuwa ndiye Amiri wa vita, na Hurqus akafungua (akalitwaa) soko la Al-Ahwaz, akakaa hapo na (mji huo wote) ukawa chini yake mpaka kufikia Tustar; kasema Al-Tabari : "Kisha hakika ya Hurqus huyu *akataharrar*[831] siku ya (vita vya) Siffin na akabakia hivyo hadi akahudhuria Nahrawaan pamoja na Harauriyya[832] (Watu wa Nahrawaan). Nayo ni (maneno) yaliyowazi kwamba Hurqus bin Zuhair Al-Sa'adi ndiye aliyefungua (soko la) Al-Ahwaaz na (mji wa) Tustar na ndiye aliyeuliwa Nahrawaan, lakini siye *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu) maarufu, kama maelezo yatavyokuja.

Baada hayo, (tunakuta kwamba) wanavyuoni wengi wamemuhisabu Hurqus bin Zuhair Al-Sa'adi kuwa ni miongoni mwa Masahaba,[833] na kwa hivyo, Ibn Hajar kamtaja katika sehemu ya kwanza, na akasema

829 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 170.

830 - Alikuwa ni mtu wa saba kusilimu, na akahajiri kwenda Uhabeshi na akahudhuria vita vya Badr na vita vyote ,naye ndiye aliyeupanga (aliyeplan mji wa) Al-Basra na kuuanzisha baada ya Umar kumfanya kuwa Liwali huko. Alikufa mwaka 15 na inasemekana (kuwa alikufa mwaka wa) 17 na inasemwa (mwaka wa) 20 A.H. Al-Dhahabi *Al-Siyar* j. 1, uk. 304-306, Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 4, uk. 438-439.

831 - *Akataharrar* yaani akawa miongoni mwa watu wa Harauraa ambao baadae ndio watu wa Nahrawaan.

832 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 2, uk. 496-497.

833 - Abu Al-Mu-uthir *Al-Siyar* j. 2, uk 313. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 2, uk. 496. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 545. Ibn Al-Athir *Usdu Al-Ghaba* j. 1, uk. 474. Al-Darjini *Al-Tabaqat* j. 2, uk. 202. Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118. Al-Fayrus Abadi *Al-Qamus* j. 2, uk. 309. Al-Zabidi *Al-Taj* j. 4, uk. 379.

kuhusu yeye: "Ametajwa katika ufunguzi wa Iraki",[834] na yatakuja (maelezo) kwamba yeye siye Dhul-Khuwaisara.[835]

3) ABDULLAHI BIN WAHB AL-RASIBI AL-AZDI, DHU AL-THAFANAT.[836] Tumetaja katika utafiti wa mwanzo[837] kwamba yeye *alibaiiwa* na watu wa Nahrawaan kabla ya kutoka kwao Al-Kufa. Na ibara za baadhi ya wanavyuoni zinaashiria kwamba hakuwa Sahaba, ambapo Abu Al-Mu-uthir anawataja Hurqus bin Zuhair na Zaid bin Hisn katika mtiririko wa utajo wa Masahaba wa Mtume (s.a.w.) na anafuatishia (hayo) kwa kauli yake: "Kisha baada yao ni Abdillahi bin Wahb Al-Rasibi".[838] Na Ibn Hajar kamtaja katika sehemu ya tatu akisema: "Ni mwenye kuwahi"[839] yaani kamuwahi Mtume (s.a.w.) na wala haikupokewa kwamba wamekutana. Na akataja Al-Dhahabi kwamba alikuwa ni miongoni mwa waliowahi (zama za) ujahilia.[840] Ama Ibn Hazm, yeye anakataa kuwa Abdullah bin Wahb ni Sahaba,[841] bali alikuwa ni katika "Tabiina wema (wafuasi wa Sahaba wema)".[842] Lakini Al-Tabari anasimulia katika habari za ufunguzi wa (mji wa) Maasabadhaan kwamba Umar bin Al-Khattab alimuandikia Sa'ad bin Abi Waqqas kwamba amtumie jeshi na katika moja ya sehemu zake mbili (za jeshi hilo) amfanye Abdullah bin Wahb Al-Rasibi kuwa ndiye Amiri.[843] Na pamoja na kuwa Ibn Hajar ananukuu kwamba alihudhuria

834 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 49, *tarjama* na. 1663.

835 - Bali kitendo cha Umar cha kumfanya Hurqus kuwa ni amiri-jeshi, kinatosha kutoa ushahidi wa kwamba Hurqus huyu alikuwa ni Sahaba kwani katika zama za Umar – kama alivyosema Ibn Hajar – walikuwa hawawafanyi Maamiri Jeshi isipokuwa Masahaba.

836 - Anasema Ibn Hajar katika *Al-Isaba* j. 5, uk 100: "Na alikuwa ni ajabu katika kuabudu sana mpaka akaitwa *Dhu Al-Thafanat,* alikuwa – kwa sababu ya kusujudu kwake sana – kafanya katika mikono yake na magoti yake kama michuniko ya ngamia (zile sehemu zinazovimba na kupiga weusi katika miguu yake,masuguru)." Tazama pia Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 135.

837 - Yaani utafiti wa mwanzo wa kitabu *Al-Khawarij Wa Al-Haqiqatu Al-Ghaiba* cha Sheikh Nassir Al-Sabi'i ambaye ndiye anayeyasema maneno haya: si utafiti wa mwanzo wa kitabu hiki.

838 - Abu Al-Mu-uthir *Al-Siyar* j. 2, uk 313

839 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 5, uk 100, *tarjama* na. 6364.

840 - Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 4, uk. 96, *tarjama* na. 4308.

841 - Ibn Hazm *Al-Fasl* j. 4, uk. 238.

842 - Ibn Hazm *Al-Jamhara* uk. 386.

843 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 2, uk. 475.

ufunguzi wa Iraki pamoja na Sa'ad bin Abi Waqqas na kwamba alikuwa katika jeshi ambalo Sa'ad (bin Abi Waqqas) alilituma,[844] lakini hakuashiria amri ya Umar aliyompa Sa'ad (bin Abi Waqqas) ya kumfanya Abdullah bin Wahb Al-Rasibi kuwa ndiye Amiri katika moja ya sehemu mbili za jeshi hilo. Na kutokana na yale yaliyotangulia kwamba Abdullah bin Wahb Al-Rasibi kawahi zama za ujahilia na kwa msingi wa kile alichokieleza Ibn Hajar kwamba wao walikuwa wakati huo hawamfanyi Amiri ila Sahaba, basi Abdullahi bin Wahb anahisabiwa kuwa katika Masahaba; na hiki ndicho wanachokisisitiza Al-Darjini[845] na Al-Baradi.[846]

4) SHAJARAT BIN AWFA AL-SULAMI: Al-Baradi na Al-Shammakhi wamemtaja kwamba alihudhuria Nahrawaan na alikuwa Sahaba aliyepigana vita vya Badri.[847]

5) ABDULLAH BIN SHAJARA AL-SULAMI: Ametajwa kuwa ni miongoni mwa waliohudhuria Nahrawaan na: Al-Baladhiri, Al-Tabari na Al-Baradi, na akamuhisabu kuwa miongoni mwa (Masahaba) waliombaii Mtume (s.a.w.) chini ya mti.[848]

6) SHURAIH BIN AWFA (AU BIN ABI AWFA) BIN DHAB'A AL-'ABSI: wamemtaja kuwa miongoni mwa waliohudhuria Nahrawaan: Al-Baladhiri, Al-Tabari na Al-Baradi, [849] na huyu wa mwisho (Al-Baradi) akamuhisabu kuwa ni miongoni mwa (Masahaba) waliombaii Mtume (s.a.w.) chini ya mti,[850] lakini yeye kasema "Al-Sulami" na inaonesha kwamba kamchanganya baina yake na baina ya Shajarat bin awfa Al-Sulami.

---

844 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 5, uk. 100.
845 - Al-Darjini *Al-Tabaqat* j. 2, uk. 201.
846 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118.
847 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118. Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 58.
848 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 133-134-147. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 120-122. Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118.
849 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 133-136-147. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 115-121-122. Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 129.
850 - Yaani Masahaba walioahidiana na Mtume (s.a.w.) chini ya mti ambao wametajwa katika Sura 48, Aya 10, 18.

7) THARMALA (WA KABILA LA BANII HANDHALA). Wamemtaja kuwa miongoni mwa walioliwa Nahrawaan: Al-Jawhari – na akamfanya kuwa ndiye *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu) mwenyewe[851] – na Al-Qalhati na Al-Baradi; na hawa wawili wa mwisho wamemtaja kwamba ni Sahaba.[852]

8) NAFI: Wamemtaja kuwa miongoni mwa waliohudhuria Nahrawaan: Abu Daud, Al-Baladhiri, Al-Tabari, Ibn Hajar, Al-Baradi na Al-Shammakhi.[853] Na hao wanne wa mwanzo wakamfanya kuwa ndiye *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu) mwenyewe anayejulikana kuwa ni *Al-Mukhaddaj* (mlemavu), navyo ndivyo inavyomaanisha nakala ya Al-Baradi na Al-Shammakhi kutoka kwa Jabir bin Zaid Al-Azdi kwamba Nafi "Dume (wa kondoo) kaukata mkono wake".[854] Na Al-Baradi akamuhisabu kuwa ni miongoni mwa Masahaba wa Mtume (s.a.w.) na (kwamba) ni *Maula* (mtumwa mkombolewa_freed slave) wa Tharmala tuliyemtaja kabla.[855] Na labda kuwa kwake ni *Maula* wa Tharmala ndiko kulikomchanganya Al-Jawhari akamfanya kuwa ndiye *Dhu Al-Thudaiyya* (Mwenye kichuchu). Lakini katika Masahaba kuna idadi (kubwa) ya wenye jina la Nafii,[856] ni vigumu kuweza kuainisha ni yupi mwenye *tarjama (biography)* hii.

9) UMAIR BIN AL-HARITH: kamtaja Al-Baradi kuwa miongoni mwa Watu wa Nahrawaan na akamnasibisha na Al-Ansar (Masahaba wa Madina).[857] Na akataja Al-Hafidh Ibn Hajar (watu) wawili ambao majina yao yameafikiana na majina ya baba zao yameshabihiana: wa kwanza ni: Umair bin Al-Harith Al-Ansari, (huyu) alihudhuria (bai'atu) Al-'Aqaba

851 - Al-Jawhari *Al-Sihah* j. 6, mlango wa Al-yaau (Yee) sehemu ya Al-Thaau (Thee) uk. 2291-mlango wa Al-yaau (Yee) sehemu ya Al-Thaau (Thee) uk. 2541.

852 - Al-Qalhati *Al-Kashf* j. 2, uk. 252. Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118.

853 - Abu Daud *Al-Sunan* mlango wa kuwapiga Al-Khawarij riwaya na. 4770. Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 149. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 125. Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118. Ibn Hajar *Nuzhatu Al-Albab* j. 1, uk. 282, nambari 1127. Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 53.

854 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 141. Al-Shammakhi *Al-Siyar* j. 1, uk. 53.

855 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 141.

856 - Ibn Hajar kawataja katika *Al-Isaba* j. 6, uk. 404, Masahaba 22 ambao wana jina la Nafi.

857 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118.

na (vita vya) Badr na (vita vya) Uhud;[858] na wa pili ni: Umair bin Haritha Al-Sulami, Sahaba aliyehudhuria (vita vya) Siffin pamoja na Ali.[859] Na wala si ajabu akawa huyu ni mtu mmoja, kwani **(**Umair) wa mwanzo (kabila yake ni) Al-Sulami vile vile kama alivyosema Ibnu Al-Athir.[860] Na kwa hivyo, itakuwa (jina) "Haritha" ni upotoshaji (*tas-hif* tu) wa (jina) Al-Harith. Na kwa msingi huu, huenda ikawa labda ndiye yule aliyemkusudia Al-Baradi, hasa hasa (ukizingatia ukweli kwamba) haikupokelewa kwamba yeye aliuliwa katika (vita vya) Siffin, na wala sikuona kutajwa tena baada ya hapo.

10) ABU AMRI BIN NAUFAL: Al-Baradi kamtaja kuwa ni miongoni mwa watu wa Nahrawaan na kuwa ni miongoni mwa Masahaba.[861]

11) HARAM BIN AMRI AL-ANSARI (KATIKA KABILA LA BANI WAQIF). Al-Baradi kamtaja kuwa ni miongoni mwa watu wa Nahrawaan,[862] na Ibn Abdul-Barri akamtaja kuwa ni miongoni mwa Masahaba na akamwita Harm bin Amri Al-Ansari,[863] na akasema kuhusu yeye: "Ni mmoja wa waliolia ambao iliwateremkia (Aya isemayo): **"Wanarejea na macho yao yanachirizika machozi…"**[864] Na akataja Ibn Al-Athir kwamba alikuwa ni mwenye kutangulia katika Uislamu na ni mmoja wa waliolia ambao walimjia Mtume (s.a.w.) ili awachukue (vitani) ikawa (Mtume (s.a.w.) hana (mnyama) wa kuwabebea wakarejea nao wanalia.[865] Na Ibn Hajar akamtaja katika *tarjama (biography)* ya Harami **(**حرمي**)** bin Amri Al-Waqifi, na akasema yanakuja (maelezo yake) katika (sehemu yenye majina ya) Harami (هرمي) kwa hee[866]……..[867]

858 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 4, uk. 714, *tarjama* na. 6030.
859 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 4, uk. 714, *tarjama* na 6032.
860 - Ibn Al-Athir *Usdu Al-Ghaba* j. 1, uk. 474.
861 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118.
862 - Al-Baradi *Al-Jawahir* uk. 118.
863 - Ibn Abdil-Barri *Usdu Al-Ghaba* j. 4, uk. 1537, nambari 2676.
864 - Surat Al-Tauba Aya ya 92. Hawa ni Masahaba saba waliomuendea Mtume (s.a.w.) ili wachukuliwe vitani, lakini Mtume (s.a.w.) akawa hana kipandwa cha kuwabebea, wakarejea huku wanalia.
865 - Ibn Al-Athir *Usdu Al-Ghaba* j. 4, uk. 616, nambari 5352, na uk. 618, nambari 5358.
866 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 53, *tarjama* na. 1676.

12) AL-KHIRRITH BIN RASHID AL-SAAMI AL-NAJI: Alihudhuria pamoja na Ali (vita vya) Jamal na (vita vya) Siffin, na alijitenga na Ali bin Abi Talib kwa sababu ya (Ali kukubali) sulhu,[868] kisha Ali akamtumia Ma'aqil bin Qais Al-Rayahi akamuua Al-Khirrith.[869]

Na Ibn Abdil-Barri[870] na Ibn Al-Athir[871] wamemtaja Al-Khirrith bin Rashid (huyu) kuwa miongoni mwa Masahaba, na Ibn Hajar (akamtaja) katika sehemu ya kwanza,[872] lakini yeye kataja (tena) katika sehemu ya tatu (kwa jina la) Al-Khirrith bin Rashid Al-Shami, akisema: "Ni mwenye kuwahi (wakati wa Mtume)"[873] akiwatafautisha kwayo baina ya (Al-Khirrith) wawili, pamoja na kuwa katika *tarjama* (*biography*) ya kila mmoja katika hao kataja yenye kuonesha kuwa wao ni mtu mmoja (tu yule yule). (Na) hio ni kwa sababu hakuna tafauti baina ya (kabila la) Al-Naji na (kabila la) Al-Saami, kwani Al-Saami ni nasaba ya Bani Saama bin Luay,[874] na Al-Naji linanasibishwa kwa Najia,[875] kabila linalotokana na Saama bin Luay (vile vile). Ama (kutajwa kwa kabila la) Al-Shami ni wazi kwamba ni upotoshaji *(tas-hif)* wa kabila la Al-Sami."[876]

---

867 - Hapa kuna maelezo nimeyaruka: sikuyafasiri kwa ajili ya kufupisha. Cha muhimu ni kuthibitisha tu kuwa huyu ni Sahaba na alikuwa miongoni mwa watu wa Nahrawaan.

868 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 177. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 137. Ibn Al-Jawzi *Al-Muntadhim* j. 5, uk. 153. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 3, uk. 364. Al-Tabari ndiye peke yake (aliyesema) kwamba (Al-Khirrith bin Rashid) kahudhuria Nahrawaan lakini hakuna utajo wa Nahrawaan katika vitabu vyengine vya historia, na hili (la kuwa Al-Khirrith bin Rashid alikuwa katika watu wa Nahrawaan) ndilo lenye uzito kwa sababu tafauti baina ya Al-khirrith na Ali zilikuwa baada ya (Ali) kuwafanya waamuzi wawili watoe hukumu.

869 - Al-Baladhiri *Al-Ansab* j. 3, uk. 179-182. Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 137.

870 - Ibn Abdil-Barri "AL-ISTIAB" j. 2, uk. 458, nambari 292.

871 - Ibn Al-Athir *Usdu Al-Ghaba* j. 2, uk. 128, namba 1437.

872 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 273, *tarjama* na. 2246.

873 - Ibn Hajar *Al-Isaba* j. 2, uk. 359-360, *tarjama* na. 2334.

874 - Al-Suyuti *Lubbu Al-Ubaab* j. 2, uk. 6, nambari 2027.

875 - Al-Suyuti *Lubbu Al-Ubaab* J. 2, Uk. 287, Nambari 3943.

876 - Mwisho wa kunukuu maneno ya Sheikh Nassir Al-Sabi'i kuhusu utafiti wa Masahaba wa Nahrawaan. Kumbuka kwamba hawa aliowataja Sheikh Nassir ni mifano miwili mitatu tu ya Masahaba hao, na Masahaba hao walikuwa wengi sana, na dhahir ni kuwa jeshi la Nahrawaan lililojitenga na Ali ndilo lililokuwa na Masahaba

MUKHTASARI WA JUMLA NA NUKTA MUHIMU

Tulichokizungumzia katika sura hii ya mwisho ni suala la kuwemo kwa Masahaba wa Mtume (s.a.w.) katika jumla ya Watu wa Nahrawaan ambao watu wanawaita kuwa ni *Khawarij*. Jambo hili watu wengi – hata wanavyuoni – walikuwa hawalijui pamoja na kuwa ukipekuwa katika vitabu utaliona liko wazi. Labda sababu ya hayo ni kuwa watu wengi – hata wanavyuoni – huwa wanapenda zaidi *kuqalliid* (kufuata) kauli za waliowatangulia na kuzifanya kuwa ni dini hata bila ya kuziweka katika mezani sahihi. Na mara nyengine – kama si mara zote – huwa muasisi wa kauli hizo ni mtu mmoja tu: na wengine wakafuata. Au wakati mwengine sababu ya hayo inaweza ikawa ni propaganda zinazotokana na misimamo ya kisiasa hususan ikiwa wahusika ni wapinzani wa mfumo tawala kama hali ilivyokuwa kwa Watu wa Nahrawaan ambao walikuwa ni wapinzani wa Ali na baadae wa Mu'awiya.

Kwa hali yoyote ile, tumethibitisha kimaandishi na kiakili kwamba katika watu hao mulikuwa na idadi kubwa ya Masahaba. Bali wao ndio waliokuwa Masahaba wa awali, Maulamaa na wacha Mungu kama ilivyothibitisha riwaya ya Ibn Abbaas. Kwa hivyo, jambo hili linatakiwa litoe msukumo mpya na njia mpya ya kulisoma kiundani zaidi sula hili la wanaoitwa *Khawarij*, kwani ni vigumu kukubali kwamba kikundi ambacho ndicho chenye Masahaba wengi zaidi, walio Maulamaa na watu wa ibada kushinda wote, kiwe na sifa mbaya za kuua watu ovyo au kiwe ndicho kilichotoka katika dini.

Kwa mukhatasari ni kuwa nilichojaribu kukielezea katika kazi hii ni:

Mosi: kutafuta nini *taarifu* (Definition au ufafanuzi) na maana ya neno *Khawarij* kitaalamu. Tumeona kwamba hakuna mwanachuoni ambaye kaweza kutoa *taarifu* ya wazi au *taarifu* pambanuzi. Na kama tulivyoeleza

---

wengi zaidi kuliko kundi la Ali na la Mu'awiya, kwani Al Quraa (wanavyuoni)wengi walikuwa katika jeshi hilo.

kabla kwamba sababu ya hayo ni kuwa sifa mbaya zote wanazopewa Watu wa Nahrawaan – kwa haki au kwa batili – pia utazikuta katika vikundi vyengine vyote.

Pili: ni kuthibitisha kwamba watu hao walipomuacha mkono Ali walikuwa na hoja za Kisharia za Qur-ani: hoja ambazo hata Ibn Abbaas zilimfanya akiri kwamba wao ndio walio katika haki na kwa hivyo alikataa kushirikiana na Ali katika kuwapiga vita watu hao na akasema kwamba Watu wa Nahrawaan: "Wameisibu njia (ya haki),"[877] na akamwambia Al-Imamu Ali:

> Wallahi ni bora nikutane na Allah pamoja na yalio katika tumbo la ardhi miongoni mwa dhahabu zake na fedha zake pamoja na vilivyojaa mgongoni kwake[878] kuliko kukutana naye na mimi nimemwaga damu ya Umma huu ili nipate Ufalme au Uamiri (uongozi).[879]

Na akasema pia Ibn Abbaas kumwambia Ali:

> Na lau kama kuchukua kwangu mali ilikuwa ni batili, basi (hilo) lingekuwa jepesi kwangu kuliko kushiriki katika (kumwaga) damu ya Muumini.[880]

Ibn Abbaas kayasema haya pamoja na kuwa alishiriki vita vyote pamoja na Ali isipokuwa vita vyake dhidi ya Watu wa Nahrawaan. Ni wazi kwamba katika vita hivi Ibn Abbaas kamtia Ali makosani. Na hii ni kwa sababu Ibn Abbaas alijadiliana na watu hao nao wakazijibu hoja zake kwa hoja za Qur-ani, na hapo akakubaliana nao.

Tatu: tumebainisha kwamba tukio la kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbaab limechukuliwa kuonesha kwamba watu hao walikuwa wakimwaga damu za wasio na hatia, nalo suala hilo la kuuliwa kwa Abdillahi bin Khabbaab ni suala ambalo dhahir lilitokea kweli, lakini

---

877 - Al-Shammakhi ,*Al-Siyar* j. 1, uk. 72.

878 - Mgongoni mwa ardhi.

879 - Al-Baladhiri, *Al-Ansab* j. 2, uk. 398. Ibn Abd Rabbi, *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 326. Na mfano wake imo katika *Al-Futuh* j. 4, uk. 75, cha Ibn A'atham.

880 - Al-Qalhati, *Al-Kashf* j. 2, uk. 251. Ibn Abdi Rabih *Al-'Iqdu Al-Farid* j. 4, uk. 331.

kuhusishwa kwake na watu hao bado ni *mushkeli* mkubwa. Na riwaya zinaeleza kwa uwazi kabisa kuwa mfanyaji wa hayo alikuwa ni Mis'ar bin Fadaki na kikosi chake kilichotoka Basra kabla hata ya kufika Nahrawaan. Na baada ya kufika Nahrawaan, riwaya zinagongana, je Watu wa Nahrawaan waliwapokea au waliwafukuza. Lakini baada ya uchunguzi wa kina utaona kwamba riwaya za kuwa watu hao walimfukuza Mis'ar bin Fadaki na kikosi chake ndizo zenye uzito, kwani:

a) Abu Bilal – mmoja wa walionusurika na kuuliwa katika vita vya Nahrawaan – alikuwa akijitenga[881] na Qarib na Zahhaf kwa sababu ya matendo yao ya kuua watu bila haki, na akijitenga na Ziad bin Abih na Samura bin JundubJundub kwa sababu hio hio. Kwa hivyo, haielekei kwamba awachukie watu fulani kwa sababu ya kufanya mauaji ya haramu, kisha awapende Watu wa Nahrawaan na kumuomba Allah amkutanishe nao lau nao walikuwa wakifanya matendo hayo.
b) Pia tumeona kwamba Mi'ar bin Fadaki alikuwa katika jeshi la Ali katika kikosi kilichoongozwa na Abu Ayyub Al-Ansari katika kuwapiga Watu wa Nahrawaan. Kama Watu wa Nahrawaan walimpokea Mis'ar bin Fadaki, ambaye ndiye aliyemuua Abdullahi bin Khabbaab, basi asingelikuwa pamoja na Ali katika vita dhidi yao. Ni wazi kwamba wao hawakumpokea.
c) Vile vile tumethibitisha kwamba riwaya hizi hazikuja kwa njia sahihi, lakini tumesema kwamba hata tukijaalia kuwa ni riwaya sahihi basi bado kitendo cha kumuua Abdillahi bin Khabbaab kinabaki kuwa ni kitendo cha kibinafsi cha Mis'ar bin Fadaki.
d) Pia tumesema kwamba tukijaalia kuwa ni kweli watu hao walimuua Abdillahi bin Khabbaab kwa dhulma, basi wengine – kama Mu'awiya na kundi lake – wameua mamia bali maelfu ya Waumini, Masahaba na Wanavyuoni wakubwa, na wakafanya ufisadi wa kila aina: kuvunja majumba, kuvunja Al-Ka'aba na kuiwasha moto na wengine hadi kufikia kuwafukua maiti na kuwachoma moto. Sasa kwanini *Khawarij* wasiwe hawa waliofanya mengi zaidi na makubwa zaidi na badala yake *Khawarij* wawe wale waliofanya machache tukijaalia kuwa ni kweli watu hao walimuua Abdillahi bin Khabbab! Hii ni mantiki

[881] - Yaani akiwachukia.

ya aina gani enyi walimwengu wenzangu? Pia wanaojiita kuwa ni wafuasi wa Ali, wamefanya mauaji haramu ya mamia kama si maelfu ya Waumini wenye itikadi tafauti na wao, na hadi leo hii wanaendelea. Sasa kwanini hawa nao wasiwe *Khawarij*?

Nne: Suala la kuuliwa kwa Al-Imamu Ali. Watu wamezoea kupewa maelezo yasiyo sahihi juu ya maudhui hii. Hakuna shaka kwamba aliyemuua Ali alikuwa ni Ibn Muljam lakini ni kipi chenye kutoa ushahidi kwamba Ibn Muljam alikuwa miongoni mwa walioitwa *Khawarij*? Utakumbuka kwamba Al-Imamu Ali alikuwa na maadui[882] wakubwa zaidi kuliko hao walioitwa Khawarij, basi kwanini tena watu wamuhusishe Ibn Muljam na walioitwa *Khawarij*: kwanini wasimuhusishe na Mu'awiya? Tumesema kwamba lau kweli Ibn Muljam alikuwa ni mwenye fikra na rai kama za Watu wa Nahrawaan na alimuua Ali kulipiza kisasi kwa watu walioiuliwa huko Nahrawaan, basi asingelishirikiana na Al-Ash'ath bin Qais katika kumuua Ali, bali angelimuanza Al-Ash'ath bin Qais kwanza kwani yeye Al-Ash'ath ndiye aliyekuwa adui mkubwa wa Watu wa Nahrawaan. Lakini kushirikiana kwa Ibn Muljam na Al-Ash'ath bin Qais – kama riwaya zinavyosema – katika kumuua Ali, kunatupa picha kwamba tukio hili kuna uwezekano mkubwa kwamba lilitendeka kwa msukumo wa Mu'awiya, kwani:

1) Al-Ash'ath bin Qais alikuwa ni jasusi wa Mu'awiya kama tulivyobainisha.
2) Wafuasi wa Ali wa zama hizo walimtuhumu Mu'awiya juu ya tukio hilo.
3) Waliokusudiwa kuuliwa ni Ali, Amru bin Al-'Aas na Mu'awiya kwa mujibu wa kisa cha Ibn Muljam na wenzake. Ali aliuliwa, lakini Amru na Mu'awiya hawakuuliwa!
4) Watu watatu hao waliyapanga mauaji hayo kwa siri kubwa, lakini hatimae tunaona kuwa kisa kimerikodiwa kiukamilifu. Baada ya kupekuwa vitabu tunamkuta Al-Mas'udi anatwambia kwamba kumbe aliyeyasimulia hayo ni yule aliyekusudia kumuua Amru

[882] - Nao ni Mu'awiya na dola yake ya Banii Umayya. Ama walioitwa Khawarij wao ndio waliopinga kitendo cha Banii Umayya cha kumuombezea Ali laana juu ya membari. Na kwa uwazi zaidi ni kuwa kikundi cha wanavyuoni wa Kiibadhi ndio waliomuendea Imamu Muadilifu Umar bin 'Abdil-'Aziz (r.a.) kumtaka aondoshe jambo hilo.

bin Al-'Aas. Mtu huyo – kwa mujibu wa riwaya hio – aliuliwa. Sasa nani aliyekisimulia kisa hicho baada ya hapo? Ni wazi kwamba Amru bin Al-'Aas ndiye msimulizi wa kisa hicho. Na – kwa hivyo – ikiwa itathibiti kwamba yeye ndiye msimulizi, basi bila shaka atakuwa ndiye mpangaji wa kisa hicho. Na hakuna maana ya kukipanga kisa hicho ila iwe kuna ubaya umetendeka unatafutiwa njia ya kuuficha.

Tano: Watu wa Nahrawaan walipojitenga na Ali, Ali hakuwa kiongozi tena kwa mujibu wa Sharia na kwa mujibu wa maahidiano yao, kwani hakutekeleza Aya ya Qur-ani iliyompa haki ya kumpiga Mu'awiya, na maahidiano yao ni kuwa watamtii kwa masharti ya kuitekeleza Qur-ani na Sunna. Ukichangnya na ukweli kwamba muwakilishi wake Abu Musa alimuuzulu; naye mwenyewe kabla ya hapo alikubali kufuta jina la Uamiri katika mkataba wa sulhu: jina ambalo ndilo aliloahidiana na Waislamu kwalo. Sasa baada ya hapa wapi Umma ulimchagua tena Ali kuwa Khalifa ili aliyetoka katika kumtii awe ameasi?

Sita: Athari zilizopatikana kwa Ali kuwaua Watu wa Nahrawaan. Baada ya kuwauwa watu wa Nahrawaan, Ali alipoteza nguvu zake zote na hakuwa tena na jeshi la kukabiliana na Mu'awiya kwani Watu wa Nahrawaan ndio waliokuwa wapiganaji wake wa nguvu kwani waliobaki pamoja naye walimfanyia khiyana wakakataa kumtii.[883] Hatima ikawa ni kudhoofika dola yake kidogo kidogo hata ilipofikia zama za watoto wake ikawa dola ya Banii Umayya imeshajijenga taqriban katika nchi zote za Kiarabu.

La saba na la mwisho Risala ninayokusudia kuifikisha katika kitabu hiki ni kuwa kweli kuna Hadithi sahihi inayosema kwamba watakuja watu ambao watatoka katika dini kama mshare unavyotoka katika kiwindwa (mnyama anayewindwa) lakini Hadithi hio haiwahusu Watu wa Nahrawaan kamwe: kuihusisha Hadithi hio na Watu wa Nahrawaan kumetokana na kuiunganisha na Hadithi nyengine za kutunga halafu watu wakaihusisha Hadithi hio na Watu wa Nahrawaan. Na hakuna katika historia nzima kitu sahihi chenye kuonesha kwamba Watu wa

883 - Al-Tabari, *Al-Taarikh* j. 6, uk. 39-40. Ibn Al-Athir *Al-Kamil* j. 2, uk. 709.

Nahrawaan wametoka katika dini na ndio maana Ali mwenyewe alikataza kuwaita watu hao makafiri au wanafiki. Kama kweli ilikuwa Hadithi hio inawahusu watu hao, basi Ali asingelikataza wao kuitwa hivyo, kwani maelezo yanayopatikana katika Hadithi hio yako wazi kwamba watu waliotabiriwa katika Hadithi hio watakuwa wametoka katika dini. Bali ninasema kwamba: hakuna katika historia nzima ya kadhia hii ushahidi wenye kuthibitisha kwamba Watu wa Nahrawaan wamekosea licha ya kutoka katika dini.

HATIMA

Hadi hapa tutakuwa tumefikia mwisho wa juzuu ya kwanza ya kitabu hiki ***Khawarij- Baina ya Ukweli na Visa vya Kutunga*** ambacho kimeelezea juu ya walioitwa *Khawarij*. Ni matarajio yangu kwamba watu watakuwa wamefahamu ukweli wa suala hili, hasa hasa wale ambao wamekuwa wakiuliza sana kuhusu jambo hili. Maudhui hii inaendelea katika juzuu zitakazofuatia *Inshaa Allah*. Tunamuomba Allah atupokelee kazi yetu hii na awafae Waislamu kwayo, na awafanye Waislamu wafahamiane na wajuane zaidi na wawe wenye kufahamu hoja za kila kundi na wafuate yalio sahihi kwani katika hayo ndio kwenye ridhaa za Allah.

Ndugu yenu:
Juma Muhammad Rashid Al-Mazrui
Mobile: (968) 92213699
E-Mail: jumamazrui@hotmail.com....jumamazrui@yahoo.com
Al-Qurm, Muscat Oman.

تم الجزء الأول ولله الحمد
ويليه الجزء الثاني في البحث عن الروايات الواردة في الخوارج

Juzuu ya kwanza imekamilika – Alhamdu li-Lahi – na itafuatiwa na juzuu ya pili ambayo itahusu Hadithi zinazosimulia *Al-Khawaarij*.